SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, S.L.P 258, 71125 Kilimani Zanzibar
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

---

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

..........................................
**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu**
Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.

2. **Uadilifu**
Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

3. **Kuwa Huru**
Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.

4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi**
Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

5. **Kutunza Siri**
Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

6. **Uwazi na Uwajibikaji**
Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO


YALIYOMO........................................................................V

ORODHA YA MAJADWELI..........................................................XI

VIFUPISHO........................................................................XVII

SHUKURANI........................................................................XIX

DIBAJI........................................................................XXI

MUHTASARI........................................................................XXIII

**SURA YA KWANZA**........................................................................1

1.0 UTANGULIZI........................................................................1

1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI........................................................................1

1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI........................2

1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI........................................3

1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA...4

1.5 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI........................................5

**SURA YA PILI**........................................................................7

2.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI........................................7

2.1 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023........................................7

2.1.1 DOSARI ZA KIUTENDAJI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI.........7

2.2 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA AJILI YA UKAGUZI........................................9

2.3 HATI ZA UKAGUZI........................................................................13

2.3.1 AINA YA HATI ZA UKAGUZI....................................................13

2.3.2 AYA YENYE MASUALA YA MSISITIZO KWENYE RIPOTI ZA MKAGUZI....................................................14

2.3.3 MASUALA MUHIMU YA UKAGUZI....................................................14

2.3.4 MSINGI WA HATI ZA UKAGUZI....................................................14

2.3.5 HATI ZA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023............15

2.4 MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI....................................................20

2.5 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA ULIOPITA....................................................20

**SURA YA TATU**....................................................23

3.0 UKAGUZI WA HESABU JUMUISHI YA SERIKALI.........................23

3.1 TAARIFA YA MAPATO KWA MWAKA 2022/2023.........................23

3.1.1 Taarifa za Mapato....................................................23

3.2 TAARIFA YA MATUMIZI KWA MWAKA 2022/2023.....................24

3.2.1 TAARIFA ZA MATUMIZI ZA TAASISI ZA KIBAJETI ZA SERIKALI NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA....................................................24

3.3 TAARIFA YA GAWIO LA SERIKALI....................................................24

3.4 TAARIFA YA DENI LA SERIKALI....................................................25

3.4.1 MWENENDO WA DENI LA NDANI....................................................25

3.4.2 DENI LA NJE....................................................25

3.4.3 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA HESABU JUMUISHI ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023...................26

**SURA YA NNE**.....33

4.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI.....33

4.1 MATOKEO YA TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI.....33

4.1.1 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....33

**SURA YA TANO**.....59

5.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....59

5.1 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS IKULU.....59

5.1.1 FUNGU A 01 - OFISI YA RAIS IKULU.....59

5.1.2 FUNGU A 02 – OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI – BLM.....60

5.1.3 FUNGU B 01 – OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS.....61

5.2 WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI.....64

5.2.1 FUNGU C 02 - BARAZA LA WAWAKILISHI.....64

5.2.2 FUNGU C 03 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR.....70

5.2.3 FUNGU C 05 – TUME YA UKIMWI ZANZIBAR.....71

5.3 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ.....77

5.3.1 FUNGU D 01 - OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ.....77

5.4 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO.....83

5.4.1 FUNGU F 01 – OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO..............83

5.4.2 FUNGU F 03 - TUME YA MIPANGO ZANZIBAR........................96

5.4.3 FUNGU F04 - AFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR....................................................................97

5.4.4 FUNGU F05 - OFISI YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI........106

5.4.5 FUNGU F06 - OFISI YA MKAGUZI MKUU WA NDANI............107

5.5 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA........................................................109

5.5.1 FUNGU G 01 - OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA...........................................................109

5.5.2 FUNGU G 02 - MAHKAMA KUU............................................111

5.5.3 FUNGU G 03 – AFISI YA MWANASHERIA MKUU....................114

5.5.4 KITUO CHA MAFUNZO YA SHERIA NA UTAFITI ZANZIBAR.....119

5.5.5 FUNGU G 05 – TUME YA KUREKEBISHA SHERIA...................121

5.5.6 FUNGU G15 - TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR..................................................................122

5.5.7 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA PEMBA............127

5.5.8 SKULI YA SHERIA ZANZIBAR............................................129

5.6 WIZARA YA AFYA..........................................................131

5.6.1 FUNGU H01 - WIZARA YA AFYA.........................................131

5.6.2 FUNGU H02 - HOSPITALI YA MNAZI MMOJA.........................141

5.7 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO..................................................................142

5.7.1 FUNGU – WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO..................................................................142

5.8 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE....................................152

5.8.1 FUNGU J01 - WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE.............152

5.8.2 FUNGU J 02 - KAMISHENI YA UTALII.......................................156

5.9 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO.........167

5.9.1 FUNGU J03 - WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO...........................................................................167

5.10 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI............................181

5.10.1 FUNGU K01 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI.......181

5.10.2 CHUO CHA KIISLAM (CCK) PEMBA.........................................191

5.10.3 BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR.......................191

5.10.4 BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR...........................................193

5.11 WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO.....195

5.11.1 FUNGU L01 - WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO...........................................................................195

5.11.2 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR (ZARI).................205

5.11.3 TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO ZANZIBAR (ZALIRI).............206

5.12 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI.............................206

5.12.1 FUNGU L02 - WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI.......206

5.13 WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI..................213

5.13.1 FUNGU N01 – WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI...........................................................................213

5.13.2 KAMISHENI YA ARDHI.............................................................217

KAMATI YA UDHIBITI WA UJENZI IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI (DCU)........................................................................220

5.14 WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI................................224

5.14.1 FUNGU N 03 - WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI...........224

5.15 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI................229

5.15.1 FUNGU P01 - WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI...................................................................229

5.16 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI...................................................................232

5.16.1 FUNGU Q01 - OFISI YA RAIS KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI...................................................................232

5.17 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA............235

5.17.1 FUNGU R01 - WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA...................................................................235

5.17.2 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR........................................238

5.17.3 TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA........................239

**6.0 HITIMISHO**.....................................................................242

**VIAMBATISHO**.................................................................243

# ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Orodha ya Wizara na Taasisi zilizowasilisha Hesabu za mwisho wa mwaka kwa Ukaguzi ........................ 10
Jadweli Nambari 2: Taasisi za Serikali zilizokaguliwa na kupata Hati za ukaguzi ........................................................ 16
Jadweli Nambari 3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi .............................. 20
Jadweli Nambari 4:Mwenendo wa deni la ndani kwa miaka mitatu (deni halisi)......................................................... 25
Jadweli Nambari 5: Tofauti ya mishahara iliyoripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka na mfumo wa mishahara. ......... 28
Jadweli Nambari 6: Tofauti baina ya "Exchequers" na Mfumo wa Mishahara.......................................................... 29
Jadweli Nambari 7: Tofauti iliyobainika katika hesabu Jumuishi ............ 30
Jadweli Nambari 8: Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani.............................. 35
Jadweli Nambari 9: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu ..................... 38
Jadweli Nambari 10: Taasisi zilizokuwa hazikufuata muongozo wa ufungaji wa hesabu ........................................ 39
Jadweli Nambari 11: Taasisi zilizokosa buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)........ 40
Jadweli Nambari 12: Vyombo vya Usafiri ambavyo Havijakatiwa Bima ... 41
Jadweli Nambari 13: Taasisi ambazo hazikutenganisha masjala ya siri na masjala bayana............................................ 45
Jadweli Nambari 14: Taasisi zisizokuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali zinazomilikiwa na Afisi......................................... 46
Jadweli Nambari 15: Taasisi ambazo hazina utaratibu wa kudhibiti vihatarishi ................................................................ 48
Jadweli Nambari 16: Taasisi ambazo hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ....... 49
Jadweli Nambari 17: Watumishi ambao hawajathibitishwa kazi ............. 50
Jadweli Nambari 18: Taasisi zilizofanya malipo bila ya kudai stakabadhi za kielektroniki.................................. 53

Jadweli Nambari 19: Taasisi ambazo hazina Mpango wa Kukabiliana na Maafa ..... 56
Jadweli Nambari 20: Taasisi ambazo hazijafanya utaratibu wa kuhesabu mali (stock taking) ..... 57
Jadweli Nambari 21: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba ..... 61
Jadweli Nambari 22: Mikataba yenye Ongezeko la Fedha ..... 63
Jadweli Nambari 23: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ..... 65
Jadweli Nambari 24: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi ..... 66
Jadweli Nambari 25: Wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa ..... 67
Jadweli Nambari 26: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ..... 68
Jadweli Nambari 27: Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu ..... 69
Jadweli Nambari 28: Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu husika ..... 71
Jadweli Nambari 29: Malipo yenye vielelezo pungufu ..... 73
Jadweli Nambari 30: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ..... 74
Jadweli Nambari 31: Watumishi ambao hawajaenda likizo lao la mwaka kwa muda mrefu ..... 75
Jadweli Nambari 32: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ..... 76
Jadweli Nambari 33: Malipo ambayo hayakukatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ..... 78
Jadweli Nambari 34: Malipo yaliofanyika bila kuzingatia masharti ya mkataba ..... 80
Jadweli Nambari 35: Mapato ambayo hayakuingizwa katika hesabu za mwisho wa mwaka ..... 81
Jadweli Nambari 36: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ..... 85
Jadweli Nambari 37: Malipo yaliyofanyika kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu ..... 86
Jadweli Nambari 38: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu ..... 90
Jadweli Nambari 39: Ukodishwaji wa majengo kwa bei ndogo ..... 92
Jadweli Nambari 40: Mikataba ambayo haikurikodiwa katika daftari maalum la Mikataba (Contract Register) ..... 93
Jadweli Nambari 41: Ubovu na uchakavu wa maduka na bekari ..... 94
Jadweli Nambari 42: Mali za Afisi ambazo hazina hati miliki ..... 95
Jadweli Nambari 43: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ..... 98

Jadweli Nambari 44: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi .......... 99
Jadweli Nambari 45: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ............... 105
Jadweli Nambari 46: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz........................................................... 106
Jadweli Nambari 47: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ............... 109
Jadweli Nambari 48: Malipo ya baadhi ya watumishi waliodhaminiwa IPA-UDOM ................................................... 110
Jadweli Nambari 49: Gari ambazo hazijafanyiwa matengenezo wala kuondolewa kwa muda mrefu............................. 113
Jadweli Nambari 50: Mali za kudumu ambazo zimekosa nyaraka za umiliki........................................................... 113
Jadweli Nambari 51: Vyombo vya Moto Ambavyo Havina Kadi za Usajili ........................................................... 114
Jadweli Nambari 52: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz........................................................... 115
Jadweli Nambari 53: Malipo nje ya Mpango wa manunuzi.................... 116
Jadweli Nambari 54: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ............... 117
Jadweli Nambari 55: Mafuta yaliyonunuliwa ambayo hati za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi ................................ 118
Jadweli Nambari 56: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz........................................................... 119
Jadweli Nambari 57: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ............... 120
Jadweli Nambari 58: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz........................................................... 121
Jadweli Nambari 59: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz........................................................... 122
Jadweli Nambari 60: Malipo yaliyofanywa kwa Mkandarasi na Mshauri Elekezi ........................................................... 124
Jadweli Nambari 61: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ............... 125
Jadweli Nambari 62: Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la Ghalani ........................................................... 126
Jadweli Nambari 63: Majengo ya Afisi ambayo hayana hati miliki .......... 128
Jadweli Nambari 64: Orodha ya madeni yanayodaiwa Skuli ya Sheria.... 129

Jadweli Nambari 65: Madeni ya wanafunzi wanayodaiwa na Skuli ya Sheria ........ 130
Jadweli Nambari 66: Malipo ya madaktari wa Cuba yasiyokuwa na mikataba ........ 134
Jadweli Nambari 67: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki ........ 135
Jadweli Nambari 68: Watumishi wanaopaswa kurejeshewa mishahara iliyozuiliwa kinyume na utaratibu ........ 138
Jadweli Nambari 69: Madeni ya muda mrefu ya Wizara ........ 139
Jadweli Nambari 70: Mali chakavu ambazo hazijauzwa wala kufanyiwa matengenezo ........ 141
Jadweli Nambari 71: Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji ........ 143
Jadweli Nambari 72: Orodha ya walinzi wanaodai ni kama ilivyoainishwa ........ 146
Jadweli Nambari 73: Malipo ya mradi wa uimarishaji maeneo ya Kihistoria ........ 149
Jadweli Nambari 74: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na ZPPDA ........ 150
Jadweli Nambari 75: Utoaji na utumiaji wa mafuta usioridhisha ........ 153
Jadweli Nambari 76: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ........ 154
Jadweli Nambari 77: Fedha zilizotumika kukarabati maeneo ya kihistoria na mapato yaliyokusanywa ........ 156
Jadweli Nambari 78: Tofauti kati ya Hesabu za Mwisho wa mwaka na Taarifa katika Mikataba ........ 157
Jadweli Nambari 79: Miradi ambayo haijaoonekana katika maeneo yake ........ 159
Jadweli Nambari 80: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa ........ 161
Jadweli Nambari 81: Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi ........ 163
Jadweli Nambari 82: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ........ 165
Jadweli Nambari 83: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz ........ 166
Jadweli Nambari 84: Vilabu vya Mpira wa Miguu vinavyodaiwa na Wizara ........ 168
Jadweli Nambari 85: Miradi ambayo imechelewa kutekelezeka ........ 170

Jadweli Nambari 86:Viwanja ambavyo havina hati miliki ........................ 171
Jadweli Nambari 87: Mapato ambayo hayakuonekana katika taarifa za benki ................................................ 174
Jadweli Nambari 88: Kutokuwiyana kwa baadhi ya taarifa za mapato za Wizara ................................................................ 175
Jadweli Nambari 89: Mchanganyiko wa taarifa za mapato .................... 177
Jadweli Nambari 90 Malipo ya ubani yaliolipwa pungufu ....................... 182
Jadweli Nambari 91: Wastaafu ambao waliendelea kupokea mishahara nje ya muda wa utumishi .................................. 185
Jadweli Nambari 92: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu bila ya kufuata taratibu ............................................ 186
Jadweli Nambari 93: Malipo ya huduma za dakhalia yenye dosari mbali mbali ........................................................ 189
Jadweli Nambari 94: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu...... 192
Jadweli Nambari 95: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz............................................................ 194
Jadweli Nambari 96: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba ............ 195
Jadweli Nambari 97: Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu husika............ 197
Jadweli Nambari 98: Madeni ya muda mrefu ya Wizara ........................ 199
Jadweli Nambari 99: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki .............. 199
Jadweli Nambari 100: Vyombo vya moto ambavyo havina kadi za usajili 201
Jadweli Nambari 101: Mali chakavu ambazo hazijauzwa wala kufanyiwa matengenezo ................................................. 204
Jadweli Nambari 102: Hati za malipo zilikosekana kwa ukaguzi ............ 207
Jadweli Nambari 103: Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa wakala wa Serikali wa Uchapaji.................................. 208
Jadweli Nambari 104: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba........... 210
Jadweli Nambari 105: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki ............ 212
Jadweli Nambari 106: Watumishi waliopatiwa mafunzo bila ya kufuatwa kwa Mpango wa Mafunzo ................................. 214
Jadweli Nambari 107: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ............... 214
Jadweli Nambari 108: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu ................................................................... 215
Jadweli Nambari 109: Madeni ya muda mrefu ya Wizara ...................... 217

Jadweli Nambari 110: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu ........................................................ 219
Jadweli Nambari 111: Mafuta yaliyonunuliwa bila ya kuwepo mkataba .. 223
Jadweli Nambari 112: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ............... 224
Jadweli Nambari 113: Orodha ya mashamba yaliochimbwa na bado hayajafanyiwa uhuishaji .................................. 227
Jadweli Nambari 114: Madeni ya muda mrefu ya Wizara ...................... 228
Jadweli Nambari 115: Vyombo vya moto ambavyo havina kadi za usajili 229
Jadweli Nambari 116: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu .............. 230
Jadweli Nambari 117: Ada ya ukaguzi ambayo haikulipwa .................... 233
Jadweli Nambari 118: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba........... 236
Jadweli Nambari 119: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki ............ 237
Jadweli Nambari 120: Watumishi waliokaimishwa nafasi kinyume na utaratibu ......................................................... 238
Jadweli Nambari 121: Madeni ya muda mrefu yanayodaiwa na Tume .... 241

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BOQ | Mchanganuo wa Gharama za Kazi |
| BoT | Benki Kuu ya Tanzania |
| BTMZ | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| COVID /UVIKO 19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona wa mwaka 2019 |
| EY | Ernst & Young |
| GBS | Misaada ya Kibajeti |
| IFRS | Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Hesabu |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| INTOSAI | Shirika la Kitamataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi |
| IPSAS | Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Taasisi za Umma |
| ISA | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu |
| ISSAIs | Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi |
| NAOT | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi |
| NHIF | Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa |
| OCAGZ | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar |
| PAC | Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali |
| PWC | Price Waterhouse Coopers |
| Shs/Tsh/Tshs/TZS | Shilingi ya Tanzania |
| SMT | Serikali ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TAC | Shirika la Ukaguzi Tanzania |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| UNICEF | Shirika la Kusaidia Watoto Duniani |
| USD | Dola ya Kimarekani |

| | |
|---|---|
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| VTA | Mamlaka ya Mafunzo ya Amali |
| WBMV | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda |
| ZAECA | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| ZBS | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| ZICTIA | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar |
| ZRA | Mamlaka ya Mapato Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| IFMIS | Intergrated Financial Management Information System |

# SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya maboresho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba, pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), Price Waterhouse Coopers (PWC), pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbali mbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia vyombo mbali mbali vya habari.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Afisi ya Mdhibiti katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora.

# DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Hesabu za Mawizara, Idara pamoja na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa kifungu cha 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Taarifa hizo zitaelezea hali halisi ya mapato na matumizi ya fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali kwenye tathmini na ukaguzi wa taarifa za fedha pamoja na nyaraka husika, mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu na mchakato wa manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali. Kufuatia kukamilika kwa ukaguzi huo nimetoa hati za ukaguzi kwa kila taasisi kuhusiana na taarifa za fedha zilizoandaliwa kama zinaonesha hali halisi ya shughuli zilizofanywa kulingana na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Nilifanya ukaguzi huo kwa kuangalia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa, kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

Nimetoa Hati za Ukaguzi kwa kuzingatia Taarifa za Fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo ilikaguliwa. Aidha, nilitoa barua za ukaguzi "Management Letters" zinazoonesha dosari zilizobainika kwa kila Shirika na Taasisi inayojitegemea iliyokaguliwa na mapendekezo ya kutekeleza ili kuboresha na kuondoa dosari zilizobainika kwa lengo la kutokujirejea mara nyengine.

Ni matumaini yangu kwamba Baraza la Wawakilishi litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za umuhimu katika kuisimamia Serikali na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za umma ili kuhakikisha kunakuwa na utoaji bora wa huduma kwa umma wa Wazanzibari ambao inawahudumia. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.

Kwa mara nyengine tena nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.

……………………………………………..

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**

## MUHTASARI

Ripoti hii imekusanya jumla ya sura tano (5) zenye kuelezea mambo mbali mbali yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kwenye Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi uliofanyika umebaini uwepo wa dosari mbali mbali ambapo dosari hizo zimewasilishwa kwenye uongozi wa Taasisi zilizokaguliwa kwa njia ya hoja za ukaguzi na kutolewa mapendekezo kwa lengo la kuimarisha dosari hizo, baadhi ya dosari ziliweza kufanyiwa kazi na Maafisa Masuuli wakati wa kipindi cha ukaguzi na kutolewa majibu kwa wakaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa dosari hizo. Aidha, baadhi ya dosari zilizobainika hazikuweza kupatiwa majibu wakati wa ukaguzi na kupelekea kuingizwa katika Ripoti hii. Mambo yaliyobainika yamefafanuliwa katika sura tofauti zilizomo katika ripoti hii kama ifuatavyo:-

**Sura ya Kwanza:** Sura hii imekusanya taarifa za Utangulizi wa ripoti ikiwemo majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, upeo na madhumuni ya ukaguzi, njia zilizotumika katika ukaguzi. Vile vile imeeleza umuhimu wa kufanya ukaguzi pamoja na taarifa za Kamati za Baraza la Wawakilishi.

**Sura ya Pili:** Sura hii inaeleza kwa muhtasari mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu pamoja na ufafanuzi wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo miongoni mwa mambo yaliyobainika ni utoaji wa hati za ukaguzi, pamoja na uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

**Sura ya Tatu:** Sura hii inatoa mrejesho wa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ikiwa ni makisio ya makusanyo na matumizi, makusanyo halisi, Fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu na matumizi yaliyofanywa na Serikali pamoja na kuelezea malengo makuu ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

**Sura ya Nne:** Sura hii inaelezea tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani inayoendeshwa ndani ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo imeelezea mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, pamoja na masuala ya utawala bora, Kamati za Ukaguzi na Kazi za Ukaguzi wa Ndani.

**Sura ya Tano:** Sura hii imeeleza kwa kina kuhusu matokeo na mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika kwa Wizara 18 pamoja na Idara na Taasisi 48 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainishwa pamoja na athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

## Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Ukaguzi ulitathmini mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwemo udhibiti katika kitengo cha ukaguzi wa ndani, kamati ya ukaguzi pamoja na Bodi ya Zabuni. Kwa ujumla tathmini iliyofanyika imebaini kujitokeza kwa maboresho makubwa katika vitengo vya ukaguzi wa ndani, Kamati za Ukaguzi pamoja na Bodi za Zabuni kwa baadhi ya Taasisi kupiga hatua za mafanikio ingawa zipo baadhi ya Taasisi zimebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali katika mfumo wa udhibiti wa ndani ambapo miongoni mwa dosari kubwa zilizobainika ni kwamba baadhi ya Taasisi zimeshindwa kushirikisha vitengo vya ukaguzi wa ndani na Kamati za Ukaguzi kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Taasisi hizo jambo ambalo lilipelekea hesabu zilizowasilishwa kuwa na dosari za kiutendaji na hatimae kurejeshwa ili ziweze kufanyiwa marekebisho katika hatua za awali za ukaguzi jambo ambalo lilipelekea kutokukamilika kwa kazi za ukaguzi kwa wakati uliopangwa.

## Tathmini katika ukusanyaji wa Mapato

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, ukaguzi ulibaini hali ya ukusanyaji wa mapato katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umeimarika ukilinganisha na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka uliopita. Hata hivyo baadhi ya taasisi zimebainika kuwa na dosari za kiutendaji ambazo zinahitaji marekebisho ya haraka ili kunusuru kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma unaotokana na baadhi ya taasisi kukusanya mapato nje ya mfumo, mapato kutumika kabla ya kuwasilishwa benki, ucheleweshwaji wa mapato kuwasilishwa sehemu husika, upotevu wa mapato, kutokulingana kwa mapato halisi yanayokusanywa na yale yanayowasilishwa benki pamoja na kutokuoneshwa kwa  mapato halisi yaliyokusanywa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu zimepelekea baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kulikosababishwa na baadhi ya watendaji kushikilia fedha za mapato mikononi pasi na kuziwasilisha sehemu husika na hatimae hesabu za taasisi hizo kutokuonesha sura halisi na sahihi.

## Tathmini ya Usimamizi wa Matumizi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi umebaini kuimarika kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali na kupelekea kuongezeka kwa hati zinazoridhisha na kuleta faraja na nidhamu juu ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Hata hivyo zipo baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi zimebainika kuwa na mapungufu mbali mbali katika nidhamu ya usimamizi wa matumizi na kupelekea kutokuzingatia matakwa ya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. Miongoni mwa dosari kubwa zilizobainika katika nidhamu ya matumizi ni kufanyika kwa malipo kwa fedha taslim, dosari katika uzuwiaji wa kodi, ucheleweshwaji wa mapato ya Serikali kuwasilishwa benki pamoja na kutokuzingatia maelekezo ya Serikali kuhusiana na kudai stakabadhi za kielektroniki wakati wa ufanyaji wa malipo.

## Tathmini ya Usimamizi wa Manunuzi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ukaguzi ulibaini uwepo wa maboresho katika Wizara, Idara na Taasisi zilizofanya manunuzi kwa kufanya manunuzi kupitia mfumo wa manunuzi pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazohusiana na manunuzi hayo, ingawa zipo baadhi ya Taasisi zilibainika kutokuzingatia Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi.

Aidha, baadhi ya taasisi zimebainika kufanya manunuzi bila ya kuzingatia ushindani wa bei, kufanya manunuzi kwa kutumia rasimu za mikataba, kufanya manunuzi bila ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia rasimu za mkataba walizoziwasilisha, kutokuambatishwa kwa nyaraka muhimu za manunuzi katika hati za malipo, kufanya manunuzi kinyume na mpango wa manunuzi, kutokuwasilishwa kwa mpango wa manunuzi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo limepelekea baadhi ya Taasisi kufanya manunuzi nje ya Mfumo wa manunuzi au kufanya manunuzi yaliyo na gharama kubwa zaidi kuliko uhalisia wa bajeti iliyowekwa kwenye mpango wa manunuzi.

## Tathmini katika Usimamizi wa Mikataba

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi ulibaini mapungufu mbali mbali yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria na taratibu za manunuzi unaotokana na baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi kushindwa kuwasilisha rasimu za mikataba yao Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kufanyiwa mapitio na kupatiwa ushauri wa kisheria juu ya namna bora ya kufanya maboresho ya dosari zilizobainika katika rasimu za mikataba hiyo.

Hata hivyo zipo baadhi ya taasisi zimebainika kutokutekeleza maagizo na mashauri yanayotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusiana na maboresho ya rasimu za mikataba na hatimae kufanya manunuzi na kuingia katika makubaliano ya kimkataba bila ya uwepo wa mikataba yenye tija na maslahi kwa Serikali na hatimae kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kutokutekelezwa kwa maagizo ya mikataba inayopitiwa na Mwanasheria Mkuu.

## Tathmini ya Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, ukaguzi ulifanyika kwa taasisi mbali mbali kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa. Kutokana na kuzingatiwa kwa vigezo vya ufungaji wa hesabu kwa taasisi za umma kumepelekea kuimarika kwa Hati za ukaguzi zinazoridhisha kwa taasisi mbali mbali zilizokaguliwa. Hata hivyo zipo baadhi ya Taasisi ziliendelea kuwa na dosari kubwa za ufungaji wa hesabu zao na kupelekea kulazimika kufanyiwa marekebisho kwa hesabu hizo.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, nilikamilisha ukaguzi wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ **66**. Kati ya Taasisi hizo jumla ya Wizara **18**, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara **48** za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutoa hati za ukaguzi kwa Taasisi **66**. Kati ya hati hizo zilizotolewa hati **63** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **95.45** ya hati zilizotolewa, na hati **3** ni hati zenye shaka sawa na asilimia **4.55** ya hati zilizotolewa na sikuwa na hati ya kushindwa kutoa maoni.

## Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa mwaka uliopita

Tathmini niliyofanya kwenye hali ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita nimebaini jumla ya mapendekezo 1,587 yalitolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi 66 zilizokaguliwa na kuwasilishiwa ripoti za ukaguzi. Kati ya mapendekezo hayo jumla ya mapendekezo 1,213 yaliweza kutekelezwa na kuondolewa ambayo ni sawa na asilimia 76.43, mapendekezo 93 yapo katika hatua ya utekelezaji sawa na asilimia 5.86. Hata hivyo, mapendekezo 85 bado hayajatekelezwa ambayo ni sawa na asilimia 5.36 na mapendekezo 124 yamejirudia sawa na asilimia 7.81 vile vile mapendekezo 72 yamepitwa na wakati sawa na asilimia 4.54. Kiujumla hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi imeimarika ambapo baadhi ya Taasisi zimeonekana kupiga hatua katika kufanya marekebisho ya dosari zilizobainika ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 dosari hizo hazikuweza kujirejea na kwa baadhi ya Taasisi zimeweza kupunguza idadi ya hoja zilizobainishwa ukilinganisha na mwaka uliopita.

Ili kusimamia vyema rasilimali za umma, napendekeza kuimarishwe udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha Sheria na taratibu zilizowekwa zinafuatwa kikamilifu. Pia, kuhakikisha kuwa mifumo ya utawala inakuwepo na inafanya kazi ipasavyo.

# SURA YA KWANZA



# 1.0 UTANGULIZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na mamlaka ya kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya Ukaguzi wa hesabu hizo.

## 1.1 Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbalimbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112(3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

a) "Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

b) Au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi."

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo kwa maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za Umma.

## 1.2 Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Ukaguzi

Ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yakiwemo Mawizara na Taasisi mbalimbali za Umma kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo pamoja na michango mbalimbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi na kujiridhisha kwamba taarifa zitakazotolewa zitaonyesha sura halisi ili kutoa uhakika kwamba taarifa za mapato na matumizi zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Taarifa za hesabu zilizokaguliwa zilijumuisha hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na taarifa mbalimbali zinazohusiana na hesabu hizo.

Mabadiliko ya mifumo ya ukaguzi na uhasibu yanayotokea kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa yamepelekea kuwepo na mafanikio makubwa katika utendaji na uwajibikaji kwenye sekta za Umma katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma.

Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa fedha pamoja na utekelezaji wa sheria mbalimbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo na kuleta tija kwa wananchi na kufanikisha lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

## 1.3 Njia Zilizotumika Katika Ukaguzi

Katika kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali mbinu na njia mbali mbali za ukaguzi zilitumika ikiwemo taratibu za ukaguzi zifuatazo: -

i. Kutoa barua za awali za maandalizi ya ukaguzi (Engagement Letter) kwa Taasisi inayokaguliwa.

ii. Kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika taasisi zinazokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa wa mazingira ya taasisi hiyo ikiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani na kubaini viashiria vitakavyoathiri udhibiti wa ndani pamoja na utendaji wa taasisi.

iii. Kuandaa mikakati ya ukaguzi kuanzia mpango wa awali hadi mpango mkuu wa ukaguzi (Pre Planning, Strategic Planing and detailed Planning) itakayozingatia muelekeo na upeo wa ukaguzi ambapo utaonyesha dira na dhamira nzima ya ukaguzi huo.

iv. Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) pamoja na uongozi wa Taasisi zinazokaguliwa.

v. Kupitia na kuhakiki nyaraka mbalimbali pamoja na kupata taarifa kutoka kwa wahusika ili kupata uelewa wa kazi za Taasisi zinazokaguliwa.

vi. Kutumia njia na mbinu mbalimbali za ukaguzi kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa ukaguzi (Compliance Audit Manual & Financial Audit Manual).

vii. Kufanya kikao cha kumaliza ukaguzi (Exit Meeting) na uongozi wa Taasisi inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi ambapo katika kikao hicho wakaguzi na uongozi wa taasisi hupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.

viii. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya awali (Management letter) kwa uongozi wa taasisi inayokaguliwa itakayoainisha hoja za ukaguzi pamoja na mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kutoa majibu na vielelezo kuhusiana na ripoti hiyo kwa muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria.

ix. Kufuatilia majibu ya hoja za ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ili kuweza kujiridhisha na majibu ya hoja hizo.

x. Kutoa Ripoti Kuu ya Mwaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

## 1.4 Umuhimu wa ukaguzi katika kuimarisha Utawala Bora

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kuhakikisha kwamba fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria inatumika ipasavyo na kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuleta ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha, ukaguzi wa hesabu unalenga kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma na kupelekea kuimarika kwa dhana nzima ya Utawala Bora.

Kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuongezeka na kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuleta tija na ufanisi na kufanikisha kutekeleza malengo yaliyopangwa na Serikali kwa wakati uliopangwa. Aidha kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi na kufanikiwa kuimarika kwa hali za wananchi kwa jumla.

Katika kufanikisha malengo ya Serikali ya kuimarisha utawala bora nchini, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na mbinu mbali mbali za ukaguzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya uhasibu na ukaguzi pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

## 1.5 Kamati za Baraza la Wawakilishi

Katika kuleta ufanisi na kufikia malengo ya Serikali iliyojipangia, Baraza la Wawakilishi ni nguzo imara katika kuimarisha uwajibikaji na kusimamia rasilimali za umma kuweza kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa jamii. Aidha, Kamati za Baraza la Wawakilishi zinatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za Umma.

Kwa kuzingatia majukumu na umuhimu wa Kamati za Baraza la Wawakilishi Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ikishirikiana na Kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama yalivyoainishwa katika Bajeti zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo upeo wa mahusiano wa Taasisi za ukaguzi duniani (SAIs) na Mabunge (Baraza la Wawakilishi) unatofautiana baina ya nchi na nchi duniani ambapo kuna baadhi ya nchi taasisi za ukaguzi huwa ni sehemu ya Bunge (Legislative) na baadhi huwa chini ya utawala (Executive) na baadhi ya nchi nyengine Taaisisi za ukaguzi huwa haziko kokote yaani sio (legislative wala Executive). Kwa hivyo taasisi za ukaguzi zina jukumu la kuzijengea uwezo Kamati za Ukaguzi za Bunge (Baraza la Wawakilishi) kwa lengo la kuzisimamia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa ushauri na mapendekezo yao kwa taasisi za umma pamoja na Serikali.

# SURA YA PILI



# 2.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI

Sura hii inaelezea muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu pamoja na ufafanuzi wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 2.1 Muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilibainika uwepo wa dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo hadi ukaguzi unakamilika hazikupatiwa majibu au majibu yake hayakuridhisha hali iliyopelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi.

### 2.1.1 Dosari za kiutendaji zilizobainika katika Ukaguzi

Katika ukaguzi wa hesabu wa mwaka wa fedha 2022/2023 kulijitokeza dosari za kiutendaji ambazo zimepelekea kuathiri utendaji wa taasisi zilizokaguliwa pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

a) Mfumo wa udhibiti wa ndani.

b) Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

c) Usimamizi wa matumizi.

d) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

e) Usimamizi wa mikataba.

#### a) Mfumo wa udhibiti wa ndani

Mfumo wa udhibiti wa ndani ni taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa fedha ambazo zinahitajika kuwa imara ili kuweza kusaidia taasisi za umma kuweza kufanya kazi zake kwa weledi na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani kwa baadhi ya Taasisi na Mawizara kwa kutokuwa na Kamati za Ukaguzi wa Ndani au kutokufanyakazi kwa kamati hizo. Kutokufanyakazi kwa kamati za ukaguzi wa ndani (Audit Committee) kunaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kuchukuliwa hatua za awali pale zinapojitokeza.

Aidha, ukaguzi umebaini vitengo vya ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit) kwa baadhi ya Taasisi na Wizara zilizokaguliwa hazikuwasilisha ripoti za ukaguzi wa hesabu katika kipindi cha ukaguzi pamoja na kushindwa kukutana kwa kamati za ukaguzi wa ndani kwa lengo la kuzifanyia kazi ripoti za ukaguzi na kutoa mapendekezo kwa uongozi wa taasisi husika.

### b) Utekelezaji wa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016

Ukaguzi umebaini kutokufuatwa kikamilifu kwa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kwa baadhi ya Wizara na Taasisi jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa dosari za ukiukwaji wa taratibu na miongozo ya sheria hizo.

### c) Usimamizi wa matumizi

Ukaguzi umebaini dosari katika Usimamizi wa matumizi kwa baadhi ya taasisi za Serikali. Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa baadhi ya matumizi kwa Wizara na Taasisi za Umma jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

### d) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato

Ukaguzi umebaini dosari katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa baadhi ya taasisi za Serikali. Kutokuwepo kwa mifumo mizuri ya ukusanyaji wa mapato kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa makusanyo yaliyokusanywa na Wizara na Taasisi za umma kwa kukosekana kwa makadirio ya mapato, mapato halisi yaliyokusanywa na kuwasilishwa pamoja na kutokujulikana chanzo kilichokusanya mapato hayo.

### e) Usimamizi wa mikataba

Ukaguzi umebaini dosari katika usimamizi wa mikataba kwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali ikiwemo kukiuka vipengele muhimu vilivyoainishwa katika mikataba hali iliyopelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kuwepo kwa ukiukwaji wa vipengele hivyo kumepelekea kwa baadhi ya miradi kutokamilika na kutofikia malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, kujitokeza kwa baadhi ya Wizara na Taasisi kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia rasimu ya Mkataba jambo ambalo linaweza kupelekea kuitia hasara Serikali kwa kukosekana ushauri wa kitaalamu kuhusiana na mikataba hiyo kwa kubainika kufanya malipo bila ya kuzingatia vipengele vya malipo na kujitokeza kwa baadhi ya wazabuni kulipwa asilimia 100 ya malipo yote bila ya kukamilika kwa kazi iliyotarajiwa na hatimae kuitia hasara Serikali.

## 2.2 Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa ajili ya ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa zitayarishe na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba uwasilishaji wa taarifa za hesabu za Serikali umeimarika ambapo hesabu hizo zimewasilishwa kwa wakati kama ifuatavyo:-

## Jadweli Nambari 1: Orodha ya Wizara na Taasisi zilizowasilisha Hesabu za mwisho wa mwaka kwa Ukaguzi

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe ya Uwasilishaji | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
| 1. | A01 | Ofisi ya Rais Ikulu | 20/09/2021 | 27/09/2022 | 27/09/2023 |
| 2. | A02 | Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi | 20/09/2021 | 28/09/2022 | 26/09/2023 |
| 3. | A07 | Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji | 24/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 4. | A0702 | Kamisheni ya Kazi | -- | 30/09/2022 | **27/10/2023** |
| 5. | A08 | Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji | -- | -- | 27/09/2023 |
| 6. | B01 | Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | 20/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 7. | C01 | Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na BLW | 03/09/2021 | 29/09/2022 | 27/09/2023 |
| 8. | C02 | Baraza la Wawakilishi Zanzibar | 21/09/2021 | 27/09/2022 | 27/09/2023 |
| 9. | C03 | Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 27/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 10. | C05 | Tume ya Ukimwi Zanzibar | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 27/09/2023 |
| 11. | Ruzuku | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 13/09/2021 | 27/09/2022 | 27/09/2023 |
| 12. | -- | Hesabu Jumuishi ya Mfuko Mkuu wa Serikali | 30/11/2021 | 31/10/2022 | 12/12/2023 |
| 13. | D01 | Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ | 29/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 14. | F01 | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | 27/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 15. | F02 | Huduma za Hesabu za Mfuko Mkuu wa Serikali | 28/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 16. | F03 | Tume ya Mipango | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 26/09/2023 |
| 17. | F04 | Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 27/09/2023 |
| 18. | F05 | Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | -- | -- | 26/09/2023 |
| 19. | F06 | Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani | -- | -- | 26/09/2023 |
| 20. | G01 | Wizara Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 28/09/2021 | 27/09/2022 | 27/09/2023 |
| 21. | G02 | Mahkama Kuu Zanzibar | 30/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 22. | G03 | Afisi ya Mwanasheria Mkuu | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 23. | G04 | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 24. | Ruzuku | Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti | -- | -- | 29/09/2023 |

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe ya Uwasilishaji | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 25. | G05 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 26. | G14 | Afisi ya Mufti Mkuu | -- | -- | 29/09/2023 |
| 27. | G15 | Tume ya Maadili ya Viongozi | 29/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 28. | E07 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | 27/09/2021 | 26/09/2022 | 26/09/2023 |
| 29. | Ruzuku | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | -- | -- | 29/09/2023 |
| 30. | E08 | Tume ya Utumishi Serikalini | 22/09/2021 | 29/09/2022 | 27/09/2023 |
| 31. | Ruzuku | Skuli ya Sheria | -- | 29/09/2022 | 26/09/2023 |
| 32. | H01 | Wizara ya Afya | 24/09/2021 | 27/09/2022 | 12/09/2023 |
| 33. | H02 | Hospitali ya Mnazi Mmoja | 30/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 34. | H03 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | -- | -- | **16/10/2023** |
| 35. | J01 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 36. | J02 | Kamisheni ya Utalii | 27/09/2021 | 28/09/2022 | 26/09/2023 |
| 37. | J03 | Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo | 30/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 38. | Ruzuku | Baraza la Kiswahili | -- | 29/09/2022 | 28/09/2023 |
| 39. | Ruzuku | Afisi ya Msajili Hakimiliki | -- | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 40. | Ruzuku | Baraza la Taifa la Michezo | -- | 29/09/2022 | 28/09/2023 |
| 41. | Ruzuku | Tume ya Utangazaji | -- | -- | 28/09/2023 |
| 42. | Ruzuku | Baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na Utamaduni | -- | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 43. | Ruzuku | Baraza la Vijana Zanzibar | -- | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 44. | K01 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 30/09/2021 | 27/09/2022 | 27/09/2023 |
| 45. | Ruzuku | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar | 22/09/2021 | 16/09/2022 | 18/09/2023 |
| 46. | Ruzuku | Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu | 24/09/2021 | 26/09/2022 | 29/09/2023 |
| 47. | Ruzuku | Afisi ya Mrajis wa Elimu | 01/10/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 48. | Ruzuku | Baraza la Mitihani Zanzibar | 27/09/2021 | 27/09/2022 | 13/09/2023 |
| 49. | Ruzuku | Taasisi ya Elimu Zanzibar | 22/09/2021 | 27/09/2022 | 28/09/2023 |
| 50. | L01 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 27/10/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 51. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | 30/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe ya Uwasilishaji | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 52. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo | 27/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 53. | Ruzuku | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | -- | 29/09/2022 | 30/09/2023 |
| 54. | L02 | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 20/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 55. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Rasilimali za Baharini | -- | -- | 29/09/2023 |
| 56. | N02 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 30/09/2023 |
| 57. | N03 | Wizara ya Maji Nishati na Madini | 29/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 58. | N04 | Kamisheni ya Ardhi | 29/09/2021 | 25/10/2022 | 23/09/2023 |
| 59. | Ruzuku | Bodi ya Kondominio Zanzibar | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 27/09/2023 |
| 60. | Ruzuku | Bodi ya Uhaulishaji Ardhi Zanzibar | 28/09/2021 | 28/09/2022 | 28/09/2023 |
| 61. | Ruzuku | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi | 24/09/2021 | 28/09/2022 | 28/09/2023 |
| 62. | Ruzuku | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | -- | 13/09/2022 | 29/09/2023 |
| 63. | P01 | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 05/10/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 64. | Ruzuku | Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo | 24/09/2021 | 13/09/2022 | 29/09/2023 |
| 65. | Ruzuku | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | -- | -- | 29/09/2023 |
| 66. | R01 | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | 30/09/2021 | 29/09/2022 | 27/09/2023 |
| 67. | Ruzuku | Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 12/09/2023 |
| 68. | Ruzuku | Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni | 27/09/2021 | 05/10/2022 | 26/09/2023 |
| 69. | Ruzuku | Tume ya Ushindani Halali wa Biashara | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 27/09/2023 |
| 70. | Ruzuku | Baraza la Ushindani Halali wa Biashara | -- | -- | 22/09/2023 |
| 71. | Ruzuku | Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar | -- | 29/09/2022 | 22/09/2023 |

## 2.3 Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi hutolewa kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho inayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana kuhusiana na iwapo taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa njia zote muhimu na kwa mujibu wa mfumo unaotumika wa kuripoti taarifa za fedha, kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRS) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu Katika Taasisi za Umma (IPSAS).

Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi namba 1200. Hili linafanikiwa kwa kufanya ukaguzi kwa njia ambayo itamuwezesha mkaguzi kupata uhakika wa kuridhisha kulingana na tathmini ya matokeo dhidi ya kipimo kilichowekwa. Pia, maoni ya ukaguzi yanajumuisha mahitimisho juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Kanuni zake, na Sheria ya bajeti na Kanuni zake.

### 2.3.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo ni:-

**Hati Inayoridhisha:** Hati hii hutolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango na mfumo unaokubalika wa utoaji wa taarifa za fedha.

**Hati Yenye Shaka**: Hati hii hutolewa pale hesabu zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa baada ya kupata vielelezo vya kutosha, mkaguzi anahitimisha kuwa makosa kwenye hesabu ama likiwa moja au yakiwekwa pamoja yanaathiri, lakini hayaathiri maeneo yote katika taarifa za fedha. Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za fedha.

**Hati Mbaya**: Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuonesha kuwa taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zinamakosa; na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata Viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

**Kushindwa kutoa Maoni**: Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha ambazo ni msingi wa kutoa hati, hivyo Mkaguzi huhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenye athari kwa sehemu zote za hesabu hizo.

Mkaguzi huwa anashindwa kutoa hati katika mazingira ya nadra sana yaliyohusisha mashaka; hivyo huhitimisha kuwa, licha ya kupata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi katika maeneo yenye shaka kwenye taarifa za fedha, haitawezekana kutoa hati kuhusu taarifa za fedha kwa kuwa kuna viashiria vya mashaka vyenye madhara kwenye taarifa za fedha.

### 2.3.2 Aya yenye masuala ya Msisitizo kwenye ripoti za Mkaguzi

Kama nitaona kuna umuhimu wa kuwaarifu watumiaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, kwa mtazamo wangu suala hilo ni muhimu na lamsingi kwa ajili ya kuleta uwelewa wa taarifa hizo, nitaiweka aya hii kwenye taarifa za ukaguzi. Aya hii itawekwa pale tu ambapo nimepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa; na inapaswa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha.

### 2.3.3 Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Aya ya masuala muhimu ya ukaguzi hutoa taarifa za ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia kuelewa masuala ya kitaalamu ya ukaguzi ambayo yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi husika. Uwasilishaji wa masuala muhimu ya ukaguzi huongeza thamani na uwazi kwenye taarifa za ukaguzi.

### 2.3.4 Msingi wa Hati za Ukaguzi

Ili kufikia kwenye hati zilizotolewa, ukaguzi ulizingatia hali halisi ya matokeo ya ukaguzi kwa kila taasisi iliyokaguliwa. Ukaguzi huo ulifanyika kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi kwenye Sekta za Umma (ISSAIs). Viwango hivyo vinanitaka kuandaa mpango wa ukaguzi, kufanya ukaguzi, na kutoa ripoti ya matokeo ya ukaguzi huo. Pia, vinanitaka kufuata maadili ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi uliofanyika una ubora unaokubalika kwa hali ya juu. Ukaguzi ulijumuisha uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kiasi cha fedha kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha. Pia, ulijumuisha tathmini ya makadirio na maamuzi yaliyofanywa na uongozi wa Wizara, Idara na Taasisi wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha, utoshelezi wa mambo yaliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha, iwapo sera za uhasibu zinazotumika zinaendana na mazingira halisi ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi inayokaguliwa na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta za Umma, na kama sera hizo zinajitosheleza na zimekuwa zikitumika mwaka hadi mwaka.

Kazi za ukaguzi zilizofanyika zilipangwa na kutekelezwa kwa namna ambayo iliwezesha ukusanyaji wa taarifa zote muhimu na maelezo ya uongozi yaliyokuwa yanahitajika ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa nyaraka kwa ajili ya kutoa uhakika iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na ubadhirifu au kwa bahati mbaya.

Nilifanya ukaguzi wangu kwa uhuru na sikuwa na mgongano wa maslahi na taasisi yoyote niliyoikaguwa kwa mujibu wa kanuni za maadili zilizotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili kwa Wahasibu pamoja na Kanuni za Maadili zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) na nilitekeleza wajibu wangu wa kimaadili kwa mujibu wa matakwa hayo.

Ni imani yangu kuwa ushahidi nilioupata ulikuwa sahihi na ulijitosheleza katika kutoa hati za ukaguzi na pale ambapo nilishindwa kupata ushahidi wa kutosha sikutoa hati za ukaguzi.

### 2.3.5 Hati za Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, nilikamilisha ukaguzi wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ **66**. Kati ya Taasisi hizo jumla ya Wizara **18**, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara **48** za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutoa hati za ukaguzi kwa Taasisi **66**. Kati ya hati hizo zilizotolewa hati **63** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **95.45** ya hati zilizotolewa, na hati **3** ni hati zenye shaka sawa na asilimia **4.55** ya hati zilizotolewa na sikuwa na hati ya kushindwa kutoa maoni. Orodha ya Taasisi nilizozikaguwa pamoja na hati za ukaguzi nilizozitoa ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 2: Taasisi za Serikali zilizokaguliwa na kupata Hati za ukaguzi

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mwaka wa Fedha 2020/2021 | Mwaka wa Fedha 2021/2022 | Mwaka wa Fedha 2022/2023 |
| 1. | A01 | Ofisi ya Rais Ikulu | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 2. | A02 | Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 3. | A07 | Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 4. | A0702 | Kamisheni ya Kazi | - | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 5. | A08 | Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji | - | - | Hati Inayoridhisha |
| 6. | B01 | Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 7. | C01 | Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 8. | C02 | Baraza la Wawakilishi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 9. | C03 | Tume ya Uchaguzi Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 10. | C05 | Tume ya Ukimwi Zanzibar | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 11. | Ruzuku | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 12. | -- | Hesabu Jumuishi ya Mfuko Mkuu wa Serikali | Hati Isiyoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | **Hati Yenye Shaka** |
| 13. | D01 | Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 14. | F01 | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 15. | F02 | Huduma za Hesabu za Mfuko Mkuu wa Serikali | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 16. | F03 | Tume ya Mipango | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 17. | F04 | Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 18. | F05 | Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | -- | -- | Hati Inayoridhisha |

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mwaka wa Fedha 2020/2021** | **Mwaka wa Fedha 2021/2022** | **Mwaka wa Fedha 2022/2023** |
| 19. | F06 | Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 20. | G01 | Wizara Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 21. | G02 | Mahkama Kuu Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 22. | G03 | Afisi ya Mwanasheria Mkuu | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 23. | G04 | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 24. | Ruzuku | Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 25. | G05 | Tume ya Kurekebisha Sheria | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 26. | G14 | Afisi ya Mufti Mkuu | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 27. | G15 | Tume ya Maadili ya Viongozi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 28. | E07 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 29. | E08 | Tume ya Utumishi Serikalini | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 30. | Ruzuku | Skuli ya Sheria | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 31. | | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 32. | H01 | Wizara ya Afya | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 33. | H02 | Hospitali ya Mnazi Mmoja | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 34. | H03 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 35. | J01 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Inayoridhisha Yenye Aya ya Msisitizo** |

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mwaka wa Fedha 2020/2021 | Mwaka wa Fedha 2021/2022 | Mwaka wa Fedha 2022/2023 |
| 36. | J02 | Kamisheni ya Utalii Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 37. | J03 | Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 38. | Ruzuku | Baraza la Kiswahili | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 39. | Ruzuku | Afisi ya Msajili Hakimiliki | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 40. | Ruzuku | Baraza la Taifa la Michezo | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 41. | Ruzuku | Baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na Utamaduni | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 42. | Ruzuku | Baraza la Vijana Zanzibar | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 43. | Ruzuku | Tume ya Utangazaji Zanzibar | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 44. | K01 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 45. | Ruzuku | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 46. | Ruzuku | Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 47. | Ruzuku | Afisi ya Mrajisi wa Elimu | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 48. | Ruzuku | Baraza la Mitihani Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 49. | Ruzuku | Taasisi ya Elimu Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 50. | L01 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | Hati Isiyoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 51. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti na Mifugo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 52. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 53. | Ruzuku | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 54. | L02 | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 55. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Rasilimali za Baharini Zanzibar (ZAFIRI) | -- | -- | Hati Inayoridhisha |

| Nam. | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mwaka wa Fedha 2020/2021** | **Mwaka wa Fedha 2021/2022** | **Mwaka wa Fedha 2022/2023** |
| 56. | N02 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 57. | N03 | Wizara ya Maji Nishati na Madini | Hati Inayoridhisha | **Hati Mbaya** | Hati Inayoridhisha |
| 58. | N04 | Kamisheni ya Ardhi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 59. | P01 | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | Hati Isiyoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 60. | Ruzuku | Mfuko wa Uwezeshaji | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 61. | R01 | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 62. | Ruzuku | Taasisi ya Viwango Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 63. | Ruzuku | Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 64. | Ruzuku | Tume ya Ushindani Halali wa Biashara | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 65. | Ruzuku | Baraza la Ushindani Halali wa Biashara | -- | -- | Hati Inayoridhisha |
| 66. | Ruzuku | Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar | -- | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

## 2.4 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Kwa ujumla takwimu zimebainisha uwepo wa ongezeko la ripoti za ukaguzi kutoka ripoti 61 zilizotolewa mwaka 2021/2022 hadi ripoti 66 kwa mwaka 2022/2023 kukiwa na ongezeko la ripoti 5 za ukaguzi sawa na asilimia 8.2. Aidha, mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/2023 ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

| Mwaka wa Fedha | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hati Yenye Shaka | Hati Mbaya | Kushindwa Kutoa Maoni | |
| 2022/2023 | 63 | 3 | 0 | 0 | 66 |
| 2021/2022 | 54 | 6 | 1 | 0 | 61 |
| 2020/2021 | 62 | 0 | 11 | 0 | 73 |
| 2019/2020 | 53 | 1 | 9 | 0 | 63 |

## 2.5 Taarifa ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Hoja za Ukaguzi kwa Mwaka Uliopita

Taarifa ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Hoja za Ukaguzi kwa Mwaka Uliopita inaeleza kwa muhtasari hali ya utekelezaji wa hoja na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika kusimamia na kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Mawizara, Maidara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Tathmini niliyoifanya kwenye hali ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita nimebaini jumla ya mapendekezo 1,587 yalitolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi 66 zilizokaguliwa na kuwasilishiwa ripoti za ukaguzi. Kati ya mapendekezo hayo jumla ya mapendekezo 1,213 yaliweza kutekelezwa na kuondolewa ambayo ni sawa na asilimia 76.43, mapendekezo 93 yapo katika hatua ya utekelezaji sawa na asilimia 5.86. Hata hivyo, mapendekezo 85 bado hayajatekelezwa ambayo ni sawa na asilimia 5.36 na mapendekezo 124 yamejirudia sawa na asilimia 7.81 vile vile mapendekezo 72 yamepitwa na wakati sawa na asilimia 4.54.

Kiujumla hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi imeimarika ambapo baadhi ya Taasisi zimeonekana kupiga hatua katika kufanya marekebisho ya dosari zilizobainika ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 dosari hizo hazikuweza kujirejea na kwa baadhi ya Taasisi zimeweza kupunguza idadi ya hoja zilizobainishwa ukilinganisha na mwaka uliopita.

# SURA YA TATU



# 3.0 UKAGUZI WA HESABU JUMUISHI YA SERIKALI

Sura ya hii inatoa mrejesho wa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ikiwa ni makisio ya makusanyo na matumizi, makusanyo halisi, Fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu na matumizi yaliyofanywa na Serikali. Malengo makuu ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 ni uwezeshaji wananchi Kiuchumi kufikia zana ya uchumi wa Buluu kwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo :-

- **Huduma za Kijamii:** Sekta ya huduma ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuimarisha Uchumi wa Zanzibar. Sekta hii inajumuisha sekta ndogo za Elimu, Chakula na Vinywaji, Afya, Malazi, Sanaa, Burudani, Ubunifu na Mawasiliano.
- **Kilimo:** Kinaendelea kuwa ni sekta ya pili ya ukuzaji uchumi wetu na kumhakikishia mwananchi upatikanaji wa chakula. Sekta hii inajumuisha sekta ndogo za Misitu, Ufugaji, Uvuvi na Mazao.
- **Viwanda:** Sekta hii inajumuisha sekta ndogo ya Uzalishaji Viwandani, Ujenzi, Uchimbaji Mawe, Mchanga, Umeme na Gesi.

## 3.1 Taarifa ya Mapato kwa Mwaka 2022/2023

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imeandaa hesabu Jumuishi za Serikali iliyojumuisha taarifa za hesabu za Taasisi za Kibajeti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwemo Wizara, Idara, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### 3.1.1 Taarifa za Mapato

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia taasisi zake, mapato yaliyokadiriwa kukusanywa kwa Taasisi za kibajeti pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni jumla ya shilingi Bilioni 1,234.04. Makadirio hayo yalitarajiwa kutoka katika vianzio mbali mbali ikiwemo makusanyo ya kodi, Gawio la Serikali kutokana na faida inayopatikana katika Mashirika ya Serikali na washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2023 jumla ya shilingi Bilioni 1,188.07 zimekusanywa ambapo ni sawa na asilimia 96.28 ya makadirio.

Aidha, Serikali ilikadiria kukusanya fedha kutoka vyanzo vya nje ikiwemo misaada na mikopo yenye riba nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kiasi cha shilingi Bilioni 687.964 kati ya fedha hizo shilingi Bilioni 71.099 ni msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, shilingi Bilioni 606.864 ni mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na shilingi Bilioni 10 kutoka mfuko wa pamoja (Busket Fund). Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 fedha iliyopatikana kutoka vyanzo vya nje ni Shilingi Bilioni 239.871 ikiwa ni sawa na asilimia 34.87 ya makadirio. Kati ya fedha hizo msaada wa kibajeti ni shilingi Bilioni 67.433 sawa na asilimia 28.11 ya fedha zilizotolewa. Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni shilingi Bilioni 59.263 sawa na asilimia 24.7 ya fedha iliyotolewa. Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni shilingi Bilioni 113.174 sawa na asilimia 47.181 ya fedha iliyotolewa.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikadiria kupata mikopo yenye thamani ya shilingi Bilioni 515 kutoka kwa taasisi za fedha za ndani kupitia hati fungani na Bondi. Jumla ya mikopo iliyopatikana ni shilingi Bilioni 27 sawa na asilimia 5.24 ya makadirio kwa mwaka wa fedha husika.

## 3.2 TAARIFA YA MATUMIZI KWA MWAKA 2022/2023

### 3.2.1 Taarifa za matumizi za Taasisi za Kibajeti za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa upande wa matumizi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikadiria kutumia jumla ya shilingi Bilioni 2,589.74 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi Bilioni 1,462.67 sawa na asilimia 56.5 ya makadirio kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

## 3.3 TAARIFA YA GAWIO LA SERIKALI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikadiria kupokea jumla ya shilingi Bilioni 32 ikiwa ni gawio kutoka katika Mashirika mbalimbali yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 gawio halisi lililopatikana ni shilingi Bilioni 18.2 ambapo ni sawa na asilimia 56.9 ya makadirio na kupelekea kujitokeza kwa upungufu wa gawio la shilingi Bilioni 13.8 sawa na asilimia 43.1 ya upungufu.

## 3.4 TAARIFA YA DENI LA SERIKALI

### 3.4.1 Mwenendo wa Deni la Ndani

Deni la ndani linajumuisha mikopo ya muda mrefu (hati fungani) na mikopo ya muda mfupi (dhamana za Serikali). Kwa mwaka 2022/23 deni la ndani limeongezeka kwa Shilingi 20,102,866,415.77 sawa na asilimia 6.3 kutoka shilingi 321,345,265,420 ya deni la ndani lililoripotiwa mwaka 2021/2022. Mwenendo ya ukuaji wa deni la ndani na ukopaji imeoneshwa kwenye jedwali hapo chini.

**Jadweli Nambari 4: Mwenendo wa deni la ndani kwa miaka mitatu (deni halisi)**

| Mwaka wa fedha | Thamani ya deni (Tsh.) | Ongezeko (Tsh.) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 2022/2023 | 341,448,131,843.77 | 20,102,866,423.77 | 6.3 |
| 2021/2022 | 321,345,265,420.00 | 127,246,350,970.00 | 66 |
| 2020/2021 | 194,098,914,450.00 | 37,297,310,610.00 | 24 |

*Chanzo: Jedwali la mwenendo wa deni la serikali kwa miaka 2020/2021, 2021/22 na 2022/2023*

Vilevile, ukaguzi ulibaini Serikali ilikopa jumla ya fedha zenye thamani ya shilingi 61,925,731,843.77 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, kati ya hizo, shilingi 34,925,731,843.77 sawa na asilimia 56 zilikuwa ni mkopo wa muda mrefu kutoka PBZ na shilingi 27,000,000,000 sawa na asilimia 44 zilikuwa ni mkopo wa muda mfupi kutoka ZSSF. Mikopo ya muda mfupi hutumika kulipia Dhamana za Serikali zilizoiva na mikopo ya muda mrefu hutumika kugharamia miradi ya Maendeleo.

### 3.4.2 Deni la Nje

Deni la nje la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/2023 limebainika kufikia jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 1,023.9 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi Zanzibar, ukijumuisha na Deni la nje linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la Dola za Kimarekani Milioni 5.7 na kupelekea Deni la nje la jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 1,029.6.

### 3.4.3 Mambo yaliyobainika Katika Ukaguzi wa Hesabu Jumuishi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi ulipokea taarifa za Hesabu Jumuishi (Consolidated Financial Statement) ya Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo imejumuisha hesabu za Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa. Hata hivyo hesabu jumuishi za Serikali haikuweza kubainisha Taarifa za Mashirika ya Umma, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea zinazotumia mfumo wa hesabu usio taslimu.

#### 3.4.3.1 Kutojumuishwa kwa taarifa za mapato na matumizi ya Mashirika na Mamlaka za Serikali zinazotumia mfumo usio wa pesa Taslim katika Hesabu Jumuishi za Serikali

Katika kupitia hesabu Jumuishi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nilibaini kutojumuishwa kwa taarifa za mapato, matumizi na taarifa za Bajeti za Mashirika na Mamlaka zinazotumia kanuni za uhasibu za "Accrual Basis" katika uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka katika hesabu Jumuishi. Taarifa hizi ni muhimu na zina uzito mkubwa katika kuhakikisha Hesabu jumuishi za Serikali zipo sahihi na zinaonesha ukweli katika uandaaji wake kwa mujibu wa miongozo ya uandaaji wa Hesabu Jumuishi Pamoja na viwango vya kitaifa na kimataifa vya uandaaji wa hesabu hizo.

Natambua jitihada za Serikali kupitia Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika kutoa mafunzo na miongozo mbalimbali ya ufungaji wa hesabu katika ngazi ya Taasisi zinazofunga hesabu na hesabu jumuishi kwa ujumla.

Suala hili nililiripoti kwenye taarifa ya Ukaguzi ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022 hata hivyo bado hesabu za Mashirika na mamlaka zinazotumia kanuni za uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa njia isiyo ya Taslim hazijajumuishwa katika hesabu jumuishi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Napendekeza kwa Serikali kupitia Idara ya Mhasiibu Mkuu wa Serikali kuandaa miongozo itakayolazimu Hesabu zote za Mashirika na Mamlaka zinazofunga hesabu za mwisho wa mwaka kufuata miongozo hiyo ili hesabu jumuishi ziweze kuonesha uhalisia.

#### 3.4.3.2 Kuchelewa kurasimishwa kwa matumizi ya Kanuni za Uhasibu za Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS Acrual Basis of Account) katika kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa muda mrefu bado inaendelea kutumia kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma kwa njia ya taslimu utaratibu ambao hautoi picha halisi ya taarifa muhimu za hesabu za Taasisi za Umma ikiwemo Mali, madeni, mitaji n.k. Utaratibu huu umepitwa na wakati na unakwaza katika kuandaa hesabu jumuishi za Serikali kutokana na baadhi ya Taasisi za Umma kutumia kanuni za uandaaji wa hesabu kwa misingi ya Accrual ikiwemo Mashirika na baadhi ya Mamlaka za Serikali.

#### 3.4.3.3 Makosa katika uwasilishaji wa taarifa za malipo ya posho za Majimbo katika Fungu la Mshahara shilingi 85,444,000

Mapitio yetu ya taarifa jumuishi za mishahara ya Serikali yalibaini kwamba Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imeripoti matumizi ya Maposho za Majimbo zenye asili ya matumizi mengineyo (Other Charges) katika fungu la matumizi ya mishahara (Personnel Emolments). Posho za Majimbo zilizochanganywa na matumizi ya mishahara ni shilingi 85,444,000.

Uwasilishaji huu unapelekea taarifa za matumizi kutokuonyesha uhalisia wa mishahara kwa kipindi husika hali inayoweza kusababisha athari mbali mbali katika mipango kwenye ngazi ya Taasisi na Serikali kwa ujumla.

Nashauri uongozi wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuzifanyia kazi dosari zilizojitokeza na kufanya maboresho.

#### 3.4.3.4 Tofauti iliyobainika katika uwasilishaji wa taarifa za malipo ya Mishahara kwa Taasisi za kibajeti za Serikali

Ukaguzi ulifanya ulinganifu wa Mishahara iliyoripotiwa katika Hesabu za mwisho wa mwaka na Mishahara iliyolipwa kupitia mfumo wa Malipo ya mishahara Serikalini kwa Taasisi 56 za kibajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini kwamba mishahara iliyoripotiwa ni pungufu kwa shilingi 92,288,743,609.90 sawa na asilimia 14.94 ya mishahara iliyoripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Mchanganuo wa utofauti wa mishahara iliyoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa mwaka ukilinganisha na Mishahara iliyolipwa kwa kipindi husika ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 5: Tofauti ya mishahara iliyoripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka na mfumo wa mishahara**

| Maelezo | Hesabu za Mwisho wa Mwaka (2022/2023) | Payroll Run (2022/2023) | Tofauti |
|---|---|---|---|
| Mishahara (Civil Servants/ Basic Salary) | 447,150,728,300.10 | 507,439,471,910.00 | 60,288,743,609.90 |
| Malimbikizo (Arrears) | - | 5,456,932,719.32 | - |
| Marekebisho ya Mshahara (Salary Adjustment) | 303,955,952.00 | - | - |
| Posho maalum (Special Allowances ) | 61,509,656,958.22 | 63,369,464,916.00 | 1,859,807,957.78 |
| Mchango wa ZSSF 13% | 26,098,386,342.77 | 56,306,501,076.00 | 30,208,114,733.23 |
| Ruzuku ya Mshahara (SS) | 82,943,347,122.00 | - | - |
| **Jumla** | **618,006,074,675.09** | **632,572,370,621.32** | **92,356,666,300.91** |

### 3.4.3.5 Tofauti iliyobainika kati ya mfumo wa Mishahara na "Exchequer" za Mishahara zilizotolewa kupitia Mfumo wa IFMIS

Mapitio ya taarifa za Mishahara katika hesabu jumuishi yamebaini kwamba mishahara iliyolipwa kupitia mfumo wa mishahara Serikalini ni pungufu kwa jumla ya shilingi 4,362,163,443.32 ukilinganisha na "Exchequer" za mishahara zilizotolewa kupitia mfumo wa IFMIS kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 6: Tofauti baina ya "Exchequers" na Mfumo wa Mishahara

| Description | Exchequers 2022/2023 | Payroll Run 2022/2023 | Variance (Payroll-Exch) |
|---|---|---|---|
| CFS | 2,360,698,148.00 | 632,572,370,621.32 | 4,362,163,443.32 |
| PE PEMBA | 97,353,215,170.00 | | |
| PE UNGUJA | 430,672,842,608.00 | | |
| SS1 UNGUJA | 92,745,340,702.00 | | |
| SS2 PEMBA | 5,078,110,550.00 | | |
| **Jumla** | **628,210,207,178.00** | **632,572,370,621.32** | **4,362,163,443.32** |

### 3.4.3.6 Tofauti ya fedha iliyobainika katika hesabu Jumuishi na Hesabu binafsi za Taasisi za Serikali

Mapitio ya taarifa za fedha katika hesabu jumuishi za mwaka wa fedha 2022/2023 yamebaini uwepo wa tofauti mbalimbali zilizobainika katika hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupelekea hesabu Jumuishi kutokuonesha uhalisia wa Taarifa zilizowasilishwa, ambapo baadhi ya maeneo yaliyobainika kuwa na tofauti hiyo ni pamoja na salio anzia, kifungu cha matumizi ya kazi mbali mbali pamoja na kifungu cha masuala ya kijamii.

Kwa kuzingatia tofauti zilizobainika ambazo zimekosa ufafanuzi, hivyo ukaguzi haukuweza kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa za fedha zilizoripotiwa katika hesabu jumuishi za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango uhakikishe kuwa taarifa za fedha zinazotolewa kwa wakaguzi kwa ajili ya ukaguzi zimepitiwa na zimesahihishwa na kukubaliana na mizani iliyojumuishwa katika taarifa za kifedha. Mchanganuo wa tofauti zilizobainika ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 7: Tofauti iliyobainika katika hesabu Jumuishi

| Jina la Taasisi | Aina ya Kifungu | Hesabu ya Taasisi | Ufafanuzi wa Fedha | Hesabu Jumuishi | Tofauti |
|---|---|---|---|---|---|
| Wizara ya Fedha na Mipango | Bakaa ya fedha ya mwanzo wa mwaka | - | 109,505,254,382.89 | 303,039,246,134.80 | 193,533,991,751.91 |

### 3.4.3.7 Kukosekana kwa mfumo mzuri wa uwekaji wa taarifa za mali za Kudumu

Kifungu nambari 29 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kimeelezea moja kati ya majukumu ya Afisa Mhasibu kuhusiana na usimamizi wa mali na madeni katika kutimiza majukumu ya usimamizi wa ni mali, kutunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa Taasisi za umma. Ukaguzi umebaini uwepo wa changamoto kubwa katika usimamizi wa mali za Umma ikiwemo kukosekana kwa daftari la kutunzia mali za kudumu (Fixed Asset Register) kwa baadhi ya taasisi za Serikali ikiwemo Mawizara, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zinazojitegemea. Aidha, mapitio ya hesabu za Taasisi zinazotumia mfumo wa hesabu usio taslim imebainika kwamba mfumo wa uwekaji wa taarifa za mali za kudumu unatofautiana baina ya Taasisi moja na nyengine hali inayopelekea kukwaza utaratibu wa kuandaa hesabu jumuishi za Mawizara, Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zinazojitegemea.

Kukosekana kwa mfumo unaofanana wa uwekaji wa taarifa na kumbukumbu za mali za kudumu unakwaza utaratibu mzima wa uandaaji wa hesabu Jumuishi za Mawizara, Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zinazojitegemea.

Nashauri Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Msajili wa Hazina kuzifanyia kazi changamoto za kukosekana kwa mfumo mzuri wa uwekaji wa taarifa na kumbukumbu za mali za kudumu.

### 3.4.3.8 Kukosekana kwa mfumo maalum wa uandaaji na ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali

Wakati wa ukaguzi wa hesabu jumuishi nilibaini kuwepo kwa utaratibu wa uandaaji wa hesabu bila ya kuwa na mfumo maalum wa uunganishaji na uandaaji wa hesabu jumuishi. Pamoja na kuwa Wizara zote za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatumia mfumo wa IFMIS katika uwekaji wa taarifa za fedha, bado kuna taasisi ambazo hazitumii mfumo wa IFMIS na taarifa zake zinajumuishwa katika hesabu Jumuishi za Serikali.

Kuandaa hesabu bila ya kutumia mfumo kunasababisha makosa mengi ya kibinadamu na kupelekea taarifa za hesabu kutoonesha sura halisi na sahihi na kupelekea marekebisho ya hesabu kuchukua muda mrefu.

Pamoja na uwepo wa changamoto katika uandaaji wa Hesabu jumuishi, nashauri kwa Serikali kuanzisha mfumo wa uandaaji wa hesabu jumuishi ambao utapunguza kwa kiwango kikubwa makosa ya kibinadamu pamoja na muda unaotumika katika kuandaa hesabu jumuishi.

# SURA YA NNE


Control Environment
Control Activities
Information & Communication
Monitoring
Risk Assessment
INTERNAL CONTROL

# 4.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI

Sura hii inaelezea tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani inayoendeshwa ndani ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Vile vile inaelezea mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, pamoja na masuala ya utawala bora, Kamati za Ukaguzi na Kazi za Ukaguzi wa Ndani.

## 4.1 Matokeo ya Tathmini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Ripoti hii inaeleza matokeo ya tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na mapendekezo pamoja na njia ambazo zinaweza kutumika katika kudhibiti na kusimamia ambapo mfumo huo unaweza kuboreshwa ili kuongeza ufanisi kwa lengo la kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

Ukaguzi wa udhibiti wa ndani ulikuwa na malengo ya kutambua mapungufu yatokanayo na utekelezaji wa matakwa ya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inayoelekeza uwepo wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani, Kamati za Ukaguzi pamoja na ufanyaji kazi wa Vitengo hivyo. Mambo yaliyojitokeza katika taarifa hii ni yale tu yanayotokana na ukaguzi, na ambayo tunaamini kuwa yanatakiwa kuletwa mbele ya umma. Hatuwezi kuwajibika na kuripoti vitu vyote vya vihatarishi vinavyohusiana na udhaifu wa udhibiti wa ndani.

Maafisa Masuuli pamoja na viongozi wa Serikali wanawajibika kwa masuala ya usimamizi na uendeshaji ambapo watalazimika kubainisha viashiria vya upotevu wa fedha za umma pamoja na kuvichukulia hatua za kiutendaji ili visiweze kujitokeza kwa mara nyengine, hata hivyo watakuwa na jukumu la kuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma katika Taasisi zao.

### 4.1.1 Dosari za ujumla zilizobainika kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kujitokeza kwa dosari mbali mbali zinazotokana na makosa ya kiutendaji pamoja na ukiukwaji wa Sheria kwa baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kukapelekea kuharibu mtazamo wa hati za ukaguzi na hatimae Wizara au Taasisi kuweza kupata hati yenye shaka.

Baadhi ya dosari za ujumla zilizobainika kutoka katika hesabu za Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kama inavyobainishwa hapo chini:-

#### 4.1.1.1 Mapungufu katika Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Mifumo ya udhibiti wa ndani ni namna ambavyo rasilimali za umma zinavyopangiliwa, zinavyosimamiwa na kupimwa. Udhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma zinazoshikika na zisizoshikika.

Katika Taasisi yoyote lengo la mfumo wa udhibiti wa ndani ni kuhakikisha shughuli za Wizara au Taasisi husika zinafanywa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria na kanuni.

Ukaguzi umebaini baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za SMZ hazina usimamizi mzuri wa udhibiti wa ndani kwa kutokuanzisha vitengo au kwa kutokufanya kazi kwa vitengo hivyo kwa mujibu wa utaratibu, au kujitokeza dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo zinakwaza kamati hizo kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria jambo ambalo linapelekea kamati za ukaguzi (Audit Committee) pamoja na kitengo cha ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit) kutokupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na kushindwa kutoa maoni ya marekebisho ya dosari na kasoro mbali mbali zilizobainishwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ukaguzi unawashauri viongozi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wanaweka udhibiti mzuri wa ndani ikiwemo kuvijengea uwezo vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na Kamati za ukaguzi kwa kuvipatia mafunzo ya muda mfupi juu ya namna bora ya kutekeleza kazi zao. Wizara na Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni kama zifuatazo:-

### Jadweli Nambari 8: Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani

| Namba | Jina la Taasisi | Dosari zilizobainika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Ukaguzi | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Kitengo cha Manunuzi/Bodi ya Zabuni |
| 1. | Afisi ya Baraza la Mapinduzi | Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi | -- | Kukosekana kwa Bodi ya Zabuni |
| 2. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Kutokutekeleza majukumu kwa mujibu wa kanuni nambari 149(2)(n) na 151(2)(a)(b) za kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021. | -- Kutokutekeleza majukumu kwa mujibu wa kanuni nambari 145(2)(4) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 na<br>-- kifungu nambari 117(6) cha sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. | |
| 3. | Tume ya Mipango | Kutokutekeleza majukumu kwa mujibu wa kanuni nambari 149(2)(b)(m)(n),150(5) na 151(2)(a)(b) za kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021. | -- | |
| 4. | Afisi ya Mufti Mkuu Pemba | -- | Kukosekana kwa kitengo cha ukaguzi wa Ndani | -- |
| 5. | Tume ya Mipango Pemba | -- | Kukosekana kwa kitengo cha ukaguzi wa Ndani | -- |
| 6. | Kamisheni ya Utalii Pemba | -- | Kukosekana kwa kitengo cha ukaguzi wa Ndani | -- |

| Namba | Jina la Taasisi | Dosari zilizobainika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Ukaguzi | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Kitengo cha Manunuzi/Bodi ya Zabuni |
| 7. | Tume ya UKIMWI | -- | -- | Kukosekana kwa Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi. |
| 8. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | -- | -- | Kukosekana kwa Mpango wa Uondoshaji wa Mali za Umma |
| 9. | Taasisi ya Utafiti Mifugo Zanzibar | Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi | -- | -- |
| 10. | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar | Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi | -- | -- |

#### 4.1.1.2 Dosari katika Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu (Fixed Assets Register)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(1)(a) (2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma atahusika na kusimamia mali za Taasisi ya Umma na katika kutimiza majumu yanayohusina na usimamizi wa mali, Afisa Mhasibu atatunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa Taasisi ya Umma".

Aidha, kifungu cha 58(c) cha Sheria namabari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Afisa Masuuli wa taasisi ya Umma atakuwa na jukumu la kuhifadhi na kuimarisha kila muda daftari la mali za umma kwa kujumuisha mali mpya za umma zinazopatikana na kuondosha vifaa vilivyoondolewa"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazina daftari la kuhifadhia mali za kudumu, au kutokufanyiwa maboresho kwa daftari hilo kwa kuwekwa mali mpya na kuondolewa zilizochakaa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokujua umiliki wake na hatimaye kupelekea kupotea kwa mali hizo.

Kukosekana daftari la kuhifadhia mali za kudumu au kutokufanyiwa maboresho kunaweza kupelekea mali zilizonunuliwa, zilizochakaa, zilizouzwa pamoja na zilizohamishwa kutokutambuliwa na kusababisha upotevu wa mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha unatekeleza matakwa ya Sheria nilizozinakili hapo juu ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya upotevu wa mali za umma bila ya kuzibaini. Mchanganuo wa taasisi zilizobainika na dosari hizo ni kama zifuatazo:-

### Jadweli Nambari 9: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu

| Namba | Jina la Taasisi | Hali ya Daftari Iliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Afisi ya Mufti Mkuu Pemba | Haina |
| 2. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba | Halijafanyiwa maboresho |
| 3. | Tume ya Mipango Pemba | Haina |
| 4. | Idara ya Hazina Ndogo Pemba | Haina |
| 5. | Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba | Haina |
| 6. | Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Pemba | Haina |
| 7. | Tume ya UKIMWI Pemba | Haina |
| 8. | Baraza la Wawakilishi Pemba | Halijafanyiwa maboresho |
| 9. | Tume ya Uchaguzi Pemba | Halijafanyiwa maboresho |
| 10. | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba | Haina |
| 11. | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba | Haina |
| 12. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Haina |
| 13. | Tume ya Mipango Zanzibar | Haina |
| 14. | Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Haina |
| 15. | Afisi ya Hakimiliki Zanzibar | Haina |
| 16. | Tume ya Kurekebisha Sheria | Haina |
| 17. | Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi | Haina |
| 18. | Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar | Haina |
| 19. | Baraza la Sanaa Sensa na Filamu | Halina |
| 20. | Skuli ya Sheria Zanzibar | Haina |
| 21. | Baraza la Kiswahili (BAKIZA) | Halina |
| 22. | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar | Haina |
| 22. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | Haina |
| 23. | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar | Halijafanyiwa maboresho |
| 24. | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar | Haina |
| 25. | | |

#### 4.1.1.3 Kutokuwepo kwa Daftari la makadirio ya Vifungu vya Matumizi (Vote Book)

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hufanya matumizi mbali mbali bila kuwepo kwa daftari la makadirio ya vifungu vya matumizi (vote book).

Kutokuwepo kwa daftari la vifungu vya matumizi kunapelekea kushindwa kufanya tathmini ya uingizwaji wa fedha za matumizi kwa kila kifungu pamoja na matumizi ya kifungu hicho jambo ambalo ni kwenda kinyume na toleo lenye kumbu kumbu namba AD.5/184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 linalowataka wahasibu kufunga hesabu zao kwa mujibu wa daftari la makadirio ya vifungu vya matumizi.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanasimamia watendaji wao kikamilifu kutekeleza maagizo ya muongozo huo kwa lengo la kuhakikisha wanafuata taratibu na misingi ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa ili kuepusha ukiukwaji wa Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya 2016.

Dosari hii imebainika kwa taasisi mbali mbali kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 10: Taasisi zilizokuwa hazikufuata muongozo wa ufungaji wa hesabu**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba |
| 2. | Tume ya Uchaguzi Pemba |
| 3. | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba |
| 4. | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba |
| 5. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba |
| 6. | Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar |
| 7. | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar |

#### 4.1.1.4 Mapungufu yaliyobainika katika buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)

Kanuni nambari 124(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vinavyotumika katika Taasisi yake vinakuwa na buku linaloonyesha matumizi ya chombo kwa safari husika".

Ukaguzi umebaini kuwa vyombo vya moto vya Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar havijawekewa buku au kutokujazwa ipaswavyo kwa buku linaloonyesha mienendo ya safari ya vyombo hivyo hali inayopelekea kushindwa kujiridhisha juu ya matumizi ya mafuta yanayonunuliwa na kutumika jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa ugumu wa kujua muda sahihi wa kuweza kufanyiwa matengenezo ya chombo husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya Utumishi wa umma ya 2014 iliyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wanaanzisha daftari maalum la kurikodia mwenendo wa gari ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kutokana na kuchelewa kufanyiwa matengenezo ya gari kwa kukosekana kwa taarifa ya mwenendo wa matumizi ya gari.

Dosari hii ilibainika kwa Wizara na Taasisi za Umma ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 11: Taasisi zilizokosa buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)**

| Namba | Jina la Taasisi | Hali halisi ya Buku |
|---|---|---|
| 1. | Afisi ya Rais Ikulu | Halina |
| 2. | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar | Halijazwi ipaswavyo |
| 3. | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma | Haina |

#### 4.1.1.5 Kutokukatiwa Bima kwa Vyombo vya Usafiri

Kwa mujibu wa kanuni 124(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, Mkuu wa Taasisi anatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri vya Serikali vilivyo chini ya mamlaka yake vinapasishwa na kukatiwa bima.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Taasisi zinamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari, piki piki na vespa ambapo baadhi ya vyombo hivyo vinatumika bila ya kukatiwa bima. Hali hii imetokana na Taasisi hizo kutoweka kipaombele cha ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya usafiri kunaweza kuisababishia Serikali kupata hasara ya utumiaji wa fedha kwa matengenezo pindipo vyombo hivyo vikipata ajali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba inaweka kipaombele cha ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri ili kunusuru kujitokeza kwa gharama zisizokuwa za lazima pale chombo kinapopata ajali. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 12: Vyombo vya Usafiri ambavyo Havijakatiwa Bima

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| **Ofisi ya Rais Ikulu** | | | | |
| 1. | Gari | Maecedes Benz | SMZ 1084 A | Ofisi ya Rais Ikulu |
| 2. | | Toyota Kluger | SMZ 914 A | |
| 3. | | Toyota Rav4 | SMZ 1153 A | |
| 4. | | | SMZ 1123 A | |
| 5. | | | SMZ 1154 A | |
| 6. | | | SMZ 1152 A | |
| 7. | | Hilux | SMZ 1124 A | |
| 8. | | | SMZ 731 A | |
| 9. | | Land Cruiser | SMZ 104 A | |
| 10. | | | SMZ 106 A | |
| **Afisi ya Baraza la Mapinduzi** | | | | |
| 11. | Gari | Toyota PRADO Station Wagon | SMZ 831A | Afisi ya Baraza la Mapinduzi |
| 12. | | | SMZ 1113A | |
| 13. | | | SMZ 465A | |
| 14. | | Toyota R4 Station Wagon | SMZ 267A | |
| **Mahkama Kuu Pemba** | | | | |
| 15. | Gari | Prado Land-Cruiser Tx New | SMZ 560A | Mahkama Kuu |
| 16. | | Prado Land-Cruiser Txl New | SMZ 259A | |
| 17. | | Prado Land- Cruiser | SMZ 1094 | |
| 18. | | Alphard | SMZ 386A | |
| 19. | | Hyundai | SMZ 314A | |
| 20. | | Toyota Surf | SMZ 224A | |
| 21. | Vespa | Bajaj | SMZ 1917C | Mahkama ya Kengeja |
| **Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba** | | | | |
| 22. | Gari | Suzuki | SMZ 820A | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba |
| 23. | | Prado Land Cruiser | SMZ 824 A | Afisi ya Mrajis wa NGO's Pemba |
| 24. | | | SMZ 768 A | Afisi Kuu Pemba |
| 25. | Vespa | Star | SMZ 725C | |
| 26. | | | SMZ 549C | |
| 27. | | | SMZ 1450C | |
| 28. | Pikipiki | Honda XL | SMZ 403C | |

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| **Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba** | | | | |
| 29. | Gari | TOYOTA | DFP 6702 | Idara ya maendeleo ya mifugo |
| 30. | | NISSAN | STL 2182 | Idara ya uendeshaji na utumishi |
| 31. | | MISTUBISH | SMZ 357 A | Idara ya misitu |
| 32. | | NISSAN | SMZ 388B | |
| 33. | | TOYOTA D4D | DFP 8264 | |
| 34. | | VOLKS WAGEN | SMZ 343B | Idara ya kilimo |
| 35. | | ISUZU | SMZ 137 B | Wakala wa matrekta |
| 36. | Pikipiki | XL honda | SMZ 1179C | Idara ya mifugo |
| 37. | | | SMZ 1187C | |
| 38. | | TRAIL110 | SMZ 626C | |
| 39. | | TUKTUK | SMZ 369C | |
| 40. | | TUKTUK | SMZ 464C | |
| 41. | | XL honda | SMZ 1182C | |
| 42. | | TONDA 150 | SMZ 855C | |
| 43. | | AG 200 | SMZ 852C | |
| 44. | | TUKTUK | SMZ 845C | |
| 45. | | TVS BAJAJ | SMZ 1631C | |
| 46. | | AG 200 | SMZ 831C | |
| 47. | | TRAIL110 | SMZ 626C | |
| 48. | | AG 200 | SMZ 272C | |
| 49. | | XL honda | STL 5329 | |
| 50. | | TVS 125 | SMZ 1608C | |
| 51. | | LONCIN | SMZ 783C | Idara ya Umwagiliaji maji |
| 52. | | LONCIN | SMZ 784C | |
| 53. | | HONDA XL 125 | SMZ 1079 C | |
| 54. | | PASOLA | SMZ 1637 C | |
| 55. | | TVS | SMZ 1633C | |
| 56. | | TVS | SMZ 1629 C | |
| 57. | | XL 125C | SMZ 1077C | |
| 58. | | YAMAHA AG200 | SMZ 1161 C | |
| 59. | | LONCIN 125 | SMZ 784C | |
| 60. | | VESPA STAR | SMZ 1004C | |
| 61. | | AG200 | SMZ 6986/ 858C | |

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| 62. | Pikipiki | HONDA WATCO | SMZ 832C | Idara ya Mipango |
| 63. | | HONDA WATCO | SMZ 999 C | |
| 64. | | VESPA | 533 C | Idara ya Uendeshaji na Utumishi |
| 65. | | VESPA | SMZ 201C | |
| 66. | | BOXA | DFPE 7209 | |
| 67. | | HONDA ACP125 | DFPA 0008 | Idara ya Utafiti |
| 68. | | HONDA EXEL | SMZ 1078C | |
| 69. | | BOXSO | SMZ 1766 C | |
| 70. | | HONDA XL 125 | SMZ 1380C | |
| 71. | | VESPA 125 STAA | SMZ 1462 | Idara ya Misitu |
| 72. | | MC | MC 375 CHR | |
| 73. | | MC | MC 377 CHR | |
| 74. | | MCH | MC 376 CHR | |
| 75. | | TVS | SMZ 2019C | |
| 76. | | | SMZ 1021C | Idara ya Kilimo |
| 77. | | | SMZ 1003C | |
| 78. | | | SMZ 837C | |
| 79. | | | SMZ 793C | |
| 80. | | | SMZ 1023C | |
| 81. | | | SMZ 1026C | |
| 82. | | | SMZ 1025C | |
| 83. | | YAMAHA AG200 | SMZ 952C | |
| 84. | | | SMZ 6985 | |
| 85. | | | SMZ 6979 | |
| 86. | | | SMZ 6986/858C | |
| 87. | | Stra HL TVS | SMZ 795C | |
| 88. | | Honda ACP125 | DFP 9797 | |
| 89. | | TVS | SMZ 1474 | |
| 90. | | TVS | SMZ 1607C | |

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| 91. | Pikipiki | TVS | SMZ 1606C | Idara ya Kilimo |
| 92. | | TVS | SMZ 1630 C | |
| 93. | | TVS | SMZ 1635 C | |
| 94. | | YAMAHA | STL 7910 | |
| 95. | | TVS 125 | SMZ 1833C | |
| 96. | | YAMAHA AG200 | STL 5331 | |
| 97. | | TVS | SMZ 1881C | Utafiti wa Mifugo (ZALIRI) |
| 98. | | TVS | SMZ 1739C | |
| **Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba** | | | | |
| 99. | Gari | Gari | SMZ 509B | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba |
| 100. | Pikipiki | Vespa | SMZ 1258C | |
| 101. | | Boxer | SMZ 1914C | |
| 102. | Gari | Gari | SMZ 910A | Mahkama ya Ardhi Pemba |
| 103. | Pikipiki | Vespa | SMZ 1259C | |
| 104. | | Boxer | SMZ 1819C | |
| **Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar** | | | | |
| 105. | Gari | Pajero | STL 905 | Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar |
| 106. | | | STL 904 | |
| 107. | | Nissan | SMZ 471A | |
| 108. | | | DFPA 2351 | |
| 109. | | Land Cruiser | DFP 7940 | |
| 110. | | | SMZ 472 A | |
| **Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar** | | | | |
| 111. | Vespa | Vespa | SMZ 1387C | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar |
| 112. | | | SMZ 1455C | |
| 113. | | | SMZ 1347C | |
| 114. | | | SMZ 1456C | |
| 115. | Pikipiki | Honda | SMZ2112C | |
| **Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar** | | | | |
| 116. | Gari | Toyota | SMZ 407 B | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar |
| 117. | | Suzuki | SMZ 461 A | |
| 118. | | Toyota Prado | SMZ 244 A | |
| 119. | | Toyota | SMZ 688 B | |
| 120. | | Toyota | SMZ 499 B | |
| 121. | Pikipiki | Vespa | SMZ 1431 C | |
| 122. | | Vespa | SMZ 1315 C | |

#### 4.1.1.6 Kutokutenganishwa kwa Ofisi ya Masjala ya Siri na Bayana

Kanuni ya 52(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa "Kila taasisi ya umma itakuwa na masjala ya siri na bayana ambazo zitahifadhi kumbukumbu zote za Taasisi husika kwa utaratibu ufuatao:-

i. Masjala ya siri itahusika na uhifadhi wa nyaraka zote za siri zinazoingia na kutoka ndani ya taasisi.

ii. Masjala ya bayana itahusika na uhifadhi wa nyaraka zote za wazi zinazoingia na kutoka ndani ya taasisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya Taasisi hazina masjala ya siri na bayana kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu zinazoingia na kutoka katika taasisi. Hali hii inaweka uwezekano wa kuchanganyika kwa majalada ya masjala ya siri na bayana hivyo kusababisha uwezekano wa kuvuja kwa taarifa za siri za Serikali.

Kutokutenganishwa ofisi za masjala ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kutenganisha ofisi za masjala ya siri na bayana ili kudhibiti uchanganyikaji wa majalada kunakoweza kupelekea uvujaji wa siri za Serikali. Mchanganuo wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 13: Taasisi ambazo hazikutenganisha masjala ya siri na masjala bayana**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Tume ya Mipango Pemba |
| 2. | Afisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba |
| 3. | Idara ya Hazina Ndogo Pemba |
| 4. | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba |
| 5. | Wizara ya Maji Nishati na Madini Pemba |
| 6. | Kamisheni ya Utalii Pemba |
| 7. | Kamati ya Udhibiti wa Ujenzi Idara ya Mipango Miji na Vijiji |

#### 4.1.1.7 Kutokuwepo kwa Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa Matengenezo wa Mali za Taasisi za Umma

Kwa mujibu wa kifungu 59(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakua na kitengo cha usimamizi wa mali katika kila taasisi ya Umma".

Aidha, kwa mujibu wa kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na mpango wa matengenezo wa mali ambao unaoonesha utaratibu mzima wa kuzifanyia matengenezo mali/vifaa vinavyomilikiwa na kutumika kwa shughuli za Taasisi jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mali na hatimae kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo au kuwepo kwa upotevu wa mali za Taasisi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na uandaaji wa mpango wa matengenezo wa mali hizo ili kuepusha uwezekano wa kutokea kwa uharibifu wa mali za Taasisi. Mchanganuo wa Taasisi zenye dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 14: Taasisi zisizokuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali zinazomilikiwa na Afisi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wizara ya Afya Pemba |
| 2. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba |
| 3. | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba |
| 4. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba |
| 5. | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba |
| 6. | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba |
| 7. | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba |
| 8. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 9. | Tume ya Mipango Zanzibar |
| 10. | Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |
| 11. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar |
| 12. | Tume ya UKIMWI Zanzibar |
| 13. | Wizara ya Afya Zanzibar |
| 14. | Hospitali ya Mnazi Mmoja |
| 15. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| 16. | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo |
| 17. | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar |
| 18. | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu |
| 19. | Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar |
| 20. | Afisi ya Mwanasheria Mkuu |
| 21. | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma |
| 22. | Chuo cha Utawala wa Umma |
| 23. | Skuli ya Sheria |
| 24. | Wizara ya Nchi (AR) Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| 25. | Tume ya Uchaguzi Zanzibar |
| 26. | Tume ya Utumishi Serikalini |
| 27. | Tume ya Kurekebisha Sheria |
| 28. | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu (BASSFU) |
| 29. | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar |
| 30. | Baraza la Wawakilishi |
| 31. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 32. | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa |
| 33. | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar |
| 34. | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar |

### 4.1.1.8 Kukosekana kwa utaratibu wa kudhibiti vihatarishi

Kanuni ya 154 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kwamba "Afisa Mhasibu anatakiwa kuandaa waraka kwa ajili ya kudhibiti vihatarishi (Risk Management Framework) ili kuhakikisha kuwepo kwa mfumo sahihi unaoendana na matakwa ya vigezo vya kimataifa vya kudhibiti majanga/vihatarishi ambao utakuwa ni sehemu ya mpango mkakati na mpango kazi wa mwaka wa Taasisi ya Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazijaandaa waraka kwa ajili ya kudhibiti vihatarishi, waraka ambao utatumika kuweka kumbukumbu, kutathmini na kutoa taarifa ili kuhakikisha kunakuwa na mfumo sahihi wa udhibiti na usimamizi wa majanga jambo ambalo linaweza kupelekea Taasisi hizo kushindwa kudhibiti vihatarishi au majanga pale yanapotokezea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuandaa utaratibu maalum wa kuvitambua na kuviainisha vihatarishi vinavyoweza kujitokeza katika Taasisi zao na kuviwekea utaratibu sahihi wa kuvidhibiti ili kuepuka kujitokeza kwa majanga kwenye Taasisi hizo. Mchanganuo wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 15: Taasisi ambazo hazina utaratibu wa kudhibiti vihatarishi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba |
| 2. | Wizara ya Afya Pemba |
| 3. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba |
| 4. | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba |
| 5. | Hospitali ya Mnazi Mmoja |
| 6. | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar |

#### 4.1.1.9 Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato

Kifungu nambari 30(1-4) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinamtaka "Afisa Masuuli kuwajibika kwa uwezo wake wote katika suala la usimamizi katika ukusanyaji wa mapato".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mujibu wa makadirio ya vyanzo vyao vya ndani vya kibajeti jambo ambalo limepelekea kuathiri utekelezaji wa kazi walizojipangia.

Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato wa vyanzo vya ndani kumetokana na baadhi ya Taasisi kuwa na mifumo duni ya ukusanyaji wa mapato au kutokutoa kipaombele cha uhamasishaji wa malipo yatokanayo na vyanzo vyao vya mapato au kuwa na ubunifu duni wa uanzishwaji wa vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato pamoja na kushindwa kuvisimamia vyanzo hivyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za umma kuongeza umakini katika ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuwapatia elimu watumishi wanaoshughulikia ukusanyaji wa mapato pamoja na kuhamasisha wananchi njia bora ya kuchangia mapato ya Serikali ikiwemo kubuni njia bora zaidi zitakazohakikisha kuwa mapato yanakusavywa kikamilifu na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha zinafikia malengo yaliyowekwa. Miongoni mwa taasisi hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 16: Taasisi ambazo hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

| Namba | Jina la Taasisi | Makadirio ya Makusanyo (Tsh.) | Makusanyo Halisi (Tsh.) | Asilimia ya Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba | 225,670,000 | 97,235,894 | 43.08 |
| 2. | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba | 97,000,000 | 26,257,450 | 27 |
| 3. | Taasisi ya Viwango Pemba | 251,496,000 | 110,129,270 | 43.8 |
| 4. | Mahkama Kuu Pemba | 315,069,860 | 163,823,468 | 52 |
| 5. | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba | 251,496,000 | 195,033,476 | 77.5 |
| 6. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba | 139,855,200 | 92,277,364 | 65.98 |
| 7. | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba | 158,558,536 | 30,278,500 | 19 |
| 8. | Wizara ya Habari,Vijana Utamaduni na Michezo Pemba | 89,997,000 | 42,036,500 | 47 |
| 9. | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba | 50,000,000 | 5,897,135 | 11.79 |
| 10. | Kamisheni ya Utalii Pemba | 167,245,000 | 112,293,994 | 67.14 |

#### 4.1.1.10 Kutokuthibitishwa kazini kwa waajiriwa waliomaliza muda wa majaribio (Probation Period)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 9(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inaeleza kwamba "Mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa mara ya kwanza atalazimika kuwemo katika majaribio ya utumishi kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa".

Ukaguzi umebaini kwamba kuwepo kwa waajiriwa waliomaliza muda wa majaribio katika Taasisi mbali mbali za Umma, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokupatiwa barua za uthibitisho wa kuthibitishwa kwao kazini kwa mujibu wa utaratibu jambo ambalo linanyima fursa na haki za watumishi hao kuweza kujiendeleza kimasomo, kupata mikopo ya muda mrefu pamoja na mambo mengineyo yanayofanana na haki za watumishi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Umma kuhakikisha unasimamia taratibu za ajira ikiwa ni pamoja na kuthibitishwa kazi kwa waajiriwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo Sheria ya Utumishi wa Umma ili kuweza kupatikana kwa haki za msingi kwa waajiriwa. Mchanganuo wa waajiriwa hao ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 17: Watumishi ambao hawajathibitishwa kazi**

| Namba | Jina la Mtumishi | Mwaka wa Ajira | Cheo | Muda wa Ajira (Miaka) |
|---|---|---|---|---|
| **Ofisi ya Rais Ikulu Pemba** | | | | |
| 1. | Muhammed Ali Muhammed | 2019 | Tarishi | 5 |
| 2. | Asha Ali Khamis | 2020 | Mhudumu | 4 |
| 3. | Fatma Khamis Omar | 2020 | Mhudumu | 4 |
| 4. | Mbarouk Hamad Ali | 2020 | Mhudumu | 4 |
| 5. | Kombo Juma Khamis | 2020 | Mhudumu | 4 |
| **Wizara ya Afya Pemba** | | | | |
| 6. | Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika | | | |
| **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba** | | | | |
| 7. | Hafidh Ali Moh'd | 09/01/1997 | Afisa Mdhamin | 26 |
| 8. | Nunu Issa Juma | 24/06/2020 | Afisa Watoto Msaidizi | 4 |
| 9. | Aisha Suleiman Omar | 02/11/2020 | Afisa Jinsia | 4 |

| Namba | Jina la Mtumishi | Mwaka wa Ajira | Cheo | Muda wa Ajira (Miaka) |
|---|---|---|---|---|
| 10. | Muzna Kombo Omar | 10/08/2020 | Mhudumu | 4 |
| 11. | Suleiman Mwidan Assaa | 07/01/2019 | Mhudumu | 5 |
| **Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba** | | | | |
| 12. | Abdalla Said Hamad | 03/02/2020 | Afisa TEHAMA | 4 |
| 13. | Bimwana Moh'd Yahya | 03/02/2020 | Mtunza Ghala | 4 |
| 14. | Adam Abdalla Said | 03/02/2020 | Afisa ufuatiliaji na Tathmini | 4 |
| 15. | Abdul-Aziz Omar Juma | 03/02/2020 | Muhudumu | 4 |
| 16. | Arafa Yussuf Ali | 03/02/2020 | Muhudumu | 4 |
| 17. | Asha Hemed Said | 27/02/2020 | Afisa Uratibu | 4 |
| 18. | Chumu Suleiman Jamali | 03/02/2020 | Afisa Sheria | 4 |
| 19. | Zeyana Azizi Simai | 03/02/2020 | Afisa Takwimu | 4 |
| 20. | Mohamed Juma Mohamed | 03/02/2020 | Karani Masjala | 4 |
| 21. | Siti Haji Khamis | 03/02/2020 | | 4 |
| 22. | Suleiman Juma Khamis | 03/02/2020 | Score Board Operator | 4 |
| 23. | Seif Salim Mussa | 03/02/2020 | Afisa Utamaduni | 4 |
| 24. | Fatma Moh'd Suleiman | 03/02/2020 | | 4 |
| 25. | Said Salim Rashid | 03/02/2020 | Mlinzi | 4 |
| 26. | Othman Bakari Moh'd | 03/02/2020 | | 4 |
| 27. | Hassan Kassim Juma | 03/02/2020 | | 4 |
| 28. | Yahya Othman Simba | 03/02/2020 | | 4 |
| 29. | Abdulkadiri Juma Khamis | 03/02/2020 | Taarishi | 4 |
| 30. | Husein Haji Faki | 03/02/2020 | Dereva | 4 |
| 31. | Mohamed Abdi Said | 03/02/2020 | | 4 |
| 32. | Masika Omar Juma | 03/02/2020 | Muhudumu | 4 |
| 33. | Ibrahim Hamad Rashi | 03/02/2020 | | 4 |
| 34. | Abuu Juma Sharif | 03/02/2020 | | 4 |
| 35. | Fatma Moh'd Winzi | 03/02/2020 | | 4 |
| 36. | Iddi Ibrahim Suleiman | 03/02/2020 | | 4 |
| 37. | Nasra Hafidh Ameir | 03/02/2020 | | 4 |
| 38. | Nawal Masoud Suleiman | 03/02/2020 | | 4 |
| 39. | Asha Said Hamad | 03/02/2020 | | 4 |
| 40. | Maryam Ali Haji | 03/02/2020 | | 4 |
| 41 | Khamis Mussa Moh'd | 27/02/2020 | Afisa Mipango | 4 |
| 42. | Abdalla Abdi Mbwana | 27/02/2020 | Studio Operator Msaidizi | 4 |
| 43. | Mohamed Mkubwa Zubeir | 27/02/2020 | Mwangalizi wa Ofisi | 4 |

| Namba | Jina la Mtumishi | Mwaka wa Ajira | Cheo | Muda wa Ajira (Miaka) |
|---|---|---|---|---|
| 44. | Khamisa Omar Hamad | 27/02/2020 | Muhudumu | 4 |
| 45. | Juma Jongo Juma | 27/02/2020 | Mlinzi | 4 |
| 46. | Ibrahim Omar Ibrahim | 27/02/2020 | | 4 |
| 47. | Abbas Said Abass | 14/08/2020 | Karani Kalamazoo | 4 |
| 48. | Jokha Mbarouk Masoud | 14/08/2020 | Muhudumu | 4 |
| 49. | Khamis Saleh Khamis | 14/08/2020 | | 4 |
| 50. | Khamis Juma Shaali | 14/08/2020 | | 4 |
| 51. | Yusra Abdulla Abdi | 14/08/2020 | | 4 |
| 52. | Raya Sharif Nassor | 14/08/2020 | | 4 |
| 53. | Aisha Juma Ali | 14/08/2020 | | 4 |
| 54. | Winfrida Cassian Gallos | 14/08/2020 | | 4 |
| 55. | Omar Suleiman | 14/08/2020 | Mlinzi | 4 |
| 56. | Hamad Salim Hamad | 14/08/2020 | | 4 |
| 57. | Ali Omar Hamd | 14/08/2020 | | 4 |
| 58. | Kassim Ali Ramadhan | 14/08/2020 | | 4 |
| 59. | Hussein Ali Ahmada | 14/08/2020 | | 4 |
| 60. | Khamis Ali Khamis | 14/08/2020 | | 4 |
| **Wizara ya Maji Nishati na Madini Pemba** | | | | |
| 61. | Jokha Makame Moh'd | 07/09/2020 | Muhudumu | 4 |
| 62. | Moh'd Abdi Said | 01/07/2020 | Dereva | 4 |
| 63. | Time Iddi Hamad | 01/07/2020 | Muhudumu Kware | 4 |
| 64. | Mkitu Juma Ali | 07/07/2019 | Muhudumu Kware | 5 |
| 65. | Nadhra Ali Said | 2020 | Muhudumu Kware | 4 |
| 66. | Zeyana Khamis Ali | 2020 | Muhudumu | 4 |
| 67. | Moh'd Makame Mussa | 2019 | Muhudumu Kware | 5 |

*Chanzo: Faili binafsi (OPF) za watumishi husika.*

#### 4.1.1.11 Malipo yaliyokosa Stakabadhi za kielektroniki shilingi 124,061,789

Kifungu cha 23(1) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi na Uratibu wa Kodi ya 2009 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021) kinaeleza kwamba "Mtu yoyote anayesambaza bidhaa au kutoa huduma iwe kwa mkopo au kwa fedha taslimu au kupokea malipo kuhusiana na bidhaa zinazotolewa au huduma inayotolewa atatoa stakabadhi ya fedha au ankara ya fedha kwa kutumia kifaa cha kielektroniki".

Ukaguzi umebaini baadhi ya Taasisi za Umma zimefanya malipo kwa ajili ya huduma mbali mbali zenye thamani ya shilingi 124,061,789 kwa watoa huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa stakabadhi za kielektroniki ili kuthibitisha uhalali wa watoa huduma kusajiliwa na kutambulika na Serikali kutokana na kodi inayopaswa kulipwa na kuingia Serikalini. Kufanya malipo bila ya kudai stakabadhi za kielektroniki ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha malipo yoyote yanayofanyika kwa watoa huduma ni vyema kudai stakabadhi za kielektroniki ili kuwepo kwa uthibitisho wa ukatwaji wa kodi ya Serikali kwa watoa huduma hao. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 18: Taasisi zilizofanya malipo bila ya kudai stakabadhi za kielektroniki**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|
| | **Afisi ya Rais Ikulu** | |
| 66/5 ya 12/05/2023 | Wakala wa SMZ wa Uchapaji | 5,669,500 |
| 59/5 ya 12/05/2023 | Visiwani General Supplier | 1,890,000 |
| 58/5 ya 12/05/2023 | Enhance Company Limited | 2,800,000 |
| 54/5 ya 12/05/2023 | Lukman Resraurant Limited | 1,372,000 |
| 50/5 ya 09/05/2023 | New Home Furniture | 1,200,000 |
| 44/5 ya 09/05/2023 | Sahara Shopping Centre | 2,640,500 |
| 38/5 ya 08/05/2023 | Visiwani General Supplier | 1,140,000 |
| 10/5 ya 28/04/2023 | Wakala wa SMZ wa Uchapaji | 1,497,300 |
| 142/1 ya 24/01/2023 | Mao General Supplier | 3,517,710 |
| 120/2 ya 23/02/2023 | Visiwani General Supplier | 2,025,000 |
| 61/7 ya 28/07/2022 | Protocol Services | 1,390,500 |

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|
| 83/5 ya 18/05/2023 | Zuze Decoration Car Accessories | 3,858,000 |
| 78/5 ya 18/05/2023 | Visiwani General Supplier | 4,292,000 |
| 10/3 ya 02/03/2023 | Sahara Shopping Centre | 3,760,000 |
| **Jumla Ndogo (A)** | | **37,052,510** |
| | **Tume ya Mipango Zanzibar** | |
| 03/02 ya 09/2022 | Swisan Ent. Ltd | 32,124,400 |
| 105/03 ya 10/3/2023 | Zanzibar Petroleum ltd | 600,000 |
| 131/03 ya 13/3/2023 | | 300,000 |
| 149/04 ya 6/4/2023 | | 618,000 |
| 148/04 ya 4/4/2023 | | 1,600,000 |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **35,242,400** |
| | **Wizara ya Maji Nishati na Madini** | |
| 20/8 ya 15/08/2022 | Feraas General Supply Limited | 993,450.98 |
| 34-37/9 ya 07/09/2022 | Katibu Mkuu WMNM | 1,134,000.00 |
| 24/10 ya 06/10/2022 | Jawaja Auto Parts | 637,000.00 |
| 22/11 ya 09/11/2022 | HM Supplier Company LTD | 953,214.00 |
| 36/11 ya 16/11/2022 | Busam Takeaway | 1,152,942.00 |
| 37/11 ya 17/11/2022 | Mpely Furniture | 2,334,957.00 |
| 68/11 ya 18/11/2022 | Royal Suites of Zanzibar Air Port Hotel Ltd | 13,732,836.00 |
| 21/03 ya 02/03/2023 | Feraas General Supply Limited | 3,585,144.00 |
| 07/05 ya 27/04/2023 | Ahmed Catering Supplier | 7,205,888.00 |
| 32/05 ya 10/05/2023 | Stone Town Traders Ltd | 8,521,739.00 |
| **Jumla Ndogo (C)** | | **40,251,170.98** |
| | **Skuli ya Sheria Zanzibar** | |
| 32/10 ya 27/10/2022 | Him & Y Technology | 2,235,293 |
| 13/05 ya 12/05/2023 | Lab Tech General Supplier | 3,170,415 |
| 17/10 ya 18/10/2022 | Wakala wa Mkonga | 3,110,000 |
| 10/08 ya 12/08/2022 | One 2 One Ltd | 3,000,000 |
| **Jumla Ndogo (D)** | | **11,515,708** |
| **Jumla Kuu (A+B+C+D)** | | **124,061,789** |

### 4.1.1.12 Kutokuwepo kwa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa

Kanuni nambari 120(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inamtaka "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kuhakikisha kwamba kunakuwepo kwa vifaa vya awali vya kukabiliana na maafa na pia kunakuwepo kwa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa kwa kila taasisi au Wizara".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazijaandaa Mpango Mkakati ambao utasimamia na kutoa muongozo wa jinsi ya kukabiliana na maafa pindipo yatakapotokea. Aidha, ukaguzi umebaini kuwepo kwa baadhi ya dosari kama zifuatazo:-

- Hazijateua afisa maalum ambae atasimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa udhibiti wa maafa. Hii ni kwenda kinyume na kanuni nambari 120(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayoeleza kwamba "Taasisi zote za umma zitaanzisha na kuweka afisa maalum kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji wa udhibiti wa maafa katika taasisi zao".
- Hazijatenga fungu maalum la fedha ambalo litatumika kwa ajili ya kukabiliana na maafa pale yatakapotokea. Hii ni kukiukwa kwa kanuni nambari 120(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayoeleza kwamba "Katika kuhakikisha kwamba mpango wa Taifa wa kukabiliana na maafa unatekelezwa kila taasisi itahakikisha kwamba katika mipango yake kunatengwa fungu maalum kwa ajili ya kukabiliana na maafa".
- Watendaji wa Taasisi kutokupatiwa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na maafa pale yatakapotokea. Hii ni kwenda kinyume na kanuni nambari 120(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayoeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha kuwa watumishi wote wa taasisi yake wanafahamu mpango na taratibu zote za kukabiliana na maafa na wanapata fursa ya kuhudhuria mafunzo ya kukabiliana na maafa".

Kutokuwepo kwa mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa kunapelekea:-

- Ukiukwaji wa Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.
- Kuwepo kwa ugumu wa kujinusuru na kukabiliana na maafa pale yatakapotokea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba unachukua hatua za haraka za kuanzisha Mpango Mkuu wa Kukabiliana na Maafa ambao utasaidia katika kurekebisha changamoto mbalimbali zinazotokana na maafa hayo pamoja na kuwapatia mafunzo na elimu watendaji juu ya kukabiliana na maafa kwa lengo la kupata uwelewa na kujua hatua za kuchukua pindipo maafa yakitokea ili kupunguza madhara yatokanayo na maafa hayo. Mchanganuo wa Taasisi zilizokuwa hazina Mpango wa Kukabiliana na Maafa ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 19: Taasisi ambazo hazina Mpango wa Kukabiliana na Maafa**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wizara ya Afya Zanzibar |
| 2. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar |

### 4.1.1.13 Kutokuwepo Taarifa za Kuhesabu Mali (Stock Taking)

Kifungu nambari 71(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba Taasisi kufanya zoezi la utambuzi wa vifaa vya taasisi kwa lengo la kujua idadi, thamani na hali halisi ya vifaa hivyo.

Aidha, kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unazitaka taasisi zote za Serikali kufanya "Stock Taking" ya Mali za Mpito (Current Assets) na kuzianisha mali hizo zilizopo hadi kufikia tarehe 30/06/2023 kwa kuainisha bakaa ya "Inventories na Receivables".

Ukaguzi umebaini baadhi ya Taasisi za Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hazikufanya zoezi hili licha ya kuwa Taasisi hizo zimebainika kuwa na bakaa ya vifaa mbali mbali ambavyo havikutumika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Muongozo nambari 2 wa utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka uliotolewa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha miongozo inafuatwa ili kuendana na mfumo sahihi wa ufungaji wa hesabu ya mwisho wa mwaka ambao umetolewa na Mhasibu Mkuu. Orodha ya Taasisi zilizokuwa hazijafanya utaratibu wa kuhesabu mali na vifaa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20: Taasisi ambazo hazijafanya utaratibu wa kuhesabu mali (stock taking)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 2. | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ |
| 3. | Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais |

# SURA YA TANO



# 5.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu na taarifa mbali mbali za hesabu ikiwemo fedha na rasilimali za umma pamoja na mfumo wa udhibiti wa ndani umekuwa ukiimarika ingawa kumejitokeza dosari za kiutendaji mbali mbali.

Katika ukaguzi huo kulijitokeza dosari za kiutendaji kwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali ambapo baadhi ya dosari ziliweza kurekebishwa na kupatiwa ufumbuzi wa hoja za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha ukaguzi, aidha baadhi ya dosari za ukaguzi hazikuweza kupatiwa ufumbuzi kutokana na kutokujitosheleza kwa majibu yaliyowasilishwa wakati wa ukaguzi wa awali (spot query) pamoja na ukaguzi wa marudio (verification) jambo ambalo lilipelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

## 5.1 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS IKULU

### 5.1.1 FUNGU A 01 - OFISI YA RAIS IKULU

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**OFISI YA RAIS IKULU PEMBA**

#### 5.1.1.1 Uwepo wa Afisi ya Katibu Muhtasi wa Wizara mbili katika afisi moja

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Katibu Muhtasi wa Afisi ya Rais Ikulu anatumia chumba kimoja na katibu muhtasi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa muingiliano wa taarifa za Afisi hizo, pamoja na kuvuja kwa taarifa za mawasiliano yanayofanyika katika Afisi husika.

Kutumia chumba kimoja kwa taasisi mbili nyeti huenda ikapelekea kuchanganyika kwa majalada ya nyaraka za Afisi hizo na hatimae kupelekea kuvuja kwa taarifa za siri za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Rais Ikulu kuzitenganisha afisi za katibu muhtasi ili kuepusha kujitokeza kuvuja kwa siri za taasisi mbili hizo hatimae kupelekea mgongano wa taarifa.

### 5.1.2 FUNGU A 02 – OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI – BLM

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.2.1 Ununuzi wa Mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 68,672,878

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 68,672,878 zimelipwa na Afisi ya Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa mtoa huduma COASTAL FUEL SERVICES LTD bila ya kufunga mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Baraza la Mapinduzi kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama Sheria inavyoelekeza.

Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa bila ya kufunga mkataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 21: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba

| Tarehe | Hundi Namba | Hati Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 19/05/2023 | TISS | A02PV2200000546 | 1,490,000 | Coastal Fuel Services LTD | Malipo kwa ajli ya ununuzi wa mafuta |
| 17/05/2023 | | A02PV2200000519 | 7,652,060 | | |
| 11/10/2022 | | A02PV2200000139 | 5,960,000 | | |
| 16/02/2023 | | A02PV2200000373 | 5,760,000 | | |
| 14/02/2023 | | A02PV2200000356 | 6,886,900 | | |
| 30/12/2022 | | A02PV2200000356 | 6,394,879 | | |
| 29/12/2022 | | A02PV2200000287 | 2,050,000 | | |
| 21/03/2023 | | A02PV2200000448 | 3,000,000 | | |
| 15/06/2023 | | A02PV2200000580 | 7,369,000 | | |
| 02/08/2022 | | A02PV2200000024 | 5,600,000 | | |
| 15/11/2022 | | A02PV2200000188 | 3,000,000 | | |
| 30/12/2022 | | A02PV2200000298 | 4,394,879 | | |
| 08/09/2022 | | A02PV2200000091 | 5,960,000 | | |
| 21/03/2023 | | A02PV2200000448 | 3,155,160 | | |
| **Jumla** | | | **68,672,878** | | |

### 5.1.3 FUNGU B 01 – OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.3.1 Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi (Performance Appraisal)

Kanuni nambari 93(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaelekeza "Kila taasisi ya umma italazimika kumfanyia tathmini ya utendaji wa kazi mtumishi wake kila mwaka. Fomu ya tathmini itatolewa na Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma".

Ukaguzi umebaini kuwa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais haifanyi tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi wake kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya Utumishi.

Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi kunapelekea kuwakosesha haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria ikiwemo kupata nyongeza ya mwaka, kupandishwa madaraja pamoja na stahiki nyenginezo zinazohusiana na mtumishi wa Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhakikisha unatekeleza wajibu wa kumfanyia mtumishi tathmini ili kuweza kupima ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa miongozo na taratibu za kiutumishi.

#### 5.1.3.2 Mikataba ya ongezeko (addendum) ambayo haikuidhinishwa na Mamlaka ya Manunuzi shilingi 83,000,500

Kanuni nambari 49(4) ya Kanuni ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2020 inaeleza kwamba "Mkataba hautaongeza bei ya jumla ya mkataba kwa zaidi ya asilimia kumi na tano ya bei ya awali bila idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (Paymaster General) au mamlaka sahihi ya kupitisha bajeti".

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi ulipitia mikataba mbali mbali ya manunuzi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kubaini baadhi ya mikataba kuwa na ongezeko (Addendum) la ziada ya asilimia kumi na tano (15) na kupelekea ongezeko la thamani ya shilingi 83,000,500. Dosari iliyobainika ni kutokuwasilishwa mikataba hiyo kwa ajili ya kuombewa idhini ya matumizi kwa mamlaka husika kwa mujibu wa sheria.

Kutokuwasilisha nyaraka za nyongeza za mikataba kwa Mamlaka ya manunuzi kunapelekea kufanyika kwa matumizi ambayo hayajaidhinishwa na Mamlaka husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuwasilisha nyaraka zote za manunuzi katika Mamlaka husika ili kuepuka dosari mbali mbali zitakazoweza kujitokeza. Mikataba hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 22: Mikataba yenye Ongezeko la Fedha

| Nambari | Nambari ya zabuni | Kiwango cha fedha katika ya mkataba | Ongezeko (Addendum) | Mzabuni | Asilimia | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya kumaliza | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SMZ/A06/ W/Q/2022-2023/35 | 146,242,280 | 47,000,500 | KIN INVESTMENT CO. LTD | 32.1 | 25/06/2023 | 25/9/2023 | Ukarabati na upanuzi wa Majengo |
| 2 | SMZ/A06/W/ RNCB/2021-2022/37 | 186,586,440 | 36,000,000 | Furaha General Traders Company Ltd | 19.2 | -- | 23/9/2022 | Uchimbaji wa visima na ujenzi wa minara. |
| **Jumla** | | | **83,000,500** | | | | | |

## 5.2 WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

### 5.2.1 C 02 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**BARAZA LA WAWAKILISHI PEMBA**

#### 5.2.1.1 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 33,459,261

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 33,459,261 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Baraza la Wawakilishi Pemba lakini baadhi ya vielelezo hivyo havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Baraza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Wawakilishi kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuthibitisha uhalali wa malipo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 23: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

| Namba | Hati Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 01/07 ya 08/07/2022 | 4,400,000 | BLW Pemba | Malipo ya safari kikazi |
| 2. | 34/07 ya 25/07/2022 | 5,000,000 | | Ununuzi wa mafuta. |
| 3. | 07/01 ya 13/01/2023 | 4,915,000 | Meneja PBZ Pemba | Malipo kwa ajili ya Afisi. |
| 4. | 08/01 ya 13/01/2023 | 900,000 | ZECO Pemba | Ununuzi wa Umeme |
| 5. | 29/03 ya 27/03/2023 | 1,000,000 | | |
| 6. | 8/10 ya 11/10/2023 | 1,069,600 | Chasasa Services Station | Ununuzi wa mafuta |
| 7. | 6/12 ya 13/12/2022 | 8,000,000 | | |
| 8. | 7/12 ya 13/12/2022 | 1,000,000 | ZECO | Ununuzi wa Umeme |
| 9. | 8/5 ya 10/5/2023 | 4,000,000 | Chasasa Service Station | Ununuzi wa mafuta |
| 10. | 9/5 ya 10/5/2023 | 511,111 | ZECO | Ununuzi wa umeme |
| 11. | 1/6 ya 2/6/2023 | 500,000 | | |
| 12. | 12/6 ya 12/6/2023 | 1,663,550 | TLM Computer Services | Ununuzi wa Kompyuta |
| 13. | 18/6 ya 12/6/2023 | 500,000 | ZECO | Ununuzi wa umeme |
| **Jumla** | | **33,459,261** | | |

*Chanzo: Hati za malipo*

### 5.2.1.2 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 17,271,394

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilling 17,271,394 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Baraza la Wawakilishi Pemba. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo pamoja na vielelezo vya matumizi husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika ambapo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kwamba hati za malipo pamoja na vielelezo vyake zinatayarishwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 24: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi

| Hati Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|
| 19/1 | 1,270,000 | Wawakilishi Sport Club |
| 2/4 | 323,000 | TRA Domestic Revenue |
| 21/4 | 8,300,000 | Khamis Yussuf Hamad |
| 26/5 | 2,943,198 | TPB Bank |
| 27/5 | 3,542,700 | Zanzibar Social Security Fund |
| 4/6 | 425,070 | Zanzibar NHIF Collection Account |
| 34/6 | 467,426 | Baraza la Wawakilishi |
| **Jumla** | **17,271,394** | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa kwenye Daftari la fedha taslimu la hesabu ya matumizi ya kawaida.*

#### 5.2.1.3 Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 13,700,000

Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha, kifungu nambari 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Wawakilishi limefanya malipo yenye jumla ya shilingi 13,700,000 kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama watoa huduma jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na usajili huo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Wawakilishi Pemba kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua bidhaa au huduma kwa wafanyabiashara au watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 25: Wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa

| Namba | Hati Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa bila Kusajiliwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 05/07 12/07/2022 | 36,260,000 | 11,200,000 | Baraza la Wawakilishi Pemba | Malipo kwa ajili ya kodi ya gari ya kamati. |
| 2. | 03/02 09/02/2023 | 2,500,000 | 2,500,000 | Nassor Moh'd Kombo | Malipo kwa ajili ya kupaka rangi nyumba ya spika. |
| **Jumla** | | | **13,700,000** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo za Baraza*

### 5.2.1.4 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 71,320,500

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Wawakilishi Pemba limefanya malipo yenye jumla ya shilingi 71,320,500 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Wawakilishi Pemba kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 26:Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

| Namba | Hati Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 01/07 ya 08/07/2022 | 4,400,000 | Baraza la Wawakilishi Pemba | Malipo ya safari za kikazi |
| 2. | 02/07 ya 12/07/2022 | 7,616,000 | | Malipo ya kazi za muda wa ziada |
| 3. | 34/07 ya 25/07/2022 | 5,000,000 | | Malipo ya ununuzi wa mafuta |
| 4. | 02/08 ya 12/08/2022 | 6,057,800 | | Malipo ya matumizi mbalimbali |
| 5. | 9/12 ya 15/12/2022 | 4,000,000 | | Malipo kwa ajili ya Kamati za Bara-za |
| 6. | 27/12 ya 28/12/2022 | 2,868,000 | | Malipo kwa ajili ya Area |
| | 01/03 ya 09/03/2023 | 7,056,700 | | Malipo ya shughuli mbalimbali za Baraza |
| 7. | 09/03 ya 16/03/2023 | 9,290,500 | | |
| 8. | 31/03 ya 27/03/2023 | 4,000,000 | | Malipo kwa ajili ya kamati |
| 9. | 3/4 ya 11/4/2023 | 4,099,500 | | Malipo ya shughuli za Baraza |
| 10. | 8/4 ya 16/4/2023 | 7,020,000 | | Malipo kwa ajili ya kizuka |
| 11. | 1/5 ya 2/5/2023 | 4,500,000 | | Marejesho ya fedha |
| 12. | 10/5 ya 10/5/2023 | 5,412,000 | | Malipo ya shughuli za Baraza |
| **Jumla** | | **71,320,500** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

#### 5.2.1.5 Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu vya bajeti shilingi 25,754,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Wawakilishi Pemba limefanya malipo yenye jumla ya shilingi 25,754,000 kwa ajili ya kupatiwa huduma mbalimbali za uendeshaji wa Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo hayo bila ya kuzingatia vifungu husika vya bajeti vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na kutokuzingatia mpango kazi ulioandaliwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea malengo ya vifungu husika kutokufikiwa, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 50(3)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Baraza la Wawakilishi Pemba kuhakikisha unazingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 27: Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu**

| Namba | Hati Nambari | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelip-wa | Kifungu Kilichotumika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/12 ya 5/12/2022 | 9,214,000 | Baraza la Wawakilishi Pemba | Major Maintenance of Buildings na Teaching Materials and Books. | Malipo kwa ajili ya posho |
| 2. | 5/12 ya 13/12/2022 | 6,470,000 | Manager PBZ Pemba | Major maintenance of buildings, Tution fees, Food and refreshment (seminers/ meeting), Government office electricity bills | Marejesho na malipo mengineo. |
| 3. | 13/4 ya 16/4/2023 | 10,070,000 | | Major maintenance of buildings | Malipo ya madereva wa Kamati |
| **Jumla** | | **25,754,000** | | | |

*Chanzo: Taarifa za Baraza*

### 5.2.2 FUNGU C 03 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi**

#### 5.2.2.1 Malipo yaliyofanyika nje ya vifungu vya Bajeti shilingi 15,452,889

Kifungu nambari 50(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inaelezea kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma anaweza kufanya mabadiliko ya fedha baina ya programu, shughuli, au baina ya vifungu vikuu ndani ya fungu katika bajeti ya mwaka wa fedha ikiwa; (a) kutakuwa na matumizi katika bajeti ya programu shughuli au baina ya vifungu vikuu ambavyo haviwezekani kutumika; (b) kiwango chote cha fedha kinachofanyiwa mabadiliko au kutokana na programu, shughuli au baina ya programu kuu ya fungu la bajeti kisizidi kiwango kilichoainishwa katika kanuni au muongozo wa programu ya bajeti.

Katika ukaguzi ulofanyika imebainika kwamba Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanya matumizi yenye jumla ya shilingi 15,452,889 kwa ajili ya huduma mbali mbali za uendeshaji wa Tume. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo hayo bila ya kuzingatia taratibu za uhaulishaji wa vifungu vya bajeti vilivyoandaliwa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokufikiwa kwa malengo ya vifungu vilivyoathirika na uhaulishaji huo. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Uchaguzi kuhakikisha unafanya matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na mpango kazi ulioandaliwa, ili kuepusha kutokufikiwa kwa malengo yaliopangwa kwa vifungu husika. Mchaganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 28: Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu husika

| Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tsh) | Kifungu kilichotumika | Kifungu sahihi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 05/2 | Adem Store | 3,786,857 | Maintenance of M/vehicles | Purchase spare parts | Ununuzi wa vifaa vya magari |
| 02/2 | T/A. A.C Solution & Refigeration | 3,710,000 | Fumigation | Maintenance and repair of equipments | Matengenezo na ununuzi wa vifaa vya AC |
| 03/5 | Zanzibar University | 955,000 | Local training | Tuition fees | Malipo ya masomo ya mfanyakazi |
| 90/6 | ZAWA | 513,643 | Government electricity bill | Water bill | Huduma ya maji |
| 46/9 | | 1,835,402 | | | |
| 92/6 | | 120,000 | | | |
| 93/6 | ZEC Expenditure | 2,931,987 | computer accessories | Telephone and telex | Malipo ya mfumo wa mawasiliano |
| 14/4 | ZEC Expenditure | 300,000 | Printing expenses | Bank charges | Huduma za kibenki PBZ |
| 14/6 | Machochoki Telecommunication | 1,300,000 | Stationery supplies | Computer accessories | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ICT |
| **Jumla** | | **15,452,889** | | | |

### 5.2.3 FUNGU C 05 – TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.2.3.1 Kutokuwepo kwa Daftari la Kuwekea Kumbu Kumbu za Mikataba (Contract Register)

Kanuni ya 47 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba "Afisa Mhasibu anatakiwa aweke daftari la mkataba lenye kufanyiwa marekebisho kwa mikataba yote walioingia kwa mwaka wa fedha husika".

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya UKIMWI Zanzibar haikuandaa daftari la kuwekea kumbukumbu za mikataba kwa ajili ya kuhifadhia taarifa mbali mbali zinazohusiana na mikataba jambo ambalo linaweza kupelekea uwezekano wa kupotea kwa kumbu kumbu muhimu za mikataba inayoingiwa baina ya Tume na watoa huduma mbali mbali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Zanzibar kuhakikisha kwamba inaandaa daftari la kuwekea kumbu kumbu za mikataba kwa mujibu wa matakwa ya kisheria.

**TUME YA UKIMWI PEMBA**

### 5.2.3.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 2,913,672.4

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 2,913,672.4 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Tume ya UKIMWI Pemba lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yaambatishwe na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuthibitisha uhalali wake. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama zinavyoonekana katka jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 29: Malipo yenye vielelezo pungufu

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/8 ya 05/08/2022 | 028507 | 637,200.90 | Pemba General Supply | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia na mawasliano |
| 22/09/2022 | 029568 | 336,275.50 | | |
| 14/7 ya 11/10/2022 | 030015 | 240,196 | | |
| 03/08 ya 30/08/2022 | 000304 | 1,700,000 | | |
| **Jumla** | | **2,913,672.4** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo.*

### 5.2.3.3 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 2,280,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya UKIMWI Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 2,280,000 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kwa kutumia njia ya benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 30: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 3/9 ya 14/9/2022 | 029333 | 520,000 | Tume ya UKIMWI Pemba | Malipo kwa ajili ya mafunzo |
| 2/9 ya 14/9/2022 | 0293333 | 820,000 | | |
| 3/5 ya 17/5/2023 | 35346 | 500,000 | | |
| 25/11 ya 23/11/2022 | 031304 | 290,000 | | Malipo kwa ajili ya uhamasishaji wa siku ya UKIMWI Duniani |
| 19/11 ya 23/11/2022 | 031266 | 150,000 | | |
| **Jumla** | | **2,280,000** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.2.3.4 Watumishi ambao hawajaenda likizo la mwaka kwa muda mrefu

Kwa mujibu wa kanuni ya 58(1)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa 'Mtumishi wa umma atastahiki kupewa likizo la siku ishirini na nane za kazi ndani ya miezi kumi na mbili na atastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu au kama itakavyofafanuliwa katika matoleo kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma. Aidha, kanuni ya 58(1)(c) inafafanua kwamba siruhusa kwa mtumishi wa umma kuakhirisha likizo yake ya mwaka kwa madhumuni ya kulimbikiza siku zake za likizo ili achanganye na za mwaka mwengine, isipokuwa kwa dharura maalum iliyokubalika'.

Baada ya kupitia majalada (Personal File) ya baadhi ya watumishi wa Tume ya UKIMWI ukaguzi umebaini kuwepo kwa watumishi ambao hawajaenda likizo lao la kawaida kwa muda mrefu jambo ambalo linaweza kupelekea kupungua kwa ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nilizozinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ya utumishi wa umma ikiwemo kuwapatia likizo watumishi kwa mujibu wa miongozo ya kisheria. Mchanganuo wa watumishi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 31: Watumishi ambao hawajaenda likizo lao la mwaka kwa muda mrefu**

| Namba | Jina la Mtumishi | Tarehe ya mwisho ya kuanza likizo | Tarehe ya mwisho ya kumaliza likizo | Idadi ya miaka ambayo hawajaenda likizo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Said Ali Najim | 01/02/2018 | 12/03/2018 | 5 |
| 2. | Ali Mbarouk Omar | 02/01/2020 | 10/02/2020 | 3 |
| 3. | Mwanaidi Juma Salim | 20/04/2021 | 31/05/2021 | 2 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Majalada Binafsi ya Watumishi*

### 5.2.3.5 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 8,404,730

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya UKIMWI Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 8,404,730 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kufanya malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kwa kutumia njia za kibenki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 32: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/7 ya 15/7/2022 | 000300 | 535,000 | Tume ya UKIMWI | Malipo kwa ajili ya shughuli za Program na waelimishaji rika. |
| 3/7 ya 20/7/2022 | 000301 | 1,650,000 | | |
| 1/8 ya 9/8/2022 | 000302 | 1,921,568 | | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya gari la Afisi. |
| 3/8 ya 30/8/2022 | 000304 | 1,700,000 | | Malipo kwa ajili ya shughuli za G.F |
| 5/9 ya 15/9/2022 | 000309 | 317,058 | Miza Mohd Ali | Malipo kwa ajili ya chakula. |
| 8/12 ya 12/12/2022 | 000327 | 1,965,810 | Awali Mussa Msafir | Malipo kwa ajili ya shughuli za Siku ya UKIMWI duniani. |
| 6/9 ya 15/9/2022 | 000310 | 115,294 | Tume ya Ukimwi Zanzibar | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 11/9 ya 30/9/2023 | T.O | 200,000 | Tume ya Ukimwi Zanzibar | Malipo kwa ajili ya utengenezaji wa vipindi. |
| **Jumla** | | **8,404,730** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.2.3.6 Kutokufikiwa kwa malengo ya Uandaaji wa Taarifa za fedha "Segment Reports"

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unazitaka taasisi zote za Serikali kuandaa "Segment Reports" kwa kuzingatia mapato na matumzi ya mwaka wa fedha husika, taarifa za mapato, matumizi pamoja na bakaa katika segments kwa jumla zionekane sawa na "Consolidated financial statements, Statement of Receipt and Payment na Statement of Comparison of Budget and Actual".

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kutofikiwa kwa lengo lililokusudiwa kwa mujibu wa muongozo uliotolewa kwa Tume ya UKIMWI Pemba kutokana na Taasisi hiyo kutopatiwa mafunzo ya kutosha ya namna ya uandaaji wa ripoti hizo pamoja na uchelewaji wa kutolewa kwa muongozo unaozitaka taasisi hizo kuandaa Taarifa za fedha "Segment Reports" jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha na taarifa za fedha zilizoandaliwa kutokana na uwepo wa dosari nyingi za kiutendaji pamoja na baadhi ya Taasisi kushindwa kuandaa taarifa hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba kuhakikisha inatoa mafunzo endelevu kwa Tume ya UKIMWI Pemba na taasisi zote zilizokuwa na uelewa mdogo wa kuandaa taarifa za fedha ili ziweze kuendana na mabadiliko yanayotarajiwa kujitokeza ya kuhama kutoka katika Mfumo wa Fedha Taslim "Cash Basis" kwenda katika Mfumo wa Madeni "Accrual Basis".

## 5.3 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

### 5.3.1 FUNGU D 01 - OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.3.1.1 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) shilingi 953,946,142.20

Kwa mujibu wa Sheria nambari 4 ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya 1998 inatoa ufafanuzi juu ya Taasisi ya Serikali iliyopewa dhamana na mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA) kuzuia kodi ya asilimia 18 kwa mfanyabiashara aliyetoa huduma kwa taasisi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 5,299,700,790 kwa kampuni ya ROM Solution LTD kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya mradi wa Mji Salama pamoja na kuvifunga (Installation) bila ya kukatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya asilimia 18 sawa shilingi 953,946,142.20 jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo, aidha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 4 ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) ya 1998.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kwamba miradi yote inayotekelezwa inakatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mujibu wa Sheria na Miongozo iliyopo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 33: Malipo ambayo hayakukatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

| Namba | Hati ya malipo | Jumla ya fedha (Tsh.) | Kodi Ongezeko la Thamani (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/8/22 ya 19/08/2022 | 1,977,720,641.84 | 355,989,715.53 | Malipo ya Mradi wa CCTV Camera kwa mwezi wa Julai 2022 |
| 2. | 3/9 ya 03/10/2022 | 989,715,148 | 178,148,726.64 | Malipo ya Mradi wa CCTV Camera kwa mwezi wa August 2022 |
| 3. | 4/10 ya 29/11/2022 | 581,907,500 | 104,743,350.00 | Malipo ya Mradi wa CCTV Camera kwa mwezi wa Septemba, 2022. |
| 4. | Dummy | 581,907,500 | 104,743,350.00 | Malipo ya Mradi wa CCTV Camera kwa mwezi wa Oktoba, 2022. |
| 5. | 3/12 ya 29/11/2022 | 581,922,500 | 104,746,050.00 | Malipo ya Mradi wa CCTV Camera kwa mwezi wa Novemba, 2022. |
| 6. | 5/01 ya 05/01/2023 | 586,527,500 | 105,574,950.00 | Malipo ya Mradi wa CCTV Camera kwa mwezi wa Disemba, 2022. |
| **Jumla** | | **5,299,700,789.84** | **953,946,142.17** | |

### 5.3.1.2 Ukiukwaji wa Masharti ya Mkataba wa Mradi wa Mji Salama Shilingi 5,299,700,790

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ iliingia makubaliano ya mkataba tarehe 04/12/2019 na kampuni ya ROM Solution kwa ajili ya kuleta vifaa vya Mji Salama "CCTV Project" pamoja na kuvifunga (Installation) kwa kipindi cha miaka mitatu kwa thamani ya USD 10,655,166.

Kipengele nambari 23.3 cha masharti ya ujumla ya mkataba (GCC) kinaelekeza kwamba mtoa huduma atakuwa na haki ya kudai malipo ya bei ya mkataba kama ilivyoonyeshwa kwenye hati ya ununuzi kwa kila bidhaa aliyoiwasilisha baada ya kuwasilisha bidhaa zote na kuzifunga (installed) pamoja na kukubaliwa kwa bidhaa hizo kwa maandishi na Mteja ambae ni Wizara ya nchi ofisi ya Rais Tawala za Mikoa kwa mujibu wa mkataba na hati zilizoambatanishwa.

Aidha, Kipengele nambari 23.4 cha masharti ya ujumla ya mkataba kinaelekeza kwamba Mteja ataanza kufanya malipo baada ya kujiridhisha kwamba bidhaa zote zimefikishwa kwa usalama, kufungwa, kujaribiwa na kukubaliwa.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imelipa jumla ya shilingi 5,299,700,790 kwa kampuni ya ROM Solutions kwa ajili ya kufanikisha ununuzi na ufungaji wa vifaa hivyo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa muhimu ya kiuchunguzi ya vifaa vilivyowasilishwa na kufungwa ili kujuwa ubora wa vifaa vilivyowasilishwa kwa mujibu wa mkataba na kuepuka kupokea vifaa ambavyo viko chini ya kiwango ambavyo vinaweza kupelekea kuingiza hasara Serikali kwa kukosekana kwa tija inayotokana na ununuzi wa vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu vya mkataba tulivyovitaja hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kwamba kunakuwa na nyaraka maalumu zinazoandaliwa kwa lengo lakuweka taarifa zote sahihi zinazohusiana na ununuzi wa vifaa vya mradi sambamba na kuwatumia wataalamu wa ndani ili kuhakikisha kwamba vifaa vyote vinavyonunuliwa vinakuwa na ubora unaotakikana. Aidha, katika uingiaji wa mikataba yenye thamani kubwa kunakuwa na usimamizi wa mshauri elekezi ili kusimamia miradi yote inayotekelezwa chini ya Wizara. Mchanganuo wa malipo yaliyokiuka masharti ya mkataba ni kama yanavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 34: Malipo yaliofanyika bila kuzingatia masharti ya mkataba

| Namba | Hati Namba | Fedha Iliyolipwa (Tsh.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/8 ya 19/08/2022 | 1,977,720,641.84 | Rom Solution Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya Mradi wa Mji Salama |
| 2. | 3/9 ya 03/10/2022 | 989,715,148 | | |
| 3. | 4/10 ya 29/11/2022 | 581,907,500 | | |
| 4. | Dummy | 581,907,500 | | |
| 5. | 3/12 ya 29/11/2022 | 581,922,500 | | |
| 6. | 5/01 ya 05/01/2023 | 586,527,500 | | |
| **Jumla** | | **5,299,700,789.84** | | |

### 5.3.1.3 Kutokuingizwa kwa Mapato katika hesabu ya mwisho wa mwaka shilingi 203,752,239.46

Ukaguzi umepitia taarifa ya fedha ya mwaka 2022/2023, taarifa za benki pamoja na madaftari ya fedha taslim (cash books) kwa hesabu ya Viwanda na kubaini kwamba jumla ya shilingi 203,752,239.46 zilizokusanywa kupitia hesabu ya viwanda kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 203,752,239.46 hazikuingizwa katika taarifa ya fedha za mwisho wa mwaka.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu za uandaaji wa taarifa za fedha pamoja na viwango vya uhasibu. Kutokuainishwa kwa fedha hizo katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka kunapelekea taarifa hizo kutokuonesha sura sahihi na halisi kulingana na miongozo ya ufungaji wa hesabu ya kitaifa na kimataifa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa viwanda sambamba na Taasisi zinazohusika katika uandaaji wa Taarifa za fedha, kuhakikisha kwamba uandaaji wa taarifa hizo unazingatia taratibu, miongozo pamoja na viwango vya uhasibu. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 35: Mapato ambayo hayakuingizwa katika hesabu za mwisho wa mwaka

| Mwezi | Mauzo ya Viatu (Tsh.) | Mapato ya Ushoni (Tsh.) | Jumla ya Mapato (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| Julai | 4,025,000.00 | 2,637,000.00 | 6,662,000.00 |
| Agosti | 2,885,000.00 | 4,492,650.82 | 7,377,650.00 |
| Septemba | 7,920,000.00 | 2,198,000.00 | 10,115,000.00 |
| Oktoba | 5,400,000.00 | 6,448,950.00 | 11,848,650.00 |
| Novemba | 7,431,500.00 | 12,743,549.82 | 20,175,049.82 |
| Disemba | 7,052,000.00 | 11,881,375.00 | 18,933,375.00 |
| Januari | 7,411,000.00 | 16,915,860.00 | 24,326,860.00 |
| Febuari | 5,146,000.00 | 15,559,500.00 | 20,705,500.00 |
| Machi | 4,263,000.00 | 11,894,750.00 | 16,157,750.00 |
| Aprili | 4,059,000.00 | 19,520,000.00 | 23,579,000.00 |
| Mei | 5,749,478.27 | 7,775,000.00 | 13,524,478.27 |
| Juni | 3,754,000.00 | 26,589,625.55 | 30,343,625.55 |
| **Jumla** | **65,095,978.27** | **138,656,261.19** | **203,748,938.64** |

*Chanzo: Taarifa za daftari la mapato, 2022/2023*

### 5.3.1.4 Kukosekana kwa Mfumo wa Kamera za Ulinzi katika Viwanda vya Ushoni

Kwa Mujibu wa Miongozo ya viwango kubalifu ya TEHAMA (Best Practises) inayoelezea juu ya Usalama wa Kimazingira ya TEHAMA (Phyisical and Enviroment Security) Taasisi inatakiwa kuwa na ulinzi kwa njia ya kidijitali kama vile "CCTV Surveillance System".

Ukaguzi umebaini kwamba uongozi wa Viwanda vya Ushoni vya Idara Maalum za SMZ haujaweka mitambo maalum ya kurikodi na kubaini matukio yanayofanyika ndani ya Viwanda hivyo ikiwemo mitambo ya "CCTV Surveillance System" pamoja na mashine mbali mbali za kubaini uhalifu unaoweza kufanyika dhidi ya vifaa pamoja na mali zenye thamani kubwa zilizopo na zinazotumika ndani ya Viwanda hivyo kama vile mashine za ushoni, vitambaa pamoja na malighafi mbali mbali.

Kutokuwepo kwa vifaa hivyo kunaweza kupelekea Idara kushindwa kupata ushahidi kwa waliohusika kufanya tukio la wizi, uhalifu, uharibifu au uhujumu wa uchumi pindipo tukio hilo likitokea katika mazingira ya Viwanda, jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza miongozo mbali mbali inayotolewa na Serikali katika kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya Idara pamoja na kutenga bajeti maalum kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa kamera na vifaa vyenginevyo vya usalama vitakavyosaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za Umma zilizomo katika maeneo ya Viwanda.

### 5.3.1.5 Kutotumika kwa Mashine za kutengeneza Viatu

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Idara Maalum za SMZ zimekuwa na dhamira njema ya uanzishwaji wa Viwanda mbali mbali kwa lengo la kuweza kujikwamua kiuchumi na kuacha kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Katika uanzishaji wa Viwanda ukaguzi ulifanya ziara maalum ili kuweza kujionea shughuli mbali mbali zinazotekelezwa katika viwanda hivyo, aidha kwa upande wa Kiwanda cha kutengenezea viatu ukaguzi umebaini kuwepo kwa mashine za aina mbili ambazo ni mashine moja (1) ya "Rubber plant" na mashine kumi (10) za "Volkcanise" ambapo mashine ya Rubber Plant hutumika kwa ajili ya kusarifu malighafi za kutengenezea viatu, mashine ya Volkcanise hutumika pale ambapo malighafi imeshasarifiwa na kuchakatwa vizuri na ndipo Volkcanise huzalisha soli za viatu.

Aidha, kwa wa upande viwanda vya ushoni ukaguzi umebaini uwepo wa ufanisi mkubwa katika uzalishaji na ufanyaji kazi wake ambapo tija iliyokusudiwa imeimarika. Hata hivyo jitihada muhimu zinahitajika katika hatua za kuongeza malighafi kwa lengo la kutanua wigo na kupatikana kwa faida kubwa.

Pamoja na uwepo wa ufanisi huo dosari iliyobainika katika ukaguzi kwa upande wa Kiwanda cha Utengenezaji wa Viatu ni uwepo wa mashine za kisasa ambazo hazifanyi kazi kwa muda mrefu na huwenda zikapelekea kuharibika na hatimae kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Kutokufanya kazi kwa mashine hizo kunaweza kukigharimu Kiwanda cha kutengenezea viatu kwa kutumia gharama kubwa ya fedha kununuwa bidhaa zisizo na ubora unaokubalika kutokana na aina ya viatu vinavyopaswa kuzalishwa, vile vile kutapelekea mashine hizo kuchakaa na kuharibika kwa haraka zaidi jambo ambalo litaigharimu Serikali na kuitia hasara kubwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais TAMISEMIM kuchukuwa jitihada za makusudi kunusuru uharibifu ambao utatokezea kwa kuharibika kwa mashine hizo au kuchakaa pindipo zitakapoendelea kukaa bila ya kutumika.

Aidha, ni vyema kufanyika jitihada za kutafuta wataalam watakaoweza kuzitumia na kutoa mafunzo kwa watendaji ili waweze kuzitumia na kufaidika kwa uwepo wa mashine hizo na hatimae kupunguza au kuondoa matumizi makubwa ya ununuzi wa malighafi kutoka nje.

#### 5.3.1.6 Kukosekana kwa vifaa vya huduma ya kwanza

Kanuni ya 125(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa Kila Mkuu wa Taasisi atalazimika kuhakikisha ndani ya Taasisi yake kunakuwa na upatikanaji wa huduma ya kwanza ya afya na vifaa vya huduma ya kwanza kwa watumishi. Aidha, kifungu nambari 85 cha Sheria nambari 8 ya Afya na Usalama Kazini ya 2005 kinazitaka Taasisi "Kuweka vifaa vya zima moto pindi janga litakapotokea".

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ haikuandaa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza (First Aid) pamoja na vifaa vya kuzimia moto (Fire extinguisher) pindi inapotokea dharura kwa watumishi na mali za Wizara. Hali hii inaweza kusababisha kutokea kwa hasara kubwa pindipo pakitokea janga la moto au mtumishi kupata ajali akiwa kazini.

Kutokuweka vifaa vya huduma ya kuzimia moto na huduma ya kwanza ndani ya majengo ya Afisi ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kufanya jitihada za kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza kwa lengo la kulinda usalama wa wafanyakazi kwa kufuata utarabibu wa Sheria na Kanuni zilizoekwa.

## 5.4 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

### 5.4.1 FUNGU F 01 – OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.4.1.1 Ununuzi wa Mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 191,446,790

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 191,446,790 zimelipwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa mtoa huduma United Group Limited kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 74,095,000 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petroli na jumla ya shilingi 117,351,790 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Dizel. Dosari ilyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama Sheria inavyoelekeza.

### 5.4.1.2 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 107,451,300

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 107,451,300 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki.

Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 36: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

| Hati namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---:|---|---|
| 25/8 ya 02/08/2022 | 21,131,100 | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Malipo kwa ajili ya Matumizi Mbalimbali |
| 34/8 ya 03/08/2022 | 4,582,000 | | |
| 40/8 ya 04/08/2022 | 11,522,000 | | |
| 45/8 ya 04/08/2022 | 17,406,200 | | |
| 50/8 ya 18/08/2022 | 11,444,000 | | |
| 22/9 ya 08/09/2022 | 9,860,000 | | |
| 34/9 ya 14/09/2022 | 11,568,000 | | |
| 128/9 ya 22/09/2022 | 11,831,000 | | |
| 93/12 ya 23/12/2022 | 2,440,000 | | |
| 68/3 ya 10/03/2023 | 1,570,000 | Naomba Juma Moh'd | |
| 103/3 ya 16/03/2023 | 945,000 | Ibrahim Abasi Maunda | |
| 55/5 ya 11/05/2023 | 2,000,000 | Masoud Shibli Makame | |
| 365/6 ya 26/06/2023 | 1,152,000 | Ibrahim Abasi Maunda | |
| **Jumla** | **107,451,300** | | |

### 5.4.1.3 Malipo yaliyofanyika kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu shilingi 248,361,770

Kwa mujibu wa muongozo wa ufungaji wa hesabu za mwaka 2022/2023 uliotolewa na Katibu Mkuu wa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia barua yenye kumbukumbu namba ACGEN/BC.195/393/01/01 ya tarehe 13/6/2023 linaeleza kwamba "Aidha, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango inaomba kutoa taarifa ya kwamba mwisho wa kufanyika matumizi ni tarehe 26/06/2023, baada ya hapo hakutakua na matumizi yatakayokubalika kufanyika ili kuondoa usumbufu unaojitokeza wakati wa ufungaji wa Hesabu za Serikali".

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 248,361,770 kwa ajili ya kulipia huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo kinyume na toleo lililobainishwa hapo juu jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa changamoto katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza miongozo ya kifedha wanayoitoa ili kuwa ni kigezo kwa Taasisi nyengine. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Malipo yaliyofanyika kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu**

| Hati Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 381/6 ya 27/6/2023 | 181,108,000 | Mfuko Mkuu wa Hazina | Uhaulishaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari mbili. |
| 383/6 ya 27/6/2023 | 4,785,000 | Saumu Khatib Haji | Malipo kwa ajili ya safari ya mafunzo ya muda mfupi IRDP. |
| 384/6 ya 27/6/2023 | 4,785,000 | Haji Ali Haji | |
| 385/6 ya 27/6/2023 | 10,785,000 | Mohammed Hassan Khamis | |
| 386/6 ya 27/6/2023 | 700,000 | Juma Suleiman Juma | Malipo kwa ajili ya kuandaa mpango wa manunuzi. |
| 387/6 ya 27/6/2023 | 700,000 | Ahsante Gharib Bilal | |
| 388/6 ya 27/6/2023 | 700,000 | Maryam Hassan Suleiman | |

| Hati Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 389/6 ya 27/6/2023 | 700,000 | Sabry Abuu Moh'd | Malipo kwa ajili ya kuandaa mpango wa manunuzi. |
| 390/6 ya 27/6/2023 | 700,000 | Zakia Juma Rashid | |
| 397/6 ya 28/6/2023 | 700,000 | Simai Silima Juma | |
| 398/6 ya 28/6/2023 | 700,000 | Nassor Khamis Juma | |
| 398/6 ya 28/7/2023 | 11,813,914 | Ministry of Finance Deposit | Malipo ya mishahara na mikato tofauti |
| 391/6 ya 27/6/2023 | 700,000 | Seif Hafidh Suleiman | Malipo kwa ajili ya maandalizi ya mpango wa manunuzi |
| 399/6 ya 28/6/2023 | 700,000 | Samha Abdulwahid Mussa | |
| 400/6 ya 28/6/2023 | 700,000 | Mwantano Salehe Abdalla | |
| 401/6 ya 28/7/2023 | 700,000 | Munira Haji Hamza | |
| 402/6 ya 28/6/2023 | 700,000 | Mauwa Ame Ameir | |
| 403/6 ya 28/7/2023 | 700,000 | Seif Mohamed Nassor | |
| 404/6 ya 28/6/2023 | 945,000 | Juma Malik Akil | Malipo ya posho la safari ya kikazi. |
| 405/6 ya 28/6/2023 | 2,500,000 | Alhaji Mwinyi Haji Mzale | |
| 406/6 ya 28/6/2023 | 700,000 | Omar Ali Khamis | Malipo ya posho la utengenezaji mfumo (OTRMIS) |
| 407/6 ya 28/7/2023 | 937,862 | TRA | Malipo ya mkato wa tafauti ya mshahara |
| 408/6 ya 30/6/2023 | 1,314,000 | Zanzibar Revenue Authorty | Malipo ya zuio la kodi |
| 409/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Abdalla Said Omar | Malipo kwa ajili ya ushiriki wa mafunzo ya bajeti. |
| 4/610 ya 30/6/2023 | 40,000 | Zena Mahmoud Hassan | |
| 411/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Hurina Saidi Mohammed | |
| 412/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Omar Mlenge Omar | |

| Hati Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 413/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Maryam Mohd Othman | Malipo kwa ajili ya ushiriki wa mafunzo ya bajeti. |
| 414/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Mulhat Ahmed Mohammed | |
| 415/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Mwanakhamis Mzee Hafidh | |
| 416/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Rauhiya Seif Juma | |
| 417/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Mwanabahati Haji Ali | |
| 418/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Hawa Said Salum | |
| 419/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Mwanaidi Ali Ahmada | |
| 420/6 ya 30/6/2023 | 160,000 | Ramadhan Ali Ramadhan | |
| 421/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Ahsante Gharib Bilal | |
| 422/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Khamis Maulid Khamis | |
| 423/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Masoud Shibli Makame | |
| 424/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Neema Stanley Chikira | |
| 425/6 ya 30/6/2023 | 40,000 | Naomba Juma Mohd | |
| 426/6 ya 30/6/2023 | 1,260,000 | Juma Malik Akil | Malipo kwa ajili ya posho mbali mbali. |
| 427/6 ya 30/6/2023 | 3,030,000 | Alhaji Mwinyi Mzale | |
| 428/6 ya 30/6/2023 | 320,000 | Masoud Shibli Makame | |
| 430/6 ya 30/6/2023 | 14,177,994 | Ministry of Finance Deposit | Malipo ya mikato ya mshahara |
| **Jumla** | **248,361,770** | | |

#### 5.4.1.4 Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 35,000,000

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 katika kibebeo kilichofunganishwa na muongozo huo kinaeleza ya kwamba ifikapo tarehe 23/06/2023 salio la fedha zilizobaki katika akaunti zitalazimika kuhaulishwa katika hesabu za Mfuko Mkuu wa Hazina.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango iliidhinisha utoaji wa fedha mnamo tarehe 23/06/2023 na kukabidhiwa Msaidizi Mshika Fedha Mkuu kuzihifadhi katika maduhuli kinyume na utaratibu wa muongozo wa ufungaji wa hesabu.

Aidha, ukaguzi ulipitia hati mbalimbali zinazohusiana na malipo ya mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2023 na kubaini uwepo wa hati za malipo zilizoambatishwa na barua za maombi ya fedha za mwaka 2022/2023, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuambatanishwa kwa vielelezo vya matumizi hayo na uhaulishaji wa fedha uliofanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Vile vile, katika tathmini iliyofanyika ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo ya fedha hayakuwa katika orodha ya fedha zenye dhamira maalum (commitments). Hii ni kwenda kinyume na kanuni nambari 21(1)(a)(b) ya kanuni za fedha za 2021 inayoeleza kwamba "Fedha ambazo hazijatumika zinaweza kubebwa hadi mwaka ujao wa fedha, tu wakati; (a) kubeba hufanywa kutekeleza ahadi bora ambayo imefanywa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha; na (b) ubebaji unafanywa kukamilisha miradi au ununuzi wa mali, ambao bado unaendelea".

Aidha, ukaguzi haukupatiwa vielelezo vinavyohusiana na maombi na ruhusa (approval) ya kutumia fedha za mwaka husika kwenye mwaka unaofuata vilivyopelekwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoka kwa afisa masuuli, jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu namba 21(2) cha kanuni za fedha za mwaka 2021 kinachoeleza kwamba "Mfuko usio na malipo unaweza tu kustahili kubebwa tu ambapo Afisa Uhasibu wa Taasisi ya Bajeti alikuwa amewasilisha kwa Paymaster General ombi la kubeba chini ya kanuni hii kwa mujibu wa Maelekezo ya Hazina na kupitishwa".

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa unafuata kikamilifu sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na fedha pale wanapotekeleza majukumu yao ya kiutendaji ya kila siku. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 38:Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu

<table>
<tr><th>Hati namba</th><th>Thamani (Tsh.)</th><th>Alielipwa</th><th>Maelezo</th><th>Maelezo ya Mkaguzi</th></tr>
<tr><td>361/6 ya 25/6/2023</td><td>35,000,000</td><td>Ministry of Finance deposit</td><td>Malipo ya masurufu kwa ajili ya safari za ndani kwa mwezi wa Julai 2023/2024</td><td>Fedha hizi kakabidhiwa Msaidizi Mshika Fedha Mkuu. Maombi ya fedha yamefanywa tarehe 23/6/2023 na mhasibu mkuu.</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="4">Mchanganuo wa Matumizi:<br><br>• Shilingi 3,434,000 kalipwa Naibu waziri kwa safari ya Dar es Salaam mualiko wa kuhudhuria hafla ya upokeaji wa fedha Euro 46,110,400 za msaada wa bajeti tarehe 5/7/2023 na kuhudhuria kikao cha mawaziri wa mambo ya nje wa India na mkutano wa 10 wa Tume ya JPC kati ya Tanzania na India tarehe 7/7/2023. Barua ya kuomba fedha ilipokelewa tarehe 3/7/2023. Kalipwa kwa cash. Imelipwa tarehe 10/7/2023.<br>• Shilingi 1,875,000 kalipwa Mh. Ali Suleiman Ameir kwa ajili ya safari ya Dodoma kuhudhuria mkutano wa mawaziri kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi wa FATF. Barua ya maombi ya fedha imepokekewa 26/6/2023. Imelipwa 10/7/2023. Kalipwa kwa fedha taslim na pia hakuna vielelezo.<br>• Shilingi 4,710,000 zimelipwa kwa watenadji watatu i.e Waheed Muhammad Ibrahim 1,890,000, Mussa Ali Juma 1,410,000 na ndugu Bakar Shaaban Bakar 1,410,000 kwa ajili ya nauli na posho la safari ya Dodoma kwa ajili ya kuangalia mfumo wa asset register kuanzia tarehe 23/7/2023 hadi 28/7/2023. Barua ya maombi ya fedha yamepokelewa tarehe 20/7/2023. Imelipwa tarehe 21/7/2023. Zimelipwa kwa mfumo wa fedha taslim.<br>• Shilingi 210,000 kalipwa Nd. Haji H. Khamis kwa ajili ya safari ya Dar es Salaam tarehe 14/7/2023 kuwasilisha pasi ya kusafiria ya Mh. Waziri wa Fedha na Mipango. Barua ya maombi ya fedha imepokelewa 14/7/2023. Imelipwa 20/7/2023. Kalipwa kwa fedha taslim.<br>• Shilingi 330,000 kalipwa Nd. Haji Khamis Hamza na shilingi 360,000 kalipwa Nd. Suleiman M. Rashid kwa ajili ya safari ya Pemba tarehe 21-22/7/2023. Imelipwa tarehe 20/7/2023. Wamelipwa kwa cash na pia Ukaguzi umebaini uwepo wa upungufu wa vielelezo vyenye thamani ya shilingi 42,000. Jumla ya vielelezo ni 34,958,000.<br>• hakuna barua ya kuomba malipo.<br>• Shilingi 10,440,000 zimelipwa kwa wafanyakazi wanne kwa ajili ya safari ya Pemba kuhudhuria mafunzo ya kutumia mfumo wa taarifa za utumishi na malipo (HRMS- PAYROLL) kwa muda wa wiki mbili kuanzia 23/7/2023 hadi 6/8/2023. Kila mmoja kalipwa shilingi 2,610,000. Wafanyakazi hao ni Nd. Hifudh Omar Saidi, Asha Hassan Juma, Abdillah Khamis Haji na Salim Othman Mohamed. Barua mualiko na kuomba malipo ya watendaji yenye kumbukumbu namba AB.483/585/01/117 ya 10/7/2023 kutoka (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala bora imeambatishwa. Barua ya uhaulishaji wa fedha yenye kumbukumbu namba BC.182/2023/07/01/01 yA 24/7/2023 imepokelewa benki tarehe 28/7/2023.</td></tr>
</table>

| Hati namba | Thamani (Tsh.) | Alielipwa | Maelezo | Maelezo ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|---|
| | • Shilingi 939,000 zimelipwa kwa Nd. Saumu K. Haji kwa safari ya Dar es Salaam kuhudhuria mkutano wa "UNICEF FINANCE DEPARTMENT" kuanzia tarehe 6/7/2023 – 8/7/2023. **Hakuna barua ya kuomba fedha kuna barua ya uhaulishaji wa fedha yenye kumbukumbu namba BC.182/2023/08/02/27 ya 21/8/2023 imeambatishwa.**<br>• Shilingi 315,000 zimelipwa kwa Nd. Juma Malik Akili na shilingi 690,000 zimelipwa kwa Nd. Alhaji Mwinyi Mzale kwa ajili ya safari ya Dar es Salaam kuhudhuria kikao cha Launch of National Financial Inclusion Frame work siku ya tarehe 4/8/2023. **Barua ya uhaulishaji wa fedha yenye kumbukumbu namba BC.182/2023/07/01/02 ya 1/8/2023 imepokelewa benki tarehe 2/8/2023.**<br>• Shilingi 765,000 kalipwa Nd. Alhaji Mwinyi Mzale na shilingi 975,000 kalipwa Nd. Juma Malik Akil kwa ajili ya safari ya Dar es Salaam kuhudhuria mkutano wa kamati ya uongozi (steering committee) kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kazi wa FATF utakaofanyika tarehe 20/7/2023. Barua yenye kumbukumbu namba CAC.450/487/01/10/115 ya 18/7/2023 kutoka BLM ya ruhusa ya ndugu Juma Malik Akili imembatishwa. **Imelipwa 20/7/2023 kwa mfumo wa fedha taslim.**<br>• Shilingi 375,000 zimelipwa kwa Nd. Saada Mkuya Salum na shilingi 210,000 zimelipwa kwa Nd. Haji H. Khamis kwa ajili ya safari ya Pemba kuhudhuria mkutano wa mawaziri kujadili ripoti ya utekelezaji wa mpango wa FATF. Barua ya kuomba fedha imepokelewa tarehe 24/7/2023. Barua ya uhaulishaji wa fedha yenye kumbukumbu namba BC.182/2023/08/01/03 ya 2/8/2023 imepokelewa benki tarehe 2/8/2023. **Hakuna vielelezo vya kuthibitisha safari.**<br>• Shilingi 1,875,000 zimelipwa kwa Nd. Saada Mkuya Salum, shilingi 1,050,000 zimelipwa kwa Nd. Haji H. Khamis na shilingi 420,000 zimelipwa kwa Nd. Abubakar Haji kwa ajili ya posho la safari ya Dar es Salaam kuhudhuria kikao cha siku moja na wasimamizi wa miradi inayofadhiliwa na benki ya dunia kwa upande wa Zanzibar. Barua ya uhaulishaji wa fedha yenye kumbukumbu namba BC.182/2023/08/01/04 ya 2/8/2023 imepokelewa benki tarehe 2/8/2023.<br>• Shilingi 885,000 kalipwa Nd. Yussuf I. Yussuf kwa safari ya Dar es Salaam kuanzia tarehe 24/7 2023 hadi 27/7/2023 kushiriki vikao vya heads of State Human Capital Summit. **Hakuna barua ya kuomba fedha.**<br>• Shilingi 5,985,000 zimelipwa kwa watendaji tofauti wa afisi kwa ajili ya kuhudhuria safari tofauti za Dar es Salaam na Pemba. Waliolipwa ni kama wafuatao: Yussuf I. Yussuf 885,000. Haji A. Haji 760,000. Mohammed H. Khamis 360,000. Suleiman M. Rashid 360,000. Aboud H. Mwinyi 3,020,000 na Ali S. Ameir 600,000. **Barua ya uhaulishaji wa fedha yenye kumbukumbu namba BC.182/2023/01/01/04 ya 14/8/2023 imepokelewa benki tarehe 16/8/2023.** | | | |

## OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO PEMBA

### 5.4.1.5 Dosari katika ukodishwaji wa majengo ya Serikali

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba inamiliki majengo mengi ikiwemo majengo ya biashara ambayo inayakodisha kwa mikataba ili kuweza kuingiza mapato Serikalini.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba inayakodisha majengo inayoyamiliki kwa thamani ndogo ikilinganisha na bei halisi ya kodi kwa maeneo husika jambo ambalo linapelekea Serikali kupata mapato madogo ukilinganisha kodi halisi inayotozwa na wamiliki wengine wanaokodisha maduka yao katika maeneo hayo jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato kamilifu, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba kuongeza umakini katika kusimamia ukodijishwaji wa majengo kulingana na bei halisi ya eneo ili kuepusha upotevu wa mapato yatokanayo na ukodishwaji wa majengo hayo. Mchanganuo wa bei za ukodishwaji wa majengo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 39: Ukodishwaji wa majengo kwa bei ndogo**

| Aina ya Jengo | Pahala Lilipo | Muda wa Mkataba | Aliyekodishwa | Kodi halisi kwa mwezi (Tshs) | Kodi halisi kwa mwaka (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| Bekari | Msingini Chake Chake | Mwaka 1 | Moh'd Omar Khamis | 30,000 | 360,000 |
| Mlango wa Duka | Miembeni Chake Chake | Mwaka 1 | Moh'd Omar Khatibu | 15,000 | 180,000 |

### 5.4.1.6 Kukosekana kwa daftari la usajili wa Mikataba

Kanuni ya 47 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba Afisa Muhasibu anatakiwa aweke daftari la mkataba lenye kufanyiwa marekebisho kwa mikataba yote waliyoingia kwa mwaka wa fedha husika.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba kwa miaka tofauti imefunga mikataba mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi lakini mikataba hiyo haijawekewa kumbukumbu katika daftari maalum kama kanuni inavyoelekeza.

Hali hii inaweza kupelekea kupotea kwa kumbukumbu muhimu za miradi au shughuli za Ofisi. Kutokuwepo kwa daftari la kuwekea kumbukumbu za mikataba ni kwenda kinyume na Kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi kuanzisha na kusimamia uwekaji wa daftari maalum la mikataba inayofungwa na Ofisi kwa lengo la kuweka taarifa za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali kupitia ofisi husika. Mchanganuo wa mikataba iliyofungwa kwa vipindi tofauti ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 40: Mikataba ambayo haikurikodiwa katika daftari maalum la Mikataba (Contract Register)

| Aina ya mkataba | Kipindi cha mkataba | Idadi ya miezi | Eneo Lililopo | Kiasi cha Fedha (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Bekari ya Mikate | 01/01/2020-31/12/2020 | 12 | Wete Pemba | 1,200,000 |
| Duka | 01/01/2017-31/12/2021 | 60 | Chake Chake Pemba | 35,000,000 |
| Bekari ya Mikate | 01/01/2022-31/12/2022 | 12 | Msingini Chake Chake | 360,000 |
| Ghala/Duka | 20/12/2016-20/12/2021 | 60 | Misufini Chake Chake | 15,000,000 |
| Bokhari/Matangi ya Mafuta | 02/02/2015-02/02/2025 | 120 | Wesha Chake Chake Pemba | 300,000,000 |
| Kiduka cha mshona Charahani | 01/07/2022-31/06/2023 | 12 | Miembeni Chake Chake Pemba | 180,000 |
| Eneo la wazi (AKB Filling Station) | 13/05/2022-13/04/2023 | 12 | Miembeni Chake Chake Pemba | 360,000 |
| Eneo la Wazi | 01/07/2022-01/07/2023 | 12 | Mkoani | 360,000 |
| Ghala/Duka | 01/11/2019-01/11/2022 | 36 | Miembeni Chake Chake Pemba | 10,800,000 |
| **Jumla** | | | | **363,260,000** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Afisi*

### 5.4.1.7 Utunzaji na Udhibiti wa maduka na majengo ya Bekari usioridhisha

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba inamiliki maduka na majengo ya bekari katika maeneo mbali mbali Pemba. Dosari ilyobainika na ukaguzi ni kuwepo kwa utunzaji na udhibiti usioridhisha wa majengo na maduka hayo kutokana na kutokufanyiwa ukarabati kwa muda mrefu hali iliyopelekea majengo hayo kuchakaa na kupungua thamani, aidha ukaguzi umebaini mikataba ya ukodishwaji wa majengo hayo imemaliza muda wa matumizi jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika hakukuwa na mikataba mipya ya ukodishwaji wa maeneo hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 6 ya ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuyafanyia matengenezo majengo kwa wakati ili kuepusha kuendelea kuchakaa na hatimae kuharibika kabisa. Hali halisi ya baadhi ya majengo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41: Ubovu na uchakavu wa maduka na bekari**

| Aina ya mkataba | Kipindi cha mkataba | Eneo Lililopo | Hali halisi |
|---|---|---|---|
| Bekari ya Mikate | 01/01/2020-31/12/2020 | Wete-Pemba | Jengo haliko katika hali nzuri na mkataba umeisha muda |
| Duka | 01/01/2017-31/12/2021 | Chake Chake Pemba | |
| Bekari ya Mikate | 01/01/2022-31/12/2022 | Msingini Chake Chake Pemba | |
| Ghala/Duka | 20/12/2016-20/12/2021 | Misufini Chake Chake Pemba | |
| Mshona Charahani | 01/7/2022-31/06/2023 | Miembeni Chake Chake Pemba | |
| Eneo la wazi (AKB Filling Station) | 13/5/2022-13/04/2023 | Miembeni Chake Chake Pemba | Eneo liko katika hali nzuri lakini mkataba umeisha muda. |
| Eneo la Wazi | 01/07/2022-01/07/2023 | Mkoani | |
| Ghala/Duka | 01/11/2019-01/11/2022 | Miembeni Chake Chake Pemba | Jengo haliko katika hali nzuri na mkataba umeisha muda |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Mali za Kudumu na Mikataba ya Ukodishwaji*

### 5.4.1.8 Kukosekana kwa hati miliki kwa baadhi ya mali za Afisi

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya Afisi na mashamba jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu mali hizo kutokana na Serikali kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hati miliki mali za Afisi. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42:Mali za Afisi ambazo hazina hati miliki**

| Namba | Aina ya Mali | Mahali Ilipo |
|---|---|---|
| 1 | Kiwanja | Tibirinzi – Chake Chake |
| | | Madungu – Chake Chake |
| | | Kizimbani – Wete |
| 2 | Bekari | Miti-Ulaya – Wete |
| | | Msingini – Chake Chake |
| 3 | Maduka | Miembeni – Chake Chake |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Mali za Kudumu za Ofisi*

### 5.4.1.9 Uwepo wa viwanja visivyoendelezwa kwa muda mrefu

Kifungu nambari 29(1)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa taasisi za Umma atahusika na usimamizi wa mali za taasisi ya Umma".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba inamiliki viwanja mbali mbali kwa muda mrefu sasa lakini viwanja hivyo vimebaki bila ya kuendelezwa jambo ambalo linaweza kupelekea kuhodhiwa na wananchi na hatimae kupelekea uwepo wa migogoro ya ardhi, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu. Hali hii inawezekana kuwa imetokana na Afisi kutokuweka vipaombele katika bajeti kwa ajili ya kuviendeleza viwanja hivyo.

### 5.4.2 FUNGU F 03 - TUME YA MIPANGO ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.4.2.1 Ununuzi wa Mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 102,443,937

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 102,443,937 zimelipwa na Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa mtoa huduma Zanzibar Petroleum Limited kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 78,028,937.08 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petroli na jumla ya shilingi 24,415,000 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Dizeli.

Dosari ilyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Tume pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Mipango kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama Sheria inavyoelekeza.

### 5.4.3 FUNGU F04 - AFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.4.3.1 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 30,490,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 30,490,000 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 43: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---:|---|
| 30/09 ya 29/08/2022 | OCGS Operating Account | 21,940,000 | Malipo ya posho kwa ajili ya kazi mbali mbali. |
| 29/11 ya 09/11/2022 | Business cencus | 765,000 | |
| 30/11 ya 05/11/2022 | | 775,000 | |
| 31/11 ya 11/11/2022 | | 1,150,000 | |
| 32/11 ya 19/10/2022 | | 900,000 | |
| 33/11 ya 11/11/2022 | | 900,000 | |
| 34/11 ya 11/11/2022 | | 200,000 | |
| 35/11 ya 11/11/2022 | | 780,000 | |
| 36/11 ya 09/11/2022 | | 400,000 | |
| 37/11 ya 09/11/2022 | | 200,000 | |
| 16/11 ya 04/11/2022 | | 880,000 | |
| 2/9 ya 10/09/2022 | | 1,400,000 | |
| 37/11 ya 04/11/2022 | | 200,000 | |
| **Jumla** | | **30,490,000** | |

### 5.4.3.2 Kutokufuatwa kwa taratibu na masharti ya Ununuzi wa Dharura shilingi 276,759,000

Kifungu nambari 67 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba Taasisi nunuzi hutakiwa kufanya ununuzi wa njia ya dharura pindipo ikitokea hali ya dharura, Afisa masuuli atazingatia ya kwamba hali hiyo ya dharura inagusa maslahi ya umma na ikiwa muda hautoruhusu kutumika kwa njia za kawaida za ununuzi wa dharura na akimaliza tu anatakiwa kumjuilisha Mlipaji Mkuu (Paymaster General) kwa hatua aliyochukua ikiwa ni pamoja na kueleza sababu iliyopelekea kutotumika kwa njia za kawaida za ununuzi.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umefanya mapitio ya taratibu za ununuzi na kubaini kuwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imefanya malipo ya shilingi 276,759,000 kwa ajili ya kumlipa mtoa huduma Yumzi Restaurant Partneship kutokana na huduma ya chakula aliyoitoa.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuzingatiwa kwa masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 ambacho kinaelezea hali ya uharaka wa utekelezaji wa ununuzi wa dharura.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kuzingatia matakwa ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kwa kuandaa mpango wa manunuzi wa kila mwaka ili kuepuka manunuzi yasiyo ya lazima.

**AFISI YA MTAKWIMU MKUU PEMBA**

### 5.4.3.3 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 483,395,827

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 483,395,827 zimetumika kwa ajili ya malipo mbalimbali ya Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Pemba lakini hati za malipo hayo hazikuweza kupatikana ili kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo pamoja na vielelezo vya matumizi vya hati husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Hali hii imesababishwa na uwepo wa udhibiti wa ndani usioridhisha pamoja na mshika fedha kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya utunzaji wa nyaraka za malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Pemba kuhakikisha hati za malipo pamoja na vielelezo vyake zinatayarishwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 44: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---:|---|
| 1/7 | 000206 | 3,502,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 2/7 | 000207 | 4,140,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 3/7 | T.O | 300,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 4/7 | 000210 | 500,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 6/7 | 000212 | 380,000 | Manager PBZ Chake |
| 7/7 | T.O | 2,476,985 | Khaira Food Supply |
| 8/7 | 000214 | 1,260,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 9/7 | 000215 | 2,250,000 | OCGS Project A/C Pemba |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 10/7 | 000216 | 390,000 | Zanzibar Petroleum LTD |
| 11/7 | 000217 | 4,000,000 | Zanzibar Petroleum LTD |
| 12/7 | 000218 | 3,810,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 13/7 | 000219 | 300,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 14/7 | 000220 | 362,158 | Khaira Food Supply |
| 15/7 | 000221 | 2,530,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 16/7 | 000222 | 2,488,431 | Halim Enterprise |
| 17/7 | 000223 | 380,625 | Bimdogo Amour Suleiman |
| 18/7 | T.O | 32,499 | PBZ – Chake |
| 1/8 | 000224 | 2,000,000 | Zanzibar Petroleum LTD |
| 2/8 | 000225 | 400,000 | Zanzibar Electricity Corporation |
| 3/8 | 000226 | 4,000,000 | Zanzibar Petroleum LTD |
| 4/8 | 000227 | 458,111 | Halim Enterprise |
| 5/8 | 000228 | 9,349 | TRA Zanzibar |
| 6/8 | T.O | 9,540 | ZRA |
| 7/8 | 000229 | 1,533,913 | Tahffif Auto Work |
| 8/8 | 000230 | 31,304 | TRA Zanzibar |
| 9/8 | T.O | 234,783 | ZRB |
| 10/8 | T.O | 558,600 | Youth Company Limited |
| 11/8 | 000231 | 29,400 | TRA |
| 12/8 | T.O | 12,000 | ZRA |
| 13/8 | 000232 | 500,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 14/8 | T.O | 6,300,000 | Mamlaka ya Mafunzo na Amali |
| 15/8 | T.O | 11,970,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 16/8 | 000233 | 120,050 | Nassor Said Nssor |
| 17/8 | 000234 | 2,450 | TRA |
| 18/8 | T.O | 18,375 | ZRA |
| 19/8 | 000235 | 2,347,218 | Halim Enterprise |
| 20/8 | T.O | 48,880 | ZRA |
| 21/8 | 000236 | 47,902 | TRA |
| 22/8 | 000237 | 400,000 | Zanzibar Electricity Corporation |
| 23/8 | 000241 | 145,040,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 24/8 | 000242 | 4,000,000 | Zanzibar Petroleum LTD |
| 25/8 | T.O | 80,000 | Said Othman Bakar |
| 26/8 | T.O | 4,200,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 27/8 | T.O | 280,000 | OCGS Project A/C Pemba |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 28/8 | 000243 | 5,000,000 | Classic Petrol Station |
| 29/8 | 000244 | 1,080,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 30/8 | 000245 | 1,289,817 | Halim Enterprise |
| 31/8 | T.O | 26,323 | TRA |
| 32/8 | T.O | 26,860 | ZRA |
| 33/8 | 000246 | 1,490,000 | Mtambile Petrol Station |
| 34/8 | T.O | 560,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 35/8 | 000247 | 4,000,000 | Classic Petrol Station |
| 36/8 | 000248 | 280,000 | Said Mohammed Said |
| 37/8 | 000249 | 480,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 38/8 | T.O | 1,560,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 39/8 | 000250 | 921,984 | Halim Enterprise |
| 40/8 | T.O | 18,816 | TRA |
| 41/8 | T.O | 19,200 | ZRA |
| 42/8 | 000251 | 4,000,000 | Classic Petrol Station |
| 43/8 | 000252 | 326,536 | Bimdogo Amour Suleimian |
| 44/8 | T.O | 6,800 | ZRA |
| 45/8 | T.O | 6,664 | TRA |
| 46/8 | T.O | 118,099 | PBZ Chake |
| 1/9 | 000253 | 600,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 2/9 | 000254 | 400,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 3/9 | T.O | 46,607 | ZRA |
| 4/9 | T.O | 50,784 | ZRA |
| 5/9 | T.O | 57,941 | ZRA |
| 6/9 | T.O | 116,493 | TRA |
| 7/9 | 000255 | 1,720,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 8/9 | 000256 | 140,000,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 9/9 | 000257 | 500,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 10/9 | 000258 | 100,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 11/9 | 000259 | 1,600,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 12/9 | 000260 | 240,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 13/9 | 000261 | 600,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 14/9 | 000261 | 480,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 15/9 | 000261 | 160,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 16/9 | 000262 | 2,210,880 | Tahfif Auto Work |
| 17/9 | T.O | 45,120 | TRA |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 18/9 | T.O | 338,400 | ZRA |
| 19/9 | 000263 | 573,300 | Fuji Traders |
| 20/9 | T.O | 11,700 | TRA |
| 21/9 | T.O | 87,750 | ZRA |
| 22/9 | 000264 | 840,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 23/9 | 000265 | 240,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 24/9 | 000265 | 840,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 25/9 | 000266 | 300,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 26/9 | 000267 | 6,000,000 | Classic Petrol Station |
| 27/9 | 000268 | 2,401,000 | Halim Enterprise |
| 28/9 | T.O | 50,000 | ZRA |
| 29/9 | T.O | 49,000 | TRA |
| 30/9 | T.O | 2,070,000 | Hospital ya Chake |
| 31/9 | T.O | 103,999 | PBZ Chake |
| 1/10 | 000269 | 1,200,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 2/10 | T.O | 185,000 | Talhia Ibrahim Suleiman |
| 3/10 | 000270 | 1,200,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 4/10 | T.O | 1,365,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 5/10 | T.O | 660,000 | Haroub Ali Massoud |
| 6/10 | 000271 | 500,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 7/10 | T.O | 33,999 | PBZ Chake |
| 1/11 | 000272 | 500,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 2/11 | T.O | 29,999 | PBZ Chake |
| 1/12 | 000273 | 500,000 | OCGS Project A/C Pemba |
| 2/12 | T.O | 29,999 | PBZ Chake |
| 1/1 | T.O | 890,000 | Faida Said Suleiman |
| 2/1 | 000274 | 500,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 3/1 | 000275 | 3,000,000 | Classic Petrol Station |
| 4/1 | T.O | 600,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 5/1 | 000276 | 813,400 | Tahfif Auto Work |
| 6/1 | T.O | 124,500 | ZRA |
| 7/1 | T.O | 16,600 | TRA |
| 8/1 | T.O | 600,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 9/1 | 000277 | 720,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 10/1 | 000278 | 1,000,000 | Classic Petrol Station |
| 11/1 | T.O | 864,360 | Khaira food Supply |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 12/1 | T.O | 18,000 | ZRA |
| 13/1 | T.O | 17,640 | TRA |
| 14/1 | 000279 | 2,722,734 | Nourbai Auto Services |
| 15/1 | T.O | 56,700 | ZRA |
| 16/1 | T.O | 55,565 | TRA |
| 17/1 | T.O | 37,999 | PBZ Chake |
| 1/2 | 000280 | 5,507,500 | Classic Petrol Station |
| 2/2 | 000281 | 500,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 3/2 | 000282 | 960,400 | Halim Enterprises |
| 4/2 | T.O | 20,000 | ZRA |
| 5/2 | T.O | 19,600 | TRA |
| 6/2 | 000283 | 16,840,000 | Classic Petrol Station |
| 7/2 | T.O | 36,400 | PBZ Chake |
| 1/3 | 000284 | 3,680,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 2/3 | 000285 | 10,880,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 3/3 | 000286 | 500,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 4/3 | 000287 | 200,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 5/3 | T.O | 600,000 | Kiwanda cha Mkonyo Pemba |
| 6/3 | 000288 | 2,881,200 | Khaira food supply and Catering |
| 7/3 | T.0 | 60,000 | ZRA |
| 8/3 | T.0 | 58,800 | TRA |
| 9/3 | 000289 | 113,039 | Pandu Book Shop |
| 10/3 | T.0 | 2,354 | ZRA |
| 11/3 | T.0 | 2,307 | TRA |
| 12/3 | 000290 | 525,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 13/3 | 000291 | 1,200,000 | Classic Petrol Station |
| 14/3 | T.0 | 150,000 | O/Rais Fedha na Mipango |
| 15/3 | 000292 | 717,300 | Classic Petrol Station |
| 16/3 | T.O | 300,000 | Manager PBZ Chake |
| 17/3 | 000293 | 2,560,426 | Ngoto Auto Accessories |
| 18/3 | T.O | 53,320 | ZRA |
| 19/3 | T.O | 52,254 | TRA |
| 20/3 | T.O | 52,380 | PBZ Chake |
| 1/4 | 000294 | 4,060,000 | Classic Petrol Station |
| 2/4 | 000295 | 2,400,000 | Classic Petrol Station |
| 3/4 | 000296 | 500,000 | OCGS Project Account Pemba |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 4/4 | 000297 | 480,000 | Manager PBZ Chake |
| 5/4 | T.O | 480,000 | Manager PBZ Chake |
| 6/4 | 000298 | 333,200 | Tahfif Auto Work |
| 7/4 | T.O | 60,000 | ZRA |
| 8/4 | T.O | 6,800 | TRA |
| 9/4 | T.O | 200,000 | O/Rais Fedha na Mipango |
| 10/4 | 000299 | 60,000 | Classic Petrol Station |
| 11/4 | T.O | 600,000 | Manager PBZ Chake |
| 12/4 | T.O | 40,400 | PBZ Chake |
| 1/5 | 000300 | 500,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 2/5 | T.O | 700,000 | Manager PBZ Chake |
| 3/5 | 000301 | 92,198 | Halim Enterprises |
| 4/5 | T.O | 1,920 | ZRA |
| 5/5 | T.O | 1,882 | TRA |
| 6/5 | 000302 | 422,576 | Classic Petrol Station |
| 7/5 | T.O | 8,800 | Manager PBZ Chake |
| 8/5 | T.O | 8,624 | Manager PBZ Chake |
| 9/5 | 000303 | 60,000 | Classic Petrol Station |
| 10/5 | T.O | 2,915,000 | Manager PBZ Chake |
| 11/5 | T.O | 1,650,000 | Manager PBZ Chake |
| 12/5 | 000304 | 100,000 | Classic Petrol Station |
| 13/5 | 000305 | 115,248 | Nafhat Salim Yahya |
| 14/5 | T.O | 2,400 | ZRA |
| 15/5 | T.O | 2,352 | TRA |
| 16/5 | T.O | 48,906 | PBZ Chake |
| 1/6 | 000306 | 1,500,000 | Classic Petrol Station |
| 2/6 | T.O | 240,000 | Manager PBZ Chake |
| 3/6 | 000307 | 500,000 | OCGS Project Account Pemba |
| 4/6 | 000308 | 720,300 | Moza Mohammed Ali |
| 5/6 | T.O | 15,000 | ZRA |
| 6/6 | T.O | 14,700 | TRA |
| 7/6 | T.O | 37,400 | PBZ Chake |
| **Jumla** | | **483,395,827** | |

*Chanzo: Daftari la fedha taslimu la hesabu ya matumizi ya kawaida.*

#### 5.4.3.4 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 3,165,000

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 3,165,000 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Pemba lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa katika hati husika za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka halali za malipo kwa wakati ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katka jadweli hapo chni: -

**Jadweli Nambari 45: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilichotumika (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 9/10 ya 12/10/2022 | T.O | 300,000 | Wafanyakazi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba. | Malipo ya huduma ya likizo |
| 2/11 ya 21/11/2022 | T.O | 1,250,000 | Mtakwimu Mkuu Pemba | Malipo ya posho ya safari kikazi |
| 3/1 ya 17/01/2023 | T.T | 840,000 | | |
| 12/10 ya 17/10/2022 | T.O | 775,000 | | |
| **Jumla** | | **3,165,000** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo.*

### 5.4.4 FUNGU F05 - OFISI YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**IDARA YA HAZINA NDOGO PEMBA**

#### 5.4.4.1 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 7,896,408

Kwa mujibu wa barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar ya tarehe 12/08/2022 yenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 inazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Idara Ndogo ya Hazina Pemba imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 7,896,408 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Idara kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 46: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 25/8 ya 9/8/2022 | 28560 | 3,097,290 | Malinge Enterptises | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 03/09 ya 02/09/2022 | 29173 | 216,090 | Capital Technology Center | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mihuri. |
| 09/09 ya 08/09/2022 | 29243 | 300,605 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 15/09 ya 12/09/2022 | 29283 | 268,912 | Massoud General Supply | Malipo kwa ununuzi wa vifaa vya vespa. |
| 31/10 ya 24/10/2022 | 30525 | 3,149,151 | Malinge Enterptises | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 42/11 ya 24/11/2022 | 31305 | 864,360 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa printa. |
| **Jumla** | | **7,896,408** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.4.5 FUNGU F06 - OFISI YA MKAGUZI MKUU WA NDANI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**OFISI YA MKAGUZI MKUU WA NDANI PEMBA**

#### 5.4.5.1 Kutokuwepo kwa mpango kazi wa Afisi

Kifungu nambari 32(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaelezea kwamba "Katika kutekeleza majukumu yaliolezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Afisa Mhasibu ataandaa mkakati na mapitio ya matumizi kwa kutayarisha mpango mkakati na uendeshaji kwa ajili ya kusaidia mahitaji ya fedha".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa mpango kazi wa Idara ya Mkaguzi wa Ndani Pemba (Action Plan) jambo ambalo linapelekea kutekeleza majukumu bila ya kuwa na vigezo vya kuvifuata (plan), aidha ni kwenda kinyume na Kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Idara kufuata Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kutayarisha mpango kazi ili kuweza kutekeleza majukumu ya Idara kwa mafanikio makubwa.

#### 5.4.5.2 Kutokuwepo kwa mpango wa manunuzi wa mwaka (Annual Procurement Plan)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa mpango wa manunuzi wa mwaka wa Idara ya Mkaguzi wa Ndani Pemba jambo ambalo linapelekea kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma bila kuwa na mpangilio maalum, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, pamoja na kifungu nambari 46 (1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Idara kutayarisha mpango wa manunuzi ambao utaiwezesha Idara kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia miongozo ya kisheria.

#### 5.4.5.3 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 33,165,593.4

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 33,165,593.4 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Idara ya Mkaguzi wa Ndani Pemba lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 47: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

| Hati nambari | Hundi nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/4 ya 24/4/2023 | 24042318 | 457,627 | ZRA | Malipo ya kodi. |
| 3/4 ya 17/4/2023 | 34746 | 3,000,000 | PBZ | Malipo ya posho mbalimbali. |
| 17/3 ya 24/3/2023 | 34116 | 1,505,000 | | |
| 3/3 ya 17/3/2023 | 33843 | 4,700,000 | | |
| 4/4 ya 24/4/2023 | 35009 | 3,240,000 | | |
| 2/3 ya 9/3/2023 | 33751 | 500,000 | ZECO | Malipo ya ununuzi wa umeme. |
| 2/2 ya 16/2/2023 | 33017 | 1,675,000 | Idara ya Mkaguzi wa Ndani Pemba | Malipo ya posho ya safari. |
| 06/01 ya 22/01/2023 | 26012332 | 513,708 | ZHELB | Malipo ya mkato wa ZHELB |
| 11/01 ya 27/01/2023 | 32831 | 980,000 | Idara ya Mkaguzi wa Ndani Pemba | Malipo ya posho mbali mbali. |
| 15/01 ya 10/01/2023 | 32258 | 2,750,000 | | |
| 1/5 ya 05/05/2023 | 35131 | 3,315,000 | | |
| 05/05 ya 18/5/2023 | 35386 | 3,530,000 | | |
| 22/05 ya 25/05/2023 | 35616 | 400,000 | Samail College | Malipo ya kodi ya Ukumbi |
| 01/06 ya 06/06/2023 | 35934 | 1,485,000 | Idara ya Mkaguzi wa Ndani Pemba | Malipo ya posho mbali mbali. |
| 02/06 ya 9/06/2023 | 36030 | 2,081,000 | | |
| 21/06 ya 23/06/2023 | -- | 2,746,000 | | |
| 22/06 ya 23/6/2023 | 70109505 | 142,178.4 | | Malipo ya kodi ya zuio |
| 23/06 ya 23/06/2023 | 300623168 | 145,080 | | |
| **Jumla** | | **33,165,593.4** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

## 5.5 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

### 5.5.1 FUNGU G 01 - OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 5.5.1.1 Kukosekana kwa mikataba ya udhamini wa mafunzo kwa watumishi shilingi 67,500,000

Kanuni nambari 76(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 kinaeleza "Mtumishi wa umma aliyepata ruhusa ya kujiunga na masomo atalazimika kufunga mkataba na Taasisi yake.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imewadhamini watumishi 39 wanaosoma Programu ya IPA-UDOM katika ngazi mbalimbali zinazotolewa katika Programu hiyo. Kati ya watumishi hao, watumishi 18 walibainika kuwa na dosari ya kutokupatikanwa kwa mikataba ya udhamini wa mafunzo wanayoendelea nayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unafunga mikataba ya mafunzo na watumishi wanaowadhamini kwenda masomoni kama kanuni inavyoelekeza. Orodha ya Watumishi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 48: Malipo ya baadhi ya watumishi waliodhaminiwa IPA-UDOM**

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 16/5 ya 2/5/2023 | Hassan J Issa | 2,500,000 | Malipo kwa ajili ya utafiti kwa watumishi wanaodhaminiwa na Serikali kupitia mashirikiano ya IPA-UDOM |
| 2. | 18/5 ya 2/5/2023 | Muhsin Juma Ali | 2,500,000 | |
| 3. | 19/5 ya 2/5/2023 | Ismail Faki Khamis | 2,500,000 | |
| 4. | 21/5 ya 2/5/2023 | Rahillat Paul Bakilana | 2,500,000 | |
| 5. | 23/5 ya 2/5/2023 | Abdalla Omar | 2,500,000 | |
| 6. | 24/5 ya 2/5/2023 | Saada Ab Seif | 2,500,000 | |
| 7. | 27/5 ya 5/5/2023 | Khadija Salum Khamis | 2,500,000 | |
| 8. | 28/5 ya 5/5/2023 | Fauzia S Suleiman | 2,500,000 | |
| 9. | 32/5 ya 5/5/2023 | Shamsia M. Mohammed | 5,000,000 | |
| 10. | 55/5 ya 6/5/2023 | Patima Kh Mussa | 5,000,000 | |
| 11. | 58/5 ya 8/5/2023 | Abdalla J Ramadhani | 5,000,000 | |
| 12. | 59/5 ya 8/5/2023 | Abubakar A Nuhu | 5,000,000 | |
| 13. | 65/5 ya 8/5/2023 | Mzee J Haji | 5,000,000 | |
| 14. | 66/5 ya 8/5/2023 | Zuweina H. Suleiman | 5,000,000 | |
| 15. | 67/5 ya 8/5/2023 | Juma H Juma | 5,000,000 | |
| 16. | 68/5 ya 8/5/2023 | Hindi K Khamis | 5,000,000 | |
| 17. | 90/5 ya 8/5/2023 | Khamis J Khamis | 5,000,000 | |
| 18. | 106/5 ya 14/5/2023 | Machano J Machano | 2,500,000 | |
| **Jumla** | | | **67,500,000** | |

## 5.5.2 FUNGU G 02 - MAHKAMA KUU

Ukaguzi wa hesabu za Mahkama Kuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.5.2.1 Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa mfumo wa Usikilizaji kesi pamoja na Ujenzi wa Mahkama za Mikoa

Kifungu nambari 96(1) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya 2011 kinaeleza "Waziri atalazimika:(a) kuendeleza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika taasisi na kudumisha ufanisi wa ndani wa utendaji na usimamizi wa uendeshaji; na kuanzisha mfumo ambao utatumika kwa ajili ya kuwezesha na kuratibu maendeleo na kukuza shughuli za utoaji huduma kwa njia ya elektroniki na kuhakikisha huduma hizo zinawafikia wananchi ambao hawana huduma za elektroniki, (2) Waziri anaweza kukasimu madaraka ya kazi zake kama yalivyoelezwa katika kifungu kidogo (4) Kiongozi wa Taasisi atalazimika kwa kuzingatia utaratibu ulioelezwa chini ya kijifungu cha (1)(a)(i)(ii) cha kifungu hiki".

Aidha, kifungu nambari 45(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha ya 2016 kinaeleza "Matumizi ya maendeleo yatatolewa katika bajeti kuu ya Serikali kwa namna ya mpango wa Serikali wa uwekezaji kwa miaka mbali mbali" na kifungu nambari 45(2) kinaeleza mipango na miradi itakayotekelezwa na taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali, kutokana na kanuni na taratibu zilizoainishwa katika kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii, itajumuishwa katika mpango wa Serikali wa uwekezaji na mpango wa sekta wa kipindi cha muda wa kati wa taasisi inayohusika na bajeti

Mahkama Kuu iliandaa Concept Note Februari, 2022 kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa kisasa wa kuendesha kesi kwa kutumia njia ya elektroniki "Case Management system" wenye thamani ya shilingi 2,158,900,000 ambapo mfumo huo ulitarajiwa kuanza Julai, 2022 hadi Juni, 2024 utakapokamilika kwa mujibu wa Medium-Term Development Plan.

Ukaguzi umebaini mradi umeanzishwa kwa hatua za awali katika mwaka 2022/2023 ambapo Mahkama Kuu ilipanga kutumia jumla ya shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kuimarisha mfumo huo na shilingi 5,500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Mahkama za Mikoa.

Katika ufuatiliaji uliofanywa na ukaguzi juu ya kupima ufanisi wa malengo yaliowekwa imebainika kujitokeza kwa dosari ya kutokupatikanwa kwa fedha kwa wakati ili kuweza kutekeleza malengo waliojipangia jambo ambalo linathiri utekelezaji wa mipango ya baadae ya Mahkama.

Ukaguzi unaishauri Ofis ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inatoa kipaombele cha upatikanaji wa fedha ili kuweza kutekeleza miradi yenye nia ya kubadili mtazamo wa Mahkama na kuwa Mahkama za kileo.

**MAHKAMA KUU PEMBA**

### 5.5.2.2 Kutokuondolewa au kufanyiwa matengenezo kwa gari chakavu

Kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinazitaka Taasisi zote za Umma kuandaa Mpango wa Matengenezo ya Mali ili kuhakikisha kwamba mali zote za Taasisi zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa na pia Taasisi itenge fedha katika bajeti zake kwa ajili ya utekelezaji bora wa mpango wa matengenezo wa mwaka. Aidha, kifungu nambari 69(1)(2) kinaeleza kwamba "Kutakuwa na Mpango wa Uondoaji wa Mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya Umma na kuwasilishwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Ofisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mahkama Kuu Pemba inamiliki mali za aina mbali mbali zikiwemo gari ambapo baadhi ya gari hizo hazitumiki, zimetelekezwa na hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu na pia hazijaombewa ruhusa ya kuziondoa kutoka Mamlaka husika jambo ambalo linaweza kupelekea gari hizo kushuka thamani na hatimae kutia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria nilivyovinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahkama Kuu Pemba kutayarisha mpango rasmi wa matengenezo wa magari pamoja na kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao za kila mwaka. Mchanganuo wa gari chakavu ambazo hazijafanyiwa matengenezo au kuondolewa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 49: Gari ambazo hazijafanyiwa matengenezo wala kuondolewa kwa muda mrefu

| Namba | Aina ya Gari | Nambari ya Usajili | Idadi ya Miaka | Mahala Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Prado Land Cruser | SMZ 259A | 2 | Gereji ya Tahfif Ole Kianga |
| 2. | Hyundai | SMZ 314A | 1 | Mahkama Kuu Chake Chake |

*Chanzo:Uchambuzi wa Taarifa za mali za kudumu*

### 5.5.2.3 Kukosekana kwa Nyaraka za umiliki wa Mali za Kudumu

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Ukaguzi umebaini kwamba Mahkama Kuu Pemba inamiliki mali za aina mbali mbali yakiwemo majengo ya ofisi, nyumba za kuishi watumishi pamoja na kiwanja bila ya kuwa na nyaraka za umiliki wa mali hizo, jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uwezekano wa kutokea migogoro baina ya Mahkama na wananchi pamoja na kupelekea upotevu wa mali hizo. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahkama Kuu Pemba kuhakikisha kwamba unachukua jitihada za makusudi za upatikanaji wa nyaraka za mali zote inazozimiliki. Mchanganuo wa Mali hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 50:Mali za kudumu ambazo zimekosa nyaraka za umiliki

| Namba | Aina ya Mali | Mahali Ilipo |
|---|---|---|
| 1. | Jengo la Mahkama Kuu Chake Chake | Kichungwani Chake Chake |
| 2. | Jengo la Mahkama ya Wete | Laini Wete |
| 3. | Jengo la Mahkama ya Konde | Konde |
| 4. | Jengo la Mahkama ya mwanzo Kengeja | Kengeja |
| 5. | Kiwanja | Mkoani |
| 6. | | Konde |
| 7. | | Wete |
| 8. | | Chake Chake |

#### 5.5.2.4 Kutokuwepo kwa kadi za usajili wa vyombo vya moto

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

Ukaguzi umebaini kuwa vyombo vya moto vinavyomilikiwa na Mahkama Kuu Pemba zikiwemo gari na vespa havina kadi za usajili jambo ambalo linaweza kupelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki wake, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahkama Kuu Pemba kuhakikisha kwamba unachukua jitihada za makusudi zitakazohakikisha upatikanaji wa kadi za umiliki kwa mali zote za kudumu inazozimiliki ikiwemo vyombo vya moto. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 51: Vyombo vya Moto Ambavyo Havina Kadi za Usajili**

| Namba | Aina ya Chombo | | Nambari ya Usajili | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Gari | Prado Land-Cruiser Tx New | SMZ 560A | Kukosekana kwa kadi ya umiliki wa chombo kwa ajili ya ukaguzi |
| 2. | | Prado Land-Cruiser Txl New | SMZ 259A | |
| 3. | | Prado Land- Cruiser | SMZ 1094 | |
| 4. | | Alphard | SMZ 386A | |
| 5. | | Hyundai | SMZ 314A | |
| 6. | | Toyota Surf | SMZ 224A | |
| 7. | Vespa | Bajaj | SMZ 1917C | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Mali za Kudumu*

### 5.5.3 FUNGU G 03 – AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Ukaguzi wa hesabu za Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.5.3.1 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 10,091,240

Kwa mujibu wa barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar la tarehe 12/08/2022 lenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 inazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Afisi ya Mwanasheria Mkuu imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 10,091,240 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 52: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 04/12 ya 23/11/2022 | Quality Traders | 8,171,240 | Ununuzi wa stationary |
| 2. | 51/03 ya 22/03/2023 | Zeynab Take Away | 1,920,000 | Malipo ya ununuzi wa chakula |
| **Jumla** | | | **10,091,240** | |

### 5.5.3.2 Malipo nje ya Mpango wa manunuzi shilingi 137,641,086

Kwa kuzingatia kifungu namba 42(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kitaandaa na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali mpango wake wa mwaka wa ununuzi na uondoshaji kwa mwaka unaofata".

Kifungu namba 42(4) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali kila baada ya miezi mitatu na kwa namna yote itakayojitokeza itafanya mapitio na kuboresha mpango wa ununuzi na uondoshaji mali" na Kifungu namba 42(7) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa manunuzi na uondoshaji wa mali za umma isipokuwa kwa hali ya haraka na dharura.

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha unaoishishia tarehe 30 Juni, 2023 Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 137,641,086 kwa kuwalipa watoa huduma kwa ajili ununuzi wa bidhaa mbalimbali dosari iliyobainika ni kufanyika kwa malipo hayo nje ya mpango wa manunuzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kuathiri matumizi yaliyopangwa kwa mujibu wa mpango wa manunuzi wa mwaka na kushindwa kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na Taasisi kwa mwaka husika aidha ni kwenda kinyume na vifungu vya sheria vilivyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhakikisha kuwa maununuzi yote yanayofanywa kufuata utaratibu kama ulivyoelezwa katika Sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 53: Malipo nje ya Mpango wa manunuzi**

| Namba | Maelezo | Thamani (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Consultancy fee | 58,900,000.00 |
| 2. | Motorcycle(Click) | 44,375,999.00 |
| 3. | Refrigerator | 34,365,087.00 |
| **Jumla** | | **137,641,086** |

### AFISI YA MWANASHERIA MKUU PEMBA

### 5.5.3.3 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 3,818,180

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 3,818,180 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama zinavyoonekana katka jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 54: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 56/10 ya 20/10/2022 | 50109226 | 500,000 | Zanzibar Petrolium Limited | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa petrol lita 167.8 |
| 22/5 ya 8/5/2023 | 50137379 | 500,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa petrol lita 179.9 |
| 6/2 ya 1/2/2023 | 50121064 | 500,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa petrol lita 167.8 |
| 132/6 ya 21/6/2023 | 50148764 | 1,818,180 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa petrol lita 666 |
| 31/6 ya 9/6/2023 | 50145049 | 500,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa petrol lita 179.9 |
| **Jumla** | | **3,818,180** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo.*

### 5.5.3.4 Kukosekana kwa hati za malipo za ununuzi wa mafuta

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa ununuzi wa mafuta lita 277.4 ambazo zimeingizwa katika daftari la ghalani la Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Pemba. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo pamoja na vielelezo vya ununuzi wa mafuta hayo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Hali hii imesababishwa na uwepo wa udhibiti wa ndani usioridhisha pamoja na mshika fedha kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya utunzaji wa nyaraka za malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Pemba kuhakikisha hati za malipo pamoja na vielelezo vyake zinatayarishwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria kanuni na miongozo iliyopo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 55: Mafuta yaliyonunuliwa ambayo hati za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi**

| Tarehe | Aliyelipwa | Lita za Mafuta |
|---|---|---|
| 17/10/2022 | Zanzibar Petroleum LTD | 94.3 |
| 21/6/2023 | | 183.1 |
| **Jumla ya lita zilizonunuliwa** | | **277.4** |

*Chanzo: Daftari la kurikodia bidhaa za ghalani*

### 5.5.3.5 Mafuta ambayo hayakurikodiwa katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani shilingi 500,000

Kanuni nambari 113 ya kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaelezea kwamba "Bidhaa zote zinazonunuliwa zipokelewe katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani na zitolewe kwa mujibu wa matumzi ya bidhaa hizo".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 500,000 zimelipwa kupitia hati nambari 6/2 ya tarehe 1/2/2023 iliyolipwa kwa hundi nambari 50121064 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta lita 167.8 lakini mafuta hayo hayakurikodiwa kwenye daftari la kurikodia bidhaa za ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya utekelezaji na usimamizi wa masuala ya fedha na rasilimali za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kwamba bidhaa zote zinazonunuliwa zirikodiwe na zitolewe kwa mujibu wa utaratibu wa sheria uliopo.

### 5.5.4 KITUO CHA MAFUNZO YA SHERIA NA UTAFITI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.5.4.1 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 13,847,012

Kwa mujibu wa mwongozo kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ya tarehe 12/08/2022 yenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 unazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar kimefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 13,847,012 kwa wafanyabiashara mbalimbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 56: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Hati Namba | Kiasi (Tsh.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---:|---|---|
| --/5 ya 12/05/2023 | 412,580 | Ali Suleiman Food Stuff | Ununuzi wa vifaa |
| 04/10 ya 07/10/2022 | 4,714,000 | ZLRC | Malipo ya chakula na viburudishaji |
| 16/10 ya 24/10/2022 | 2,016,840 | Sashi Catering | |
| 07/12 ya 27/12/2022 | 1,152,480 | Ram Catering | |
| 09/12 ya 21/12/2022 | 5,551,112 | Swisan Enterprises Ltd | Malipo kwa ununuzi wa printer na desktop |
| **Jumla** | **13,847,012** | | |

### 5.5.4.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 26,066,916

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 26,066,916 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar lakini baadhi ya vielelezo hivyo havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Kituo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuthibitisha uhalali wa malipo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 57: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani ya Fedha (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 08/06 ya 20/06/2023 | Black Roots Investiment | 576,240 | Malipo ya kikundi cha maigizo |
| 10/06 ya 21/06/2023 | Pandu Ameir Kificho | 21,724,200 | Malipo ya jengo Jan -Dec 23 |
| 12/06 ya 22/06/2023 | Spicy Restaurant | 1,212,596 | Malipo ya chakula |
| 02/10 ya 04/10/2022 | Zanzibar Quality Tailoring Ltd | 1,401,400 | Malipo ya majoho 13 |
| 07/12 ya 27/12/2022 | Ram Catering | 1,152,480 | Malipo ya chakula |
| **Jumla** | | **26,066,916** | |

### 5.5.5 FUNGU G 05 – TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.5.5.1 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 8,643,453

Kwa mujibu wa mwongozo kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar wa tarehe 12/08/2022 lenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 unazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 8,643,453 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 58: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Hati namba | Aliyelipwa | Thamani (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 12/07ya 12/06/2022 | Sami Enterprises | 6,300,077 | Kufanya Ukarabati wa Jengo |
| 13/02 ya 06/02/2023 | | 2,343,376 | |
| **Jumla** | | **8,643,453** | |

### 5.5.6 FUNGU G15 - TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.5.6.1 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 27,093,086

Kwa mujibu wa barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ya tarehe 12/08/2022 yenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 inazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 27,093,086 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 59: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Hati namba | Thamani (Tsh) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---:|---|---|
| 02/03 ya 06/03/2023 | 1,863,920 | Amani garage | Malipo ya matengenezo ya gari |
| 02/03 ya 31/01/2023 | 1,777,452 | Ram Catering | Malipo kwa ajili ya chakula |
| 32/04 ya 05/05/2023 | 1,441,176 | Ram Catering | |
| 15/11 ya 28/11/2022 | 8,700,000 | Wakala wa SMZ | Ununuzi wa fomu za tamko |
| 18/11 ya 28/11/2022 | 4,957,648 | Double Two General | Ununuzi wa Shajala |
| 12/05 ya 15/12/2022 | 1,556,470 | Zonga Decoration | Upambaji wa ukumbi |
| 12/06 ya 15/12/2022 | 5,643,478 | Wellorth hotel sand | |
| 51/06 ya 24/06/2023 | 1,152,942 | Ram Catering | Ununuzi wa chakula |
| **Jumla** | **27,093,086** | | |

### 5.5.6.2 Miradi iliyochelewa kukamilika shilingi 65,339,837.50

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilisaini hati ya makubaliano yenye kumbukumbu nambari ZAPLEC/GOZ/CW 1/20222023/01 ya tarehe 3/4/2023 kwa thamani ya shilingi 65,339,837.50 na mtoa huduma M/s Zanzibar Building Agency kwa ajili ya mradi wa ukarabati wa Afisi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Chake Chake Pemba

Ukaguzi umefanya mapitio ya mkataba wa makubaliano ya ukarabati wa jengo hilo na kubaini ya kwamba mkataba huo ulisainiwa tarehe 3/4/2023 ambapo ulitarajiwa kukamilika tarehe 3/7/2023. Pamoja na makubaliano hayo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

- Kuchelewa kuanza kwa mradi kwa mujibu wa Mpango kazi ambapo mradi huo ulipangwa kuanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 badala yake ulitekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.
- Kwa mujibu wa mkataba mkandarasi alitakiwa kuanza kazi tarehe 3/4/2023 hadi tarehe 8/5/2023 Mshauri elekezi alitoa barua kumtaarifu mkandarasi ya kwamba amechelewa kuanza kazi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wao.
- Kutokana na kitendo cha kuchelewa kuanza kazi mkandarasi aliomba kupewa muda wa nyongeza wa miezi miwili (2) ya utekelezaji wa mradi huo na kuahidi kuukamilisha tarehe 3/09/2023, ombi hilo aliliwasilisha Afisi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa barua ya tarehe 28/6/2023 ambapo hadi ukaguzi unakamilika haukupatiwa majibu ya kukubaliwa au kukataliwa ombi alilowasilisha mkandarasi.

Kutokana na kitendo cha mkandarasi kuchelewa kuanza utekelezaji wa mradi kinaweza kupelekea matumizi ya gharama za ziada kunakotokana na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kuhakikisha kwa mara ijayo itakapotekeleza mradi wa maendeleo ni vyema kuweka kipengele katika rasimu ya mkataba cha tozo ya adhabu na fidia (liquidated damage) kutokana na ucheleweshwaji wa kukabidhiwa kazi kwa wakati. Mchanganuo wa malipo ambayo yameshalipwa kwa Mkadharasi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 60: Malipo yaliyofanywa kwa Mkandarasi na Mshauri Elekezi

| Tarehe | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 16/4 ya 12/4/2023 | Wakala wa Majengo Miradi Pemba | 9,800,976 | Malipo ya Ukarabati wa Jengo |
| 10/6 ya 07/03/2023 | | 12,087,870 | |
| 53/6 ya 24/06/2023 | | 19,204,260 | |
| 20/6 ya 19/06/2023 | Shirika la Nyumba Mapato | 2,286,894 | |
| **Jumla** | | **43,380,000** | |

**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA PEMBA**

### 5.5.6.3 Malipo yenye vielelezo Pungufu shilingi 32,226,404

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu.

Ukaguzi umebaini kwamba Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Pemba imetumia jumla ya shilingi 32,226,404 kwa ajili ya matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma kwenye shughuli mbalimbali za Tume ya Maadili ya Viongozi Pemba, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Kutokuambatishwa kwa baadhi ya vielelezo kwenye hati ya malipo kunaweza kuwa kumetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi Pemba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi Pemba kuambatanisha vielelezo vyote husika katika hati za malipo mara tu baada ya malipo kukamilika. Mchanganuo wa hati za malipo ambazo hazikukamilika vielelezo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 61: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

| Hati nambari | Hundi nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 37/10 ya 26/10/2022 | TT | 598,000 | Chake Petrol Station | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel lita 200. |
| 39/10 ya 26/10/2022 | TT | 336,274 | Gombani Garage Corporation | Malipo kwa ajili ya services ya gari SMZ 407B. |
| 10/6 ya 7/6/2023 | T T | 12,087,870 | Wakala wa majengo mradi Pemba | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya jengo la Afisi. |
| 53/6 ya 24/6/2023 | TT | 19,204,260 | Wakala wa majengo mradi Pemba | |
| **Jumla** | | **32,226,404** | | |

*Chanzo: Hati za Malipo*

### 5.5.6.4 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani shilingi 5,356,710

Kanuni nambari 113 ya kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaelezea kwamba "Bidhaa zote zinazonunuliwa zipokelewe katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani na zitolewe kwa mujibu wa matumzi ya bidhaa hizo".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 5,356,710 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa kwenye daftari la kurikodia bidhaa za ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Pemba kuhakikisha bidhaa zote zinazonunuliwa zinarikodiwa kwenye vitabu maalum vya kuwekea kumbukumbu za ghalani mara tu baada ya taratibu za manunuzi kukamilika kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyopo. Mchanganuo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 62: Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la Ghalani

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 4/9 ya 12/9/2022 | TT | 1,117,500 | Chake Chake Petrol Station | Ununuzi wa diesel lita 200 kwa matumizi ya Afisi. |
| 6/1 ya 19/1/2023 | | 834,210 | | Ununuzi wa mafuta lita 200 diesel kwa matumizi ya Afisi. |
| 3/1 ya 5/1/2023 | | 3,405,000 | Khamis Yussuf Hamad | Ununuzi wa vifaa vya samani za Afisi. |
| **Jumla** | | **5,356,710** | | |

### 5.5.6.5 Dosari katika matumizi ya Mafuta lita 2,410.7

Kanuni nambari 124(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014, kinamtaka Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kuhakikisha vyombo vyote vilivyomo katika Taasisi yake vinakuwa na buku linaloonyesha matumizi ya safari ya chombo hicho.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa gari nambari SMZ 407B ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Pemba imetumia jumla ya lita 2,410.7 za mafuta, dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa kumbukumbu za safari za gari hiyo zilizofanyika kutokana na kutokuwepo kwa buku linaloonyesha mwenendo wa safari, jambo ambalo linapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Pemba kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kuyatumia mafuta yanayonunuliwa kwa kuzingatia utaratibu wa kisheria.

## 5.5.7 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA PEMBA

### 5.5.7.1 Kutokuwepo kwa kadi za usajili wa vyombo vya moto

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa Vespa aina ya Star iliyopo Wete yenye nambari SMZ 6925 inayomilikiwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba ambayo haina kadi ya usajili jambo ambalo linaweza kupelekea kutokuthibitika kwa uhalali wa umiliki wake jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba kuhakikisha vyombo vyote vya moto vinapatiwa kadi za usajili.

### 5.5.7.2 Kukosekana kwa hati miliki kwa baadhi ya mali za Afisi

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya Afisi na mashamba jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hati miliki mali zote za kudumu za Kamisheni. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 63: Majengo ya Afisi ambayo hayana hati miliki

| Namba | Nambari ya Nyumba | Jina la Mkodishwaji | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|
| 1. | WH.1 | Juma Mohammed Said | Misufini Chake Chake |
| 2. | WH.2 | Suleiman Salum Issa | |
| | | Khalef Kassim Hamed | |
| | | Moh'd Salum Issa | |
| | | Issa Abdalla Issa | |
| | | Rashid Gharib Ali | Miembeni Chake Chake |
| | | Yakoub Ali Mohammed | |
| | | Nassor Mohammed Dadi | |
| | | Mzee Ali Abdalla | |
| | | Abdalla Ali Masoud | |
| | | Juma Faki Khatib | |
| | | Ahmed Abdalla Issa | |
| | | Masoud Omar Juma | |
| | | Zahor Saleh Ali | |
| | | Ali Muradi Dilshad | |
| | | Mohammed Hassan Khamis | |
| 3. | WH.3 | Humoud Mohammed Humoud | |
| | | Hassan Abdalla Nuhu | |
| 4. | WH.4 | Ali Said Ali | Misufini Chake Chake |
| | | Kassim Juma Mussa | |
| | | Said Ame Said | |
| 5. | WH.5 | Ashraf Ikbal Ibrahim | Miembeni Chake Chake |
| | | Salum Mbaraka Salum | |
| | | Alkhalil Omar Kombo | Sokoni Chake Chake |
| | | Seif Mbaraka Salim | |
| 6. | WH.7 | Saleh Nassor Suleiman | Kipangani Wete |
| | Block No.2 | Raya Khamis Hamad | Mtemani Wete |
| | | Mussa Salim Bajaka | |
| 7. | WH.9 | Mwanaisha Ali Salim | Selem Wete |
| | WH.6 | Khamis Yussuf Hahad | Mkungu Malofa |
| | | Khamis Juma Ali | |
| | | Juma Khamis Juma | |
| | | Idrissa Khamis Sabour | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Kamisheni*

### 5.5.8 SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Skuli ya Sheria Zanzibar umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.5.8.1 Malimbikizo ya Madeni inayodaiwa shilingi 19,493,871.40

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Skuli ya Sheria inadaiwa jumla ya shilingi 19,493,871.40 zinazotokana na kupatiwa huduma kutoka kwa watoa huduma mbalimbali, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Skuli ya Sheria katika kuyalipa madeni hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Skuli ya Sheria kuhakikisha inatoa kipaumbele katika kufanya malipo ya madeni yanayodaiwa kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 64: Orodha ya madeni yanayodaiwa Skuli ya Sheria**

| Namba | Jina | Thamani (Shs) |
|---|---|---|
| **Madeni ya Watoa Huduma** | | |
| 1. | Tanzania Std Newspaper | 653,871.40 |
| | **Jumla ndogo (A)** | **653,871.40** |
| **Madeni ya Taasisi za Serikali** | | |
| 2. | Wakala wa Majengo | 17,000,000 |
| 3. | Wakala wa Uchapaji | 1,840,000 |
| | **Jumla ndogo (B)** | **18,840,000** |
| | **Jumla kuu (A+B)** | **19,493,871.40** |

### 5.5.8.2 Madeni ya wanafunzi wanayodaiwa na Skuli ya Sheria shilingi 19,265,000

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa wanafunzi wa miaka mbalimbali waliopatiwa huduma na Skuli ya Sheria ambapo hadi ukaguzi unakamilika bado wanafunzi hao hawajakamilisha malipo kwa mujibu wa utaratibu wa huduma waliopatiwa na kupelekea uwepo wa deni la shilingi 19,265,000.

Kutokana na uwepo wa orodha ya wanafunzi wengi wanaodaiwa kwa miaka tofauti ya masomo, ukaguzi unaishauri Skuli ya Sheria kutengeneza sera maalum itakayowabana wanafunzi kutokuendelea na masomo ya mwaka unaofuata wa masomo kabla ya kuhakikisha inakamilisha deni linalotokana na mwaka wa nyuma wa masomo yake. Orodha ya wanafunzi hao ni kama wanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 65: Madeni ya wanafunzi wanayodaiwa na Skuli ya Sheria**

| Namba | Nambari ya usajili | Ada (Tshs) | Muhula wa kwanza (Tshs) | Muhula wa Pili (Tshs) | Deni (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Madeni wanayodaiwa Wanafunzi wa Cohort 1** | | | | | |
| 1. | CLP/LSZ/1/22/016 | 1,590,000 | 400,000 | - | 1,190,000 |
| 2. | CLP/LSZ/1/22/008 | 1,590,000 | 1,000,000 | 300,000 | 290,000 |
| 3. | CLP/LSZ/1/22/018 | 1,590,000 | 750,000 | - | 840,000 |
| 4. | CLP/LSZ/1/22/020 | 1,590,000 | 1,000,000 | 300,000 | 290,000 |
| 5. | CLP/LSZ/1/22/021 | 1,590,000 | 750,000 | 500,000 | 340,000 |
| **Jumla ndogo (A)** | | | | | **2,950,000** |
| **Madeni wanayodaiwa Wanafunzi wa Cohort 2** | | | | | |
| 6. | CLP/LSZ/2/2023/002 | 1,590,000 | 920,000 | 640,000 | 30,000 |
| 7. | CLP/LSZ/2/2023/003 | 1,590,000 | 940,000 | - | 650,000 |
| 8. | CLP/LSZ/2/2023/004 | 1,590,000 | 600,000 | 400,000 | 590,000 |
| 9. | CLP/LSZ/2/2023/006 | 1,590,000 | 940,000 | - | 650,000 |
| 10. | CLP/LSZ/2/2023/007 | 1,590,000 | 1,000,000 | | 590,000 |
| 11. | CLP/LSZ/2/2023/011 | 1,590,000 | 940,000 | 655,000 | 5,000 |
| 12. | CLP/LSZ/2/2023/012 | 1,590,000 | 800,000 | - | 790,000 |
| 13. | CLP/LSZ/2/2023/015 | 1,590,000 | 500,000 | 450,000 | 640,000 |
| 14. | CLP/LSZ/2/2023/016 | 1,590,000 | 600,000 | - | 990,000 |
| 15. | CLP/LSZ/2/2023/017 | 1,590,000 | 700,000 | 220,000 | 670,000 |
| 16. | CLP/LSZ/2/2023/018 | 1,590,000 | 650,000 | 290,000 | 650,000 |

| Namba | Nambari ya usajili | Ada (Tshs) | Muhula wa kwanza (Tshs) | Muhula wa Pili (Tshs) | Deni (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 17. | CLP/LSZ/2/2023/019 | 1,590,000 | 1,300,000 | - | 290,000 |
| 18. | CLP/LSZ/2/2023/020 | 1,590,000 | 650,000 | - | 940,000 |
| 19. | CLP/LSZ/2/2023/023 | 1,590,000 | 700,000 | 240,000 | 650,000 |
| 20. | CLP/LSZ/2/2023/025 | 1,590,000 | 940,000 | 450,000 | 200,000 |
| 21. | CLP/LSZ/2/2023/026 | 1,590,000 | 650,000 | - | 940,000 |
| 22. | CLP/LSZ/2/2023/027 | 1,590,000 | 740,000 | 470,000 | 380,000 |
| 23. | CLP/LSZ/2/2023/028 | 1,590,000 | 700,000 | 300,000 | 590,000 |
| 24. | CLP/LSZ/2/2023/029 | 1,590,000 | 700,000 | - | 890,000 |
| 25. | CLP/LSZ/2/2023/030 | 1,590,000 | 940,000 | - | 650,000 |
| 26. | CLP/LSZ/2/2023/031 | 1,590,000 | 400,000 | 500,000 | 690,000 |
| 27. | CLP/LSZ/2/2023/033 | 1,590,000 | 660,000 | 330,000 | 600,000 |
| 28. | CLP/LSZ/2/2023/034 | 1,590,000 | 920,000 | - | 670,000 |
| 29. | CLP/LSZ/2/2023/035 | 1,590,000 | 700,000 | 500,000 | 390,000 |
| 30. | CLP/LSZ/2/2023/036 | 1,590,000 | 940,000 | - | 650,000 |
| 31. | CLP/LSZ/2/2023/037 | 1,590,000 | 650,000 | - | 940,000 |
| 32. | CLP/LSZ/2/2023/010 | 1,590,000 | 500,000 | - | 590,000 |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **42,930,000** | **20,680,000** | **5,445,000** | **16,315,000** |
| **Jumla Kuu (A+B)** | | | | | **19,265,000** |

## 5.6 WIZARA YA AFYA

### 5.6.1 FUNGU H01 - WIZARA YA AFYA

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.6.1.1 Mapungufu yaliojitokeza katika ripoti ya utekelezaji wa Mpango kazi wa mwaka

Kifungu nambari 41(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza "Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuisha Mpango Kazi na Mpango wa Ununuzi.

Wizara ya Afya Zanzibar imetayarisha mpango kazi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Katika kupitia mpango kazi huo ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali zilizosababishwa na utayarishaji wa ripoti ya mpango kazi kwa kutumia mfumo wa "narrative" ambao haujitoshelezi. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutofanyika kwa uwiano wa shughuli makhususi ziliopo baina ya mpango kazi na ripoti ya utekelezaji wake.
- Kutojulikana kwa fedha halisi na asilimia ya uingizwaji wa fedha za shughuli makhususi zilizopangwa katika kila idara ziliomo kwenye Wizara.
- Kutofanyika kwa uwiano wa fedha za makisio na fedha halisi zilizoingizwa kwa kila shughuli iliopangwa kufanyika.
- Kutojulikanwa kwa asilimia ya upatikanaji wa fedha za kila shughuli makhususi za kila idara ziliopo katika Wizara.
- Kutojulikanwa kwa utekelezaji halisi wa shabaha za shughuli makhususi zilizoainishwa kwenye mpango kazi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba wanasimamia na kurekebisha dosari zinazojitokeza kwenye mfumo wa "narrative" ili kuandaa taarifa za utekelezaji wa mpango kazi kwa usahihi na kwa mujibu bajeti kutoka kila kitengo kulingana na shughuli zake ili kupima ufanisi uliopatikanwa kwa mujibu wa fedha halisi zilizoingizwa.

### 5.6.1.2 Kutokuwepo kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring Plan)

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali za Wizara ya Afya zinazohusu Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa mpango kazi kwa kuzingatia shughuli na vipaombele vya Wizara kwa mwaka husika.

Katika kupitia taarifa hizo, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ambao ungesaidia katika ufuatiliaji, upimaji na utekelezaji wa shughuli makhususi zilizopangwa kwenye mpango kazi huo jambo ambalo linaweza kupelekea kutotekelezeka kwa mpango kazi kama ulivyopangwa pamoja na kuchelewa kubaini dosari zinazoweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unatayarisha mpango wa ufuatiliaji na tathmini mara tu baada ya kupangwa kwa mpango kazi wa mwaka ili kuweza kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi za Wizara.

### 5.6.1.3 Kukosekana kwa Mpango wa likizo (leave roaster)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 58(1)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa 'Mtumishi wa umma atastahiki kupewa likizo la siku ishirini na nane za kazi ndani ya miezi kumi na mbili na atastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu au kama itakavyofafanuliwa katika matoleo kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Afya haikuandaa mpango wa likizo wa mwaka ambao utasaidia katika kutoa dira kwa watumishi kuweza kutambua siku wanayopaswa kwenda likizo ili waweze kujipanga katika kuweka sawa majukumu ya kazi pamoja na kukabidhi majukumu hayo kwa watendaji wengine, aidha kutokuwepo kwa mpango wa likizo kunarejesha nyuma mipango ya taasisi katika kuweza kutambua idadi ya watumishi wanaopaswa kwenda likizo kwa mwaka husika sambamba na kujua watumishi ambao watapatiwa huduma za malipo ya likizo kwa mujibu wa kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unasimamia na kutekeleza matakwa ya sheria juu ya uandaaji wa mpango wa likizo kwa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya watumishi hao na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

## WIZARA YA AFYA PEMBA

### 5.6.1.4 Malipo kwa madaktari wa Cuba bila ya kufunga mikataba shilingi 20,632,800

Wizara ya Afya Pemba imepokea madaktari mbali mbali kutoka Cuba kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya nchini sambamba na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia baina ya Zanzibar na Cuba.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Afya imefanya malipo ya shilingi 20,632,800 kwa ajili ya madaktari hao bila kuwepo mikataba ya kazi jambo ambalo linaweza kupelekea uhalali wa malipo yaliyofanyika kutokuthibitika kisheria, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 96 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kuwajazisha mikataba watumishi wa kigeni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kuwajazisha mikataba watumishi wa kigeni kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria. Hali halisi ni kama inavyoonekna katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 66: Malipo ya madaktari wa Cuba yasiyokuwa na mikataba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 36/10 ya 05/10/2022 | 29950 | 1,882,400 | Wizara ya Afya Pemba | Malipo kwa ajili ya kujikimu kwa madaktari wa Cuba |
| 47/10 ya 18/10/2022 | 030126 | 1,882,400 | | |
| 21/11 ya 08/11/2022 | | 1,872,000 | | |
| 75/11 ya 22/11/2022 | 031039 | 1,872,000 | | |
| 61/12 ya 29/12/2022 | 32045 | 1,882,000 | | |
| 78/01 ya 26/01/2023 | 32792 | 1,872,000 | | |
| 19/03 ya 07/03/2023 | 33690 | 1,872,000 | | |
| 28/11 ya 08/11/2022 | | 1,872,000 | CRDB Bank | |
| 74/11 ya 22/11/2022 | | 1,872,000 | | |
| 62/12 ya 29/12/2022 | 2012398 | 1,882,000 | | |
| 13/03 ya 07/03/2023 | 903201 | 1,872,000 | | |
| **Jumla** | | **20,632,800** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo.*

### 5.6.1.5 Kukosekana kwa hatimiliki za mali za Wizara

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Wizara ya Afya Pemba ambazo hazina hatimiliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya afisi na vyombo vya moto jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Wizara kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya Pemba kuongeza juhudi za kufanya ufuatiliaji wa upatikanaji wa hatimiliki zinazohusiana na mali hizo ili kuepusha Wizara kuingia katika migogoro isiyokuwa ya lazima. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki**

| Namba | Aina ya Mali | Namba | Aina ya Mali |
|---|---|---|---|
| **Majengo** | | | |
| 1. | Kituo cha afya Maziwani | 2. | Wesha |
| 3. | Kituo cha afya Shumba ya Vyamboni | 4. | Ukutini |
| 5. | Kituo cha afya Msuka Ungi | 6. | Makangale PHCU+ |
| 7. | Kituo cha afya Pandani | 8. | Mnarani Makangale |
| 9. | Kituo cha afya Chambani | 10. | Mjini Kiuyu |
| 11. | Kituo cha afya Mvumoni | 12. | Michenzani |
| 13. | Kituo cha afya IRCH Mkoani | 14. | Tumbe Magharibi |
| 15. | Kituo cha afya Ukutini | 16. | Kiuyu minungwini |
| 17. | Kituo cha afya Finya | 18. | Mbuzini |
| 19. | Mchangamdogo Vumba | 20. | Shamiani Mwambe |
| 21. | Ngomeni Chake chake | 22. | Makoongwe |
| 23. | Gando Junguni | 24. | Fundo |
| 25. | Kituo cha afya Kisiwani | 26. | Kituo cha afya Maziwani |
| 27. | Kituo cha afya Maziwang'ombe | 28. | Kituo cha afya Chambani |
| 29. | Kituo cha afya Msuka | 30. | Kiuyu Minungwini |
| 31. | Mvumoni Furaha | 32. | Gombani eneo litakalojengwa Ofisi |
| 33. | Kengeja | 34. | Mfikiwa eneo la EOC |
| 35. | Kituo cha afya Muambe | 36. | Vitongoji eneo litalojenjwa Esenereta |
| 37. | Kambini | 38. | Kituo cha afya Kangani |

| Namba | Aina ya Mali | Namba | Aina ya Mali |
|---|---|---|---|
| 39. | Bogoa | 40. | Kituo cha afya Uwandani |
| 41. | Chonga | 42. | Kituo cha afya Ole |
| 43. | Shungi | 44. | Kituo cha afya Chwale |
| 45. | Kibokoni | 46. | Kituo cha afya Vikunguni |
| 47. | Pandani | 48. | Wesha |
| **Vyombo vya Moto** | | | |
| 49. | Pikipiki | 50. | Toyota Japan |
| 51. | Pikipiki | 52. | Toyota Japan |
| 53. | Pikipiki | 54. | Toyota |
| 55. | Pikipiki | 56. | Toyota Japan |
| 57. | Honda | 58. | Nissan S/Africa |
| 59. | Pikipiki | 60. | Toyota Motor |
| 61. | Honda Japan | 62. | Toyota Motor |
| 63. | Honda | 64. | Nissan |
| 65. | Vespa | 66. | Nissan |
| 67. | Honda | 68. | Toyota |
| 69. | Honda | 70. | Toyota |
| 71. | Pikipiki | 72. | Toyota Leyland |
| 73. | Honda | 74. | Nissan |
| 75. | Honda | 76. | Nissan |
| 77. | Vespa | 78. | Mitsubishi |
| 79. | Honda | 80. | Toyota |
| 81. | Vespa | 82. | Nissan |
| 83. | Pikipiki | 84. | Toyota |
| 85. | Vespa | 86. | Nissan |
| 87. | Honda | 88. | Toyota |
| 89. | Honda | 90. | Toyota |
| 91. | Honda | 92. | Toyota |
| 93. | Honda | 94. | Toyota |
| 95. | Toyota South | 96. | Toyota L/cruiser |
| 97. | Toyota | 98. | Toyota |
| 99. | Toyota | 100. | IVECO |
| 101. | Isuzu | 102. | Toyota Hilux |
| 103. | Toyota Japan | 104. | Pick-Up4DD |
| 105. | Land Rover Discovery | 106. | Pick-Up4DD |
| 107. | Land Rover | 108. | Vocks Wagon |
| 109. | Toyota | 110. | Toyota |
| 111. | Toyota | 112. | Toyota |
| 113. | Toyota | 114. | VAICO |
| 115. | Toyota | 116. | VAICO |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Wizara*

### 5.6.1.6 Dosari katika utoaji wa ruhusa ya likizo bila ya malipo

Wizara ya Afya Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetoa likizo bila ya malipo kwa jumla ya watumishi nane (8) kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 08/06/2023 kwa lengo la kujiunga na kampuni binafsi ya Lancet. Katika utoaji wa likizo hiyo ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali kama ifuatavyo: -

i) Barua ya tarehe 14/06/2023 yenye kumbukumbu NAM.AB.149/260/05/21 inaonesha kwamba watumishi hao walianza likizo bila malipo kati ya tarehe 01/06/2023 na 02/06/2023 lakini mishahara ya watumishi hao imezuiliwa kulipwa kuanzia mwezi wa Mei, 2023 kabla hawajaanza likizo jambo ambalo ni kuwakosesha watumishi hao haki yao ya msingi ya mshahara walioutumikia kwa mwezi wa Mei, 2023.

ii) Katika majalada ya watumishi hao hakuna barua yoyote inayoonesha sababu za kuzuiliwa mshahara kwa wafanyakazi hao kabla ya mwezi walioanza likizo kufika.

iii) Kutokuwiana kwa taarifa zilizomo katika barua ya ruhusa ya likizo bila malipo na barua ya kuzuiliwa mishahara kwa watumishi hao jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa zuio la mshahara wa shilingi 5,433,349 lililofanywa kwa watumishi hao.

Kuwepo kwa dosari hizi kunapelekea uhalali wa zuio la mshahara lililofanywa kutokukubalika kisheria jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 13(1-3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya Pemba kuhakikisha unarejesha zuio la mishahara kwa watumishi hao pamoja na kuimarisha vyema udhibiti wa ndani katika kuandaa taarifa za watumishi na kuwapatia stahiki zao kwa kuzingatia miongozo ya kiutumishi. Watumishi wanaopaswa kurejeshewa mishahara yao iliyozuiliwa kinyume na utaratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 68: Watumishi wanaopaswa kurejeshewa mishahara iliyozuiliwa kinyume na utaratibu**

| Namba | Jina | Nambari ya Mshahara | Tarehe ya kuanza likizo | Tarehe ya kumaliza likizo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fatma Hamad Hilal | 962609 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 2. | Hussein Abdalla Khamis | 767776 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 3. | Bakar Kheir Silima | 362588 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 4. | Zuhura Mussa Zaid | 555137 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 5. | Omar Khamis Omar | 368071 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 6. | Riziki Hemed Said | UNGUJA | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 7. | Ali Juma Moh'd | 354893 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |
| 8. | Aziza Hamad Salim | 562710 | 01/06/2023 | 31/05/2024 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Majalada binafsi ya Watumishi*

### 5.6.1.7 Dosari katika utoaji wa ruhusa ya kwenda masomoni

Kwa mujibu wa kanuni nambari 9(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Mtumishi wa Umma aliyekuwepo katika muda wa majaribio hatoruhusika kwenda katika mafunzo ya muda mrefu mpaka baada ya kutimiza miaka miwili ya ajira yake".

Ukaguzi umebaini uwepo wa mtumishi **ndugu Hashim Ali Khamis** aliyepewa ruhusa ya kwenda kuendelea na mafunzo ya muda mrefu katika chuo kikuu cha KCMUCo kilichopo Moshi kwa barua yenye kumbukumbu namba WA/T/OPF/H.879327/B ya tarehe 12/10/2023 kabla ya mtumishi huyo kutimiza muda wa miaka miwili ya uajiri ambapo kwa mujibu wa kumbukumbu za uajiri aliajiriwa tarehe 02/01/2023 na ilipofika tarehe 12/10/2023 alipewa ruhusa ya kwenda masomoni akiwa na miezi tisa (9) tangu kuajiriwa kwake.

Kutokana na ukiukwaji wa kanuni nambari 9(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 uliofanywa na Katibu Mkuu Wizara ya Afya ya kutoa ruhusa kwa mtumishi huyo kinyume na utaratibu ilipelekea mgongano wa maamuzi baina ya Katibu Mkuu na Afisa Mdhamini ambapo kwa mujibu wa barua ya tarehe 28/08/2023 iliyoandikwa na ndugu Hashim Ali Khamis kuomba ruhusa ya masomo kwa Afisa Mdhamini alijibiwa kuwa "Nashauri asubirie, kaajiriwa tarehe 02/01/2023" kwa vile mtumishi huyo yupo katika kipindi cha majaribio (Probation Period) kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi na ndipo Katibu Mkuu Wizara ya Afya alipovunja maamuzi ya Afisa Mdhamini na kuamuru kutoa ruhusa kinyume na utaratibu wa kisheria jambo ambalo ni kumtenza nguvu na kumnyima uhuru Afisa Mdhamini kusimamia misingi ya kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kutoa ruhusa ya kwenda masomoni kwa watumishi kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria uliopo.

### 5.6.1.8 Malimbikizo ya Madeni shilingi 473,240,475

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Afya Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 473,240,475 ambapo miongoni mwa madeni hayo ni stahiki za wafanyakazi pamoja na madeni yatokanayo na kupatiwa huduma kutoka kwa watoa huduma mbali mbali, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kuyalipa madeni hayo.

Hali hii imesababishwa na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia na kufanya malipo ya madeni hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 69: Madeni ya muda mrefu ya Wizara**

| Namba | Mtoa Huduma | Huduma Iliyopatikana | Deni Halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Stahiki za watumishi | Malipo baada ya saa za kazi | 22,221,016 |
| 2. | | Malipo ya ufiwa | 11,700,000 |
| 3. | | Posho la matibabu | 800,000 |
| 4. | | Posho la kukamilisha ajira za wafanyakazi | 1,400,000 |
| 5. | | Call na outrich | 25,799,000 |
| 6. | Tahfif auto works, Nurbhai auto services na ngoto auto accessories | Vifaa vya matengenezo ya magari. | 5199,000 |
| 7. | - | Gharama za kumsafirisha mgonjwa. | 12,008,000 |
| 8. | Wapangishaji wa nyumba | Kodi nyumba za Madaktari | 17,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | UMAWA | Huduma ya Ulinzi | 21,500,000 |
| 10. | Jumuiya ya Kukuza Usafi | Huduma ya Usafi | 39,900,000 |
| 11. | Mamlaka ya Maji | Huduma ya Maji | 34,384,100 |
| 12. | Nassor Said Nassor | Matengenezo ya majengo | 26,700,774 |
| 13. | Salim Seif Ali | Kusafirisha viungo bandia | 2,764,000 |
| 14. | Shirika la Umeme | Huduma za Umeme | 185,361,872 |
| 15. | Tanzania Atomic | Leseni ya ex-ray | 1,929,000 |
| 16. | Stahiki za watumishi | Safari kikazi | 1,285,000 |
| 17. | Africom | Vifaa vya mfumo wa e-office | 890,000 |
| 18. | Ali Juma Hamad | Vifaa vya usafi | 1,532,000 |
| 19. | Ally Aboud Ally | Chakula cha wagonjwa | 8,887,000 |
| 20. | - | Contingent | 51,979,713 |
| **Jumla** | | | **473,240,475** |

*Chanzo: Orodha ya madeni ya Wizara*

#### 5.6.1.9 Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa mali chakavu

Kifungu nambari 69(1)(2) kinaeleza kuwa "Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya umma na kuwasilishwa katika Afisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Afisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya mali za kudumu zinazomilikiwa na Wizara ya Afya Pemba hazifanyiwi matengenezo kwa wakati wala kuondolewa kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria jambo ambalo linapelekea mali hizo kuzidi kuchakaa na hatimae kuharibika kabisa, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unaandaa mpango wa uondoshaji au wa matengenezo kwa mali chakavu kwa lengo la kuziepusha mali hizo kuendelea kuharibika. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 70: Mali chakavu ambazo hazijauzwa wala kufanyiwa matengenezo

| Namba | Aina ya chombo | Namba ya chombo | Namba ya Chassis | Mwaka | Sehemu ilipo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Toyota | SMZ 212B | PN133JV-2508262759 | 2012 | K/ufundi |
| 2. | Toyota | SMZ 729A | KDN 201-0078625 | 2011 | A/Mzee |
| 3. | Isuzu | DFP5332 | MPATASSA-H8H522296 | 2008 | Utumishi |
| 4. | Toyota | SMZ730A | KDH201 | 2011 | A/Mzee |
| 5. | Toyota | DFPA | JTERB71J500075709 | 2014 | Chake Hospi |
| 6. | Toyota Japan | DFP5053 | JTERB71J500042645 | 2002 | Wete Hosp. |
| 7. | Nissan S/ Africa | DFP 8693 | ADNCPUD22Z0013987 | 2011 | DHMT Mkoani |
| 8. | Toyota Motor | SMZ561A | SXU10-0030670 | 2000 | Mkemia |
| 9. | Suzuki Motor | SMZ803A | TD52W-100158 | 2004 | HIMS |
| 10. | Toyota Motor | SMZ301A | JTMBH33V30D004398 | 2002 | Tiba |
| 11. | Nissan S/ Africa | SMZ106B | ADNCJUD22Z0010223 | 2010 | Malaria |
| 12. | Nissan | DFPA2884 | ADNCPUD22 | 2015 | Utumishi |
| 13. | Nissan | DFP325 | ADNCPUD22Z0037804 | 2014 | UKIMWI |
| 14. | Toyota | SMZ370B | LN106-0003944 | 2006 | ZFDA |
| 15. | Toyota Thyland | DFP6798 | AHTFR22G-706022440 | 2009 | Mama na Mtoto |
| 16. | Toyota | SMZ24A | 516108574 | 2000 | Malaria |
| 17. | Honda | SMZ937C | LTM.02195 | 2015 | |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za mali za kudumu za Wizara*

### 5.6.2 FUNGU H02 - HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.6.2.1 Kutokuwepo kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring Plan)

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali za Hospitali ya Mnazi Mmoja zinazohusu Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa mpango kazi kwa kuzingatia shughuli na vipao mbele vya Hospitali kwa mwaka husika.

Katika kupitia taarifa hizo, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ambao ungesaidia katika ufuatiliaji, upimaji na utekelezaji wa shughuli makhususi zilizopangwa kwenye mpango kazi huo jambo ambalo linaweza kupelekea kutotekelezeka kwa mpango kazi kama ulivyopangwa pamoja na kuchelewa kubaini dosari zinazoweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha unatayarisha mpango wa ufuatiliaji na tathmini mara tu baada ya kupangwa kwa mpango kazi wa mwaka ili kuweza kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi za Hospitali.

## 5.7 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

### 5.7.1 FUNGU – WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO PEMBA**

#### 5.7.1.1 Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji shilingi 14,448,674

Kifungu nambari 35 cha Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya mwaka 2018 kimezitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zake zote za Uchapaji na Mahitaji ya vifaa vya Afisi na vifaa vya kuandikia kwa wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba imefanya ununuzi ya vifaa vya kuandikia vyenye jumla ya shilingi 14,448,674 kutoka kwa Wasambazaji bila ya kuwepo kwa ruhusa kutoka kwa Wakala kama utaratibu unavyoelekeza jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imesababishwa na kutokuombwa kwa ruhusa kutoka kwa wakala kabla ya Wizara kuamua kununua vifaa kwa wasambazaji wengine wanaoonekana katika mtandao. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kununua vifaa kwa Wakala husika au kuomba ruhusa kwa Wakala ili kuweza kununua vifaa hivyo kwa wasambazaji wengine pale inapotokezea Wakala kutokuwa na vifaa vinavyohitajika kununuliwa. Mchanganuo wa vifaa vilivyonunuliwa nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji ni kama vinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 71: Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilichotumika (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 03/08 ya 12/08/2022 | - | 1,437,334 | Pemba General Supply | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 12/09 ya 15/09/2022 | 029382 | 1,173,118 | | |
| 06/10 ya 12/10/2022 | 030053 | 1,128,922 | | |
| 10/10 ya 12/10/2022 | 032355 | 1,185,608 | | |
| 05/12 ya 12/12/2022 | 031566 | 1,279,764 | | |
| 21/12 ya 19/12/2022 | 031607 | 648,530 | Misufini Stationary Supply | |
| 41/12 ya 21/12/2022 | 031634 | 177,746 | Pandu Book Shop | |
| 11/02 ya 10/02/2023 | 032944 | 3,703,344 | Pemba General Supply | |
| 15/03 ya 09/03/2023 | - | 1,271,118 | | |
| 27/04 ya 19/04/2023 | - | 115,296 | Adult Trainig Centre | |
| 01/05 ya 02/05/2023 | 035061 | 1,122,590 | Khatib Holdings | |
| 38/06 ya 22/06/2023 | - | 1,205,304 | Adult Training Centre | |
| **Jumla** | | **14,448,674** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo za Wizara*

## 5.8 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

### 5.8.1 FUNGU J01 - WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 5.8.1.1 Ukusanyaji wa Mapato kwa kutumia njia isiyo rasmi

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi ulifanya ziara katika vituo mbali mbali vya Kihistoria ikiwemo Kituo cha Kwa Bi Hole, Mji wa Kale, Makumbusho ya Pete, Msikiti wa Kizimkazi na Jambiani Kuumbi Cave.

Katika ziara hiyo ilibainika uwepo wa mapungufu mbalimbali yanayowakabili watunzaji na washughulikiaji wa vituo vya Kihistoria, miongoni mwa changamoto zilizobainika ni kutokujuulikana kwa thamani halisi ya fedha inayokusanywa kwa kila kituo kwa mujibu wa wageni wanaofika katika vituo hivyo kwa lengo la kujifunza na kujionea mambo mbali mbali ya kihistoria.

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na wasimamizi wakuu wa vituo hivyo ili kuweza kujua mbinu inayotumika kukusanya mapato ya Serikali na kuyawasilisha mapato hayo kwa mujibu wa utaratibu.

Kilichobainika katika vituo hivyo ni ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia isiyokuwa rasmi ikiwemo njia ya simu ya mkononi pamoja na upokeaji wa mapato kwa njia ya fedha taslim, jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa takwimu sahihi ya fedha inayokusanywa pamoja na vielelezo vinavyohusiana na ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hatimae kutia shaka juu ya uhalali wa kima cha fedha kinachokusanywa na kubainishwa kama mapato ya siku yatokanayo na uingiaji wa wageni katika vituo hivyo.

Kukusanya mapato kwa kutumia njia isiyo rasmi kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato ya Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na muongozo nambari 2 wa ufungaji wa hesabu uliotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali wa mwaka 2022/2023.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha unachukuwa juhudi za makusudi kuweka mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato katika vituo vya kihistoria ili kuiwezesha Serikali kutambua kima halisi cha fedha kilichokusanywa, pamoja na idadi ya wageni waliotembelea vituo vya kihistoria kwa mwaka.

### 5.8.1.2 Kukosekana kwa nyaraka za makabidhiano ya chanzo cha Mapato

Miongoni mwa vivutio vya utalii ambavyo huchangia pato la Serikali ni uwepo wa Kisiwa cha Changuu (Prison Island) ambapo kutokana na mazingira ya kisiwa hicho wageni wengi hupendelea kutembelea mahali hapo kwa lengo la kupumzika, kujifunza pamoja na kujionea mambo mbali mbali yaliyopo katika kisiwa hicho.

Ukaguzi umebaini kwa muda mrefu mapato yatokanayo na kivutio hicho cha utalii husimamiwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa makusanyo ya kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni, 2023 yaliyokusanywa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ambapo dosari mbali mbali zilibainika kama ifuatavyo:-

- Uwepo wa makusanyo unaoendelea kufanywa na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kupitia chanzo hicho bila ya kupatikana hati ya makabidhiano ya usimamizi wa chanzo cha makusanyo.
- Kutokujuulikana kwa thamani halisi ya fedha iliyokusanywa kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni, 2023.
- Kukosekana kwa makabidhiano ya fedha zilizokusanywa kutoka Idara ya Makumbusho kwenda Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.
- Kutokupatikana kwa nyaraka zinazothibitisha kupata idhini kutoka Taasisi husika zikiwemo ripoti ya makabidhiano pamoja na kumbukumbu za Kamati Tendaji.

Uwepo wa dosari hizo huwenda zikapelekea kutokujuulikana kwa kima halisi cha fedha kilichokusanywa, kilichokabidhiwa, na kitakachobainishwa katika ufungaji wa hesabu wa Taasisi mbili hizo jambo ambalo linaweza kupelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali na usahihi wa hesabu zinazowasilishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo ni vyema kufanya makabidhiano ya maandishi kwa taarifa yoyote ya Serikali ili kuepusha usumbufu utakaoweza kujitokeza pindipo taarifa hizo zikihitajika kwa matumizi ya Serikali.

### 5.8.1.3 Malimbikizo ya Deni la muda mrefu shilingi 66,726,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa deni lenye thamani ya shilingi 66,726,000 linalodaiwa na watumishi 13 wa ajira ya mkataba kwa ajili ya huduma ya ulinzi inayotolewa katika vituo mbali mbali vya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

Kutokulipwa kwa posho za watoa huduma hao kwa wakati kunapelekea kuondoa ari ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba yao jambo ambalo linaweza kuitia hasara Serikali pale watumishi hao watakapoamua kuacha malindo yao na kwenda kujitafutia shughuli nyengine za kiuchumi pasi na Wizara kuwa na taarifa ya kutokuwepo kwao kwenye maeneo ya kazi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha unaweka kipaombele cha kufanya malipo kwa watumishi hao ili kuwapunguzia ugumu na ukali wa maisha wanaoendelea kuupata kwa kutokujua khatma ya stahiki zao. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 72: Orodha ya walinzi wanaodai ni kama ilivyoainishwa

| Namba | Jina la Mdai | Kituo cha Kazi | Malipo ya Mwisho | Idadi ya Miezi ya Deni | Malipo kwa Mwezi (Tsh) | Deni Analodai (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Suleiman Mselem Salami. | Bi Khole | Juni 2021 | 26 | 150,000 | 3,900,000 |
| 2. | Khami Mabula Kulindwa | | | 26 | 150,000 | 3,900,000 |
| 3. | Othman Adam Aini | | | 26 | 150,000 | 3,600,000 |
| 4. | Simai Mngwali Khamis | Fukuchani | Julai 2021 | 25 | 150,000 | 3,750,000 |
| 5. | Simai Ngwali Khamis | | | 25 | 150,000 | 3,750,000 |
| 6. | Haji Mula Haji | | | 25 | 150,000 | 3,750,000 |
| 7. | Khamis Ameir Hija | Pete | Juni 2021 | 26 | 150,000 | 3,900,000 |
| 8. | Ameir Hji Ali | | | 26 | 150,000 | 3,900,000 |
| 9. | Yussuf Vuai Ali | | | 26 | 150,000 | 3,900,000 |
| 10. | Haji Musa Haji | | | 26 | 150,000 | 3,900,000 |
| 11. | Hamad Bakari Hamad | Boti ya Mfalme Bandarini Malindi | Aprili 2021 | 28 | 339,000 | 9,492,000 |
| 12. | Haji Juma Haji | | | 28 | 339,000 | 9,492,000 |
| 13. | Hassan Abeid Omar | | | 28 | 339,000 | 9,492,000 |
| **Jumla** | | | | | | **66,726,000** |

### 5.8.1.4 Kukosekana kwa Kibali cha Uajiri wa Walinzi wa Mkataba kutoka Tume ya Utumishi

Katika kupitia kumbukumbu mbalimbali za Wizara , Ukaguzi umebaini uwepo wa watendaji ambao wameajiriwa kwa Mkataba toka mwaka 2019 hadi 2023 bila ya Kibali cha ruhusa kutoka Tume ya Utumishi Serikalini kinachotoa mamlaka ya kuajiri watumishi kwa Mkataba. Baadhi ya maeneo ambayo kunawaajiriwa wa Mkataba ni Sehemu za makumbusho ya Kihistoria ambazo kunapatikana Tozo la mapato ya vivutio. Baadhi ya maeneo yenye watumishi wa mkataba ni Pete na Jambiani Kuumbi Cave.

Kukosekana kwa Kibali cha Uajiri wa Mkataba kwa watumishi inapelekea kwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na miongozo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba Sheria, Miongozo ya Utumishi wa Umma inafuatwa katika kutekeleza majukumu yake.

#### 5.8.1.5 Kutokukamilika kwa taratibu za kuwaombea ajira ya kudumu watumishi wa kutwa

Kwa mujibu wa kanuni ya 135 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014, inaeleza kuwa hakutakiwi kuwepo kwa wafanyakazi wa kutwa katika Utumishi wa Umma na kama kuna ulazima wa kuwepo Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika na kumjazisha mkataba, ambapo mtumishi wa utumishi wa kutwa hatozidi miezi sita.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilibainika kuwa na watumishi wa kutwa ambao wanaendelea kutumikia kwa baadhi ya maeneo ya Kihistoria yakiwemo Pete na Jambiani Kuumbi Cave kuanzia mwaka 2019 hadi sasa.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni uwepo wa watumishi wa kutwa kwa zaidi ya miaka mitatu (3) bila ya kupata ithibati ya kuwepo kwa kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya kupata idhini. Hali hii inaweza ikapelekea kujitokeza kwa migogoro isiyo ya lazima pindipo mtumishi wa kutwa atakapokosa sifa za uajiri wa kudumu au kujitokeza kwa uajiri wa mtumishi asiyekuwa na maadili mema.

Kuwatumia watumishi wa ajira za kutwa kwa muda mrefu ni kwenda kinyume na Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2014 kama nilivyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuendelea kufuatilia vibali vya ajira ili kuweza kuwaajiri katika ajira ya kudumu wale wote wanaoweza kuajirika kisheria.

#### 5.8.1.6 Kutokukamilka kwa wakati kwa Mradi wa ujenzi wa Ras Mkumbuu

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilisaini hati ya makubaliano na mkandarasi Yassi and Sons CO Ltd mnamo tarehe 6/5/2023 kwa thamani ya shilingi 2,407,316,675 kwa ajili ya ukarabati wa Kivutio cha Kihistoria cha Rasi Mkumbuu.

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka unaoishia Juni, 2023 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilitenga bajeti yenye jumla ya shilingi 2,407,316,675 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambapo kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa ufungaji wa hesabu wa mwaka 2022/2023 ilibainika kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kutokana na uwepo wa dosari mbalimbali za kiutendaji kama ifuatavyo:-

- Kutoanza kwa ujenzi wa ukuta unaozuia maji ya bahari kuathiri eneo la kihistoria.
- Kutokukamilka kwa wakati kwa ujenzi wa nyumba 3, Ofisi, Mgahawa, Duka, Kisima na hodhi la maji.
- Kutokuwa na Mshauri Elekezi katika Mradi wa Ras Mkumbuu kutoka Mamlaka ya Majengo.
- Kutoanza kufanyiwa matengenezo ya magofu ya Msikiti, Makaburi na nyumba ya makaazi ya watu wa zamani.
- Kuwepo kwa Karani wa ufuatiliaji wa mradi wa eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu ambae yuko ndani ya kipindi cha uangalizi (Under probation) ambae amepewa barua ya usimamizi wa mradi huo AB.135/157/01/9 ya tarehe 11/01/2024.
- Kufanyika kwa malipo bila ya kuwepo kwa Cheti cha kumuombea malipo Mkandarasi kutoka kwa Mshauri Elekezi.
- Mjenzi kutoelezea vifaa vya ujenzi vitapatikana kutoka nchi gani (Manufacture of goods).
- Kukosekana kwa ripoti za Mhandisi wa usimamizi wa ujenzi kuanzia kipindi ulipoanza mradi.
- Kuwepo kwa mipasuko (nyufa) katika Vivutio vilivyoanzwa kujengwa.

Kujitokeza kwa dosari hizo kunapelekea kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa jambo ambalo linaweza kuikosesha Serikali mapato ambayo yangeweza kupatikana kutokana na ada za makusanyo zitokanazo na wageni wanaoingia katika maeneo ya kihistoria kwa lengo la kujifunza, kujionea pamoja na matembezi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unakuwa makini katika usimamizi wa mikataba iliyosainiwa ili iweze kutekelezwa kama ilivyobainishwa na hatimaye kupatikanwa kwa tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 73: Malipo ya mradi wa uimarishaji wa maeneo ya Kihistoria

| Hati namba | Aliyelipwa | Thamani (Tsh) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| J04pv2300219 | TRA | 7,201,016.83 | Malipo kwa ajili ya mkato wa TRA mradi wa uimarishaji maeneo ya kihistoria Ras Mkumbuu |
| J04pv2300221 | Yassin & Sons Co. Ltd | 217,830,758.87 | Malipo kwa ajili ya mradi wa uimarishaji maeneo ya Kihistoria Ras Mkumbuu. |
| **Jumla** | | **225,031,775.7** | |

### 5.8.1.7 Kukosekana kwa uhalisia wa vifaa vilivyonunuliwa shilingi 22,500,000

Kwa mujibu wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na miongozo mbalimbali ya ununuzi inaelekeza kufanya ununuzi kwa kuzingatia sifa na vigezo vya mahitaji ya mtumiaji. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imefanya ununuzi kutoka kwa mtoa huduma Home Funiture bila ya kufuata sifa na aina ya mahitaji.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya hati za malipo na kubaini kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kupitia hati namba 1071 ya 07/9/2023 ilifanya ununuzi wa viti vya mbao ngumu 50 kwa thamani ya shilingi 22,500,000.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kupokelewa kwa viti 50 maalum vya wageni (visitor's chair) kupitia Delivery Note nambari 1503 ya 11/9/2023 ambavyo vilibainika kutokuendana na uhalisia wa mahitaji kulingana na hati ya maombi iliyowalishwa.

Kuleta vifaa kinyume na mahitaji yaliyoombwa inapelekea uwezekano wa kufanya malipo kinyume na uhalisia na vilevile kunaweza kupelekea kukosekana kwa tija itokanayo na dhamira ya uwepo wa viti vilivyopangwa kununuliwa ambavyo vingeweza kuwa ni kichocheo cha utalii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba inasimamia ipaswavyo mipango iliojipangia pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango hiyo kwa lengo la kubaini mapungufu pale yanapojitokeza na kuweza kuchukuliwa hatua za haraka.

#### 5.8.1.8 Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 108,588,800

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha, kifungu namba 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 108,588,800 kwa wafanyabiashara mbali mbali ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama ni watoa huduma jambo ambalo linaweza kupelekea kuikosesha serikali mapato yatokanayo na utoaji wa huduma hiyo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani kwa kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia malipo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua bidhaa au huduma kwa watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa malipo kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na mamlaka ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 74: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na ZPPDA**

| Hati namba | Aliyelipwa | Vifaa vilivyonunuliwa | Thamani (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| 0347 ya 16/10/2023 | Home Furniture | Table (hard wood) | 9,750,000 |
| | | Coffee table (Hard wood) | 1,350,000 |
| | | Conference table (Hardwood) | 4,000,000 |
| 01552 ya 15/6/2023 | | Viti (hardwood) | 22,500,000 |
| | | Meza ya mapokezi ya mbao | 900,000 |
| | | Viti vya wageni (hardwood) | 2,500,000 |
| | | Kabati milango 3 (hard wood) | 800,000 |

| Hati namba | Aliyelipwa | Vifaa vilivyonunuliwa | Thamani (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| 01552 ya 15/6/2023 | | Kabati mlango 1 (hardwood) | 400,000 |
| | | Kabati milango 2 (hardwood) | 5,400,000 |
| | | Executive table (hardwood) | 4,800,000 |
| | | Meza 1.6 (hardwood) | 7,000,000 |
| | | Meza 1.8 (hardwood) | 15,000,000 |
| | | Office cabinet (hardwood) | 1,200,000 |
| | | Sofa set full black | 7,000,000 |
| 1033 ya 2/3/2023 | Feyus Printing Solution and Supplies | Rangi | 40,000 |
| | | Rangi | 40,000 |
| | | Red oxide | 87,000 |
| | | Brush | 12,000 |
| | | Domet ngumu | 72,000 |
| | | Domet laini | 66,000 |
| | | Dust been kubwa | 30,000 |
| | | Window cleaner | 135,000 |
| | | Laboratory coat | 204,000 |
| | | Vitambaa | 100,000 |
| | | Turubali | 200,000 |
| | | Tool box | 150,000 |
| | | Water tank | 550,000 |
| | | Kigari | 2,300,000 |
| | | Projector | 5,000,000 |
| | | Screen | 6,900,000 |
| | | Showcases | 9,382,800 |
| | | Projector celing mount | 250,000 |
| | | Stand | 470,000 |
| **Jumla** | | | **108,588,800** |

### 5.8.1.9 Kukiukwa kwa Taratibu za Ununuzi shilingi 186,370,000

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilisaini hati ya makubaliano na mtoa huduma Home furniture yenye kumbukumbu nambari SMZ/J04/G/OQ/2022-23/21 ya tarehe 02/06/2022 kwa thamani ya shilingi 94,370,000 ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa samani.

Vile vile Wizara ilisaini hati ya makubaliano na mtoa huduma M/S Africom Ltd yenye kumbukumbu nambari SMZ/J04/G/NCB/2022-23/01 ya tarehe 01 Juni, 2022 kwa thamani ya shilingi 92,000,000 ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta za Wizara. Hadi ukaguzi unakamilika imebainika Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imefanya malipo kwa watoa huduma wote wawili yenye thamani ya shilingi 17,043,478.32 ambapo pamoja na kufanyika kwa malipo hayo dosari mbali mbali zilibainika ikiwemo kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi kwa mujibu wa kifungu 23(2), 35(2)(1), 45(3)(a), 42(c), 42(2) na 43(1).

Kutokana na ukiukwaji mkubwa wa taratibu ukaguzi unatia shaka juu ya huduma itakayotolewa na watoa huduma hao huwenda ikawa chini ya kiwango kilichokusudiwa kutokana na kukosekana kwa uwazi katika mchakato wa uitishwaji wa zabuni hatimae kutokupatikanwa kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha unatekeleza ipasavyo misingi na taratibu za ununuzi ili kuweza kufanya manunuzi yenye ubora, tija na yanayoendana na thamani halisi ya fedha.

## 5.8 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE - PEMBA

### 5.8.1 FUNGU J01 - WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

#### 5.8.1.1 Utoaji na utumiaji wa mafuta usioridhisha

Kanuni nambari 124(2) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vinavyotumika katika taasisi yake vinakuwa na buku linaloonyesha matumizi ya chombo kwa safari husika (log Book)".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutumika jumla ya lita 1,729 za mafuta kwa ajili ya shughuli za Wizara. Dosari iliyobainika ni kutolewa na kutumika kwa mafuta kusivyoridhisha kutokana na mafuta hayo kutolewa kwa jumla kwa wakati mmoja bila ya kubainishwa masafa ya safari zilizofanyika na mafuta yaliyoingizwa na kutumika kwa kila chombo, jambo ambalo linaweza kupelekea uhalali wa matumizi ya fedha na mafuta husika kutokuthibitika kisheria, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika matumizi ya rasilimali za umma ikiwemo kufanya matumizi mazuri ya mafuta na vyombo husika. Mchangamano wa utoaji wa utumiaji wa mafuta usioridhisha kama unavyoonekana katika jedwali hapo chini:-

## Jadweli Nambari 75: Utoaji na utumiaji wa mafuta usioridhisha

| Tarehe | Nambari ya Kiballi | Nambari ya gari | Idadi ya lita za mafuta |
|---|---|---|---|
| 5/11/2023 | 5598 | SMZ 943, SMZ 1078A, SMZ 1430 | 103 |
| 24/12/2022 | 6544 | SMZ 794, SMZ 2788 | 100 |
| 19/1/2023 | 8210 | SMZ 609, SMZ 251, SMZ 548 | 100 |
| 1/3/2023 | 8244 | SMZ 820A | 303 |
| 3/6/2023 | 10013 | SMZ 974A, SMZ 605A | 120 |
| 28/1/2023 | 8225 | SMZ 588, SMZ 788 | 120 |
| 4/4/2023 | 9228 | SMZ Idara ya Utalii | 108 |
| 5/4/2023 | 9230 | SMZ 794, SMZ 788 | 135 |
| 5/4/2023 | 9231 | SMZ 943, SMZ 150B | 80 |
| 11/4/2023 | 9237 | SMZ 821, SMZ 548, SMZ 175B | 100 |
| 22/5/2023 | 9250 | SMZ 605, SMZ 260 | 100 |
| 3/6/2023 | 10013 | SMZ 155A, SMZ 974A | 140 |
| 15/6/2023 | 10023 | SMZ 650, SMZ 548 B | 100 |
| 24/1/2023 | 8225 | SMZ 588, SMZ 788 | 120 |
| **Jumla** | | | **1729** |

*Chanzo: Daftari la ghalani la kurikodia mafuta*

### 5.8.1.2 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 24,268,073

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 24,268,073 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na Kanuni iliyobainishwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

### Jadweli Nambari 76: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/8 ya 4/8/2022 | 028475 | 3,695,983 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | Malipo kwa ajili ya huduma mbali mbali za Wizara. |
| 5/8 ya 4/8/2022 | 028479 | 450,000 | | |
| 11/8 ya 11/8/2022 | 028603 | 2,546,244 | | |
| 34/8 ya 26/8/2022 | 028865 | 414,136 | | |
| 8/9 ya 14/9/2022 | 029366 | 7,862,227 | | |
| 9/9 ya 16/9/2022 | 029390 | 4,375,000 | | |
| 14/9 ya 22/9/2022 | 029556 | 3,244,998 | | |
| 38/9 ya 30/9/2022 | 029688 | 1,679,485 | | |
| **Jumla** | | **24,268,073** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.8.1.3 Kutokutumika kwa mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji wa mapato shilingi 2,578,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, kinaelezea "Afisa Mhasibu, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato. Aidha toleo la barua yenye kumb.No.CA.319/398/01/02/19 ya tarehe 14/02/2022 kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafafanua kwamba matumizi yote ya Taasisi za Umma yafanyike kupitia Mfumo wa ZanMalipo".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mapato yenye jumla ya shilingi 2,578,000 yamekushanywa kwa miezi ya Julai, 2022 hadi Septemba, 2023 kupitia stakabadhi za mkononi badala ya kutumia mfumo wa ZanMalipo ambapo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria na muongozo kama niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kukusanya mapato kupitia mfumo wa ZanMalipo.

#### 5.8.1.4 Ukusanyaji wa mapato usioridhisha katika maeneo ya kihistoria

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba inamiliki maeneo ya Kihistoria yasiyopungua arobaini na tano (45) yakiwemo maeneo yenye kuvutia ya Pango la Watoro, Pango la Kijiji, Makumbusho ya Twaka Tumbe na Ras Mkumbuu ambayo Serikali imetoa fedha nyingi kufanyiwa ukarabati ili kudhibiti historia za maeneo hayo pamoja na kuingiza mapato Serikalini.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,336,755,869.3 zilitumika kukarabati maeneo ya kihistoria ya Pango la Watoro, Pango la Kijiji, Makumbusho ya Twaka Tumbe na Ras Mkumbuu.

Pamoja na ukarabati uliofanyika ambao umegharimu fedha nyingi, ukaguzi umebaini kutokuakisi uhalisia wa kiwango cha mapato cha jumla ya shilingi 649,500 kilichopatikana kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutokana na vivutizi vya kihistoria katika maeneo yaliyofanyiwa ukarabati jambo ambalo huwenda likapelekea kutumia muda wa zaidi ya wastani wa miaka mia moja (100) ya urejeshwaji wa gharama zilizotumika katika ukarabati wa maeneo hayo pindipo jitihada za makusudi hazitochukuliwa kudhibiti mapato yatokanayo na vivutizi hivyo.

Ukaguzi unaishauri Serikali Kuu kupitia Idara ya Makumbusho kuhakikisha jitihada za makusudi zinachukuliwa ili kuendana na uhalisia wa thamani ya fedha iliyotumika na tija itakayopatikana kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali, hivyo ni vyema kutumia vyombo mbali mbali vya habari kuhamasisha utalii wa ndani kwa lengo la kuipatia Serikali mapato. Vyenginevyo kama hali itaendelea kama ilivyo sasa kuna uwezekano mkubwa wa majengo hayo kuchakaa na kurudi katika hali ya awali kabla ya nusu ya gharama zilizotumika kuweza kurejeshwa kupitia mapato hayo. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 77: Fedha zilizotumika kukarabati maeneo ya kihistoria na mapato yaliyokusanywa**

| Tarehe | Nambari ya Udhibiti | Eneo la Kihistoria | Fedha iliyotumika kukarabati (Tshs) | Mapato yaliyokusanywa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Julai, 2022 Juni, 2023 | 200420008018 | Ras Mkumbuu | 240,731,667.5 | 297,000 |
| | 200420017308 | Pango la Kijiji | 441,787,781.90 | 123,000 |
| | 200420016222 | Pango la Watoro Chwaka Tumbe | 654,236,419.9 | 50,000 |
| | | | | 179,500 |
| **Jumla** | | | **1,336,755,869.3** | **649,500** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Mapato ya maeneo ya Kihistoria*

### 5.8.2 FUNGU J 02 - KAMISHENI YA UTALII

Ukaguzi wa hesabu za Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.8.2.1 Tofauti iliyojitokeza baina ya Hesabu ya Mwisho wa mwaka na Mikataba halisi iliyofungwa shilingi 87,126,930

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unazitaka Taasisi za Serikali kutayarisha taarifa sahihi za mapato na matumizi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa uwiyano wa taarifa za fedha baina ya taarifa za fedha zilizoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa mwaka na taarifa zilizomo katika mikataba halisi iliyofungwa na Kamisheni jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 87,126,930 baina ya taarifa hizo. Aidha, inapelekea taarifa za Hesabu zilizoandaliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kutokuonyesha sura halisi na sahihi kulingana na vigenzo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa ikiwemo toleo la ufungaji wa Hesabu nililolinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha unaingiza taarifa sahihi za mapato na matumizi katika Taarifa za Hesabu za mwisho wa mwaka ili kuweza kuonyesha sura sahihi na halisi kwa muijibu wa viwango vya ufungaji wa Hesabu vya Kitaifa na Kimataifa. Hali halisi ya tofauti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 78: Tofauti kati ya Hesabu za Mwisho wa mwaka na Taarifa katika Mikataba

| Kifungu cha matumizi | Fedha za Mikataba iliyoainishwa katika Hesabu ya mwisho wa mwaka (Tshs) | Aina ya Mikataba iliyofungwa 2022/2023 | Thamani (Tshs) | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Contracting fees | 90,945,000 | Mkataba wa utunzaji wa bustani Bungi kwa Bihole<br>600,000 kwa mwezi | 7,200,000 | **87,126,930** |
| | | Mkataba wa huduma ya ulinzi (Bungi)<br>Tzs 1,200,000 kwa mwezi | 14,400,000 | |
| | | Mkataba wa huduma ya ulinzi Kamisheni shs 1,020,000 kwa mwezi | 12,240,000 | |
| | | 361 Degrees Africa (SMS- Private) Ltd | 68,960,950 | |
| | | Tea Party Zanzibar (TPZ) | 73,370,980 | |
| | | Tea Part Zanzibar addendum | 1,900,000 | |
| **Jumla** | **90,945,000** | | **178,071,930** | **87,126,930** |

### 5.8.2.2 Tofauti iliyobainishwa kati ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka na Taarifa za Mapato shilingi 724,427,202

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unaeleza kwamba taarifa zote za mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali ziingizwe katika Taarifa za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement)".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa tofauti ya taarifa za fedha za Kamisheni ya Utalii baina ya taarifa ya mapato zilizoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka ambazo ni shilingi 5,710,528,729 na taarifa za makusanyo ya leseni zilizoripotiwa kupitia kumbukumbu za mapato ya Kamisheni yenye jumla ya shilingi 4,986,101,527 jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa tofauti ya mapato yenye jumla ya shilingi 724,427,202 kati ya taarifa hizo.

Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za Hesabu za Mwisho wa mwaka kutokuonyesha Sura halisi na Sahihi kulingana na muongozo wa ufungaji wa Hesabu uliounakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unaingiza taarifa sahihi katika Hesabu za mwisho wa mwaka zinazolingana na Taarifa za Mapato zilizobainishwa kupitia kumbukumbu za mapato sambamba na kufanya usuluhishi wa kibenki ili kuweza kubaini tofauti zinazoweza kujitokeza katika taarifa za mapato.

### 5.8.2.3 Kutokuingizwa kwa makusanyo yatokanayo ya Tamasha la ZITITE katika Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka USD 3,465

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unaeleza kwamba taarifa zote za mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali ziingizwe katika Taarifa za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement)".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii ilikusanya jumla ya USD 3,465 zinzotokana na Tamasha la Utalii la ZITITE. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuainishwa kwa mapato hayo pamoja na matumizi yake katika Taarifa za Hesabu za Kamisheni jambo ambalo linapelekea Taarifa za Hesabu zilizowasilishwa kutokuonyesha Sura halisi na sahihi, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unasimamia utaratibu unaohusiana na ukusanyaji wa mapato, ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka pamoja na utayarishaji wa usuluhishi wa kibenki ili kuweza kubaini tofauti ya mapato na kufanya marekebisho katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

### 5.8.2.4 Kutoonekana kwa maeneo halisi ya miradi 10 ambayo imepata leseni kutoka Kamisheni ya Utalii

Ukaguzi ulikaguwa majalada ya miradi arobaini na tisa (49) kati ya majalada mia saba na kumi (710) ya miradi iliyopewa leseni na Kamisheni ya Utalii, baada ya kutembelea maeneo iliyopo miradi hiyo ukaguzi umebaini kwamba kati ya miradi hiyo 49 uliyoitembelea miradi kumi (10) haikuonekana kwa ajili ya ukaguzi ili kuweza kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo.

Kutoa leseni kwa miradi ambayo haipo katika maeneo husika ni matumizi mabaya ya rasilimali za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha kwamba ukaguzi wa awali unafanyika katika maeneo ya mradi kabla ya utoaji wa leseni haujafanyika ili kuweza kujiridhisha na maeneo sahihi yaliopo miradi hiyo. Miradi yenyewe ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 79: Miradi ambayo haijaoonekana katika maeneo yake**

| Namba | Jina la mradi | Eneo ulipo |
|---|---|---|
| 1. | Cinnamon Hotel Lited (Marafiki Bungalows (***) | Kiwengwa |
| 2. | Shelly Bungallows (A) | Bwejuu |
| 3. | Nakupenda Stone town (*) | Hurumzi |
| 4. | PPBD Work's Limited (AA) | Bwejuu |
| 5. | Fesste Company Limited (Bondeni Beach House (*) | Jambiani |
| 6. | Zawadi House (APP) | Jambiani |
| 7. | K – Consaltant | Mjini |
| 8. | Grass Root Travel Ltd | Kiembesamaki |
| 9. | G. P Selena (*) | Forodhani |
| 10. | Arco Zanzibar Ltd (*) | Kiembesamaki |

#### 5.8.2.5 Dosari katika uanzishwaji wa Kikosi cha Police Utalii pamoja na matumizi yaliyofanyika shilingi 181,691,420

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii imefanya matumizi ya jumla ya shilingi 181,691,420 kwa ajili ya kuwalipa maposho Kikosi cha Police Utalii kwa ajili ya kusaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni (watalii). Katika kupitia kumbu kumbu zinahusiana na ulipwaji wa fedha hizo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatavyo:-

- Kukosekana kwa nyaraka za maandishi ya kupata Baraka ya uanzishwaji wa Kikosi cha Police Utalii.
- Kukosekana kwa barua kutoka katika Taasisi zilizotoa watendaji wao kwa ajili ya kuunda kikosi cha Police Utalii.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kukosekana kwa uhalali wa malipo yaliyofanyika sambamba na uwepo viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unasimamia na kutekeleza matakwa ya kisheria juu ya uwekwaji wa kumbukumbu za Uanzishwaji wa Kikosi cha Police Utalii ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yanayofanyika kwa ajili ya kikosi hicho.

#### 5.8.2.6 Mapungufu katika mpango wa manunuzi wa mwaka (Annual Procurement Plan)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 linaelekezea juu ya kupanga mipango ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma za Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kamisheni ya Utalii imeandaa Mpango wa Manunuzi kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa Fedha 2022/2023. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuingizwa fedha za Tamasha la ZITITE zenye jumla ya shilingi 133,110,038.18 katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka jambo ambalo linapelekea kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma bila ya kuwa na mpangilio maalum, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha taarifa zote za manunuzi yanayofanyika zinainishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka kwa mujibu ya sheria na miongozi iliyowekwa na Serikali.

### 5.8.2.7 Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 136,536,485.62

Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha kifungu namba 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar limefanya malipo yenye jumla ya shilingi 136,536,485.62 kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama watoa huduma jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na usajili huo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua bidhaa au huduma kwa wafanyabiashara au watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 80: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Namba | Hati namba | Aliyelipwa | Thamani (Shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | J02Pv0358 ya 10/2/2023 | Tea party Zanzibar | 24,486,797 | Malipo kwa ajili ya shughuli za Maonyesho ya ZITITE |
| 2. | J02Pv0356 ya 9/2/2023 | | 4,104,000 | |
| 3. | J02Pv0354 ya 9/2/2023 | | 35,995,592.24 | |
| 4. | J02Pv0464 ya 17/3/2023 | | 5,720,000 | |
| 5. | J02Pv0509 ya 25/03/2023 | 361 Degrees Africa Ltd | 33,115,048.19 | |
| 6. | J02Pv0510 ya 25/3/2023 | | 33,115,048.19 | |
| **Jumla** | | | **136,536,485.62** | |

### 5.8.2.8 Matumizi yaliokiuka Taratibu za Manunuzi Shilingi 136,536,485.62

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya matumizi yenye jumla ya shilingi 136,536,485.62 kwa ajili ya kupatiwa huduma mbalimbali katika tamasha la ZITITE. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi kama ifuatavyo:-

a) Kukosekana kwa ripoti ya tathmini kinyume na kifungu nambari 29(g) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

b) Kutotangazwa kwa Zabuni kinyume na kifungu nambari 29(j) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

c) Kukosekana kwa idadi ya Wazabuni walioomba zabuni kinyume na kifungu nambari 29(l) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

d) Kupata taarifa ya ruhusa ya kutumia njia mbadala kama kifungu nambari 45 (3)(a) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

e) Kutokujumuisha bajeti ya ununuzi na mipango ya ununuzi kinyume na kifungu nambari 42 (d) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

f) Kugawa ununuzi wa bidhaa kwa lengo la kutokutumia utaratibu wa ununuzi kinyume na kifungu nambari 42 (c) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

g) Kutoingizwa katika mpango wa Manunuzi kinyume na kifungu nambari 29(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016

h) Kushindwa kupatiwa taarifa za maandishi kabla ya kuanza manunuzi kinyume na kifungu nambari 43(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

i) Kukosekana kwa Baraka ya Mwanasheria Mkuu ya kuridhia Mkataba.

j) Kukosekana kwa hati za Madai ya Malipo kutoka kwa Mtoa huduma.

Kufanya hivyo kunapelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma unaosababishwa na uvunjwaji wa vifungu vya Sheria katika kufanya manunuzi ya Umma jambo ambalo linaweza kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza matakwa ya Sheria na miongozo iliyopo katika kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa ajili ya kuimarisha maendeleo. Mchanganuo wa matumizi yaliyofanyika bila kufuata utaratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 81: Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi**

| Namba | Hati namba | Aliyelipwa | Thamani (Shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | J02Pv0358 ya 10/2/2023 | Tea party Zanzibar | 24,486,797 | Malipo kwa ajili ya shughuli za Maonyesho ya ZITITE |
| 2. | J02Pv0356 ya 9/2/2023 | | 4,104,000 | |
| 3. | J02Pv0354 ya 9/2/2023 | | 35,995,592.24 | |
| 4. | J02Pv0464 ya 17/3/2023 | | 5,720,000 | |
| 5. | J02Pv0509 ya 25/03/2023 | 361 Degrees Africa Ltd | 33,115,048.19 | |
| 6. | J02Pv0510 ya 25/3/2023 | | 33,115,048.19 | |
| **Jumla** | | | **136,536,485.62** | |

### 5.8.2.9 Kukosekana kwa nyaraka za makubaliano ya kuwasafirisha wageni kutoka Arusha shilingi 6,814,800

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 6,814,800 kupitia hati namba J02Pv0509 kwa ajili ya kuwasafirisha wageni 19 kutoka Arusha kuja Zanzibar kwa lengo la kushiriki katika Tamasha la ZITITE.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa nyaraka ya makubaliano ya kuwasafirisha wageni hao kutoka Arusha kuja Zanzibar ikiwemo hati ya makubaliano yenye kuonyesha muhusika mwenye jukumu la kuwasafirisha wageni pamoja na Barua ya mualiko jambo ambalo linapelekea kutokuthibitika kwa uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unaandaa na kuweka kumbukumbu zote za matumizi yaliyofanyika kama kanuni inavyoelekeza.

### 5.8.2.10 Fedha zilizotumika bila ya kuidhinishwa katika Mpango kazi wa Mwaka shilingi 247,706,500

Kifungu nambari 41(2)(c) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kuwa "Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuisha mpango kazi na mpango wa manunuzi"

Katika kufanikisha shughuli za maonyesho ya Utalii na Uwekezaji zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023 Kamisheni ya Utalii ilitumia jumla ya shilingi 247,706,500 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya maonyesho hayo.

Ukaguzi ulipitia kumbukumbu na nyaraka mbali mbali pamoja na mpango kazi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar na kubaini kuwa fedha zilizotumika kwa ajili ya maonyesho hayo hazikuingizwa katika mpango kazi wa Kamisheni wa mwaka na kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaonyesha kutekelezwa kwa shughuli ambazo hazikupangwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokutekelezeka kwa shuguli zilizopangwa katika mpango kazi kutokana na kutumika kwa fedha hizo kwa ajili ya maonyesho ya Utalii na Uwekezaji na hatimae kupelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unasimamia matumizi yote ya fedha za Umma ili kuhakikisha yanafanywa kulingana na mpango kazi wa mwaka kwa lengo la kuepuka kutumika kwa fedha kinyume na mipango ya Kamisheni iliyowekwa.

### 5.8.2.11 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 27,570,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 27,570,000 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 82: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu**

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | PV 16/04 | Pili Juma Suleiman | 4,900,000 | Malipo ya posho mbali mbali |
| 2. | PV 02/6 ya 02/06/2023 | | 1,700,000 | |
| 3. | PV 02/6 ya 07/06/2023 | | 4,680,000 | |
| 4. | PV 03/6 ya 12/06/2023 | Amina Alawi Yussuf | 3,710,000 | |
| 5. | PV 04/6 ya 12/6/2023 | Pili Juma Suleiman | 5,020,000 | |
| 6. | PV 04/6 ya 06/06/2023 | | 4,680,000 | |
| 7. | PV 06/6 ya 17/06/2023 | | 2,880,000 | |
| **Jumla** | | | **27,570,000** | |

### 5.8.2.12 Kutelekezwa kwa majengo ya Mradi wa Bi Khole yaliyogharimu shilingi 1,791,715,815.36

Kifungu nambari 61(2) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinawata maafisa masuuli kuhakikisha kwamba mali za Umma zinatumika kwa tija na manufaa kulingana na jukumu litakalo tekelezwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,791,715,815.36 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya mradi wa Utalii kwa wote (Bi Khole) ambao ulitekelezwa kwa kipindi cha Aprili, 2019 hadi 2022 katika maeneo ya Bungi.

Pamoja na ujenzi uliofanyika ambao umegharimu fedha nyingi za Serikali, ukaguzi umebaini kutokuanza kutumika kwa mradi huo jambo ambalo huwenda likapelekea kutukufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na hatimae kukosekana kwa tija pamoja na kuingizia hasara Serikali kutokana na gharama kubwa ya fedha za ujenzi zilizotumika.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar inaendelea kutumia fedha za ziada kwa ajili ya kuwalipa walinzi pamoja na watunza Bustani katika maeneyo ya majengo hayo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamisheni imelipa jumla ya shilingi 28,380,000 jambo ambalo ni kuiongezea Serikali gharama bila ya kufikiwa kwa mafanikio yaliokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha jitihada za makusudi zinachukuliwa ili kuendana na uhalisia wa thamani ya fedha iliyotumika na tija itakayopatikana kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali, vyenginevyo kama hali itaendelea kama ilivyo sasa kuna uwezekano mkubwa wa majengo hayo kuchakaa kabla ya gharama zilizotumika kuweza kurejeshwa kupitia mapato yaliyotarajiwa kupatikanwa katika maeneo hayo.

### 5.8.2.13 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 38,835,048

Kwa mujibu wa barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar la tarehe 12/08/2022 lenye kumbukumbu nambari MUUMU. BA.156/370/01/27 inazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 38,835,048 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 83: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | J02PV0509 ya 25/3/2023 | TISS | 361 Degrees Africa Ltd | 33,115,048 | Fedha kwa ajili ya maonesho ya ZITITE |
| 2. | J02PV0464 ya 17/3/2023 | | Tea Party Zanzibar | 5,720,000 | |
| **Jumla** | | | | **38,835,048** | |

## KAMISHENI YA UTALII PEMBA

### 5.8.2.14 Mtumishi anaekaimu nafasi kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa kanuni nambari 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki hakuna nafasi ya kukaimu zaidi ya muda wa miezi kumi na mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea."

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari AC.161/383/01/70 ya tarehe 22/07/2019 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar inaelezea kuhusu kupewa Mtumishi jukumu la kukaimu kwa nafasi ya Uratibu katika Kamisheni ya Utalii Pemba, lakini hadi ukaguzi huu unakamilika bado Mtumishi huyo anaendelea kukaimu nafasi hiyo ambapo ni kipindi cha zaidi ya miaka minne (4) tangu kukaimishwa kwake.

Kufanya hivyo kunapelekea mtumishi huyo kukosa moyo wa kuitendea haki nafasi hiyo kwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni iliyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha mtumishi huyo anathibitishwa au anateuliwa mtumishi mwengine mwenye sifa za toshelevu za kushika nafasi hiyo.

## 5.9 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

### 5.9.1 FUNGU J03 - WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.9.1.1 Malimbikizo ya madeni ya mapato shilingi 6,900,000

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo Zanzibar inazidai taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya shilingi 6,900,000 kutokana na huduma za ukodishwaji wa uwanja wa michezo wa Mao. Madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na wadaiwa kuhakikisha wanalipa madeni wanayodaiwa kwa wakati.

Kufanya hivyo ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangetumika katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali walizojipangia.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza jitihada za kuwakumbusha na kuwafuatilia mara kwa mara wadaiwa wote ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 84: Vilabu vya Mpira wa Miguu vinavyodaiwa na Wizara**

| Namba | Jina la Timu | Deni Halisi (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | KMKM Sports Club | 1,500,000 |
| 2. | Mafunzo Sports Club | 2,700,000 |
| 3. | Zimamoto Sports Club | 2,700,000 |
| **Jumla** | | **6,900,000** |

### 5.9.1.2 Mapungufu yaliojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara kupitia Idara ya maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilitekeleza miradi ya Maendeleo yenye thamani ya shilingi 952,991,339 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya mafunzo ya ushoni na Mabanda ya Kuku kwa Unguja na Pemba ambapo miradi hiyo ilitekelezwa na mkandarasi M/S Shamjo Co. ltd na M/S Star Construction Co. ltd. Ukaguzi baada ya kutembelea maeneo ya miradi ulibaini uwepo wa dosari mbali mbali katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo:-

- Uwepo wa ongezeko la ujenzi wa vyoo viwili na kupelekea vyoo hivyo kuwa vinne (4) badala ya viwili kama vilivyoaninishwa katika mkataba, ambavyo vimetekelezwa wakati ujenzi unaendelea bila kutayarishwa mkataba mwengine wa nyongeza (addendum) wa vyoo hivyo.
- Baadhi ya kazi ambazo zilizokuwa hazikuainishwa kwenye mkataba wa awali kwa Mradi wa Bweleo kama vile utiaji wa tiles kwenye madarasa.

Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa Mapungufu katika suali zima la uibuwaji wa Miradi hiyo kwa Wananchi ikiwemo utekelezaji wa Miradi bila ya kufanyika kwa upembezi yakinifu, kutokushirikishwa kwa walengwa katika uibuwaji wa Miradi na badala yake vijana ambao wanaoshiriki wanakuwa ni wale ambao hawajawa na utayari katika kutekeleza miradi husika.

Kutokuzingatiwa kwa mapungufu hayo katika utekelezaji wa Miradi katika maeneo yanayolengwa kunaweza kukapelekea kutokupatikana tija iliyokusudiwa kwa jamii pamoja na kuitia hasara Serikali kwa kutofikia malengo yake ya ajira kwa vijana.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kunafanyika Upembuzi Yakinifu kabla ya utekelezaji wa mradi kwa lengo la kupatikana tija na kufikia malengo ya Serikali katika kuboresha maisha ya vijana kupitia miradi hiyo.

### 5.9.1.3 Miradi iliyochelewa kukamilika shilingi 952,991,339

Ukaguzi umepitia taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa mabanda ya kuku pamoja na mabanda ya ushoni iliyotekelezwa kwa Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, ukaguzi ulitembelelea maeneo ya miradi hio ili kujiridhisha na hali halisi ya utekelezaji wake ambapo ukaguzi ulibaini dosari zifuatazo:-

- Kutokamilika kwa muda sahihi wa makubaliano ya ujenzi wa mabanda ya kuku.
- Kuwepo kwa nyufa katika kuta za banda la Ushoni liliopo Pemba.
- Kutokukamilika uchimbaji wa Kisima.
- Kutokamilika kwa ujenzi wa vyoo.

Hadi ukaguzi unakamilika miradi ya mabanda ya kuku ya Pangeni na Kangani haijakamilika mabanda ya ushoni ya Bweleo na Kinyasini ukaguzi haujajiridhisha kwakuwa hakuna makabidhiano ya majengo hayo kutoka kwa mkandarasi kwenda kwa Wizara kwa ajili ya matumizi kwa vijana kama ilivyokubaliwa.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi kunapelekea ongezeko kubwa la gharama pamoja na ucheleweshwaji wa huduma kwa jamii zinazonufaika na miradi hio.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa mujibu wa makubaliano yaliyoingiwa kwenye mkataba husika ili kupunguza gharama zinazoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko ya bei ya mara kwa mara.

Hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

### Jadweli Nambari 85: Miradi ambayo imechelewa kutekelezeka

| Mkandarasi | Nambari ya Mkataba | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Idadi miezi ya ucheleweji | Thamani (Tsh) | Mradi/Eneo la mradi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shamjo co ltd | SMZ/SOI/W/ SS/2021-2022/39 | 17/4/2022 | 30/9/2022 | 3 | 280,000,000 | Banda la ushoni Kinyasini Pemba |
| Shamjo co ltd | SMZ/SOI/W/ SS/2021-2022/39 | 29/4/2022 | 30/9/2022 | 3 | 395,152,420 | Mabanda ya kuku Kangani Pemba na Pangeni Unguja |
| Star construction co ltd | SMZ/SOI/W/ RCB/2021/22/42 | 16/5/2022 | 30/11/2022 | 3 | 277,838,919 | Banda la ushoni Bweleo Unguja |
| **Jumla** | | | | | **952,991,339** | |

**WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO PEMBA**

### 5.9.1.4 Kutokuwepo kwa hatimiliki kwa baadhi ya mali za Wizara

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Pemba inamiliki mali nyingi zikiwemo majengo na viwanja vya michezo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwepo kwa hatimiliki kwa baadhi ya mali za Wizara jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa migogoro baina ya Wizara na wananchi pale itakapotokezea wananchi kuvamia maeneo hayo kwa ajili ya shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Kutokuwepo kwa hatimiliki kumetokana na kuwepo kwa uwelewa mdogo wa sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo miongozo ya kiutumishi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa wizara kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kuhakikisha zinapatikana hatimiliki za mali zikiwemo viwanja na majengo. Orodha ya mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 86: Jengo na viwanja ambavyo havina hati miliki

| Namba | Jina la Kiwanja | Eneo Kilipo | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiwanja cha Mradi wa Vijana wa Ufugaji wa Kuku | Kangagani - Chake Chake | Viwanja vilivyopimwa lakini havina hati miliki. |
| 2. | Kiwanja cha Mpira 4 In 1 | Skuli ya Sekondari Micheweni | |
| 3. | Kiwanja cha Mpira 4 In 1 | Skuli ya Sekondari M/ Mdogo | |
| 4. | Kiwanja cha Mpira 4 In 1 | Polisi Wete | |
| 5. | Kiwanja cha Mpira 4 In 1 | Skuli ya Mtangani Mkoani | |
| 6. | Kiwanja cha Mpira 4 In 1 | Kangagani – Mkoani | |
| 7. | Kiwanja cha Mpira wa Miguu | Kishindeni - Micheweni | |
| 8. | Kiwanja cha Mpira wa Miguu | Ndugukitu Chake Chake | |
| 9. | Kiwanja cha Kituo cha Wajasiriamali Vijana | Pujini - Chake Chake | |
| 10. | Kiwanja cha Mradi wa Ushoni Vijana | Weni - Wete | |
| 11. | Kiwanja cha mpira wa Net ball, Basket Ball, Volley Ball na Long Tenis | Tenis – Chake Chake | |
| 12. | Jengo la Sinema | Wete | |

#### 5.9.1.5 Malipo ya safari kikazi yaliyokosa uthibitisho shilingi 3,840,000

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 3,840,000 kupitia hati nambari 02/08 ya tarehe 25/08/2022 ambapo maelezo yanafafanua kwamba watumishi hao walisafiri mnamo tarehe 18/08/2022 saa 19:40 PM kwa tiketi nambari 44312688629 ya ndege ya Unity Air kwenda Unguja kikazi, Watumishi hao ni Ndugu Salma Kombo Moh'd na Ndugu Sheila Makungu Mwinyi.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa uthibitisho wa kusafiri katika orodha maalumu za abiria wanaosafiri (Manifest sheets) jambo ambalo linatia shaka juu ya uhalali wa malipo yaliofanywa kwa watumishi hao. Aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka halisi za malipo kwa wakati ili kuthibitisha uhalali wa malipo.

#### 5.9.1.6 Ukiukwaji wa Maagizo ya Baraza la Mapinduzi

Kwa mujibu wa kanuni nambari 20(4) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Iwapo Mtumishi wa Umma atateuliwa kushikilia nafasi hiyo ya ngazi ya Uteuzi wa Rais atapewa barua rasmi ya kukaimu itakayoonesha tarehe ya kuanza kukaimu na itakapofikia muda wa kumaliza kukaimu mtumishi huyo atapewa barua yake ya kusitisha kukaimu".

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeridhia barua ya kwenda likizo kwa Afisa Mdhamini kwa barua yenye kumbukumbu namba KUU/P/OPF/S/KH.M.KH.611/45 inayoeleza "Napenda kukujulisha kwamba, kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba BLM/64/LMW/C.4/VOL.V/95 ya tarehe 05/04/2023 kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi inayomkaimisha **ndugu Khamis Masoud Khamis** nafasi ya Afisa Mdhamini Pemba kuanzia tarehe 17/04/2023 hadi tarehe 29/05/2023 pale Afisa Mdhamini atakaporejea kazini".

Pamoja na uwepo wa barua halali ya kukaimisha nafasi ya Afisa Mdhamini ukaguzi umebaini Afisa Mdhamini wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kukaidi maagizo halali ya Serikali yaliyomtaka kwenda likizo kwa mujibu wa barua ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuendelea kufanya malipo mbali mbali kwa kipindi ambacho alikuwa likizo kwa mujibu wa barua niliyoinakili hapo juu jambo ambalo ni kinyume na toleo la barua husika pamoja na miongozo ya fedha.

Kutokana na ukiukwaji wa taratibu za kiutumishi kumepelekea kuendelea kufanya maamuzi, kutoa maelekezo ya kiofisi pamoja na uidhinishaji wa matumizi mbali mbali ya fedha kinyume na matakwa ya kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha unazingatia misingi ya Utumishi wa Umma kama inavyoelekeza ikiwa ni pamoja na kujiepusha katika kujiingiza kwenye mgongano wa kimaslahi kwa kuondoa utashi binafsi na badala yake kuendelea kujenga imani kwa watumishi wanaokaimishwa nafasi mbali mbali pale inapohitajika.

### 5.9.1.7 Dosari katika makusanyo na matumizi ya mapato shilingi 2,130,000

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba imekusanya jumla ya shilingi 2,130,000 kupitia Uwanja wa Michezo Gombani. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokutumia mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji mapato, kutokuingizwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina, na kukosekana kwa idhini ya matumizi ya mapato hayo kutoka Hazina jambo ambalo linatia shaka juu ya usahihi wa taarifa za mapato na uhalali wa matumizi ya mapato hayo, aidha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Dosari hii imetokana na uwepo wa udhaifu katika udhibiti wa ndani na kukosekana kwa umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia mapato hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kubuni njia bora zaidi za ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kwamba mapato hayo yanaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina au kutumika kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

### 5.9.1.8 Kutokutumika kwa mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji wa mapato shilingi 30,678,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato. Aidha toleo la barua yenye kumb. No.CA.319/398/01/02/19 ya tarehe 14/02/2022 kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafafanua kwamba makusanyo yote ya Taasisi za Umma yafanyike kupitia Mfumo wa ZANMALIPO".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mapato yenye jumla ya shilingi 30,678,000 yamekushanywa na idara za BASSFU, Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji kwa miezi ya Julai, 2022 hadi Juni, 2023 kupitia stakabadhi za mkononi badala ya kutumia mfumo wa ZanMalipo jambo ambalo linaweza kupelekea kupungua kwa mapato ya Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria na muongozo kama niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kukusanya mapato kupitia mfumo wa ZanMalipo.

### 5.9.1.9 Upotevu wa fedha za Makusanyo shilingi 9,090,000

Kifungu nambari 30(1-4) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinamtaka "Afisa Masuuli kuwajibika kwa uwezo wake wote katika suala la usimamizi katika ukusanyaji wa mapato".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 9,090,000 zimekusanywa kupitia nambari za udhibiti za mfumo wa ZanMalipo, dosari iliyobainika ni kutokuonekana kwa mapato hayo katika taarifa za benki jambo ambalo linatia shaka juu ya usahihi na uhalali wa mapato hayo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kwa mujibu wa taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na kuonekana kwa mapato hayo katika taarifa za benki. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 87: Mapato ambayo hayakuonekana katika taarifa za benki**

| Mwezi | Idara ya Habari Maelezo (Tshs) (A) | Tume ya Utangazaji (Tshs) (B) | Jumla (Tshs) (A+B) |
|---|---:|---:|---:|
| Oktoba, 2022 | 740,000 | - | 740,000 |
| Novemba, 2022 | 280,000 | - | 280,000 |
| Desemba, 2022 | 120,000 | - | 120,000 |
| Januari, 2023 | 320,000 | 1,500,000 | 1,820,000 |
| Febuari, 2023 | 320,000 | - | 320,000 |
| Machi, 2023 | 300,000 | 5,180,000 | 5,480,000 |
| Aprili, 2023 | 150,000 | - | 150,000 |
| Mei, 2023 | 60,000 | - | 60,000 |
| Juni, 2023 | 120,000 | - | 120,000 |
| **Jumla** | **2,410,000** | **6,680,000** | **9,090,000** |

### 5.9.1.10 Kutokuwiana kwa baadhi ya taarifa za mapato za Wizara

Kwa mujibu wa muongozo wa utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za hesabu (IPSAS 1) unafafanua kwamba taarifa za fedha zinazohusiana na mapato na matumizi zinapaswa kuwa na uwiano.

Katika ukaguzi uliofanyika imebaini kwamba kutokuwepo kwa uwiyano wa taarifa za fedha baina ya taarifa zilizoripotiwa katika daftari la mapato, taarifa za benki pamoja na risiti za mapato zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, jambo ambalo linapelekea kutokujulikana kwa mapato sahihi yaliyokusanywa. Aidha ni kwenda kinyume na muongozo wa utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za hesabu kama niliounakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa kutokuongeza umakini katika kuzipitia taarifa za fedha ili kujiridhisha iwapo fedha zinazonekana katika taarifa za fedha zinawiyana.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha wanaandaa usuluhishi wa kibenki kwa kila mwezi ili kuweza kubaini sababu iliyochangia uwepo wa tofauti ya mapato iliyoripotiwa benki na taarifa ya mapato iliyorikodiwa katika daftari la kukusanyia mapato. Mchanganuo wa taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 88: Kutokuwiyana kwa baadhi ya taarifa za mapato za Wizara

| Mwezi | Idara | Daftari la Mapato (Tsh) | Taarifa za Benki (Tsh) | Risiti za Makusanyo (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| Septemba, 2022 | | 1,219,500 | 1,052,500 | 930,000 |
| | | 1,175,000 | 1,302,000 | 1,070,000 |
| Januari, 2023 | | 4,944,000 | 4,934,999 | 4,020,000 |
| | | 960,000 | 640,000 | 640,000 |
| Februari, 2023 | | 2,055,000 | 2,369,000 | 1,175,000 |
| | | 1,520,000 | 1,205,000 | 1,525,000 |
| Machi, 2023 | BASSFU | 1,920,000 | 1,920,000 | 1,025,000 |
| | Habari Maelezo | 800,000 | 500,000 | 500,000 |
| Aprili, 2023 | | 150,000 | 154,500 | 75,000 |
| | | 550,000 | 400,000 | 400,000 |
| Mei, 2023 | | 2,579,500 | 2,279,500 | 1,605,000 |
| | | 360,000 | 300,000 | 300,000 |
| Juni, 2023 | | 854,500 | 854,500 | 640,000 |
| | | 120,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **19,207,500** | **17,911,999** | **13,905,000** |

## Dosari katika udhibiti wa mfumo wa ZanMalipo

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba inakusanya mapato kupitia mfumo wa ZanMalipo kwa kila Idara zikiwemo Idara ya BAKIZA, Tume ya Utangazaji na Idara ya Habari Maelezo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa dosari ya upatikanaji wa taarifa za makusanyo ya Idara nyengine ndani ya Idara moja, hali hii imetokana na ukaguzi kuingia katika mfumo kupitia Tume ya Utangazaji Pemba na kuangalia makusanyo yake na kubaini uwepo wa taarifa za makusanyo ya BAKIZA Unguja na Idara ya Habari Maelezo ndani yake.

Kuwepo kwa dosari hizi kunatia shaka juu ya udhibiti wa mfumo wa ndani wa Wizara,

ambapo inaweza kupelekea kuingizwa taarifa zisizo sahihi na halisi ndani ya mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba kuhakikisha unaweka udhibiti katika mfumo wa ZanMalipo ili kuweza kupatikana kwa taarifa sahihi na zinazohitajika kwa idara husika. Hali halisi ya mchanganyiko wa taarifa za mapato ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 89: Mchanganyiko wa taarifa za mapato

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1003 - BAKIZA – UNGUJA** | | | | | | | |
| **Tanzanian Shilling (TZS) Collections** | | | | | | | |
| | **Control Number** | **Bill Reference** | **Payer/Item details** | **Remark** | **Generated Date** | **Expiry Date** | **Billed Amount** |
| 1. | 200400000421 | 2004009286222857344139 | ALI HAMADI ALI | | 10/13/22 | 10/19/22 | 500.00 |
| 2. | 200400000422 | 2004009286222857344139 | ALI HAMADI ALI | | 10/13/22 | 10/19/22 | 500.00 |
| | | | | | | **Currency Total : TZS:** | **1,000.00** |
| **1005 - ZANZIBAR BROADCASTING COMMISSION** | | | | | | | |
| **Tanzanian Shilling(TZS) Collections** | | | | | | | |
| **Sn.** | **Control Number** | **Bill Reference** | **Payer/Item details** | **Remark** | **Generated Date** | **Expiry Date** | **Billed Amount** |
| 1. | 200400001481 | 2004014086231512834544 | PEMBA CABLE CENTER | | 3/27/23 | 3/30/23 | 4,680,000.00 |
| 2. | 200400001361 | 2004014066235928457555 | PDS ZANZIBAR | | 3/7/23 | 3/31/23 | 100,000.00 |
| 3. | 200400001001 | 2004008012232103248402 | RADIO JAMII MICHEWENI | | 1/12/23 | 1/14/23 | 500,000.00 |
| 4. | 200400000981 | 2004014010232137554540 | RADIO JAMII MICHEWENI | | 1/10/23 | 1/11/23 | 1,000,000.00 |
| | | | | | | **Currency Total : TZS:** | **6,280,000.00** |
| **1006 - IDARA YA HABARI MAELEZO** | | | | | | | |
| **Tanzanian Shilling(TZS) Collections** | | | | | | | |
| **Sn.** | **Control Number** | **Bill Reference** | **Payer/Item details** | **Remark** | **Generated Date** | **Expiry Date** | **Billed Amount** |
| 1. | 200400001781 | 2004009117231723963698 | ZBC | | 4/27/23 | 5/27/23 | 100,000.00 |
| 2. | 200400001262 | 2004011046233637666326 | SKULI YA MNGELEMA MSINGI | | 2/15/23 | 2/22/23 | 30,000.00 |
| 3. | 200400001261 | 2004011046233637666326 | SKULI YA MNGELEMA MSINGI | | 2/15/23 | 2/22/23 | 30,000.00 |
| 4. | 200400001221 | 2004011044235352864040 | BIRIKAU SEKONDARI | | 2/13/23 | 2/23/23 | 60,000.00 |
| 5. | 200400000901 | 2004009348225419800690 | WIZARA YA KILIMO PEMBA | | 12/14/22 | 1/13/23 | 30,000.00 |

| Sn. | Control Number | Bill Reference | Payer/Item details | Remark | Generated Date | Expiry Date | Billed Amount |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | 200400000881 | 2004010347224157725081 | WAKALA WA SEREKALI MTANDAO PEMBA | | 12/13/22 | 1/12/23 | 60,000.00 |
| 7. | 200400000861 | 2004011340223048634064 | ZCSRA PEMBA | | 12/6/22 | 1/5/23 | 60,000.00 |
| 8. | 200400000841 | 2004009339221139244592 | TUME YA UKIMWI | | 12/5/22 | 12/25/22 | 300,000.00 |
| | 200400000821 | 2004011336220636080680 | IDARA YA MIFUGO | | 12/2/22 | 12/7/22 | 60,000.00 |
| 10. | 200400000801 | 2004010335220650858323 | SKULI YA MAVUNGWA | | 12/1/22 | 12/3/22 | 30,000.00 |
| 11. | 200400000761 | 2004014333225626772192 | PENBRO | | 11/29/22 | 12/4/22 | 30,000.00 |
| 12. | 200400000741 | 2004014332221301941312 | WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE PEMBA | | 11/28/22 | 12/28/22 | 60,000.00 |
| 13. | 200400000721 | 2004013332220310110843 | W/M/JAMII /JINSIA WAZEE NA WATOTO | | 11/28/22 | 12/8/22 | 60,000.00 |
| 14. | 200400000701 | 2004008329224138319955 | MAHKAMA KUU PEMBA | | 11/25/22 | 12/10/22 | 330,000.00 |
| 15. | 200400000681 | 2004014328222010881193 | MAHKAMA KUU PEMBA | | 11/24/22 | 11/29/22 | 330,000.00 |
| 16. | 200400000661 | 2004012326220653863171 | ZCSRA PEMBA | | 11/22/22 | 11/29/22 | 60,000.00 |
| 17. | 200400000581 | 2004011306223021240573 | WAKALA WA SERIKALI MTANDAO PEMBA | | 11/2/22 | 11/17/22 | 60,000.00 |
| 18. | 200400000561 | 2004008305220955784564 | WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE PEMBA | | 11/1/22 | 11/11/22 | 60,000.00 |
| 19. | 200400000521 | 2004014293225848502253 | ZURA | | 10/20/22 | 10/25/22 | 120,000.00 |
| 20. | 200400000501 | 2004010293221840822866 | WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE | | 10/20/22 | 10/23/22 | 60,000.00 |
| 21. | 200400000483 | 2004010290221118192161 | WAKALA WA SEREKALI MITANDAO | | 10/17/22 | 10/27/22 | 60,000.00 |
| 22. | 200400000482 | 2004008290221808498743 | KAMESHENI YA UTALII | | 10/17/22 | 10/21/22 | 400,000.00 |

| Sn. | Control Number | Bill Reference | Payer/Item details | Remark | Generated Date | Expiry Date | Billed Amount |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 23. | 200400000481 | 2004008290220430081081 | WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE | | 10/17/22 | 10/20/22 | 60,000.00 |
| 24. | 200400000441 | 2004012286221350708859 | WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE | | 10/13/22 | 10/16/22 | 60,000.00 |
| 25. | 200400000381 | 2004011285225332040780 | KAMISHENI YA UTALI | | 10/12/22 | 10/16/22 | 400,000.00 |
| 26. | 200400000261 | 2004008279223900472009 | WAKALA WA SEREKALI MTANDAO | | 10/6/22 | 10/16/22 | 60,000.00 |
| | | | | | | **Currency Total : TZS:** | **2,970,000.00** |
| **1007 – COSOZA** | | | | | | | |
| **Tanzanian Shilling(TZS) Collections** | | | | | | | |
| **Sn.** | **Control Number** | **Bill Reference** | **Payer/Item details** | **Remark** | **Generated Date** | **Expiry Date** | **Billed Amount** |
| 1. | 200400001741 | 2004010111234550700261 | KHAMIS ABDALLAH ALLY | | 4/21/23 | 5/21/23 | 5,000.00 |
| 2. | 200400001521 | 2004009088235035830009 | MBAROUK FAKI MBAROUK | | 3/29/23 | 4/28/23 | 3,000.00 |
| | | | | | | **Currency Total : TZS:** | **8,000.00** |

### 5.9.1.12 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya mauzo ya picha za viongozi

Kifungu Nambari 30(1-4) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za umma ya 2016 kinaelezea kwamba Afisa Masuuli awajibike kwa uwezo wake wote katika suala la usimamizi katika ukusanyaji wa mapato.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara imepokea picha za viongozi wa kitaifa bila ya makabidhiano na kutoa kwa kuziuza picha hizo bila uwepo wa kumbukumbu sahihi za mauzo hayo. Aidha imebainika kutokujulika kwa idadi ya picha zilizopokelewa na zilizouzwa jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha zitokanazo na mauzo ya picha hizo ambapo pia ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa uimara wa udhibiti wa ndani na kutokuongeza umakini katika kukusanya na kudhibiti mapato ili kuepusha uwezekano wa upotevu wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaweka udhibiti katika ukusanyaji wa mapato ili kuweza kupatikana kwa taarifa sahihi za mapato hayo.

### 5.9.1.13 Dosari katika upokeaji na utumiaji wa fedha kwa baadhi ya Idara

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya idara zilizomo ndani ya Wizara ambazo ni BAKIZA, Hakimiliki, Tume ya Utangazaji, Baraza la Michezo Taifa na Baraza la Vijana zinaingiziwa fedha za matumizi kutoka Afisi Kuu za Idara hizo Unguja kupitia Hesabu ya Amana (Deposite Account) inayosimamiwa na Wizara ya Fedha kutokana na Idara hizo kutokuwa na Hesabu ya kupokea na kutoa fedha hizo na baadae Idara hizo kuziomba fedha hizo kwa ajili ya matumizi.

Dosari iliyobainika ni kutokujulikana na kwa fedha zilizoingizwa na kutumika kutokana na kutokupatikana kwa taarifa za benki, na taarifa za matumizi ya fedha hizo jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza udhibiti katika upokeaji wa fedha za matumizi ili kuepusha uwezekano wa kufanyika matumizi mabaya ya fedha hizo.

#### 5.9.1.14 Matumizi yaliyofanywa bila ya bajeti shilingi 42, 889,000

Mapato na matumizi ya fedha za Serikali yanapaswa kufanyiwa bajeti na baadae kuidhinishwa bajeti hiyo na Serikali kupitia Baraza la Wawakilishi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara imefanya matumizi yenye jumla ya shilingi 42,889,000 kupitia Hesabu ya Youth and Development bila kuwepo kwa bajeti iliyoandaliwa na kupitishwa na Mamlaka husika ili fedha hizo ziweze kutumika kihalali, jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za Umma, aidha ni kwenda kinyume na miongozo ya kisheria iliyopo ya kitaifa na kimataifa.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kuandaa bajeti na kufanya malipo kwa mujibu wa bajeti iliyoandaliwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuandaa bajeti na kufanya malipo kulingana na bajeti iliyoandaliwa.

## 5.10 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

### 5.10.1 FUNGU K01 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.10.1.1 Malipo ya ubani yaliolipwa kinyume na muongozo wa Utumishi

Kwa mujibu wa Kanuni namba 121(5) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kuwa "Ikiwa mtumishi atafiwa na mzazi wake baba au mama, mume au mke au mtoto wa kumzaa atapatiwa malipo ya ubani. Ikiwa kifo hicho kimetokea nje ya kituo chake cha kazi lakini ndani ya Tanzania, Taasisi inaweza kumsaidia nauli ya usafiri ya kwenda na kurudi msibani".

Aidha, kwa mujibu wa muongozo wenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/5 wa tarehe 07/12/2020 unaeleza ya kwamba mtumishi aliefiliwa atapatiwa ubani wa mara mbili ya kima cha chini cha mshahara wa mtumishi wa kawaida ambacho ni sawa na shilingi 600,000.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya watumishi 44 wamelipwa malipo ya ubani ya shilingi 13,200,000 ambapo malipo hayo ni sawa na shilingi 300,000 kwa kila mfiwa jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni na muongozo wa malipo niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha unatekeleza miongozo iliotolewa ili kuepusha kujitokeza kwa migogoro ya baadhi ya watumishi kulalamikia stahiki pungufu wanazolipwa ukilinganisha na idara au Taasisi nyengine. Aidha, ni vyema jitihada za makusudi kuchukuliwa ikiwemo uandaaji wa bajeti ya kutosha ili kuweza kukabiliana na changamoto ya uwepo wa malipo pungufu na hatimae kuweka usawa wa malipo yanayolingana na Taasisi nyengine. Mchanganuo wa malipo yaliofanyika kinyume na utaratibu wa muongozo wa Utumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 90: Malipo ya ubani yaliolipwa pungufu

| Namba | Namba ya ajira | Jina la Mtumishi | Kituo Cha Kazi | Tarehe ya kifo | Tarehe aliyo wasilisha barua |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 550893 | Tatu Moh'd Hassan | Skuli ya Bumbwini Msingi | 16/09/2022 | 10/11/2022 |
| 2. | 824132 | Sheha Yahya Sheha | Chumbuni Msingi | 17/09/2022 | 17/10/2022 |
| 3. | | Khadija Abubakar Hussein | Unguja Ukuu Sekondari | 27/06/2022 | 27/7/2022 |
| 4. | | Mtumwa Khamis Ali | Mwanakwerekwe 'B' Sekondari | 25/08/2022 | 01/09/2022 |
| 5. | 825883 | Halima Ameir Haji | Skuli ya Mandalizi Msingi 'B' | 09/12/2021 | 04/01/2022 |
| 6. | 755430 | Arafa Puju Salum | Kijitoupele 'B' | 02/07/2022 | 08/07/2022 |
| 7. | 930905 | Zaituni Kh Haji | Bungi | 19/10/2022 | 25/11/2022 |
| 8. | 523400 | Mafunda Maftah Fadhil | Mandalizi na Msingi Jang'ombe 'B' | 10/10/2022 | 27/10/2022 |
| 9. | 729876 | Maimuna Juma Makame | Jumbi Maandalizi | 10/09/2022 | 20/09/2022 |
| 10. | 427491 | Amina Hussein Mtumwa | Bububu 'A' Msingi | 03/07/2022 | 01/11/2022 |
| 11. | 118319 | Mtumwa Khamis Kai | Kiyongwe Msingi | 13/09/2022 | 29/11/2022 |
| 12. | | Mwaka Ali Haji | Kijigoni Maandalizi | 06/11/2022 | 18/11/2022 |

| Namba | Namba ya ajira | Jina la Mtumishi | Kituo Cha Kazi | Tarehe ya kifo | Tarehe aliyo wasilisha barua |
|---|---|---|---|---|---|
| 13. | 375159 | Patima Chum Hamad | Tunguu Ms/ Maandalizi | 22/10/2022 | 9/11/2022 |
| 14. | 431135 | Khadija Nassor Ali | Ndijani Mseweni | 20/11/2022 | 28/112022 |
| 15. | | Aziza Amour Mussa | Hub Mahonda | 10/07/2021 | 31/08/2021 |
| 16. | 919996 | Ali Haji Khamis | Mkwajuni Sekondari | 06/09/2022 | 07/10/2022 |
| 17. | 825648 | Arafa Ali Shoka | Kilima Hewa 'B' Msingi | 09/10/2022 | 08/11/2022 |
| 18. | | Issa Mohammedi Maulid | Ndijani Sekondari | 23/07/2022 | 18/10/2022 |
| 19. | 535024 | Arafa Rashid Khamis | Chuini Sekondari | | 05/10/2022 |
| 20. | | Abeida Khamis Moh'd | Kitope Msingi | 16/03/2021 | 18/08/2022 |
| 21. | 819613 | Ruwaida Juma Abdalla | Uzini Msingi | 04/08/2022 | 30/08/2022 |
| 22. | 745865 | Zahra Tahir Ali | Shaurimoyo | 23/09/2022 | 26/10/2022 |
| 23. | 731113 | Ali Nassor Ali | Tunguu Sekondari | 20/11/2022 | 05/12/2022 |
| 24. | 721329 | Mati Mussa Amour | Chaani Sekondari | 28/10/2022 | 06/12/2022 |
| 25. | 436636 | Jokha Ali Ramadhan | K/Samaki Msingi 'A' | 25/10/2022 | 11/11/2022 |
| 26. | 729998 | Kazija Issa Mgongo | Jang'ombe 'A' | 19/09/2022 | 01/12/2022 |
| 27. | 836697 | Chausiku Khatib Masoud | Kajificheni | 21/06/2022 | 30/06/2022 |
| 28. | 231344 | Mwatatu Ali Masoud | Unguja Ukuu Msingi | 12/11/2022 | 13/12/2022 |
| 29. | 721507 | Omar Ali Omar | Kituo Cha Walimu Cha Taifa(NTRC) | 10/11/2022 | 30/11/2022 |
| 30. | 574423 | Rajab Hassan Abdalla | Chukwani Msingi | 11/11/2022 | 05/12/2022 |
| 31. | 135678 | Mwanamrisho Ali Masoud | K/Upele 'B' | 12/11/2022 | 13/12/2022 |
| 32. | | Bakari Khatib Ame | Gamba Sekondari | 21/07/2022 | 03/08/2022 |

| Namba | Namba ya ajira | Jina la Mtumishi | Kituo Cha Kazi | Tarehe ya kifo | Tarehe aliyo wasilisha barua |
|---|---|---|---|---|---|
| 33. | | Fathiya Omar Khatib | Muungano Msingi | 02/08/2022 | 04/10/2022 |
| 34. | 525726 | Ridhia Hassan Haji | Mwanakwerekwe 'A' | 09/10/2022 | 26/10/2022 |
| 35. | 466903 | Kazija Choum Hamad | Kibele Msingi | 22/10/2022 | 22/11/2022 |
| 36. | | Miza Makame Suweid | Msingi Bwereu | 05/06/2022 | 13/06/2022 |
| 37. | 221973 | Mwantanga Khamis Amour | Mwanakwerekwe 'C' Sekondari | 30/07/2022 | 16/08/2022 |
| 38. | 221762 | Sulaiman Salum Khatib | Donge Mtambile | 03/11/2022 | 15/11/2022 |
| 39. | 336887 | Bimkubwa Abdalla Saleh | Mwanakwerekwe 'G' | 15/09/2022 | 06/12/2022 |
| 40. | 275425 | Makame Juma Makame | Makoba Sekondari | 10/09/2022 | 20/09/2022 |
| 41. | | Zainab Sururu Vuai | Mgonjani | 04/11/2022 | 21/01/2022 |
| 42. | 350778 | Jina Juma Makame | Mgambo Ms na Sekondari | 10/09/2022 | 20/09/2022 |
| 43. | 632100 | Subira Suleiman Omar | Regeza Mwendo Msingi | 21/11/2022 | 04/12/2022 |
| 44. | 478173 | Zainab Ali Said | K/Samaki 'A' | 11/11/2022 | 15/11/2022 |

#### 5.10.1.2 Wafanyakazi waliolipwa mishahara wakiwa wamemaliza muda wao wa utumishi Serikalini shilingi 25,062,000

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika Wizara ya Elimu kuendelea kuwalipa mshahara baadhi ya watumishi ambao wamemaliza muda wao wa utumishi na kutakiwa kustaafu kwa mujibu wa Sheria kwa kutimiza muda wao wa utumishi Serikalini na kuendelea kulipwa mshahara wenye thamani ya shilingi 25,062,000**.**

Kulipa mishahara wakati mtumishi ameshamaliza muda wake wa utumishi kunapelekea kuitia hasara Serikali na kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma na ni kwenda kinyume na Sheria nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya 2011.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuhakikisha inachukua jitihada za makusudi kwa kuweka mfumo ambao utaweza kuwasaidia kuweza kutambua watumishi wanaotakiwa kustaafu kwani ukiangalia ni taasisi yenye idadi ya watumishi wengi hivyo itawawia vigumu kwa kufanya manual pasi na kutumia mfumo wa kileo ambao ndio utawapa taarifa kitengo kinacho husiana na masuala ya kiutumishi. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 91: Wastaafu ambao waliendelea kupokea mishahara nje ya muda wa utumishi**

| Nambari ya Ajira | Mwaka wa kuzaliwa | Mwaka wa kustaafu | Kiwango cha mshahara (Tshs) | Miezi ya ziada | Malipo nje ya Utumishi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 231263 | 1962 | 30/06/2022 | 942,000 | 6 | 5,652,000 |
| 222061 | 10/10/1962 | 09/10/2022 | 806,000 | 9 | 7,254,000 |
| 217234 | 1962 | 30/06/2022 | 1,322,000 | 5 | 6,610,000 |
| 120602 | 1962 | 30/06/2022 | 1,109,200 | 5 | 5,546,000 |
| **Jumla** | | | | | **25,062,000** |

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI PEMBA

### 5.10.1.3 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 86,131,920

Kanuni nambari 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 86,131,920 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kufanya malipo kwa njia ya benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 92: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu bila ya kufuata taratibu

| Namba | Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 66/05 ya 19/05/2023 | 035413 | 1,350,000 | WEMA | Malipo kwa ajili safari kikazi |
| 2. | 64/05 ya 19/05/2023 | 035410 | 305,000 | | |
| 3. | 71/05 ya 26/5/2023 | 035412 | 1,660,000 | | Malipo kwa ajili ya mazingira magumu |
| 4. | 51/05 ya 16/05/2023 | 035314 | 6,538,000 | | Malipo kwa ajili kushiriki kwenye tamasha |
| 5. | 60/04 ya 17/04/2023 | 034552 | 7,000,000 | | Malipo kwa ajili ya mafunzo ya walimu wapya |
| 6. | 69/05 ya 17/05/2023 | 035412 | 3,050,000 | | Malipo kwa ajili ya metroni. |
| 7. | 57/04 ya 03/04/2023 | 034487 | 270,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mchele |
| 8. | 51/04 ya 04/04/2023 | 034486 | 3,000,000 | | Malipo ya posho mbali mbali |
| 9. | 49/04 ya 31/03/2023 | 034487 | 180,000 | | |
| 10. | 44/04 ya 04/04/2023 | 034486 | 3,050,000 | | |
| 11. | 37/04 ya 19/04/2023 | 034975 | 1,270,000 | | |
| 12. | 32/04 ya 21/4/2023 | 034633 | 1,124,040 | | Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi waliozuiliwa mishahara yao |
| 13. | 11/01 ya 09/01/2023 | 032304 | 4,380,000 | | Malipo kwa ajili ya kuwapatia mafunzo elekezi waajiriwa wapya. |
| 14. | 12/01 ya 13/01/2023 | 032305 | 700,000 | | Malipo ya Ununuzi wa umeme |
| 15. | 10/01 ya 09/01/2023 | 032304 | 900,000 | | Malipo kwa ajili ya upakiaji na usambazaji wa viti na meza. |
| 16. | 08/01 ya 09/01/2023 | 032304 | 600,000 | | Malipo kwa ajili ya matibabu ya mwaalimu. |
| 17. | 31/05 ya 19/5/2023 | 036572 | 3,000,000 | | Malipo kwa ajili ya walimu wa (Part time) |
| 18. | 30/06 ya 31/55/2023 | 035999 | 499,500 | | Malipo ya ununuzi wa chakula |

| Namba | Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 19. | 43/10 ya 15/08/2022 | 030108 | 912,380 | | Malipo kwa ajili ya utengezaji na utiaji wa dirisha na mlango |
| 20. | 39/10 ya 18/10/2022 | 030108 | 2,000,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa umeme |
| 21. | 58/09 ya 19/09/2022 | 029495 | 3,050,000 | | Malipo ya posho wanazolipwa metroni |
| 22. | 37/10 ya 10/10/2022 | 030110 | 200,000 | | Malipo kwa ajili ya kuungiwa umeme |
| 23. | 34/10 ya 18/10/2022 | 030108 | 750,000 | | Malipo ya awamu ya tatu ya ununuzi wa vespa |
| 24. | 33/10 ya 12/10/2022 | 030110 | 3,565,000 | | Malipo ya watendaji walioshiriki katika usaili wa walimu. |
| 25. | 32/10 ya 27/09/2022 | 029875 | 450,000 | | Malipo kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Wizara. |
| 26. | 31/10 ya 10/10/2022 | 030110 | 800,000 | | Malipo kwa ajili ya kuhamisha vitabu. |
| 27. | 30/10 ya 10/10/2022 | 030110 | 200,000 | WEMA | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 28. | 24/10 ya 19/10/2022 | 029374 | 4,050,000 | | Malipo kwa ajili ya ukodishwaji wa nyumba |
| 29. | 16/10 ya 10/10/2022 | 030115 | 700,000 | | Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa umeme |
| 30. | 01/10 ya 10/10/2022 | 030108 | 2,700,000 | | Malipo ya posho kwa walimu wa (Part time) |
| 31. | 07/02 ya 20/02/2023 | 033246 | 4,780,000 | | Malipo kwa ajili ya walimu wanaofanya mitihani |
| 32. | 08/02 ya 20/02/2023 | 033247 | 1,190,000 | | Malipo kwa ajili ya uhamishaji wa mali chakavu. |
| 33. | 108/06 ya 27/06/2023 | 036869 | 3,450,000 | | Malipo kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya WEMA. |
| 34. | 109/6 ya 26/06/2023 | 036872 | 1,150,000 | | Malipo kwa ajili ya watendaji wa WEMA. |
| 35. | 109/06 ya 28/06/2023 | 036872 | 710,000 | | Malipo kwa ajili ya safari kikazi. |

| Namba | Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 36. | 109/06 ya 28/06/2023 | 036872 | 7,528,000 | WEMA | Malipo kwa ajili ya matumzi mbali mbali ya WEMA. |
| 37. | 109/06 ya 28/6/2023 | 036872 | 1,420,000 | | Malipo kwa ajili ya safari kikazi |
| 38. | 110/06 ya 28/06/2023 | 036873 | 7,650,000 | | Malipo kwa ajili ya watendaji wa Wizara. |
| **Jumla** | | | **86,131,920** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.10.1.4 Dosari katika matumizi ya mafuta lita 2309

Kanuni nambari 124(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vinavyotumika katika taasisi yake vinakuwa na buku linaloonyesha matumizi ya chombo kwa safari husika (log Book)".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya lita 1,013 za petrol na lita 1,296 za Diesel zimeingizwa na kutumika katika Gari No. SMZ 1058A bila ya kuwepo kwa buku linaloonyesha mienendo ya safari zilizofanyika kulingana na mafuta yaliyotumika (log Book), jambo ambalo linapelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi ya mafuta hayo, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba kuongeza umakini katika kusimamia buku linaloonyesha mienendo wa vyombo vya moto ili kuepusha kufanyika kwa matumizi mabaya ya fedha pamoja na rasilimali za umma.

### 5.10.1.5 Dosari katika utoaji wa huduma za dakhalia shilingi 973,352,190.17

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba imepokea na kutumia jumla ya shilingi 973,352,190.17 kwa ajili ya utoaji wa huduma za Dakhalia**.**

Dosari iliyobainika wakati wa ukaguzi ni kama ifuatavyo: -

a) Kukosekana kwa baadhi ya nyaraka za matumizi ya fedha hizo ikiwemo Risiti za Malipo yaliyofanyika ambapo ni kwenda kinyume na Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021

b) Kukabidhiwa fedha hizo kwa watendaji wasiokuwa na taaluma ya masuala ya fedha jambo ambalo limepelekea kutokuwekwa kwa kumbukumbu za matumizi ya fedha hizo ikiwemo daftari la fedha taslimu.

c) Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu ambapo ni kwenda kinyume na Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

d) Kufanya malipo bila ya kuwepo kwa hati za malipo husika ambapo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

e) Kuwepo kwa malipo yasiyokuwa na stakabadhi za kielektroniki ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 7 ya Uongozi na Taratibu za Kodi ya 2009 (iliyorekebishwa 2021).

Kuwepo kwa dosari hizi kunaweza kupelekea uwezekano wa kujitokeza kwa udanganyifu katika matumizi ya fedha,ubadhirifu pamoja na matumizi mabaya ya fedha za umma jambo ambalo linaweza kuisababishia Serikali kupata hasara pamoja na kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa ya uingizwaji wa fedha hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufuatwa taratibu zote za malipo. Mchanganuo wa matumizi ya fedha za dakhalia kwa kila Wilaya ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 93: Malipo ya huduma za dakhalia yenye dosari mbali mbali

| namba | Wilaya | Jina la Skuli | Fedha Zilizoingizwa na Kutumika (Tshs) | Nambari ya Hesabu iliyopokea fedha |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mkoani | Skuli ya Sekondari Moh'd Juma Pindua | 257,858,682.17 | 0403816000 |
| 2. | | Skuli ya Sekondari Kengeja Ufundi | 189,630,626 | 0703106000 |
| 3. | Micheweni | Skuli ya Sekondari Micheweni | 52,795,000 | 0785310001 |
| 4. | Wete | Skuli ya Sekondari Utaani | 105,429,789 | 0703005000 |
| 5. | | Skuli ya Sekondari Chasasa | 186,498,111 | 0403791000 |
| 6. | Chake Chake | Skuli ya Sekondari Fidel Castro | 181,139,982 | 0403485000 |
| **Jumla** | | | **973,352,190.17** | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za hati za malipo*

#### 5.10.1.6 Udhibiti na utunzaji usioridhisha wa kemikali na vifaa vya maabara

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa baadhi ya skuli zenye kemikali na vifaa vya maabara vinavyotumiwa na wanafunzi katika mitihani ya majaribio na mitihani ya taifa.

Dosari zilizobainika na ukaguzi ni kama ifuatavyo: -

a) Kuwepo kwa kemikali zilizoishiwa na muda bila ya kutumika, hali iliyosababishwa na kutokuwa makini wakati wa kufanya mgao wa kemikali, ambapo imebainika baadhi ya skuli zenye wanafunzi wachache na zile zenye wanafunzi wengi kupata mgao sawa.

b) Uhifadhi wa kemikali katika chupa zenye vifungashio dhaifu (plastic package) hali iliyopelekea kemikali katika chupa hizo kuingia hewa na hatimae kuharibika.

c) Udhibiti na uhifadhi usioridhirisha wa tindikali (acid) katika magaloni ya plastiki badala ya kuhifadhi katika chupa maalumu za vigae hali ambayo inaweza kupelekea galoni hizo kupasuka na hatimae kuleta athari kwa wanafunzi na walimu, aidha tindikali zinaweza kuharibika kabla ya kutumika.

Kuwepo kwa kemikali zilizoishiwa muda bila ya kuangamizwa, hali inayoweza kuleta athari kwa wanafunzi na walimu na skuli kwa ujumla, aidha hupelekea kutokuleta matokeo mazuri wakati wa kufanya utafiti katika mitihani ya taifa na ya mihula. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 27(1) cha Sheria ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kutokufikiwa kwa malengo ya Wanafunzi, Wizara na Serikali kwa ujuma katika utafiti kwenye mitihani ya taifa na ya mihula, aidha huweza kusababisha madhara makubwa kwa watumiaji wa kemikali na tindikali hizo wakiwemo walimu na wanafunzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuongeza umakini katika kusimamia masuala mbali mbali ya Wizara yakiwemo masuala ya kemikali na tindikali katika maabara za Skuli mbali mbali Kisiwani Pemba.

## 5.10.2 CHUO CHA KIISLAM (CCK) PEMBA

### 5.10.2.1 Kukosekana kwa vitengo vya Hesabu na Tehama

Ukaguzi umebaini kwamba Chuo cha Kiislamu Pemba kinatekeleza shughuli zote za kiuhasibu ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato na kufanya malipo mbali mbali bila kuwepo kwa Afisa Muhasibu/Kitengo cha Hesabu na pia Afisa Tehama/Kitengo cha Tehama, ambapo imebainika kwamba majukumu ya vitengo hivyo hufanywa na walimu wa kawaida wasiokuwa na uzoefu wala taaluma ya masuala ya Uhasibu na Fedha pamoja na utumiaji wa Mfumo wa ZanMalipo.

Kutokuwepo kwa Kitengo cha Tehama na Kitengo cha Hesabu na Afisa Mhasibu kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma pamoja na matumizi mabaya yasiozingatia miongozo ya kifedha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo kuanzisha vitengo hivyo pamoja na kutafuta wataalamu ili majukumu yaweze kufanyika kwa ufanisi na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

## 5.10.3 BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU PEMBA**

### 5.10.3.1 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 22,175,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 22,175,000 kwa njia ya fedha taslimu jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 kama ilivyobainishwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo kupitia benki. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 94: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/7 ya 20/7/2022 | 000131 | 1,110,000 | Mratibu Pemba | Malipo kwa ajili ya mafunzo elekezi. |
| 2. | 4/7 ya 20/7/2022 | 000132 | 1,300,000 | | Malipo kwa ajili ya uombaji wa mikopo. |
| 3. | 5/7 ya 14/8/2022 | 000132 | 1,200,000 | | |
| 4. | 1/8 ya 2/9/2022 | 000135 | 2,850,000 | | |
| 5. | 2/8 ya 2/8/2022 | 000137 | 830,000 | | |
| 6. | 4/8 ya 14/8/2022 | 000138 | 415,000 | | Malipo kwa ajili ya posho mbali mbali. |
| 7. | 5/8 ya 14/8/2022 | 000138 | 580,000 | | |
| 8. | 6/8 ya 14/8/2022 | 000138 | 610,000 | | |
| 9. | 7/8 ya 30/8/2022 | 000138 | 430,000 | | |
| 10. | 8/8 ya 30/8/2022 | 000139 | 610,000 | | |
| 11. | 9/8 ya 30/8/2022 | 000139 | 165,000 | | Bakaa ya Malipo |
| 12. | 1/9 ya 21/9/2022 | 000140 | 610,000 | | Malipo kwa ajili ya posho mbali mbali. |
| 13. | 2/9 ya 21/9/2022 | 000140 | 775,000 | | |
| 14. | 3/9 ya 21/9/2022 | 000140 | 820,000 | | |
| 15. | 1/10 ya 17/10/2022 | 000141 | 660,000 | | |
| 16. | 2/10 ya 17/10/2022 | 000141 | 480,000 | | |
| 17. | 1/10 ya 17/10/2022 | 000141 | 660,000 | | |
| 18. | 2/10 ya 17/10/2022 | 000141 | 480,000 | | |
| 19. | 3/10 ya 17/10/2022 | 000141 | 610,000 | | |
| 20. | 1/11 ya 10/11/2022 | 000143 | 800,000 | | |
| 21. | 1/12 ya 26/12/2022 | 000144 | 820,000 | | |
| 22. | 2/12 ya 27/12/2022 | 000144 | 445,000 | | |
| 23. | 1/1 ya 9/1/2023 | 000145 | 640,000 | | |
| 24. | 1/2 ya 22/2/2023 | 000147 | 650,000 | | |
| 25. | 3/1 ya 13/1/2023 | 000145 | 610,000 | | |
| 26. | 5/1 ya 23/1/2023 | 000146 | 640,000 | | |
| 27. | 6/3 ya 24/3/2023 | 000149 | 2,375,000 | | |
| **Jumla** | | | **22,175,000** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.10.3.2 Kutokutumika kwa mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji wa mapato shilingi 81,983,756.02

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato. Aidha, toleo la barua yenye kumbukumbu namba CA.319/398/01/02/19 ya tarehe 14/02/2022 kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafafanua kwamba makusanyo yote ya Taasisi za Umma yafanyike kupitia Mfumo wa ZanMalipo".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mapato yenye jumla ya shilingi 81,983,756.02 yamekushanywa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba kuanzia mwezi wa Julai, 2022 hadi Oktoba, 2023 bila ya kutumia mfumo wa ZanMalipo jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mapato, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria na muongozo kama ilivyobainishwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kukusanya malipo kupitia mfumo wa ZanMalipo.

## 5.10.4 BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi**

### 5.10.4.1 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 9,080,500

Kwa mujibu wa barua kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar yenye kumbukumbu nambari MUUMU.BA.156/370/01/27 ya tarehe 12/08/2022 inazitaka taasisi zote za Serikali kufanya manunuzi kupitia mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 15/08/2022.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mitihani limefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 9,080,500 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama e-Proz, jambo ambalo linaweza kupelekea kununua bidhaa zenye viwango duni na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yafuate utaratibu wa kutumia mfumo wa Manunuzi kwa mujibu wa Toleo la Barua hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 95: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa e-Proz**

| Namba | Tarehe | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | 11/5/2023 | Lendram company ltd | 411,600 |
| 2. | 4/5/2023 | Raptek techno and service | 900,000 |
| 3. | 11/5/2023 | Zan catering and take away | 1,121,826 |
| 4. | 11/5/2023 | Nasam general supplier ltd | 3,552,174 |
| 5. | 16/5/2023 | Done deal dealer ltd | 3,100,000 |
| **Jumla** | | | **9,085,600** |

### 5.10.4.2 Ununuzi wa Mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 104,879,590

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 104,879,590 zimelipwa na Baraza la Mitihani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa watoa huduma mbalimbali bila ya kufunga mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Baraza pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mitihani kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba wa watoa huduma kama sheria inavyoelekeza. Mchanganuo wa bidhaa ya mafuta iliyonunuliwa bila ya kufunga mkataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 96: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba**

| Namba | Hati namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | 01/08 ya 02/08/2022 | BMP-Ununuzi wa Mafuta | 4,760,080 |
| 2. | 03/10 ya 04/10/2022 | Zanzibar Petroleum LTD | 6,414,510 |
| 3. | 23/10 ya 21/10/2022 | BMP-Ununuzi wa Mafuta | 20,000,000 |
| 4. | 24/10 ya 21/10/2022 | Zanzibar Petroleum LTD | 30,000,000 |
| 5. | 23/11 ya 18/11/2022 | Zanzibar Petroleum LTD | 26,000,000 |
| 6. | 03/12 ya 02/12/2022 | BMP-Ununuzi wa Mafuta | 12,000,000 |
| 7. | 01/02 ya 02/02/2023 | Zanzibar Petroleum LTD | 5,705,000 |
| **Jumla** | | | **104,879,590** |

## 5.11 WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

### 5.11.1 FUNGU L01 - WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.11.1.1 Ununuzi wa Mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 274,469,824

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 274,469,824 zimelipwa na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa watoa huduma mbalimbali wakiwemo Kijangwani Petrol Station, M/S United Group Limited na M/S Costal Fuel Services LTD bila ya kufunga mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama sheria inavyoelekeza.

#### 5.11.1.2 Malipo yaliyofanyika nje ya vifungu vya Bajeti shilingi 33,756,054.62

Kifungu nambari 50(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inaelezea kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma anaweza kufanya mabadiliko ya fedha baina ya programu, shughuli, au baina ya vifungu vikuu ndani ya fungu katika bajeti ya mwaka wa fedha ikiwa; (a) kutakuwa na matumizi katika bajeti ya programu shughuli au baina ya vifungu vikuu ambavyo haviwezekani kutumika; (b) kiwango chote cha fedha kinachofanyiwa mabadiliko au kutokana na programu, shughuli au baina ya programu kuu ya fungu la bajeti kisizidi kiwango kilichoainishwa katika kanuni au muongozo wa programu ya bajeti.

Katika ukaguzi ulofanyika imebainika kwamba Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imefanya matumizi yenye jumla ya shilingi 33,756,054.62 kwa ajili ya huduma mbali mbali za uendeshaji wa Wizara. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo hayo bila ya kuzingatia taratibu za uhaulishaji wa vifungu vya bajeti vilivyoandaliwa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokufikiwa kwa malengo ya vifungu vilivyoathirika na uhaulishaji huo. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafanya matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na mpango kazi ulioandaliwa ili kuepusha kutokufikiwa kwa malengo yaliopangwa kwa vifungu husika. Mchaganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 97: Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu husika

| Hati Namba | Thamani (Tsh) | Kifungu kilichotumika | Kifugu kinachotakiwa kulipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 55/12 | 96,655.31 | Minor civil work 2211001 | Purchases of feeds 2208005 | Malipo ya chakula cha makobe misitu |
| | 62,048.86 | Transport Allowance 2111006 | | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| | 33,498.57 | Stationary supplies 2206001 | | Malipo ya safari kwa Mh.Waziri na PA wake. |
| | 19,042.88 | Petrol 2203003 | | Manunuzi ya vifaa vya usafi |
| 57/12 | 51,604.73 | Internet Service 2201006 | Stationary supply 2206001 | Malipo ya Bima kwa vyombo vya Wizara ya Kilimo |
| | 500,000 | Telephone and telegram 2201001 | | Malipo ya ulinzi-Utumishi na Uendeshaji |
| | 231,435.27 | Overtime 2111007 | | Malipo ya ununuzi wa laptop |
| 61/12 | 2420,000 | Leave travel 2111005 | Domestic travel 2203001 | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 39/12 | 900,711 | Petrol 2203003 | Cleaning supply 2206023 | Malipo ya ununuzi wa mafuta-Utumishi. |
| 40/12 | 11,310,250 | Minor civil work 2211001 | Insurance and road license 2210005 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya pikipiki |
| 51/11 | 600,000 | Cleaning supply 2206023 | | Ununuzi wa Farniture |
| 52/11 | 3,554,902 | Pur. of furnit. /Desk/ chair/cabinet/shelve 6112222 | Perchases of computer 6112208 | Ununuzi wa vifaa vya internet Kilimo |
| 74/12 | 917,792.00 | Repair and Maintenance of equipment 2210001 | Stationary supply 2206001 | Matengenezo ya gari ya Mh. Waziri |
| 76/12 | 812,650 | Telephone and telegram 2201001 | Petrol 2203003 | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia mifugo |
| 53/2 | 526,260.00 | Transport allowance 2111006 | Purchases of spare part 6112221 | Ununuzi wa mapazia utumishi |

| Hati Namba | Thamani (Tsh) | Kifungu kilichotumika | Kifugu kinachotakiwa kulipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 64/2 | 2,842,000 | Minor civil work 2211001 | Pur.furnit. /desk/ tables/chairs/ cabinet/shelves 6112222 | Malipo ya chakula cha makobe misitu |
| 3/4 | 3,624,930 | Minor civil work 2211001 | Internet Service 2201006 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 75/4 | 1,029,000 | Purchase of computer 6112206 | Purchase of spare part 6112221 | Malipo ya safari kikazi kwa Mh.Waziri na PA wake. |
| 83/06 | 1,136,274 | Minor Civil Work 2211001 | Stationary supply 2206001 | ununuzi ya vifaa vya usafi |
| 99/6 | 3,087,000 | Printing expenses 2206002 | Curtain,Bedsheet and flooring 6112224 | Malipo Bima kwa vyombo vya wizara ya Kilimo |
| **JUMLA** | **33,756,054.62** | | | |

### WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO PEMBA

#### 5.11.1.3 Malimbikizo ya Madeni shilingi 32,337,880

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 32,338,508 ambapo miongoni mwa madeni hayo ni stahiki za wafanyakazi na madeni yatokanayo na kupatiwa huduma ya maji, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kuyalipa madeni hayo.

Kufanya hivyo ni kuiongezea Serikali mzigo mkubwa wa madeni na hatimae kusababisha migogoro baina ya Wizara na wadai. Hali hii imesababishwa na kutokuwa na udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia na kufanya malipo ya madeni hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni kwa wakati. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 98: Madeni ya muda mrefu ya Wizara

| Namba | Mtoa Huduma | Huduma Iliyopatikana | Deni Halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Huduma ya Maji | 17,958,880 |
| 2. | Wafanyakazi | Kufanyakazi muda wa ziada | 754,000 |
| 3. | | Ubani | 6,000,000 |
| 4. | | Safari kikazi | 7,625,000 |
| **Jumla** | | | **32,337,880** |

*Chanzo: Orodha ya madeni ya Wizara*

### 5.11.1.4 Kukosekana kwa hati miliki kwa baadhi ya mali za Wizara

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo Pemba ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya afisi na mashamba jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mali hizo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hati miliki mali za Wizara. Mchanganuo wa mali hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 99: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki

| Namba | Aina ya Mali | Mahala Ilipo |
|---|---|---|
| 1. | Shamba la mikarafuu na minazi | Makuwe-Mgogoni |
| 2. | Shamba la mikarafuu | Daya-Mtambwe |
| 3. | Shamba la minazi | Chwaka-Tumbe Mashariki |
| 4. | Shamba la mikarafuu na minazi | Vikutani-Gando |
| 5. | Shamba la mpunga | Msaani-Pandani |

| Namba | Aina ya Mali | Mahala Ilipo |
|---|---|---|
| 6. | Shamba la mpunga | Chambani-Mkoani |
| 7. | Shamba la minazi | Fufuni-Kangani |
| 8. | Shamba la mpunga | Pujini-Chakechake |
| 9. | Shamba la mpunga | Dodeani-Ole |
| 10. | Shamba la mpunga | Kiyuni-Ngwachani |
| 11. | Shamba la miti | Maziwa Ng'ombe |
| 12. | Shamba la miti | Mitondooni-Kengeja |
| 13. | Shamba la mipira | Sanaa-Finya |
| 14. | Shamba la mipira | Maziwani |
| 15. | Shamba la mipira | Pogwe-Kifundi |
| 16. | Shamba la mipira | Makangale |
| 17. | Shamba la mipira | Kangani |
| 18. | Up land area | Matangatuani-Kifundi |
| 19. | Orchard Plantation | Wesha |
| 20. | Shamba la minazi | Fundo |
| 21. | Shamba la minazi | Tumbe Mashariki |
| 22. | Shamba la mazao | Gando |
| 23. | Shamba la malisho ya wanyama | Chamanangwe – Kiuyu |
| 24. | Shamba la malisho ya wanyama | Fueni-Minungwini |
| 25. | Shamba la malisho ya wanyama | Magome-Vikunguni |
| 26. | Livestock Carantine | Nziwengi-Gando |
| 27. | Msitu wa Hifadhi | Ngezi-Makangale |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Wizara*

### 5.11.1.5 Kutokuwepo kwa kadi za usajili wa vyombo vya moto

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya vyombo vya moto vinavyomilikiwa na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo Pemba havina kadi za usajili jambo ambalo linapelekea uhalali wa matumizi ya vyombo hivyo kutokukamilika, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kuvifanyia usajili vyombo vya moto kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria uliopo. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 100: Vyombo vya moto ambavyo havina kadi za usajili

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | GARI | Pickup Nissan | SMZ 560B | Idara ya Maendeleo ya Mifugo |
| 2. | | Toyota | DFP 6702 | |
| 3. | | Volks Wagen | SMZ 341B | Idara ya Umwagiliaji Maji |
| 4. | | Nissan | SMZ 540B | |
| 5. | | Mistubish | SMZ126B | Idara ya Mipango |
| 6. | | Mitsubish | SMZ 196B | Idara ya Uendeshaji na Utumishi |
| 7. | | Nissan | STK417 | |
| 8. | | Nissan | STL2182 | |
| 9. | | Nissan | SMZ388B | Idara ya Misitu |
| 10. | | Toyota D4d | DFP 8264 | |
| 11. | | Toyota | SMZ 272B | Idara ya Kilimo |
| 12. | | Toyota | SMZ 607B | |
| 13. | | Volks Wagen | SMZ 343B | |
| 14. | | Fowdrdwagen | SMZ 592B | |
| 15. | PIKIPIKI | XL Honda | SMZ1179C | Idara ya Mifugo |
| 16. | | -- | SMZ1187C | |
| 17. | | Trail 110 | SMZ626C | |
| 18. | | Tuktuk | SMZ369C | |
| 19. | | -- | SMZ6951 | |
| 20. | | Tuktuk | SMZ464C | |
| 21. | | XL Honda | SMZ1182C | |
| 22. | | TVS Bajaj | SMZ 1460C | |
| 23. | | TVS Bajaj | SMZ 1636C | |
| 24. | | TVS Bajaj | SMZ 1631C | |
| 25. | | AG 200 | SMZ 831C | |
| 26. | | TVS Bajaj | SMZ 1821 | |
| 27. | | Trail 110 | SMZ 626C | |
| 28. | | AG 200 | SMZ 272C | |
| 29. | | XL Honda | STL 5329 | |

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| 30. | PIKIPIKI | TVS 125 | SMZ 1608C | |
| 31. | | Honda Xl 125 | SMZ 1079 C | Idara ya U/Maji |
| 32. | | Honda Xl 125 | SMZ 1146 | |
| 33. | | Xl 125C | SMZ 1077C | |
| 34. | | Yamaha 125 | SMZ 1705C | |
| 35. | | Yamaha 125 | SMZ 1706C | |
| 36. | | Yamaha AG200 | SMZ 1161 C | |
| 37. | | Loncin 125 | SMZ 784C | |
| 38. | | Vespa Star | SMZ 1004C | |
| 39. | | AG 200 | SMZ 6986/ 858C | |
| 40. | | Honda Watco | SMZ 832C | |
| 41. | | Honda Watco | SMZ 999 C | Idara ya Mipango |
| 42. | | TVS Bajaj | | |
| 43. | | Vespa | SMZ 201C | Idara ya U/Utumishi |
| 44. | | Vespa | SMZ 214C | |
| 45. | | Boxa | DFPE 7209 | |
| 46. | | Yamaha | STL 5332 | |
| 47. | | Honda Acp125 | DFPA 0008 | Idara ya Utafiti |
| 48. | | TVS | SMZ 1379C | |
| 49. | | Honda XL | SMZ 1078C | |
| 50. | | Boxso | SMZ 1766 C | |
| 51. | | Boxso | SMZ 1767 C | |
| 52. | | Vespa- PX125 | DFP 8737 | Idara ya Misitu |
| 53. | | Honda Xl125 | SMZ 1380C | |
| 54. | | Toyo | SMZ 6729 | |
| 55. | | Toyo | SMZ6731 | |
| 56. | | MC | MC 375 CHR | |
| 57. | | MC | MC 377 CHR | |
| 58. | | MCH | MC 376 CHR | |
| 59. | | TVS Bajaji | SMZ 1567 C | Wakala wa Matrekta |
| 60. | | TVS Bajaji | SMZ1568 | |
| 61. | | TVS Bajaji | SMZ1856 | |
| 62. | | TVS Bajaji | SMZ1854 | |
| 63. | | Yamaha | SMZ6683 | Idara ya Kilimo |

| Namba | Aina ya Chombo | Kabila | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| 64. | PIKIPIKI | Yamaha AG200 | SMZ 6547 | Idara ya Kilimo |
| 65. | | TVS | SMZ 1026C | |
| 66. | | TVS | SMZ 1375 | |
| 67. | | Yamaha AG200 | SMZ 952C | |
| 68. | | Yamaha AG200 | SMZ 6985 | |
| 69. | | Yamaha AG200 | SMZ 6979 | |
| 70. | | Yamaha AG200 | SMZ 6986 /858C | |
| 71. | | Stra HL TVS | SMZ 795C | |
| 72. | | Honda ACP125 | DFP 9797 | |
| 73. | | TVS | SMZ1474 | |
| 74. | | TVS | SMZ 1607C | |
| 75. | | TVS | SMZ 1606C | |
| 76. | | TVS | SMZ 1630 C | |
| 77. | | TVS | SMZ 1635 C | |
| 78. | | Yamaha | STL 7910 | |
| 79. | | TVS | SMZ 1564 | |
| 80. | | TVS 125 | SMZ I602C | |
| 81. | | TVS 125 | SMZ 835C | |
| 82. | | TVS 125 | SMZ 1833C | |
| 83. | | Yamaha Ag200 | STL5330 | |
| 84. | | TVS 125 | SMZ 1070C | |
| 85. | | Yamaha Ag200 | STL 5331 | |
| 86. | | Yamaha Ag200 | SMZ 2050C | |
| 87. | | Yamaha Ag200 | SMZ 1428C | |
| 88. | | TVS | SMZ 1302C | |
| 89. | | TVS | SMZ 1881C | Utafiti wa Mifugo (ZALIRI) |
| 90. | | TVS | SMZ 1739C | |

*Chanzo: Taarifa za Wizara*

#### 5.11.1.6 Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa Mali chakavu

Kifungu nambari 69(1)(2) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa "Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya umma na kuwasilishwa katika Afisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Afisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya mali za kudumu zinazomilikiwa na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo Pemba zikiwemo pikipiki, pasola na vespa zimetelekezwa na pia hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu jambo ambalo linaweza kupelekea kutokea kwa uharibifu mkubwa wa mali za Wizara na hatimae kupelekea kutumia gharama kubwa za matengenezo au kuwepo kwa upotevu wa mali hizo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuziondoa au kuzifanyia matengenezo ili kuepusha kuchakaa na hatimae kuingiza hasara Serikali. Mchanganuo wa mali zenyewe ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 101: Mali chakavu ambazo hazijauzwa wala kufanyiwa matengenezo**

| Namba | Aina ya Chombo | Namba ya Usajili | Idara Husika |
|---|---|---|---|
| 1. | Pasola | SMZ 1014 C | Idara ya Kilimo |
| 2. | | SMZ 1017 C | |
| 3. | | SMZ 1015 C | |
| 4. | | SMZ 952 C | |
| 5. | Pikipiki | SMZ 486 C | |
| 6. | | SMZ 556 C | |
| 7. | | SMZ 359 C | |
| 8. | | SMZ 538 C | |
| 9. | | SMZ 1385 C | |
| 10. | | SMZ 855 C | Idara ya Mifugo |
| 11. | | SMZ 1146 C | Idara ya U/Maji |
| 12. | | SMZ 784 C | |
| 13. | | SMZ 783 C | |
| 14. | | SMZ 1161 C | |
| 15. | | SMZ 858 C | |
| 16. | | SMZ 837 C | |

| Namba | Aina ya Chombo | Namba ya Usajili | Idara Husika |
|---|---|---|---|
| 17. | Pikipiki | SMZ 1380 C | Idara ya Misitu |
| 18. | | Z 108 BU | |
| 19. | | SMZ 831 C | Idara ya Misitu |
| 20. | | SMZ 845 C | Idara ya Mifugo |
| 21. | | SMZ 1279 C | |
| 22. | | STL 5330 | |
| 23. | | SMZ 844 C | Idara ya Kilimo |
| 24. | | SMZ 793 C | |
| 25. | | SMZ 464 C | Idara ya Mifugo |
| 26. | | SMZ 847 C | |
| 27. | | SMZ 626 C | |
| 28. | | SMZ 538 C | |
| 29. | Vespa | SMZ 782 C | |

*Chanzo: Taarifa za Wizara.*

## 5.11.2 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR (ZARI)

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.11.2.1 Kupotea kwa mapato katika shamba la viungo shilingi 8,107,000

Ukaguzi umebaini kwamba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inakusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake tofuati vya ndani katika Mashamba, Mauzo ya mazao na Ada ya Uingizaji Wageni.

Ukaguzi umepitia taarifa za mapato ya ada ya uingizaji wageni na kubaini kwamba kuna upotevu wa mapato kiasi cha shilingi 8,107,000 zinazotokana na kutolipa kwa thamani sahihi ya ada inayotozwa kutokana na idadi ya watembeza wageni hao bila ya sababu yoyote.

Watembeza wangeni kutolipa kwa vizuri kunapelekea kushuka kwa mapato na Taasisi kutofikia kwa malengo waliojipangia.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi kuimarisha usimamizi wa makusanyo ili kuweza kukusanya ipasavyo kwa lengo la kuongeza mapato.

### 5.11.3 TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO ZANZIBAR (ZALIRI)

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.11.3.1 Kutokuwepo kwa uzio katika eneo la Taasisi

Kifungu nambari 58(d) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma atakuwa na jukumu la kuhakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondoa wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya.

Baada ya kupitia maeneo mbalimbali yanayomilikiwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, ukaguzi umebaini kutokujengwa kwa uzio katika eneo la Taasisi. Hali hii inaweza kupelekea uvamizi na uharibifu mkubwa wa mali za Serikali ikiwemo Majengo ya Taasisi hiyo pamoja na mali zilizomo ndani yake.

Kutokujengewa uzio kwa maeneo ya Taasisi ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu pamoja na vifungu vya 29(a) na 112(2)(e) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi kuhakikisha kwamba wanatenga fedha za kutosha katika bajeti yao ya mwaka zitakazowezesha maeneo yote yanayomilikiwa na Taasisi kujengewa uzio.

## 5.12 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 5.12.1 FUNGU L02 - WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

## WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA

### 5.12.1.1 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 6,386,580

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 6,386,580 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba lakini hati za malipo hayo hazikuweza kupatikana kwa ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Kukosekana kwa hati za malipo kunaweza kupelekea kutothibitika kwa malipo yaliyofanyika, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba kuhakikisha hati za malipo pamoja na vielelezo vyake zinatayarishwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Mchanganuo wa hati hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 102: Hati za malipo zilikosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 25/12 ya 29/12/2022 | 32055 | Meneja PBZ Islamic Division | 1,000,000 |
| 2. | 04/03 ya 14/03/2023 | 33804 | | 1,540,000 |
| 3. | 28/03 ya 27/03/2023 | 034234 | | 640,000 |
| 4. | 27/04 ya 17/04/2023 | 034714 | | 3,206,580 |
| **Jumla** | | | | **6,386,580** |

*Chanzo: Daftari la fedha taslimu la hesabu ya matumizi ya kawaida.*

#### 5.12.1.2 Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji shilingi 26,873,721

Kifungu nambari 35 cha Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya 2018 kimezitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zake zote za Uchapaji na Mahitaji ya vifaa vya Afisi na vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba imefanya ununuzi wa vifaa vya kuandikia vyenye jumla ya shilingi 26,873,721 kutoka kwa Wasambazaji bila ya kuwepo kwa ruhusa kutoka kwa Wakala kama utaratibu unavyoelekeza jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imesababishwa na kutokuombwa kwa ruhusa kutoka kwa Wakala kabla ya Wizara kuamua kununua vifaa kwa wasambazaji wengine wanaoonekana katika mtandao. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kununua vifaa kwa Wakala au vyenginevyo kuomba ruhusa kwa Wakala ili kuweza kununua vifaa hivyo kwa wasambazaji wengine pale inapotokezea Wakala kutokuwa na vifaa vinavyohitajika kununuliwa. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 103: Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 05/08 ya 12/08/2022 | 28640 | 1,896,253 | Malinge Enterprises | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 2. | 26/08 ya 25/08/2022 | 28779 | 388,195 | | |
| 3. | 26/10 ya 17/10/2022 | 030135 | 1,000,737 | | |
| 4. | 01/12 ya 06/12/2022 | 31460 | 782,200 | Halim enterprises | |
| 5. | 02/12 ya 06/12/2022 | 31461 | 7,200,000 | Malinge Enterprises | Malipo ya ununuzi wa computer kwa matumizi ya Afisi. |
| 6. | 05/01 ya 10/01/2023 | 32274 | 1,468,800 | Amo Computer Services | |

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. | 08/01 ya 10/01/2023 | 32277 | 2,900,736 | Adult Training Centre | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 8. | 01/03 ya 14/03/2023 | TT | 3,456,000 | Amo Computer Services | Malipo ya uunuzi wa kompyuta. |
| 9. | 06/03 ya 14/03/2023 | 033805 | 2,121,600 | Pandu Book Shop | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 10. | 29/03 ya 27/03/2023 | 034235 | 2,880,000 | Hidaya Hassan Mussa | |
| 11. | 10/06 ya 23/06/2023 | 036541 | 1,339,200 | Capital Technology Centre | |
| 12. | 27/06 ya 21/06/2023 | 036894 | 1,440,000 | Malinge Enterprises | |
| **Jumla** | | | **26,873,721** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 5.12.1.3 Dosari katika utoaji wa likizo bila ya malipo

Kwa mujibu wa kanuni nambari 63(1)(C) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kwamba "Likizo bila ya malipo zitaidhinishwa na Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi ikiwa mtumishi wa umma anataka kujihusisha na siasa".

Baada ya kufanya uhakiki wa majalada ya baadhi ya watumishi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba ukaguzi umebaini kwamba ndugu Machano Ali Machano kuwa na dosari katika likizo bila ya malipo aliyopatiwa kutokana na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuanzia tarehe 22/09/2022 ambapo imebainika Mtumishi huyo kuendelea kulipwa mshahara wa mwezi Oktoba, 2022 licha ya kuwa hakuhudhuria kazini jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 13(1-3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kufanya malipo ya mshahara kwa mtumishi anayestahiki kulipwa mshahara.

#### 5.12.1.4 Ununuzi wa Mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 76,711,022

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 76,711,022 zimelipwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa watoa huduma ya mafuta wakiwemo Chasasa Service Station na Ole Filling Station bila ya kufunga mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama sheria inavyoelekeza.

Mchanganuo wa bidhaa ya mafuta iliyonunuliwa bila ya kufunga mkataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 104: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 02/08 ya 12/08/2022 | 28637 | 4,357,502 | Chasasa Service Station | Malipo ya ununuzi wa mafuta kwa ajili ya shughuli za Wizara. |
| 03/08 ya 12/08/2022 | 28638 | 1,792,000 | Zanzibar Petroleum ltd | |
| 17/09 ya 29/09/2022 | 029661 | 6,278,024 | Chasasa Service Station | |
| 03/10 ya 18/10/2022 | 030137 | 1,133,760 | Chake Petrol Station | |
| 20/10 ya 26/10/2022 | 030589 | 280,000 | Chasasa Serive Station | |
| 01/11 ya 10/11/2022 | 30756 | 5,596,226 | Chasasa Serive Station | |
| 04/11 ya 11/11/2022 | 030759 | 5,452,941 | Chake Petrol Station | |
| 25/11 ya 28/11/2022 | 031359 | 1,980,000 | Chake Petrol Station | |
| 29/11 ya 29/11/2022 | 031362 | 1,793,000 | Classic Petrol Station | |

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 08/12 | 031628 | 10,308,684 | Chasasa Service Station | Malipo ya ununuzi wa mafuta kwa ajili ya shughuli za Wizara. |
| 09/12 ya 20/12/2022 | 031629 | 1,045,406 | Chake Petrol Station | |
| 03/02 ya 15/02/2023 | 033003 | 1,000,000 | Chasasa Service Station | |
| 04/02 ya 15/02/2023 | 033004 | 6,798,138 | Chakechake Service Station | |
| 10/03 ya 15/03/2023 | 033810 | 2,076,000 | Classic Petrol Station | |
| 01/04 ya 12/04/2023 | 034542 | 11,443,600 | Chasasa Service Station | |
| 07/04 ya 13/04/2023 | 034560 | 2,000,000 | Chake Petrol Station | |
| 02/05 ya 04/05/2023 | 035103 | 1,756,960 | Chasasa Service Station | |
| 04/06 ya 21/06/2023 | 036539 | 1,953,000 | Classic Petrol Station | |
| 05/06 ya 21/06/2023 | 036543 | 2,156,037 | Chake Petrol Station | |
| 07/06 ya 21/06/2023 | 036543 | 7,509,744 | Limbani Service Station | |
| **Jumla** | | **76,711,022** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Wizara*

### 5.12.1.5 Kukosekana kwa hati miliki kwa baadhi ya mali za Wizara

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya afisi na mashamba jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Serikali kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hati miliki mali za Wizara. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 105: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki

| Namba | Aina ya mali | Mahala ilipo |
|---|---|---|
| 1. | Jengo la Afisi Kuu ya Wizara | Limbani - Wete |
| 2. | Nyumba ya wageni | Limbani – Wete |
| 3. | Soko la Tumbe | Tumbe |
| 4. | Ofisi ya PECCA | Wesha |
| 5. | Kiwanja (ZAFICO) | Shumba mjini |
| 6. | Kiwanja (ZAFICO) | Ndagoni |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Wizara*

### 5.12.1.6 Kuchelewa kukabidhiwa boti kwa wakulima wa Mwani

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake za kuimarisha Sera ya Uchumi wa Buluu na kwa lengo la kuwaondoshea shida mbalimbali wananchi wa Zanzibar zikiwemo za kiuchumi kupitia mradi wa UVIKO 19 iliamua kununua maboti ya saizi tofauti kwa ajili ya Uvuvi wa kisasa wa samaki na ukulima wa mwani Unguja na Pemba.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa boti zilizotengenezwa kwa ajili ya kilimo cha mwani zenye ukubwa wa mita 5 ambapo kati ya boti hizo, boti 165 zimetolewa kwa wakulima na kubakia jumla ya boti 228 ambazo hadi ukaguzi huu unakamilika imebainika kutokukabidhiwa kwa walengwa badala yake zimewekwa katika eneo la Afisi za Wizara ya Uchumi wa Buluu Wete, aidha imebainika kuwepo kwa wakulima wa mwani 111 ambao wameomba kupatiwa boti hizo.

Kuchelewa kukabidhiwa kwa boti kwa wakulima wa mwani kunaweza kupelekea kuchakaa na hatimae kuharibika jambo ambalo hupelekea kutofikiwa kwa lengo la Serikali lililokusudiwa kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba kuhakikisha unasimamia ipasavyo sera ya uchumi wa Buluu ikiwa ni pamoja na kuharakisha utolewaji wa boti kwa wakulima kama ilivyokusudiwa.

## 5.13 WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

### 5.13.1 FUNGU N01 – WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.13.1.1 Kutokufuatwa kwa Mpango Maalum wa Mafunzo

Kanuni nambari 74(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inazitaka "Taasisi zote za Serikali kuandaa mpango maalum wa mafunzo pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo". Aidha kwa mujibu wa waraka wenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/54 na CAB.40/158/01/37 kutoka Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unazitaka Wizara na Taasisi za umma kufanya maandalizi ya mpango wa mafunzo ili kujua mahitaji (Training Needs Assessment) na kuwasilisha mpango wa mafunzo.

Ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imetumia jumla ya shilingi 5,655,258 kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu ikiwa ni malipo ya awamu ya kwanza, ambapo kwa mujibu wa mpango wa Wizara ni kusomesha wafanyakazi wawili (2) kwa kozi za muda mrefu, badala yake imesomesha wafanyakazi wanne (4), kati ya hao wafanyakazi watatu (3) hawakuwemo katika mpango wa mafunzo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi licha ya kuwa hawamo katika mpango wa mafunzo lakini pia wafanyakazi hao wametoka katika kitengo kimoja na wamechukua fani moja. Kutokana na uwepo wa dosari hiyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa vigezo vilivyotumika kuwapata watumishi waliopewa nafasi za mafunzo ya muda mrefu, vile vile kushindwa kujiridhisha juu ya uhitaji wa Wizara kwa nafasi za mafunzo yaliyotolewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhakikisha unaandaa mpango wa mafunzo, mpango wa tathmini ya mahitaji pamoja na bajeti ya mafunzo ili kuepusha kujitokeza kwa mizozo au malalamiko kwa watumishi wa umma watakaonyimwa nafasi ya kushiriki katika mafunzo. Mchanganuo wa watumishi waliopatiwa mafunzo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 106: Watumishi waliopatiwa mafunzo bila ya kufuatwa kwa Mpango wa Mafunzo

| Namba | Jina | Kitengo | Chuo | Fani | Miaka | Kiasi (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Abubakar Mzee Mwinyikombo | Mawasiliano ya Kompyuta | Eastern Africa Statistical Training Centre | Shahada ya Kwanza ya Data Science | Mitatu (3) (17/10/2022-17/10/2025) | 1,425,000 |
| 2. | Juma Kheri Khamis | Mawasiliano ya Kompyuta | University of Dar | Shahada ya pili ya data science | Miwili (2) (7/11/2022 -7/11/2024) | 2,115,125 |
| 3. | Fatma Mataka Juma | Mawasiliano ya Kompyuta | University of Dar | Shahada ya pili ya data science | Miwili (2) (7/11/2022 -7/11/2024) | 2,115,125 |
| **Jumla** | | | | | | **5,655,250** |

### 5.13.1.2 Malimbikizo ya Madeni shilingi 43,051,720

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar inadaiwa madeni na Taasisi mbalimbali za Serikali yenye jumla ya shilingi 43,051,720 kutokana na kupatiwa huduma mbali mbali kutoka kwa watoa huduma. Madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo.

Kufanya hivyo ni kuiongezea Serikali mzigo mkubwa wa madeni na hatimae kusababisha migogoro baina ya Wizara na watoa huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 107: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu

| Namba | Idara iliyopatiwa huduma | Deni Halisi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 12,505,500 |
| 2. | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 22,235,924 |
| 3. | Mahakama ya Ardhi | 8,310,296 |
| **Jumla** | | **43,051,720** |

## WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI PEMBA

### 5.13.1.3 Malimbikizo ya Madeni ya Mapato shilingi 1,145,619,444

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba inazidai taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya shilingi 1,145,619,444 kutokana na huduma za ushauri elekezi iliyotolewa katika miradi mbali mbali iliyofanyika pamoja na ukodishwaji wa nyumba za Serikali, ambapo huduma hizo zilizotolewa kufuatia maagizo kutoka Serikalini. Madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo.

Kufanya hivyo ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangetumika katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali ikiwemo miradi ya maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya ufuatiliaji wa madeni ili yaweze kukusanywa kama ilivyopangwa. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 108: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu**

| Namba | Jina la Taasisi | Huduma iliyotolewa | Mahala ilipo | Deni halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KMKM | Kodi ya nyumba SMZ 5 | Wete | 3,300,000 |
| 2. | Mahkama | Kodi ya nyumba SMZ 9A | | 2,700,000 |
| 3. | Wizara ya Elimu | Kodi ya nyumba SMZ 9C | | 100,000 |
| 4. | Wizara ya Afya | **Kodi ya nyumba:** SMZ 8A, SMZ 9B, SMZ 9D, SMZ 10A, SMZ 10B, SMZ 10C, SMZ 10D, SMZ 10E, SMZ 10F, SMZ 5. | | 28,550,000 |
| | | **Kodi ya nyumba:** SMZ 6, SMZ 9, SMZ 11, SMZ 12, SMZ 7, SMZ 15. | Chake Chake | 14,650,000 |
| 5. | Wizara ya Habari | Kodi ya nyumba SMZ 17 | | 550,000 |

| Namba | Jina la Taasisi | Huduma iliyotolewa | Mahala ilipo | Deni halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 6. | Wizara ya Mawasiliano | Kodi ya nyumba SMZ 9 | | 920,000 |
| 7. | DPP | Kodi ya nyumba SMZ 16 | | 890,000 |
| 8. | Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. | Ujenzi wa soko la wajasiriamali | Tumbe - Micheweni | 144,444,444 |
| | | Ujenzi wa soko la wajasiriamali | Michakaini - Chake Chake | 150,300,000 |
| | | Ujenzi wa soko la wajasiriamali | Kifumbikai - Wete | 171,000,000 |
| | | Ujenzi wa soko wajasiriamali | Kipitacho, Mkoani | 150,300,000 |
| | | Ujenzi wa soko | Machomane-Chake Chake | 92,700,000 |
| | | Ujenzi wa stendi | Kinowe, Micheweni | 93,870,000 |
| | | Ujenzi wa Garden | Mwana-mashungi, Chake Chake | 125,100,000 |
| | | Ujenzi wa soko | Mtambile - Mkoani | 52,380,000 |
| 9. | Afisi ya Uhamiaji Zanzibar | Ukarabati wa nyumba ya Afisa Uhamiaji | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 7,800,000 |
| | | Ujenzi wa jengo la Ofisi na makaazi | Wilaya ya Mkoani | 79,005,000 |
| | | Ukarabati wa jengo la Ofisi | Wilaya ya Chake Chake | 18,900,000 |
| | | Ukarabati wa nyumba ya makaazi | Fletini, Wilaya ya Chake Chake | 8,160,000 |
| **Jumla** | | | | **1,145,619,444** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za madeni ya Wizara*

#### 5.13.1.4 Malimbikizo ya Madeni shilingi 21,340,514.42

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 21,340,514.42 ambapo miongoni mwa madeni hayo ni stahiki za wafanyakazi pamoja na madeni yatokanayo na kupatiwa huduma mbali mbali, madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kuyalipa. Kufanya hivyo ni kuiongezea Serikali mzigo mkubwa wa madeni na hatimae kusababisha migogoro kati ya Wizara na wadai.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

### Jadweli Nambari 109: Madeni ya muda mrefu ya Wizara

| Namba | Mtoa Huduma | Huduma Iliyopatikana | Deni Halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Maji Zanzibar | Huduma ya Maji | 3,972,802.42 |
| 2. | Shirika la Magazeti | Huduma ya magazeti | 90,000 |
| 3. | Wafanyakazi | Safari Kikazi | 13,899,000 |
| 4. | Wafanyakazi | Likizo ya Kawaida | 200,000 |
| 5. | Wafanyakazi | Mfanyakazi Bora | 200,000 |
| 6. | Wafanyakazi | Kufanyakazi katika muda wa ziada | 2,478,712 |
| 7. | Mfanyakazi Mstaafu | Zawadi | 500,000 |
| **Jumla** | | | **21,340,514.42** |

*Chanzo: Orodha ya madeni ya Wizara*

## 5.13.2 KAMISHENI YA ARDHI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Kamisheni ya Ardhi umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.13.2.1 Kukosekana kwa Mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia majalada ya Uhaulishaji wa Ardhi

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Mkakati wa Kidijitali wa Serikali (Government Digital Strategy) unaosimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar unaozitaka Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi ulifanya mapitio ya utaratibu wa uwekaji wa kumbukumbu za majalada ya uhaulishaji ardhi kwa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar na kubaini kutokuwepo kwa mfumo wa kielektoniki wa uwekaji wa kumbukumbu za majalada ya uhaulishaji, badala yake Kamisheni inaweka kumbukumbu za majalada ya uhaulishaji ardhi kwa kutumia njia za kawaida na programu ya Excel jambo ambalo linapelekea ugumu katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo ufuatiliaji wa kumbukumbu za majalada ya uhaulishaji wa ardhi.

Kukosekana kwa mfumo wa kielektroniki kunapelekea Kamisheni kutoweza kufanya kazi zake kwa umakini na ufanisi jambo ambalo linaweza kupelekea uwepo wa ongezeko la migogoro ya ardhi kutokana na kuchelewa kufanyiwa maamuzi yanayotokana na umiliki wa ardhi na hatimae kushindwa kufikia malengo na tija iliyokusudiwa kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Ardhi kuhakikisha unaanzisha mfumo wa kielektroniki utakaoweza kusimamia, kutunza taarifa na kufuatilia majalada ya utendaji wa shughuli za Kamisheni kwa urahisi ili kuweza kupatikana ufanisi wa taarifa pamoja na kuimarisha usalama wa taarifa za majalada hayo.

### 5.13.2.2 Kutokuandaliwa kwa Mpango Mkakati (Strategic Planning)

Mpango Mkakati ni mfumo wa maandishi unaonyesha kazi zinazotakiwa kufanywa na hatua mbalimbali za kufikia malengo ya muda mrefu yaliyowekwa kwa muda wa kipindi cha miaka mitatu au miaka mitano kwa lengo la kuleta ufanisi katika taasisi husika. Ukaguzi umebaini kwamba Kamisheni ya Ardhi Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 imeshindwa kuandaa Mpango Mkakati (strategic plan) unaohusiana na Taasisi hiyo.

Kufanya hivyo kunapelekea kutopatikana kwa udhibiti na ufatiliaji wa vipaumbele vinavyohitajika kufanywa na Kamisheni jambo ambalo linaweza likapelekea kutoenda sambamba na Mpango Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar kusimamia kwa karibu uandaaji wa mpango mkakati kwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi kutokana na malengo yaliyokusudiwa.

### 5.13.2.3 Malimbikizo ya Madeni ya Mapato shilingi 7,750,000

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Ardhi Zanzibar inazidai taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya shilingi 7,750,000 kutokana na huduma za kazi ya upimaji wa Ardhi iliyotolewa na Kamisheni. Madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Kamisheni katika kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo.

Kufanya hivyo ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangetumika katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali ikiwemo miradi ya maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya ufuatiliaji wa madeni ili yaweze kukusanywa kama ilivyopangwa. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 110: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu**

| Namba | Jina la Taasisi | Eneo la Kazi | Deni Halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkuu wa Wilaya ya Micheweni/WHVUM | Kishindeni | 500,000 |
| 2. | Mkuu wa Wilaya ya Micheweni | Tehama Micheweni | 250,000 |
| 3. | | Kiwanja cha Ofisi | 500,000 |
| 4. | Baraza la Mji Wete | Wete Jamhuri Hall | 500,000 |
| 5. | Wizara ya Habari V/U/Michezo | Wete, Weni | 400,000 |
| 6. | Afisa Mdhamini NBM | Ikulu Micheweni | 400,000 |
| 7. | Afisa Mdhamini Kilimo | Micheweni | 300,000 |
| 8. | | Matrekta | 500,000 |
| 9. | Mkuu wa Wilaya ya Mkoani/Whvum | Michezo Kangani | 500,000 |
| 10. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini | Kinyasini | 1,000,000 |
| 11. | | Chasasa Wajasiriamali | 500,000 |
| 12. | Mkurugenzi H/Micheweni | Tumbe W/Amali | 400,000 |
| 13. | | Konde Bus Stand | 400,000 |
| 14. | Wizara ya Elimu | Vitongoji | 600,000 |
| 15. | | Tumbe/Giningi | 1,000,000 |
| **Jumla** | | | **7,750,000** |

## KAMATI YA UDHIBITI WA UJENZI IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI (DCU)

### 5.13.2.4 Fedha ambazo hazikuhaulishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha mwisho wa mwaka shilingi 56,624,398

Kwa mujibu wa Toleo nambari AD.5/184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 kipengele D kinaeleza kwamba Bakaa ya fedha za Wizara/Idara/Mikoa na Taasisi za SMZ (Central Government) zilizokua zimepangiwa kutumika kwa baadae (Commitment) zote ziingizwe katika hesabu Kuu ya Serikali iliyoko Benki Kuu nambari 9928161804 (C. Miscellaneous Deposit Account) na bakaa ambazo hazina Commitment zirejeshwe Mfuko Mkuu wa Hazina (Mfuko Mkuu wa hazina hesabu nambari 0404381000).

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 56,624,398 zimeonekana kubakia katika Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Vibali vya Ujenzi (DCU) bila ya kufanyiwa uhaulishwaji na kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali hesabu nambari 0404381000 ili kuendana na miongozo iliyotolewa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na toleo nambari AD.5/184/01/07/80 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Vibali vya Ujenzi kuhakikisha unafuata sheria na miongozo ya fedha kiukamilifu ikiwemo kuhaulisha fedha katika mfuko mkuu wa Hazina baada ya kufikiwa na muda wa kufunga mahesabu.

### 5.13.2.5 Ukiukwaji wa ukusanyaji wa Kodi ya Ardhi (Land lease Rent)

Ukaguzi umebaini kwamba kodi inayotokana na uhaulishaji wa ardhi (Land Lease Rent) inakusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) badala ya kukusanywa na Kamisheni ya Ardhi ikiwa ni moja ya kianzio chake cha mapato. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilipewa mamlaka ya kukusanya kodi hiyo kwa barua yenye kumb. no. MUNA/3/C100. VOL.XYIII/131 ya 4/3/2009 inayohusu kukusanya Kodi za Ardhi na Madeni inayoeleza katika kipengele cha kwanza kwamba "Mamlaka ya ZRA imepewa ruhusa na Waziri kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi na usajili kukusanya kodi za Ardhi (zilizokodishwa), kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya barua hii."

Aidha, kwa barua hiyo Mamlaka ya kukusanya kodi ya Ardhi inatakiwa iwe imesharudishwa kwa Taasisi husika kwa njia ya maandiko ya kisheria.

Ukusanyaji wa mapato hayo kupitia kwa Mamlaka ya Mapato ni kwenda Kinyume na kifungu 22(3) cha Sheria nambari 6 ya 2015 ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Ardhi.

Kuendelea kukusanywa kwa fedha hizo kupitia Mamlaka ya mapato (ZRA) ni kwenda kinyume na maelekezo ya barua hiyo na kunaweza kusababisha kuipunguzia mapato yake Kamisheni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuchukua hatua zinazofaa kwa mujibu wa sheria yao kuhakikisha kwamba mapato hayo yanarudi chini ya usimamizi wa Kamisheni.

### 5.13.2.6 Kukosekana kwa idhini ya matumizi ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari shilingi 96,226,530

Ukaguzi umebaini kuwa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Vibali vya Ujenzi (DCU) imetumia jumla ya shilingi 96,226,530 ambayo ni fedha iliotengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari na kutumika kwa matumizi mengine ambayo hayakupangwa. Aidha matumizi hayo hayakufuata utaratibu wowote wa uhaulishaji wa kifungu unaokubalika kisheria.

Hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa nyaraka zilizoruhusu kufanyika kwa matumizi hayo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 20(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Vibali vya Ujenzi (DCU) kufuata sheria na kanuni za fedha za umma za 2021 kwa lengo la kufanya utekelezaji kulingana na fedha zilizopangwa kwa kila shughuli iliyoainishwa katika mpango wa bajeti.

## KAMISHENI YA ARDHI PEMBA

### 5.13.2.7 Kukosekana kwa hati miliki ya Jengo la Afisi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Ukaguzi umebaini kuwa jengo la Afisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba lililopo eneo la Machomane Chake Chake bado halina hati miliki jambo ambalo linaweza kupelekea kutokea kwa migogoro inayohusiana na umiliki wa eneo hilo na hatimae kuitia hasara Serikali kutokana na kukosekana uthibitisho wa hati ya umiliki, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kuhakikisha unasimamia taratibu za upatikanaji wa hati miliki ya jengo ili kuepusha uwezekano wa kutokea migogoro ya umiliki baina ya wananchi na Kamisheni.

### 5.13.2.8 Ununuzi wa Mafuta bila ya Kuwepo Mkataba Shilingi 24,598,930

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa mali za Umma ya 2016 kinachoeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 24,598,930 zimelipwa na Kamisheni ya Ardhi Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kutoka Chake Chake Petrol Station bila ya kuwepo kwa mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uwezekano wa kukosa huduma bora na ya uhakika, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani, pamoja na kukosa umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kufunga mikataba na watoa huduma kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 111: Mafuta yaliyonunuliwa bila ya kuwepo mkataba

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Fedha Zilizolipwa (Tsh) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 11/8 ya 22/8/22 | 28724 | 3,393,650 | Chake Petrol Station | Ununuzi wa mafuta ya diesel |
| 2. | 5/9 ya 6/9/2022 | 29204 | 149,500 | | |
| 3. | 2/10 ya 5/10/22 | 29932 | 2,930,200 | | |
| 4. | 19/12ya 29/12/22 | -- | 2,995,980 | | |
| 5. | 23/2 ya 23/2/23 | 33419 | 170,430 | | |
| 6. | 24/2 ya 28/2/23 | 33573 | 3,226,210 | | |
| 7. | 26/3 ya 30/3/23 | 34425 | 2,747,560 | | |
| 8. | 5/5 ya 17/5/23 | 35175 | 3,497,400 | | |
| 9. | 20/6 ya 19/9/23 | 36263 | 5,488,000 | | |
| **Jumla** | | | **24,598,930** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa hati za malipo za Kamisheni.*

### 5.13.2.9 Malimbikizo ya madeni shilingi 13,217,008

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Ardhi Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 13,217,008 na watumishi wake kutokana na stahiki mbalimbali jambo ambalo linaweza kupelekea kushuka kwa ufanisi katika utendaji wa kazi kwa watumishi hao, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nllichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni kutoa kipaumbele kwa kufanya malipo ya stahiki za watumishi ili kuwaongezea ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi zao. Mchanganuo wa malimbikizo ya madeni hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 112: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu

| Nambari | Mtoa Huduma | Huduma Iliyotolewa | Deni halisi (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wafanyakazi (5) | Likizo | 500,000 |
| 2 | Wafanyakazi | Safari Kikazi | 4,478,000 |
| 3 | Wafanyakazi (22) | Overtime | 641,108 |
| 4 | Wafanyakazi | Deni La Masomo | 5,197,900 |
| 5 | Wafanyakazi (5) | Ufiwa | 2,400,000 |
| **Jumla** | | | **13,217,008** |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za madeni ya Kamisheni.*

## 5.14 WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

### 5.14.1 FUNGU N 03 - WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.14.1.1 Dosari zilizojitokeza katika Usimamizi wa Rasilimali zisizorejesheka

Katika kuhakikisha wakazi wa Zanzibar wananufaika na huduma za maji safi na salama, upatikanaji na ufanisi wa nishati endelevu kwa usambazaji kirahisi na kupunguza gharama kwa kutoa huduma nafuu, endelevu, zenye ubora kwa watu wote na katika mazingira yanayowezesha utoaji huduma bora katika Maji, Nishati na Madini ndipo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipoanzisha wazo la uwepo wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mujibu wa kifungu nambari 42 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na marekebisho yake.

Pamoja na uanzishwaji wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini mnamo mwezi Novemba, 2020 ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbalimbali zinazojitokeza katika usimamiaji wa maliasili zisizorejesheka, miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- **Kutokuwepo kwa Sheria, Kanuni na Sera za Kusimamia Mali Asili zisizorejesheka**

Kutokana na kukosekana kwa Sheria, Kanuni na Sera kunapelekea Wizara kutokuwa na nguvu ya kisheria ya utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka badala yake inatumia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwka 2015 na kanuni yake kinyume na malengo ya uanzishwaji wa Wizara.

- **Kukosekana kwa Mapato yatokanayo na usafirishaji na uingizaji wa Madini**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar kupitia kanuni yake ya Uingizaji na Usafirishaji wa Madini ya Thamani au Vito ya 2022. Kwa mwaka wa fedha unaishia 30 Juni, 2023 Wizara ya Biashara ilikusanya jumla ya shilingi 242,919,628 zinazotokana na usafirishaji wa madini. Licha ya wizara ya biashara kuwa na kanuni hiyo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ndio mwenye jukumu la kusimamia na kutoa leseni za usafirishaji wa madini. Hadi ukaguzi unamalizika Wizara haina sheria wala kanuni ya usimamizi wa madini hayo ambayo imepelekea kukosekana kwa mapato hayo.

Kukosekana kwa Kanuni na Sheria za usimamizi wa maliasili zisizorejesheka kumepelekea Wizara kuunda Kamati ya Usimamizi wa Makosa ya Maliasili zisizorejesheka kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi jambo ambalo ni kwenda kinyume na utaratibu wa kisheria.

Kutokana na kitendo cha kuundwa kwa Kamati hiyo ambayo haina nguvu kisheria kuna uwezekano mkubwa wa kuisababishia hasara Serikali pindipo itakaposhtakiwa na kupandishwa mahakamani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaandaa utaratibu wa upatikanaji wa sheria za maliasili zisizorejesheka ili kutoa nguvu ya kisheria ya ufanyaji kazi wa Kamati ya Usimamizi wa makosa ya rasilimali zisizorejesheka pamoja na uandaaji wa kanuni za usimamizi wa madnini kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na wadau wengineo.

### 5.14.1.2 Kutokuwepo kwa Dhamana kwa Mashamba yalioruhusiwa Kuchimbwa Mali Asili Zisizorejesheka

Kifungu nambari 33(2)(3) cha sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015, inaeleza, Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kibali cha uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka kitatolewa kwa kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ukarabati wa eneo lililochimbwa lililotolewa na taasisi inayohusika. Vile vile mtu aliyepewa kibali cha kuchimba maliasili zisizorejesheka atatakiwa kuweka dhamana ya utendaji wa mazingira (Environmental Performance Bond) kwa taasisi inayohusika na maliasili zisizoweza kurejeshwa.

Wakati wa ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaishia 30 June, 2023 ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea mashamba yaliochimbwa na yanayochimbwa mali asili zisizorejesheka na kubaini kati ya mashamba hayo hakuna shamba hata moja lililoweka dhamana ya utendaji wa mazingira (Environmental Performance Bond) kwa wizara ya maji, nishati na madini.

Kutokuwepo kwa dhamana kwa mashamba yalioruhsiwa kuchimbwa mali asili zisizorejesheka kunapelekea udhibiti unaibua wasiwasi kuhusu uwajibikaji wa mazingira na uendelevu wa shughuli za uchimbaji na kwenda kinyume na kifungu nambari 33 (2) (3) cha sheria ya usimamizi wa mazingira Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuhakikisha kwamba mashamba yote ya uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka yanatimiza matakwa ya kutoa dhamana za utendaji wa mazingira (Environmental Performance Bond).

### 5.14.1.3 Kutoyafanyia Uhuishaji Mashamba yaliochimbwa Mali Asili Zisizorejesheka (Mchanga)

Kifungu nambari 34(1)(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2015, kinaeleza kuwa mtu ambaye atapewa kibali cha uchimbaji wa maliasili zisizo rejesheka atakuwa na jukumu la kukarabati eneo lililochimbwa. Vile vile itakuwa ni wajibu wa taasisi inayohusika na maliasili zisizorejesheka ili kuhakikisha ukarabati mzuri wa eneo lililochimbwa.

Wakati wa ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea mashamba yote yaliochimbwa mchanga na kubaini kuwa kuna mashamba bado hayajafanyiwa uhuishaji.

Kutofanyiwa uhuishaji mashamba yaliyochimbwa maliasili zisizorejesheka kunaweza kuathiri mazingira maeneo hayo hatimae kusababisha mmong'onyoko wa udongo, upotevu wa viumbe hai, na uchafuzi wa maji na mabadiliko ya tabia nchi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kufatilia uhuwishaji wa maeneo yaliyochimbwa maliasili zisizorejesheka ili kuepusha athari mbali mbali zinazoweza kujitokeza zitokanazo na uharibifu uliofanyika katika maeneo hayo. Mashamba yenyewe ni kama yanavyoonekana katika jadweli lililopo hapo chini: -

**Jadweli Nambari 113: Orodha ya mashamba yaliochimbwa na bado hayajafanyiwa uhuishaji**

| Namba | Mmiliki wa shamba | Eneo liliopo | Kufanyiwa uhuishaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Abdillah Mgeni Kassim | Mkokotoni | |
| 2. | Abbas Ussi na Asha Ibrahim | Donge Muwanda | |
| 3. | Abdillah Mgeni Kassim | Mkokotoni | |
| 4. | Kamna Ali Abeid | Donge Mchangani | |
| 5. | Hamadi Juma | Donge Kipange | Bado |
| 6. | Othman Khamis | Donge Mchangani | |
| 7. | Shamba la Serikali la fidia | Donge Muwanda | |
| 8. | Rashid Abdalla Khamis | Donge Muwanda | |
| 9. | Bibi Tatu Haji Mkuja | Zingwezingwe | |

*Chanzo: Ufuatiliaji wa maeneo ya maliasili zisizorejesheka*

**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI PEMBA**

### 5.14.1.4 Malimbikizo ya Madeni shilingi 12,518,613.17

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Maji, Nishati na Madini Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 12,518,613.17 na watoa huduma mbalimbali, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kuyalipa madeni hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni kwa wakati. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 114: Madeni ya muda mrefu ya Wizara

| Namba | Mtoa Huduma | Huduma Iliyotolewa | Deni halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba | Ununuzi wa Vitabu vya Stakabadhi | 9,850,000.00 |
| 2. | | Ukodishwaji wa Ukumbi | 500,000.00 |
| 3. | Mamlaka ya Maji | Huduma ya Maji | 1,968,613.17 |
| 4. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | Ukodishwaji wa Vipaza Sauti | 200,000.00 |
| **Jumla** | | | **12,518,613.17** |

*Chanzo: Orodha ya madeni ya Wizara*

### 5.14.1.5 Kutokuwepo kwa kadi za usajili wa vyombo vya moto

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya vyombo vya moto vinavyomilikiwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini Pemba havina kadi za usajili jambo ambalo linapelekea uhalali wa umiliki wa vyombo hivyo kutokukamilika, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kuvifanyia usajili vyombo vya moto kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 115: Vyombo vya moto ambavyo havina kadi za usajili

| Namba | Aina ya Chombo | Nambari ya Usajili | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|
| 1. | Gari | SMZ 760A | Wizara |
| 2. | | SMZ 603B | Idara ya Nishati na Madini |
| 3. | Pikipiki | SMZ 1605C | |
| 4. | | SMZ 1604C | |

## 5.15 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### 5.15.1 FUNGU P01 - WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.15.1.1 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 12,942,580,833.23

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 12,942,580,833.23 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi lakini baadhi ya vielelezo hivyo havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Wizara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuthibitisha uhalali wa malipo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 116: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Fedha iliyotumika (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 3/5 ya 8/05/23 | M/S Coastal Dredging Co. Ltd | 996,634,814.23 | Malipo ya bakaa ya Deni |
| 2. | 4/5 ya 12/5/23 | M/S Orkun Group Z'bar ltd (CCECC) | 4,559,280,000.00 | Ujenzi wa bandari |
| 3. | 1/10 ya 19/10/22 | M/S Clyde | 481,183,926 | Malipo ya kumlipa mshauri elekezi |
| 4. | 231/06 ya 19/6/23 | M/S Orkun Group Z'bar ltd (CCECC) | 6,905,482,093 | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa bandari. |
| **Jumla** | | | **12,942,580,833.23** | |

### 5.15.1.2 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika Daftari la Ghalani shilingi 35,280,000

Kanuni nambari 113 ya kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaelezea kwamba "Bidhaa zote zinazonunuliwa zipokelewe katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani na zitolewe kwa mujibu wa matumzi ya bidhaa hizo".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 35,280,000 zimelipwa kupitia hati nambari 273/6 ya tarehe 26/06/2023 kwa ajili ya ununuzi wa mipira ya gari lakini mipira hiyo haikurikodiwa kwenye daftari la kurikodia bidhaa za ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya utekelezaji na usimamizi wa masuala ya fedha na rasilimali za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba bidhaa zote zinazonunuliwa zinarikodiwa katika vitabu vya uwekaji wa kumbukumbu za vifaa vya ghalani mara tu taratibu za ununuzi zinapokamilika.

### 5.15.1.3 Ununuzi wa Bidhaa mbalimbali bila ya kuwepo mkataba shilingi 427,381,563.34

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 427,381,563.34 zimelipwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa kwa watoa huduma mbalimbali bila ya kufunga mkataba maalum wa ununuzi wa bidhaa hizo, jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuka kwa migogoro baina ya wafanyabiashara hao na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama sheria inavyoelekeza.

## 5.16 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

### 5.16.1 FUNGU Q01 - OFISI YA RAIS KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**OFISI YA RAIS KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI PEMBA**

#### 5.16.1.1 Kutokulipwa kwa ada ya ukaguzi shilingi 9,323,600

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58 cha Sheria nambari 15 ya Vyama vya Ushirika ya 2018 kinaeleza kwamba "Mkurugenzi anaweza, katika mazingira na namna inavyoelezwa katika kanuni, na kwa maombi ya mdai wa chama cha ushirika, kufanya ukaguzi wa kawaida au kuwataka baadhi ya watu kwa maandishi kufanya ukaguzi wa vitabu vya chama cha Ushirika". Aidha kanuni namba 58 ya Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya 2019 inaeleza kwamba "Chama cha Ushirika kitalipia ada ya ukaguzi kwa mujibu wa muongozo wa ada kama utakavyotolewa na Waziri".

Ukaguzi umebaini kutokulipwa kwa ada ya ukaguzi wa vyama vya ushirika yenye jumla ya shilingi 9,323,600, ada itokanayo na chanzo cha ukaguzi ambayo ni sawa na asilimia 5 ya faida ya chama baada ya kufanyiwa ukaguzi jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na chanzo hicho, aidha ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria na Kanuni nilizozinakili hapo juu.

Hali hii imesababishwa na kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia ada hiyo kwa kutovichukulia hatua stahiki vikundi vinavyodaiwa au kuvifikisha katika vyombo vya sheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kusimamia kikamilifu sheria, kanuni pamoja na miongozo ikiwemo kukusanya ada ya mapato yatokanayo na ukaguzi wa vyama vya ushirika kwa wakati. Mchanganuo wa ada hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 117: Ada ya ukaguzi ambayo haikulipwa

| Namba | Jina la Kikundi | Wilaya Kilipo | Faida (Tshs) | Ada Iliyolipwa (Tshs) | Deni lililosalia (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hapa Kazi Tu | Wete | 2,825,000.00 | 30,000.00 | 111,250.00 |
| 2. | Wengi Si Hoja | | 700,000.00 | 30,000.00 | 5,000.00 |
| 3. | Nia Safi | | 800,000.00 | 30,000.00 | 10,000.00 |
| 4. | Haturudi Nyuma | Mkoani | 5,910,000.00 | 0 | 295,500.00 |
| 5. | Umasikini Si Kilema | Micheweni | 1,350,000.00 | 30,000.00 | 37,500.00 |
| 6. | Tudumishe Maendeleo | Chake Chake | 870,000.00 | 30,000.00 | 13,500.00 |
| 7. | Ushirika ni Nguvu | Chake Chake | 900,000.00 | 30,000.00 | 15,000.00 |
| 8. | Mtarazaki | Wete | 700,000.00 | 30,000.00 | 5,000.00 |
| 9. | Wanaharakati | | 800,000.00 | 30,000.00 | 10,000.00 |
| 10. | Umoja ni Ngao Yetu | | 670,000.00 | 30,000.00 | 3,500.00 |
| 11. | Kilimo Hai Kwa Vijana | | 1,200,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 |
| 12. | Maelewano | | 650,000.00 | 30,000.00 | 2,500.00 |
| 13. | Mkombozi Saccoss | Mkoani | 1,200,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| 14. | Abdalla Mzee Saccos | | 3,100,000.00 | 100,000.00 | 55,000.00 |
| 15. | Mtaka Mbele Mpishe | Chake Chake | 1,300,000.00 | 30,000.00 | 35,000.00 |
| 16. | Sio Siri | | 700,000.00 | 30,000.00 | 5,000.00 |
| 17. | Chekeni | | 760,000.00 | 30,000.00 | 8,000.00 |
| 18. | Bora Liwe Jema | | 780,000.00 | 30,000.00 | 9,000.00 |
| 19. | Hatubadiliki | | 900,000.00 | 30,000.00 | 15,000.00 |
| 20. | Ubunifu Coop | Wete | 970,000.00 | 30,000.00 | 18,500.00 |
| 21. | Tushirikiane Kifumbikai | | 15,811,000.00 | 30,000.00 | 760,550.00 |
| 22. | Kibubu Hakijai | | 650,000.00 | 30,000.00 | 2,500.00 |
| 23. | Tuko Fiti | Mkoani | 6,070,000.00 | 30,000.00 | 273,500.00 |
| 24. | Katumeni | | 650,000.00 | 0 | 32,000.00 |
| 25. | Bado Tuko Hai | | 900,000.00 | 30,000.00 | 15,000.00 |
| 26. | Nia Moja | Micheweni | 1,200,000.00 | 0 | 60,000.00 |
| 27. | Yataka Moyo | | 7,460,000.00 | 0 | 373,000.00 |
| 28. | Hapa Kazi Tu | | 1,703,000.00 | 30,000.00 | 55,150.00 |
| 29. | Tushirikiane Mtemani | | 870,000.00 | 30,000.00 | 13,500.00 |
| 30. | Nia Moja Mtemani | Micheweni | 980,000.00 | 0 | 49,000.00 |
| 31. | Choka Ni Ngao | | 760,000.00 | 30,000.00 | 8,000.00 |
| 32. | Yataka Moyo | | 750,000.00 | 0 | 37,500.00 |

| Namba | Jina la Kikundi | Wilaya Kilipo | Faida (Tshs) | Ada Iliyolipwa (Tshs) | Deni lililosalia (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 33. | Interpole | Chake Chake | 300,000.00 | 0 | 15,000.00 |
| 34. | Tujiwezeshe | | 1,260,000.00 | 30,000.00 | 33,000.00 |
| 35. | Team Work | Wete | 680,000.00 | 30,000.00 | 4,000.00 |
| 36. | Mwendo Kasi | | 1,850,000.00 | 30,000.00 | 62,500.00 |
| 37. | Tunaweza | | 1,450,000.00 | 30,000.00 | 32,500.00 |
| 38. | Tumain Bopwe | | 760,000.00 | 30,000.00 | 8,000.00 |
| 39. | Tasini | Mkoani | 760,000.00 | 30,000.00 | 8,000.00 |
| 40. | Tushirikiane | | 1,900,000.00 | 30,000.00 | 65,000.00 |
| 41. | Tuwe Imara | | 238,000.00 | 0 | 11,900.00 |
| 42. | Penye Rizikihapakosi Fitina | | 879,000.00 | 0 | 43,950.00 |
| 43. | Tuhamasike | Micheweni | 1,000,000.00 | 30,000.00 | 20,000.00 |
| 44. | Nia Njema Hairogwi | | 1,300,000.00 | 30,000.00 | 35,000.00 |
| 45. | Kitonga Coop | | 1,250,000.00 | 0 | 62,500.00 |
| 46. | Nguvu ni Hazina | | 2,000,000.00 | 30,000.00 | 70,000.00 |
| 47. | Tafakar | | 800,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 |
| 48. | Penye Nia Ipo Njia | | 549,000.00 | 0 | 27,450.00 |
| 49. | Tujali Wakati | | 900,000.00 | 30,000.00 | 15,000.00 |
| 50. | Kichumbini | Wete | 35,335,000.00 | 0 | 1,766,750.00 |
| 51. | Kisiwani Salt | | 900,000.00 | 0 | 45,000.00 |
| 52. | Haturudi Nyuma | Micheweni | 5,910,000.00 | 0 | 295,500.00 |
| 53. | Matumbawe | | 890,000.00 | 0 | 44,500.00 |
| 54. | Siri ya Maendeleo | | 1,000,000.00 | 30,000.00 | 20,000.00 |
| 55. | Fitina Mbaya | Wete | 8,490,000.00 | 30,000.00 | 394,500.00 |
| 56. | Hatuyumbi | | 760,000.00 | 30,000.00 | 8,000.00 |
| 57. | Masumbuko | | 5,050,000.00 | 0 | 252,500.00 |
| 58. | Haturudi Nyuma | | 80,000.00 | 0 | 4,000.00 |
| 59. | Masota Salt | | 4,680,000.00 | 30,000.00 | 204,000.00 |
| 60. | Mshikamano | Chake Chake | 8,270,000.00 | 0 | 413,500.00 |
| 61. | Muamko | | 7,400,000.00 | 30,000.00 | 340,000.00 |
| 62. | Mtaji Wa Masikini | | 16,250,000.00 | 30,000.00 | 782,500.00 |
| 63. | Muungu Tupe Baraka | | 7,000,000.00 | 30,000.00 | 320,000.00 |
| 64. | Tunaweza Makange | | 680,000.00 | 0 | 340,000.00 |
| 65. | Almujitahid | | 680,000.00 | 30,000.00 | 4,000.00 |

| Namba | Jina la Kikundi | Wilaya Kilipo | Faida (Tshs) | Ada Iliyolipwa (Tshs) | Deni lililosalia (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 66. | Kwa Tego Miling | Mkoani | 9,050,000.00 | 0 | 452,500.00 |
| 67. | Hatuyumbi | | 4,836,000.00 | 30,000.00 | 211,800.00 |
| 68. | Kukuu Fishing | | 743,000.00 | 30,000.00 | 7,150.00 |
| 69. | Kukuu Women | | 789,000.00 | 0 | 39,450.00 |
| 70. | Chakarika Jonza | | 3,200,000.00 | 0 | 160,000.00 |
| 71. | Vunja Ukimya | | 789,000.00 | 30,000.00 | 9,450.00 |
| 72. | Tumaini Jipya | Wete | 3,360,000.00 | 30,000.00 | 138,000.00 |
| 73. | Wembe Coop | | 754,000.00 | 0 | 37,700.00 |
| 74. | Mambo Waa | | 1,430,000.00 | 30,000.00 | 41,500.00 |
| 75. | Jiwezeshe | | 675,000.00 | 0 | 33,750.00 |
| 76. | Umoja ndio Dira ya Maendeleo | | 796,000.00 | 0 | 39,800.00 |
| **Kiwango cha Fedha Kinachodaiwa** | | | | | **9,323,600.00** |

## 5.17 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

### 5.17.1 FUNGU R01 - WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA PEMBA**

#### 5.17.1.1 Ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo mkataba shilingi 45,541,599

Kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba “Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 45,541,599 zimelipwa kwa Chasasa Service Station bila ya kufunga mkataba maalum wa ununuzi wa mafuta, jambo ambalo linaweza kuleta migogoro baina ya mfanyabiashara huyo na Wizara pale inapotokezea kutokufahamiana, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufunga mikataba kwa watoa huduma kama Sheria inavyoelekeza. Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa bila ya kufunga mkataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 118: Ununuzi wa Mafuta bila kufunga mkataba

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 01/08 ya 10/08/2022 | 028565 | 4,831,840 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 2. | 02/08 ya 10/08/2022 | 028566 | 1,254,580 | |
| 3. | 17/08 ya 22/08/2022 | 028720 | 610,064 | |
| 4. | 03/09 ya 09/09/2022 | 029260 | 1,480,000 | |
| 5. | 28/09 ya 21/09/2022 | 029527 | 610,000 | |
| 6. | 02/10 ya 12/10/2022 | 030068 | 3,490,640 | |
| 7. | 21/10 ya 27/10/2022 | 030627 | 1,999,580 | |
| 8. | 01/11 ya 16/11/2022 | 030869 | 4,726,110 | |
| 9. | 02/12 ya 06/12/2022 | 031448 | 596,000 | |
| 10. | 03/01 ya 02/01/2023 | 032130 | 3,352,500 | |
| 11. | 12/01 ya 05/01/2023 | 032208 | 1,873,745 | |
| 12. | 01/02 ya 01/02/2023 | 032864 | 1,231,040 | |
| 13. | 02/02 ya 16/02/2023 | 033034 | 4,065,000 | |
| 14. | 19/02 ya 27/02/2023 | 033539 | 1,877,000 | |
| 15. | 14/03 ya 30/03/2023 | 034399 | 3,549,000 | |
| 16. | 18/03 ya 31/03/2023 | -- | 1,932,480 | |
| 17. | 01/05 ya 15/05/2023 | 035276 | 4,089,000 | |
| 18. | 22/05 ya 30/05/2023 | 035839 | 1,309,380 | |
| 19. | 05/06 ya 16/06/2023 | 036147 | 1,830,000 | |
| 20. | 13/06 ya 19/06/2023 | 036253 | 833,640 | |
| **Jumla** | | | **45,541,599** | |

*Chanzo: Taarifa za Wizara*

### 5.17.1.2 Kukosekana kwa hati miliki kwa baadhi ya mali za Wizara

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa majengo ya Wizara ambayo hayana hati miliki jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Wizara kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hatimiliki mali za Wizara. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 119: Mali za Wizara ambazo hazina hati miliki**

| Namba | Aina ya Mali | Mahala lilipo | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mtaa | Shehia | Wilaya |
| 1. | Ghala la Akiba | Kwa mpika tango | Ng'ombeni | Mkoani |
| 2. | Ghala la Akiba | Kilimandege | Bopwe | Wete |
| 3. | Kiwanda cha mafuta ya Nazi | Bopwe | Bopwe | Wete |

*Chanzo: Taarifa za Wizara*

### 5.17.1.3 Kukaimu nafasi kinyume na utaratibu

Kanuni ya 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa "Hakutokuwa na nafasi ya kukaimu ya zaidi ya muda wa miezi kumi na mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa watumishi wawili wa Wizara walioteuliwa kukaimu nafasi tofauti kwa zaidi ya miezi kumi na mbili (12). Hadi ukaguzi huu unakamilika bado watumishi hao wanaendelea kukaimu nyadhifa hizo bila ya kuthibitishwa wala nafasi hizo kujazwa na watumishi wengine wenye sifa.

Kutokuthibitishwa kwa wakati kwa watumishi kunaweza kupelekea kuwavunja moyo watumishi hao katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa, jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kuwathibitisha watumishi waliokaimu inapofikia muda au kuteua watumishi wengine waliokidhi vigezo ili kujaza nafasi hizo. Mchanganuo wa watumishi hao ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 120: Watumishi waliokaimishwa nafasi kinyume na utaratibu**

| Namba | Jina la Mtumishi | Barua ya Kukaimu | Tarehe ya Kukaimishiwa | Muda wa Kukaimu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Said Shaame Bakari | IAA/IBA/S.960040/C/33 | 21/03/2022 | Miezi 23 |
| 2. | Salim Suleiman Mgeni | WBMV/P4/28/VOL.III/15 | 26/9/2022 | Miezi 17 |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za majalada binafsi ya watumishi*

### 5.17.2 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**TAASISI YA VIWANGO PEMBA**

#### 5.17.2.1 Kutokuwepo kwa maabara za kupimia bidhaa Pemba

Taasisi ya Viwango Pemba ina wajibu wa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ili kuweza kufikia malengo yake kwa utaratibu mzuri unaokubalika, uhakika na ufanisi zaidi.

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa maabara za kupimia sampuli za bidhaa zinazoingia Pemba jambo ambalo linapelekea sampuli hizo kusafirishwa kwenda maabara za Taasisi ya Viwango Zanzibar makao makuu Unguja ili kufanyiwa vipimo na baadae kurejeshwa majibu kwa Taasisi Pemba jambo ambalo hupelekea kuchelewa upatikanaji wa huduma kwa jamii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi ya Viwango Pemba kuendelea kufuatilia upatikanaji wa maabara kwa upande wa Pemba ili kuweza kupelekea Taasisi kufanyakazi kwa uhakika na ufanisi zaidi.

### 5.17.3 TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA PEMBA**

#### 5.17.3.1 Kutokuwepo kwa makadirio ya mapato na matumizi

Kifungu nambari 41(2)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza "Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuisha makadirio ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa programu".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 haikuandaa makadirio ya mapato na matumizi (bajeti) jambo ambalo limepelekea Tume kufanya matumizi bila ya kuwa na muongozo wa kibajeti uliopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea Tume kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli zake, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kuandaa makadirio ya mapato na matumizi kila mwaka wa fedha.

#### 5.17.3.2 Kukosekana kwa mpango kazi na mpango wa ununuzi wa Tume

Kifungu nambari 41(2)(c) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza "Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuisha Mpango kazi na mpango wa ununuzi".

Ukaguzi umebaini kwamba Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 haikutayarisha mpango kazi na mpango wa ununuzi jambo ambalo linapelekea kufanyika kwa manunuzi ya bidhaa na huduma bila ya kuwa na muongozo halali pamoja na kupelekea ugumu katika utekelezaji wa majukumu ya Tume, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kutayarisha mpango kazi na mpango wa manunuzi kama sheria inavyoelekeza.

### 5.17.3.3 Kutokutumika kwa hesabu ya matumizi ya kawaida ya Tume

Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Pemba inawajibu wa kuendesha na kusimamia shughuli zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kifedha ili kufikia malengo yake kwa ufanisi zaidi.

Ukaguzi umebaini kuwa mnamo mwezi Mei, 2023 Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Pemba ilifungua hesabu nambari 0852184001 katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa ajili ya matumizi ya Tume, hadi ukaguzi unakamilika hesabu hii haijawahi kuingiziwa fedha za matumizi, hali inayopelekea matumizi ya Afisi ya Tume Pemba kuendelea kufanywa na Afisi Kuu ya Tume Unguja. Kufanya hivyo kunapelekea ugumu katika utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa upande wa Pemba jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kuandaa utaratibu wa kuihuisha hesabu iliyofunguliwa ikiwemo kuomba kuingiziwa fedha kutoka Ofisi Kuu ya Tume Unguja ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Tume.

### 5.17.3.4 Malimbikizo ya madeni shilingi 20,034,000

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 20,034,000 ambapo miongoni mwa madeni hayo ni stahiki za wafanyakazi pamoja na madeni yatokanayo na kupatiwa huduma ya pango la jengo, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Tume katika kuyalipa.

Kufanya hivyo ni kuiongezea Serikali mzigo mkubwa wa madeni na hatimae kusababisha migogoro baina ya Tume na wadai, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni kwa wakati. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 121: Madeni ya muda mrefu yanayodaiwa na Tume**

| Namba | Mtoa Huduma | Huduma Iliyotolewa | Deni halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Wafanyakazi (8) | Likizo | 800,000 |
| 2. | Wafanyakazi | Nyongeza ya mshahara na maposho | 2,434,000 |
| 3. | ZSSF Pemba | Kodi ya ofisi | 16,800,000 |
| **Jumla** | | | **20,034,000** |

*Chanzo: Orodha ya madeni ya Tume*

### 5.17.3.5 Kutokuteketezwa kwa bidhaa zilizoondoshwa sokoni shilingi 5,714,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 5 ya Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya 2018 kinaeleza kwamba "Ni jukumu la Tume kuziondoa sokoni na kuzuia bidhaa zozote zilizobainika kuwa haziko salama au ni za bandia". Aidha kifungu nambari 67(1) cha Sheria hiyo kinaeleza kwamba "Bidhaa zozote zilozobainika kuwa haziko salama au ni za bandia zitateketezwa na Tume kwa utaratibu maalum ulioelezwa katika kanuni".

Ukaguzi umebaini kuwa mnamo tarehe 8/11/2022 Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Pemba ilifanikiwa kuziondoa sokoni na kuzuia jumla ya katuni 306.5 za Kareem Tomato Sauce sawa na galoni 1226 zenye ujazo wa lita 5 kwa kila galoni na thamani ya shilingi 5,714,000.

Hadi ukaguzi unakamilika, bidhaa hizo hazikufanyiwa uteketezaji jambo ambalo linaweza kupelekea kuzuia nafasi ambayo ingetumika kwa kazi nyengine pamoja na kuwepo kwa uwezekano wa kuvuja na kusababisha uharibifu wa mazingira katika eneo lililohifadhiwa bidhaa hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kuharakisha mchakato wa kuziteketeza bidhaa zilizoondolewa sokoni kutokana na kukamilika kwa taratibu zote za uteketezaji zinazohitajika.

## 6.0 HITIMISHO

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 nilifanya ukaguzi kwa kuzingatia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za juu za hesabu zinazotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi ambazo zinahusu ukaguzi wa kisekta.

Nimetoa hati za ukaguzi kwa kuzingatia taarifa za fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo niliikagua. Aidha, nilitoa barua ya ukaguzi (Management letter) zinazoonyesha dosari kwa kila Taasisi niliyoikagua na pale ambapo dosari hiyo ilikosa majibu na ushahidi sahihi ilichukuliwa na kubainishwa katika kitabu hichi kuwa ni dosari iliyokosa majibu.

Ni matumaini yangu kwamba watumiaji wa taarifa hii watanufaika na kujifunza kwa yale yote yaliyoelezwa na kubainishwa kwa uwazi ikiwemo Wakuu wa Taasisi kuweza kuyafanyia kazi na kufanya maboresho ili dosari hizo zisiweze kuendelea kujitokeza kwa mwaka ujao. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi au kunipa miongozo ya namna ya kutanua wigo wa kazi zangu katika siku zijazo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukua kuijengea uwezo Afisi yangu katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo kuboresha stahiki na maslahi ya watumishi, kunipa nguvu na kuniunga mkono wakati wa uwasilishaji wa taarifa zangu pamoja na kuzitolea maelezo na maelekezo kwa Viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya namna ya kufanya maboresho ya dosari zinazobainika katika Taasisi zao.

Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wote wanaotenga muda wao kumshauri Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kumuunga mkono na kumpa moyo katika harakati za kuliongoza Taifa hili na nia yake njema ya kuliletea maendeleo na mafanikio ikiwemo kuboresha maslahi ya mwananchi mmoja mmoja katika uibuaji wa miradi ya maendeleo yenye lengo la kukuza kipato na uchumi wa nchi hii.

Mwisho kabisa niwashukuru wale wote waliojitokeza kuniunga mkono kwa namna moja au nyengine na kufanikisha upatikanaji wa taarifa hii bila ya kuwasahau Waandishi wa Habari kwa namna walivyojitoa kuitangaza na kuifikisha taarifa hii kwa kutumia vyombo vyao mbali mbali vya ndani na nje ya nchi.

# KIAMBATISHO NAMBARI 1

## Kiambatisho Nambari 1: Watumishi ambao hawajathibitishwa

| Namba | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Cheo |
|---|---|---|---|
| 1. | Mtumwa Ubwa Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 2. | Fatma Abdalla Suleiman | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Maabara |
| 3. | Rukayya Mahmoud Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 4. | Sahnam Wahabi Massoud | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 5. | Salma Mbarouk Khamis | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 6. | Fathiya Othman Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 7. | Mafunda Said Saleh | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 8. | Zulekha Rashid Khalfan | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 9. | Halima Maulid Abdulrahman | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 10. | Aisha Omar Salim | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 11. | Aisha Talib Abdulla | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 12. | Kadhia Mahmoud Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 13. | Aisha Khamis Silima | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 14. | Abdulmajid Moh'd Rashid | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 15. | Mariamu Juma Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 16. | Aziza Shavuai Omar | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 17. | Salahi Ali Moh'd | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 18. | Hamad Juma Hamad | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 19. | Time Malik Haji | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 20. | Asila Pandu Salim | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 21. | Omar Othuman Nahoda | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 22. | Kassim Mohammed Abdalla | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 23. | Khadija Asaa Moh'd | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 24. | Zulfa Hassan Abdalla | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 25. | Nadhra Ali Haji | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 26. | Latifa Omar Moh'd | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 27. | Ahlam Salum Ahmed | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 28. | Fatma Omar Juma | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 29. | Shamis Omar Abdalla | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 30. | Hafidh Said Suleiman | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 31. | Abdul- kadir Salim Said | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 32. | Saide Ahmed Thabit | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 33. | Said Othman Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 34. | Salma Hilal Seif | 09/01/2022 | Muuguzi |

| Namba | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Cheo |
|---|---|---|---|
| 35. | Abdul- halim Salim Abdalla | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 36. | Said Rashid Hamad | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 37. | Fatima Seif Khamis | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 38. | Yussuf Ali Juma | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 39. | Aisha Othman Khalfan | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 40. | Hamad Ali Faki | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 41. | Ruwaida Machano Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 42. | Samha Moh'd Khamis | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 43. | Amina Ibrahim Suleiman | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 44. | Jokha Amour Moh'd | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 45. | Halima Said Khamis | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 46. | Juma Issa Ali | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 47. | Rutihiya Abdalla Baho | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 48. | Abdul- hamid Salim Juma | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 49. | Hairat Abuu- Bakar Juma | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 50. | Maimuna Abdalla Talib | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 51. | Asma Haji Moh'd | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 52. | Mohamed Issa Ali | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 53. | Rahma Abdullatif Hassan | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 54. | Ghalim Abdulkadir Abdulla | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 55. | Massoud Hamza Msellem | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 56. | Talha Mussa Makame | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 57. | Hudna Juma Haji | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 58. | Raya Nassor Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 59. | Bimkubwa Bakar Nassor | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 60. | Mbarouk Ali Saleh | 09/01/2022 | Fundi Sanifu Madawa |
| 61. | Sabra Mohamed Omar | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 62. | Ali Khamis Ali | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 63. | Rahma Saleh Salum | 09/01/2022 | Muuguzi |
| 64. | Salum Ali Salum | 2019 | Daktari Wa Binadamu |
| 65. | Mariam Ismail Ali | 11/05/2019 | Muhudumu Wa Afya |
| 66. | Salum Moh'd Ali | 08/05/2020 | Muuguzi |
| 67. | Moh'd Saleh Kassim | 06/01/2020 | Muhudumu Wa Afya |
| 68. | Safia Salim Moh'd | 12/01/2019 | Fundi Sanifu Maabara |
| 69. | Salha Said Moh'd | 11/02/2019 | Fundi Sanifu Maabara |
| 70. | Zabibu Ali Mzee | 12/01/2020 | Muhudumu Wa Afya |

| Namba | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Cheo |
|---|---|---|---|
| 71. | Bimkubwa Kombo Kai | 07/08/2020 | Muuguzi |
| 72. | Zainab Salum Moh'd | 07/08/2020 | Muuguzi Msaidizi |
| 73. | Khairat Aziz Said | 02/03/2020 | Muuguzi |
| 74. | Warda Mohd Said | 02/03/2020 | Orderly |
| 75. | Ali Mzee Juma | 04/01/2020 | H-Oderly |
| 76. | Maryam Matora Hussein | 06/03/2020 | H-Oderly |
| 77. | Hijra Suleiman Baraka | 06/01/2020 | Afisa Utumishi Msaidizi |
| 78. | Sada Mohammed Zahran | 06/09/2020 | H-Oderly |
| 79. | Suleiman Miraji Haji | 07/03/2020 | Lab-Technician |
| 80. | Amina Mohammed Abdalla | 08/01/2020 | Orderly |
| 81. | Hassan Ali Hassan | 09/01/2020 | Pho |
| 82. | Mauwa Hussein Rashid | 10/05/2020 | Orderly |
| 83. | Iddi Suleiman Ali | 12/01/2020 | Afisa Afya |
| 84. | Farid Moh'd Khamis | 12/01/2020 | Muhudumu Wa Afya |
| 85. | Mwanaharus Ali Amour | 12/01/2020 | Muhudumu Wa Afya |
| 86. | Ramla Abdalla Omar | 12/01/2020 | Afisa Manunuzi Msaidizi |
| 87. | Haji Said Haji | 12/01/2020 | Afisa Afya |
| 88. | Salha Ali Abdalla | 12/01/2020 | Afisa Afya |
| 89. | Mgeni Juma Said | 12/01/2020 | Afisa Afya |
| 90. | Salum Abeid Hemed | 09/01/2020 | Afisa Afya |
| 91. | Maryam Khamis Ali | 03/06/2019 | Daktari Wa Binadamu |
| 92. | Sheikha Abdulla Salim | 10/07/2020 | Muuguzi Msaidizi |
| 93. | Rashid Hamoud Hemed | 12/02/2019 | Afisa Tabibu |
| 94. | Bakar Ali Haji | 04/01/2020 | Mhudumu |
| 95. | Maryam Massoud Juma | 07/10/2020 | Muuguzi |
| 96. | Mkitu Othuman Masoud | 03/02/2020 | Mhudumu |
| 97. | Asma Khamis Ali | 11/05/2019 | Muuguzi |
| 98. | Mulhat Juma Hamad | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 99. | Sumaiya Mwarab Suleiman | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 100. | Samira Issa Ally | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 101. | Samira Juma Shaaban | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 102. | Salma Masoud Shaaban | 07/10/2020 | Muuguzi |
| 103. | Nahya Said Hamad | 07/10/2020 | Muuguzi |
| 104. | Mussa Juma Said | 01/07/2019 | Muuguzi |
| 105. | Mohd Shaali Khatib | 06/03/2020 | Mhudumu |
| 106. | Fatma Zahor Abdalla | 06/03/2020 | Mhudumu |

| Namba | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Cheo |
|---|---|---|---|
| 107. | Salim Said Abdulla | 12/02/2019 | C/O |
| 108. | Shanaina Said Ahmed | 11/05/2019 | C/O |
| 109. | Faudhia Hamad Ali | 06/01/2020 | Mhudumu |
| 110. | Zuwena Maulid Majaaliwa | 06/01/2020 | Mhudumu |
| 111. | Wahida Asaa Ali | 04/02/2020 | Mhudumu |
| 112. | Mukhtar Yassir Khalfan | 12/01/2020 | Mhudumu |
| 113. | Salma Mohd Mussa | 01/07/2019 | Mhudumu |
| 114. | Halima Rashid Abdalla | 02/07/2019 | Mhudumu |
| 115. | Awatif Masoud Juma | 10/07/2019 | Muuguzi |
| 116. | Yunus Mohd Juma | 11/05/2019 | Mhudumu |
| 117. | Abdalla Saleh Abdalla | 06/01/2020 | Mhudumu |
| 118. | Shufaa Khamis Salim | 09/02/2020 | Afisa Afya |
| 119. | Nassor Kassim Maalim | 12/01/2020 | Mhudumu |
| 120. | Muhammed Mbarouk Muh'd | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 121. | Khamis Ali Khamis | 03/02/2020 | Mhudumu |
| 122. | Asha Hamad Faki | 12/01/2020 | Mhudumu |
| 123. | Latifa Ibrahim Mohd | 08/03/2020 | Muuguzi |
| 124. | Abdalla Ali Bakar | 04/01/2020 | Mhudumu |
| 125. | Ali Juma Ali | 12/01/2020 | Mhudumu |
| 126. | Haji Omar Faki | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 127. | Abdul Salum Hamad | 07/10/2020 | Muuguzi |
| 128. | Rahma Ali Hamad | 11/05/2019 | Lab/Tech |
| 129. | Muzney Amour Saleh | 12/02/2019 | Lab/Tech |
| 130. | Ali Hamad Khamis | 06/01/2020 | G/Nurse |
| 131. | Zainab Ahmed Salum | 11/05/2019 | Dent. Therapist |
| 132. | Haji Ali Hamad | 11/05/2019 | Lab/Tech |
| 133. | Zaina Fadhil Ali | 06/02/2020 | Muuguzi |
| 134. | Said Ali Fadhil | 10/01/2019 | Muuguzi |
| 135. | Fatma Salim Hamad | 12/01/2020 | Mhudumu |
| 136. | Suwadi Hamad Yussuf | 12/01/2020 | Mhudumu |
| 137. | Sharif Makame Chande | 08/03/2020 | G/Nurse |
| 138. | Sharabil Suleiman Khatib | 11/07/2019 | Lab/Tech |
| 139. | Mbarouk Suleiman Hamad | 06/03/2019 | M.D |
| 140. | Shuwena Hamad Bakari | 10/01/2019 | G/Nurse |
| 141. | Asha Abdulrahman Mussa | 10/07/2020 | G/Nurse |
| 142. | Khamis Juma Makame | 06/03/2019 | M.D |

| Namba | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Cheo |
|---|---|---|---|
| 143. | Ali Khamis Ali | 06/03/2019 | M.D |
| 144. | Nasra Mohd Seif | 06/03/2019 | M.D |
| 145. | Nadhra Faki Mbarouk | 03/02/2020 | Mhudumu |
| 146. | Othman Khalfan Haji | 01/07/2019 | Mhudumu |
| 147. | Mohd Salum Mohd | 04/03/2020 | Mhudumu |
| 148. | Ali Rashid Salim | 12/01/2020 | C/O |
| 149. | Raiya Ayoub Khamis | 05/01/2019 | Md |
| 150. | Tawhida Khamis Hamad | 11/05/2019 | C/O |
| 151. | Ahmad Salim Moh'd | 01/07/2019 | Physio |
| 152. | Fathia Mbarouk Mussa | 12/02/2019 | C/O |
| 153. | Ummulkulthum Bakari Salim | 06/02/2020 | Muuguzi |
| 154. | Ghania Haroub Ali | 05/08/2020 | Muhudumu |
| 155. | Nassor Ali Hamad | 05/08/2020 | Muhudumu |
| 156. | Said Hamad Hassan | 11/05/2019 | C/O |
| 157. | Ali Masoud Nassor | 07/09/2020 | R/Nurse |
| 158. | Suleiman Omar Said | 03/02/2020 | Muhudumu |
| 159. | Mohd Ali Said | 01/02/2019 | Mhudumu |
| 160. | Suleiman Makame Ali | 07/01/2020 | G/Nurse |
| 161. | Msuri Abrahman Massoud | 12/01/2022 | Daktari Wa Binadamu |

*Chanzo: Faili binafsi (OPF) za watumishi husika.*